11 MEI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Sita- Tarehe 11 Mei, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. JANETH P. PINDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini, aulize swali lake.

Na. 292

Kupandisha Hadhi Zahanati za Jimbo la Moshi Mjini

MHE. IBRAHIM M. SHAYO aliuliza:-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Zahanati za Bondeni, Kaloleni, Njoro na Kibororoni kutokana na ongezeko la wagonjwa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Jafar Seif.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupandisha hadhi kituo cha kutolea huduma kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu unazingatia miongozo mbalimbali iliyotolewa na Wizara ya Afya ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeainisha vigezo vya uanzishaji au upandishaji hadhi wa vituo vya kutolea huduma za

afya hususani ngazi ya afya ya Msingi kwa kuangalia idadi ya wagonjwa, idadi ya wakazi wa eneo husika, umbali kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine, miundombinu, watumishi, vifaa tiba na ukubwa wa eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imewasilisha maombi Hazina ya shilingi bilioni 23.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati 94 ambapo Kata ya Kibororoni imetengewa jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya zahanati za Bondeni, Kaloleni, Njoro na Kibororoni ili ziendelee kutoa huduma bora, wakati Serikali ikitafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vingine vya afya katika Kata za Kimkakati katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, swali la nyongeza.

MHE. IBRAHIM M. SHAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Kata ya Pasua ni kata ambayo ina wakazi wengi sana na kata ile tayari wananchi wana kiwanja kwa ajili ya kujenga zahanati; mpaka sasa hawajawezeshwa kujenga zahanati. Je, ni lini Serikali itakwenda kufanya ujenzi wa zahanati pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kata ya Shirimatunda ni kata ambayo ina zahanati bora, lakini kata ile haina mfumo, haina jenereta. Je, ni lini Serikali itapeleka jenereta pale kuokoa *operation* ndogo ndogo za akina mama? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia changamoto mbalimbali katika jimbo lake. Nianze kwa

kumpongeza kwa kuuliza suala la jenereta katika kituo cha Shirimatunda awali ilikuwa zahanati, lakini mwaka 2024 ambapo Mheshimiwa Rais aliidhinisha shilingi 250,000,000 kwenda kujenga *maternity complex* na majengo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika kituo hiki cha afya, tayari halmashauri ilitenga jumla ya shilingi 70,000,000 kwa ajili ya kununua jenereta na nimwelekeze tu Mkurugenzi siku ya kwenda kukabidhi jenereta hili Mheshimiwa Mbunge awepo ili atuwakilishe na atusemee vizuri kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ameuliza kuhusu Pasua, tayari katika eneo hili katika kituo hiki cha afya tumetuma timu yetu ya wataalam ya halmashauri na Ofisi ya *DMO* kwenda kuangalia ukubwa wa eneo ili kuweza hasa kuona kwamba tunafaa kujenga zahanati au kituo cha afya. Kwa hiyo, baada ya ile timu ya wataalam kutupa, mrejesho sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaweza kumpatia majibu Mheshimiwa Mbunge na kuona tunaenda kujenga zahanati au kituo cha afya. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona, Mheshimiwa Morris Makoi.

MHE. MORRIS J. MAKOI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika Kata ya Kindi kuna zahanati ikiwemo Zahanati ya Kijiji cha Chekereni, Weruweru haina maabara. Ni lini Serikali itaweka maabara au itaanzisha mpango wa kuweka maabara katika zahanati hii? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunakubali idadi ya wahitaji wa zahanati hizi katika jimbo ambalo Mheshimiwa Mbunge anatoka. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutajenga maabara ili iweze kutoa vipimo kwa wahitaji wetu, wagonjwa wetu kwa wakati na nimhakikishie baada ya Bunge hili Mheshimiwa Mbunge tuonane ili tuweze kutoa msisitizo katika kujenga maabara katika zahanati hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimemwona, Mheshimiwa Issa Mchungahela.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema amejibu majibu vizuri kabisa, lakini tunajaribu kuangalia *effect* ya vituo vya afya vingi na zahanati nyingi ambazo zimejengwa, kuwa hazina watumishi. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wanapatikana hususani kwenye jimbo langu, kuna vituo vya afya viwili na vina mtumishi mmoja mmoja, Kituo cha Chikoropora na Kituo cha Namwanga?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa ujumla.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela. Kwanza, tunakubali kwamba kuna ongezeko la vituo vya afya nchini. Tumejenga zahanati nyingi na tumejenga hospitali za halmashauri, lakini kuna upungufu wa watumishi katika sekta ya afya na Mheshimiwa Rais alitoa vibali vya kuajiri watumishi 12,000, wakiwemo wale 5,000 wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tunaendelea kuwaelekeza Wakurugenzi kuendelea kuainisha hasa katika maeneo yenye uhitaji mkubwa na kuendelea kutoa ajira za zile mkataba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela, pamoja na Wabunge wengine kwamba, tutaendelea kulifanyia kazi hili ili kuona tunazidi kuongeza watumishi katika vituo vyetu vya afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tinnar Chenge.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Muungano kilichoko Wilaya ya Bariadi kinahudumia wanawake wajawazito zaidi ya 500; na kwa kuwa, zaidi ya wanawake 150 wanajifungua katika kituo kile. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya wazazi katika kituo hiki cha afya? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kujenga na kuboresha miundombinu katika vituo vyetu vya afya na kwa idadi kubwa hii ya mama zetu wanaojifungua katika kituo hiki, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge nitampa ushirikiano wa dhati ili kwenda kujenga *maternity complex* ambayo itaweza ku-*accommodate* wagonjwa wetu katika kituo hiki cha afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paschal Chinyele.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Dodoma sasa ndiyo Jiji ambalo ni Makao Makuu ya Nchi, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika Kata za Matumbulu, Mpunguzi, Mbabala, Chigongwe pamoja na Mbalawala? Ahsante, *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na kupokea maombi ya kuongeza vituo vya afya. Tukiacha vile vya kimkakati ambavyo vimeshajengwa 120, lakini kuna vile 94 na bado tumeendelea kupokea maombi haya kupitia randama mbalimbali za mikoa na tumekuwa tukiwaelekeza Wakurugenzi kuendelea kutenga bajeti ili kuboresha miundombinu katika zahanati zetu na kuweza kuzipandisha kuwa vituo vya afya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Chinyele, makao makuu ya nchi lazima tuendelee kujenga vituo vya afya hivi ili viweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, nimwite Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, aulize swali lake.

Na. 293

Hitaji la Watumishi Idara ya Elimu na Afya – Ludewa

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajaza nafasi za Watumishi waliohamishwa Ludewa kutokana na ongezeko la shule mpya, Zahanati na Vituo vya Afya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuajiri kwa miaka mitano mfululizo, ambapo kati ya mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya watumishi 37,921 wa kada za afya na walimu 63,887 wa msingi na sekondari wameajiriwa na kupangwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali imeajiri jumla ya watumishi 12,000 na kuwapanga katika Mamlaka za Serikali za mitaa kote nchini ambapo watumishi wa sekta ya afya walikuwa 5,000 na wale wa elimu 7,000. Aidha, halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imepangiwa jumla ya watumishi 178, wakiwemo watumishi wa Kada ya Afya 42 na walimu 34 wa msingi na 102 wa sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kada za afya na elimu kwa kadri ya bajeti, ili kuziba pengo la upungufu wa watumishi lililosababishwa na ongezeko la vituo na shule mpya, uhamisho, kustaafu na kufariki kwa watumishi wetu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kamonga, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, niishukuru sana Serikali kwa kusikiliza changamoto cha wananchi tunazoleta sisi Wabunge hapa ndani. Wiki iliyopita tumepokea walimu 62 Ludewa. Kwa hiyo, ninamwona Mheshimiwa Profesa Shemdoe, amejikausha pale, lakini alishiriki katika kunisikiliza na kunisaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kutuletea watumishi hao 62 wiki iliyopita, bado Ludewa ina zahanati zaidi ya 80 na vituo vya afya sita na hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, bado upungufu ni mkubwa kulingana na ikama iliyotolewa na Serikali. Je, ikitokea kuna Watanzania wazalendo wa nchi hii hasa wazawa wa wilaya ile, wako tayari kwenda kufanya kazi kule. Je, Serikali iko tayari niwalete orodha, iweze kuwahamishia hao Ludewa? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa. Kwanza, ametoa pongezi kwa Serikali kuendelea kupeleka watumishi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa ushauri ambao na ombi ambalo amelitoa sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumelipokea kwa mikono miwili, atuletee orodha ya hao watumishi ambao; kwanza wanataka warudi nyumbani Ludewa kwenda kuokoa maisha ya ndugu zetu na kufundisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Serikali ilikuwa ni kudahili watumishi kwenye maeneo yao wanayotoka ili hasa kupunguza uhamisho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kamonga, ninaomba hiyo orodha ili tuweze kuwapeleka watumishi hao kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kumekuwa na tabia ambayo si ya kuridhisha ya watumishi wa halmashauri pindi wanapopewa ajira, wanapofika wanarudi tena kwenda kwenye maeneo mengine na mfano upo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, tumepokea watumishi wengi lakini wanaomba uhamisho na kadhia hiyo iko Makao Makuu ya TAMISEMI. Ni lini watakomesha huo utaratibu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunakubaliana hapa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Utumishi alitoa maelekezo mahususi kwamba watumishi wetu wanapokwenda kwenye vituo vya kazi wakae angalau kwa miaka mitatu ndiyo waanze kuomba uhamisho, wale wa dharura tu, ndiyo wanaoweza kuruhusiwa kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba, hili liko TAMISEMI tunalifanyia kazi na tutaendelea kulifuatilia kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba watumishi hawa ambao Serikali inawapeleka kwenda kutoa huduma kwa wananchi wetu waweze kutoa huduma ambazo wamesomea na tunadhibiti suala la uhamisho holela. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakuona, Mheshimiwa Boniphace Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nchi yetu tumekuwa na hamasa ya *Samia Scholarship* na hamasa yenyewe inahitaji walimu wa sayansi. Jimbo la Bunda 45% ndiyo waliopo, zaidi ya 55% walimu hawapo. Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa sayansi kwenye Jimbo la Bunda?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba,

tunavyoendelea kuwachakata walimu wa sayansi tutahakikisha tunaongeza walimu wa sayansi katika jimbo lake ili tuweze kupata madaktari na walimu wazuri kutoka kwake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere aondoe shaka, tutaendelea kuelekeza walimu katika jimbo lake ili waweze kupata wataalam. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea, bado tupo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimwite sasa Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Itwangi, aulize swali lake.

Na. 294

Kukamilisha Ujenzi wa Maboma ya Zahanati – Itwangi

MHE. AZZA H. HAMAD aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Maboma ya Zahanati yaliyopo Jimbo la Itwangi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Jimbo la Itwangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 na mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 36.68 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 426 ya zahanati kote nchini. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ilipokea jumla ya shilingi 194,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tano za Nshishinulu, Bukumbi, Mwakatola, Isela na Puni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizokusanywa hadi kufikia mwezi Novemba, mwaka wa jana zinaonesha kuwa maboma ya zahanati 1,934 kote nchini. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina maboma 28 yanayohitaji takriban shilingi bilioni 1.85 kuyakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Azza Hamad, swali la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, niipongeze Serikali na niishukuru sana kazi kubwa inayoifanya katika utoaji wa huduma za afya. Dhamira kuu ya Serikali kugawa jimbo ni kuhakikisha inasogeza huduma kwa wananchi wake, Jimbo la Itwangi ni jimbo jipya, ninaomba kurekebisha kidogo taarifa ya Mheshimiwa Naibu Waziri zahanati ya Mwakatola haipo Jimbo la Itwangi, ipo Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Jimbo la Itwangi, tuna vituo vya afya viwili tu kati ya kata 14. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kupandisha hadhi Zahanati ya Usule na Zahanati ya Didia kwa kuijengea majengo ili viwe vituo vya afya na tuweze kusogeza huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa Jimbo la Itwangi tuna maboma mengi ya zahanati na katika Mfuko wa Jimbo wa Mbunge umekwenda kupaua zahanati mbili, Zahanati ya Mwamkanga na Zahanati ya Bunonga. Je, Serikali iko tayari kwenda kukamilisha majengo haya ili yaweze kuanza kutoa huduma kwa wananchi wake? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya

Mheshimiwa Mbunge Azza. Kwanza nimpongeze kwa kuendelea kufuatilia changamoto hasa katika jimbo lake kwenye sekta ya afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda na nilifanya ziara katika Jimbo hili la Itwangi. Ni miongoni mwa majimbo mapya kweli na kweli ana kata 14 na kuna vituo viwili vya afya vya kutolea huduma pamoja na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakaa na halmashauri hii na sisi kama Serikali tutaendelea kujenga na kuboresha miundombinu ili kupandisha baadhi ya vituo vya afya ndani ya Jimbo la Itwangi ili kuongeza huduma kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutampa ushirikiano wa dhati kuhakikisha kwamba tunakamilisha miundombinu ambayo inahitajika kukamilisha vituo vya afya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze kwenye swali la pili kwamba tunaona hapa Mfuko wa Jimbo ulienda kupaua zahanati hii. Niendelee kumwelekeza Mkurugenzi kuendelea kuona umuhimu wa kupeleka nguvu katika zahanati hii ambayo Mheshimiwa Mbunge naye pia alipeleka hela yake ya Mfuko wa Jimbo pale ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi. Sisi kama Serikali Kuu Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, muda wote iko wazi na tunaweza kuonana na Mbunge, Mheshimiwa Azza ili kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma na miundombinu katika zahanati hizi ili ziendelee kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilimwona Mheshimiwa Cornel Maghembe.

MHE. CORNEL L. MAGEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Ichwankima yenye takribani watu 12,000 waliamua kuanzisha ujenzi wa kituo cha afya katika Kijiji cha Imarabupina. Katika michango ya wananchi wenyewe halmashauri iliweza kupeleka takribani shilingi milioni 40 na mimi kama Mbunge wao nimepeleka mifuko 100 ya simenti,

lakini mpaka sasa ujenzi ule umesimama na unasuasua. Je, kama Mbunge, wananchi pamoja na halmashauri wamepeleka fedha, Wizara inatusaidiaje ili kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Imarabupina katika Kata ya Ichwankima? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cornel Magembe, Mbunge wa Chato Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kupeleka mifuko 100 ya simenti kuunga mkono juhudi za Serikali. Pia, niendelee kumwelekeza Mkurugenzi kwamba hatua iliyofikia ni hatua ambayo sasa Mkurugenzi aweke fedha kidogo pale kwenye jengo letu lile ili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge Cornel Magembe kwa sababu ninatoka Mkoa wa Geita baada ya Bunge hili Tukufu kwenye zile siku za likizo tutakwenda moja kwa moja pale jimboni kwenda kuangalia ujenzi wa kituo hiki cha afya na ili kuleta msisitizo wa Serikali katika kuwekeza hizi fedha na kutoa huduma kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Magembe kwamba, tutakwenda kukamilisha majengo na miundombinu stahiki katika jimbo lake.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Jimbo la Solwa, Kata ya Mwenge kuna jengo katika Kijiji cha Mpango na Salawe katika Kijiji cha Amani pamoja na Solwa kuna jengo la mama na mtoto halijakamilika. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kukamilisha maboma hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Mnzava, Daktari wetu bingwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali aliyouliza ni ya msingi na tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, imeshafanya tathmini ya maboma yale ya zahanati na yale ya vituo vya afya ili kuangalia mchakato wa kupata fedha na kuomba fedha Hazina na kuweza kuyakamilisha maboma yote. Ndiyo kipaumbele cha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuhakikisha yale maboma yote yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi na maboma yote ambayo yameanzishwa kwa fedha za halmashauri tuone tunavyoweza kuyakamilisha ili yaweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. Nimpongeze Mheshimiwa Mnzava kwa swali hili na tutahakikisha tunakamilisha maboma haya.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, bado tupo Wizara hiyo hiyo. Sasa nimwite Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Chemba, aulize swali lake.

Na. 295

Upungufu wa Nyumba za Watumishi – Wilaya ya Chemba

MHE. KUNTI Y. MAJALA aliuliza:-

Je, lini Serikali itatatua tatizo la upungufu wa nyumba za Watumishi wa Wilaya ya Chemba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji mkubwa uliopo wa nyumba za watumishi wa Serikali nchini. Tathmini ya

mahitaji ya nyumba za watumishi katika Halmashauri ya Chemba inaonesha kuwa mahitaji ya nyumba za watumishi ni 995, nyumba zilizopo ni 448 ambapo jumla ya watumishi ni 394. Nyumba za watumishi wa afya 43 na nyumba za watumishi wa utawala ni 11. Upungufu uliopo ni nyumba 507 sawa na upungufu wa 53%. Kati ya nyumba 995 zinazohitajika, nyumba za walimu ziko 877, nyumba za watumishi wa afya zipo 69 na nyumba za utawala zipo tisa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano, Serikali imetoa shilingi bilioni 1.91 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba na kujenga nyumba 24, nyumba 18 upande wa elimu, na nyumba tatu kwa upande wa nyumba za utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mpango maalum wa ujenzi wa nyumba za watumishi ambapo bajeti itatengwa kila mwaka wa fedha ili kupunguza upungufu katika Halmashauri ya Chemba na Halmashauri nyingine kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, maswali ya nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa nyumba za watumishi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chemba umepelekea watumishi wengi kuja kuchukua *check number* na kuondoka kwenye Halmashauri yetu na wananchi wetu kukosa huduma za msingi ikiwemo tasnia ya afya lakini na elimu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko tayari kutumia taasisi zake: *National Housing* ambayo ipo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; *Watumishi Housing* ambayo ni taasisi ipo chini ya Wizara ya Utumishi; pamoja na *TBA* ambayo ipo Wizara ya Uchukuzi kuwapeleka Wilayani Chemba kuondoa tatizo na

changamoto ya nyumba za watumishi ili wananchi wa Wilaya ya Chemba waweze kuhudumiwa vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Serikali iko tayari kurudisha posho ya mazingira magumu kwa watumishi wetu iwe kama chachu ya watumishi wetu wanaokwenda kukutana na mazingira magumu ikiwemo upotevu ama upungufu wa nyumba za kukaa ili ziweze kuwapa motisha na kuendelea kufanya kazi kwenye mazingira hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Kunti Majala kwa kuuliza maswali madogo ya nyongeza hasa yakiwagusa watumishi kwa ujumla, lakini hasa hasa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali uko bayana tumeeleza kwamba tumefanya tathmini ya ujenzi wa nyumba zaidi ya 2,000. Tunakadiria kutenga na kutafuta fedha kama shilingi bilioni 241 ili angalau kwenda kujenga nyumba hizi. Tumeelekezwa kwamba nyumba hizi tukazijenge kwenye zile halmashauri za pembezoni zaidi ambazo hata nyumba za kupanga za hadhi ya watumishi hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kushirikiana na *Watumishi Housing*, *TBA* na *NHC* ambapo ushauri huu tuliupata kutoka Wizara ya Mipango ili kuhakikisha kwamba tuna-*engage private sector* katika eneo hili ili kukamilisha nyumba hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la posho, tunaendelea kulifanyia kazi na lilikuwepo kweli na sasa tunaendelea kusisitiza kwamba tuendelee kutoa motisha kwa watumishi wale ambao wapo pembezoni ili wabaki kwenye maeneo yao ya kazi na waendelee kutoa huduma. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Mwita Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba zoezi la kujenga nyumba kwa watumishi katika halmashauri itachukua miaka mingi. Je, Serikali haioni kama kuna haja sasa ya kubadilisha utaratibu wa kujenga nyumba au kama wanatafuta fedha watafute, lakini waende kwenye *so called housing allowances* ili wale watumishi wapate namna ya kuishi katika halmashauri zetu na wafanye kazi kuwahudumia watu wetu? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tumeshapokea ushauri kutoka katika Kamati ya TAMISEMI, lakini pia tuna-*engage private sector* kuhakikisha kwamba watumishi wajengewe nyumba katika maeneo ya kazi na waweze kupata zile nyumba bora na kwa gharama nafuu. Hili tunalichukua na kwenda kulifanyia kazi.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Alan Thomas.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitoe shukrani kwa niaba ya wananchi wa Kakonko kwa kupokea watumishi wa afya zaidi ya 80. Sasa kwa sababu tuna uhaba mkubwa wa nyumba za watumishi kwenye zahanati zetu hasa Zahanati ya Nyagwijima, Mugunzu, Rumashi, Ruhuru, Nyakayenze na Njomulole, nini mpango wa Serikali kuona namna ya kujenga nyumba za watumishi katika maeneo hayo? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali

inaona changamoto ya upungufu wa nyumba za watumishi na tutaelekeza ujenzi wa nyumba hizi katika halmashauri zile za pembezoni zaidi ili kuweza kuwapa faraja na motisha watumishi wetu waweze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge utaratibu tunaenda nao Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuhakikisha kwamba tunajenga nyumba hizi, hata kama itakuwa ni kwa awamu, lakini tuhakikishe kwamba mwendo tunauanza ili kuweza kutoa motisha kwa watumishi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Kibona katika Kata ya Kononi pamoja na Kituo cha Afya cha Nyabiyonza katika Kata ya Nyabiyonza viko pembezoni na watumishi wanapata shida kupata nyumba za kupanga kutokana na *nature* ya maeneo ya vituo hivi. Je, ni lini Serikali itawajengea watumishi nyumba? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bashungwa, kaka yangu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kujenga nyumba hizi za watumishi na tumeshaanza mchakato wa tathmini na kuona hasa maeneo yale ya pembezoni ambayo yana uhitaji mkubwa zaidi. Nimhakikishie Mheshimiwa Bashungwa tutaendelea kujenga nyumba katika maeneo hayo ya watumishi ambayo umeyaainisha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Vituo vya

Afya vya Ruaha Mbuyuni, Kata ya Ilula na Kata ya Nyalumbu vimejengwa, lakini hakuna nyumba za kuishi madaktari. Kwa hiyo, wananchi wanapata shida sana kwa sababu pia kutokana na miundombinu mibovu iliyopo katika Wilaya ya Kilolo. Je, wanatusadiaje kwa haraka zaidi ili nyumba za watumishi wa afya ziweze kujengwa kwa haraka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunakiri upungufu wa nyumba hizi kama ambavyo nimeshatoa maelezo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunalichukua hili ili kwenda kulifanyia kazi katika tathmini ile ambayo tumeshaiwasilisha hapa katika Bunge lako Tukufu kuhakikisha kwamba tunaanza mchakato wa ujenzi wa nyumba hizi ili kuweza kuleta faraja na tija kwa watumishi wetu katika maeneo ya pembezoni zaidi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Sasa nimwite Mheshimiwa George Venance Lugomela, Mbunge wa Maswa Mashariki, aulize swali lake na swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi.

Na. 296

Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Maswa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI K.n.y. MHE. GEORGE V. LUGOMELA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Stendi ya Mabasi ya Maswa kwa kiwango stahiki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali Mheshimiwa George Venance Lugomela, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Stendi ya Wilaya ya Maswa iliyopo katika eneo la Stendi Mpya lenye ekari 14 ina upungufu wa baadhi ya miundombinu muhimu. Ili kuiwezesha kutoa huduma ipasavyo, Halmashauri ya Wilaya Maswa kupitia fedha ya Mfuko wa Jimbo na mapato ya ndani katika mwaka wa fedha 2023/2024, iliendelea kuboresha stendi ya Mabasi Maswa kwa kumwaga vifusi vya moramu eneo la kupakilia na kushushia abiria, barabara za kuingia na kutoka eneo la stendi na kuchimba na kujengelea mitaro ili kuzuia maji kutuama eneo la stendi. Maboresho haya yaligharimu jumla ya shilingi 70,000,000. Ujenzi wa miundombinu hii umekamilika na inatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha stendi hii kuendelea kutumika, Serikali imeendelea kuiboresha ambapo katika mwaka wa fedha 2026/2027, kiasi cha shilingi 60,000,000 kimetengwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Maswa ni wilaya kongwe imezaa Mkoa mzima wa Simiyu ukiondoa Wilaya ya Busega, lakini hali ya stendi yake kwa kweli bado hairidhishi kabisa. Sasa ningependa kujua, kiwango cha pesa shilingi 60,000,000 ni kidogo sana na stendi ile kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kubwa shilingi 60,000,000 hazitoshi. Serikali kuu inaonaje kuongeza fedha hizo ili kuisaidia halmashauri ya wilaya iweze kukamilisha stendi hii kwa kiwango kinachotakiwa? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mashimba Ndaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunaanza na hizi ambazo tayari tumetenga kupitia halmashauri yetu Bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 shilingi 60,000,000 ili kuendelea kuboresha. Stendi hizi baada ya kubainisha eneo tunajenga kwa awamu ili kuhakikisha kwamba tunafanya mwendelezo wa ujenzi huu ili kukamilisha stendi hizi ziendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kutenga fedha ili tuweze kukamilisha miundombinu katika stendi hii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutenga fedha kwa kadri tunavyozipata ili kuweza kukamilisha stendi hii. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Dkt. Catherine.

MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Nganga - Mfumuni iliyopo Manispaa ya Moshi ulianza mwaka 2019 na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2021. Hadi hivi sasa ujenzi wa stendi hiyo umefikia 63%. Swali langu; je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha stendi hii ya mabasi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Catherine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu uhitaji wa stendi hii kwa wananchi wetu katika hili na Serikali iliridhia kuanza ujenzi katika mwaka 2019 na ujenzi Mheshimiwa Mbunge anakiri

umefikia 63%. Maendeleo ni hatua tumekwisha kuanza kuchukua hatua na tutaendelea kuweka fedha kutenga bajeti kwa ajili ya ukamilishaji wa stendi hii ili iendelee kutoa huduma kwa wananchi wetu. Nimhakikishie Mheshimiwa Catherine tutaendelea kutenga fedha ili wananchi wetu wapate huduma hii ili na wao waguswe na tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa George Malima.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mji wa Mpwapwa hauna stendi ya kisasa, eneo linalotumika sasa kama stendi ni eneo la soko. Je, ni lini Serikali itajenga stendi ya kisasa katika Mji wa Mpwapwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge George Malima na nimpongeze kwa swali lake la nyongeza, lakini pia nimpongeze tulifanya ziara na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Jimbo lake la Mpwapwa na wananchi wanampenda sana kwa sababu walifurika kwenye mkutano ule wa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa George; kwanza niwaelekeze wataalamu wetu wa halmashauri kupitia Mkurugenzi waweze kuleta andiko pale Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ili tuone namna ya kuanza ujenzi wa stendi hii na hitajio la wananchi wa Halmashauri ya Mpwapwa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea. Tuko Wizara hiyo hiyo swali la mwisho.

Sasa nimwite Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Nyasa, aulize swali lake.

Na. 297

Uhamisho wa Watumishi wa Umma Nyasa

MHE. JOHN J. NCHIMBI aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kuhamisha Watumishi wengi kwenye Wilaya za pembezoni ikiwemo Nyasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, ninaomba kujibu swali Mheshimiwa John John Nchimbi, Mbunge wa Jimbo la Nyasa na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho katika utumishi wa umma huzingatia masuala muhimu ikiwemo, kuthibitishwa kazini baada ya kuajiriwa, ridhaa ya uhamisho kutoka kwa mwajiri na sababu zingine kama vile ugonjwa au kumfuata mwenza, ambapo mhusika hulazimika kuambatisha vielelezo vinavyothibitisha hitaji la uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni, Serikali iliendesha zoezi la Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi kote nchini kwa lengo la kubaini mahitaji ya rasilimali watu katika utumishi wa umma. Kupitia zoezi hilo, Serikali imetambua maeneo yenye watumishi wengi, yenye uhitaji na yenye upungufu wa watumishi. Kwa kuzingatia hayo, Serikali imeanzisha programu ya kufanya msawazo kwa taasisi za umma zikiwemo za pembezoni utakaokidhi mahitaji ya watumishi katika taasisi na maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhama kwa watumishi wengi kwenye wilaya za pembezoni ikiwemo Nyasa, Serikali imeendelea kudhibiti uhamisho uSIYO na lazima kwa watumishi ili kuziwezesha halmashauri zote kuwa na uwiano mzuri wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John John Nchimbi, maswali ya nyongeza.

MHE. JOHN J. NCHIMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza, wakati Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma mwaka jana ilipeleka watumishi 15 wapya wa afya Wilaya ya Nyasa, Wizara ya TAMISEMI ilihamisha watumishi 60 Wilaya ya Nyasa kuwapeleka sehemu nyingine. Je, hii haiioneshi Wizara kwamba wakati Wizara nyingine inajenga nyingine inabomoa katika Wilaya ya Nyasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; unapohamisha watu kuwapeleka wilaya nyingine maana yake huko umeongeza idadi ya watu. Kwa nini kule unapowapeleka wale ambao wameongezeka kule wasihamishwe wao kupelekwa Wilaya ya Nyasa na kuwabadilisha badala ya kuwajaza sehemu moja? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mbunge Mheshimiwa John John Mchimbi kwa kuuliza maswali madogo ya nyongeza hasa yakilenga maeneo ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumekwisha kuanza programu maalum ya kufanya msawazo wa watumishi na kingine ni namna ya kuwadahili watumishi hawa. Tulielekeza watumishi hawa wadahiliwe kwenye mikoa yao ili angalau wasiwe na uwezo wa kuomba uhamisho kwa maana ya kwamba wanakuwa ni wazoezi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tumekwishawasiliana na wenzetu Ofisi ya Utumishi kwamba wale wanaojitolea katika

maeneo yetu tuwaombee ili waweze kupata ajira kwa maana tayari wanajitolea kwenye maeneo hayo, wameshapata uzoefu kwenye maeneo hayo hawawezi wakahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufuatilia na kuhakikisha tunaweka msawazo wa watumishi wa umma katika maeneo hasa ya halmashauri za pembezoni. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Abdallah Chikota.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ni miongoni mwa halmashauri ambazo ziko pembezoni mwa nchi hii na watumishi wakipangwa, muda mfupi baada ya kuripoti wanaleta vyeti kwamba, wana magonjwa mazito ambayo hayatibiwi kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara na ya Kanda, inabidi wasogee Muhimbili na Benjamin Mkapa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia changamoto kama hizi, ili wilaya za pembezoni kuwe na watumishi wa kutosha?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu; ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chikota, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeanza kufanya utaratibu huu wa kuweka msawazo wa watumishi, lakini pia, kupitia namna ya kuwapata watumishi hawa, tuwapate kwenye maeneo yao ya kazi. Pia, tunawaomba watumishi wetu, kupitia Bunge lako Tukufu, wawe wazalendo, utumishi wakiwapeleka waende wakafanye kazi, ambayo wameomba, ili kuweza kuwahudumia wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya *Njombe DC* ni miongoni mwa halmashauri ambazo watumishi

wengi wamekuwa wakiripoti, hasa pembezoni mwa Jimbo langu la Lupembe kule Madeke, Mfiriga, Ukalawa na kule Kitole, wanaripoti baada ya ajira wanahama na watumishi wengi wamejaa sana mijini. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwa nini Serikali msipunguze watumishi wengi ambao wamejaa mijini kwenda vijijini? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Swalle, wa Njombe *DC*. Kwa taarifa tu, nimefika katika jimbo lake, nimefika katika Hospitali yetu ya Halmashauri ya Wilaya ya *Njombe DC* na wapo watumishi pale wanachapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhama na upungufu wa watumishi, hili tunalichukua kama Wizara. Maelekezo ya Serikali, hata katika ajira mpya hizi ambazo Ofisi ya Rais, Utumishi inapanga, tumeelekeza wapange sana kwenye halmashauri za pembezoni kwa sababu, ukipanga kwenda mjini, tayari mjini wapo na bado wataomba kuhamia kwenda mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ni kuendelea kuwapanga watumishi katika halmashauri za pembezoni, ili hata wanapoomba uhamisho, angalau wanabakia wale wengine kufanya kazi kule. Pia, tunawaomba watumishi wetu, wanapopangiwa kwenda kutoa huduma kwa wananchi wetu, waende kwa moyo wa dhati wa kizalendo, ili waweze kutoa huduma kwa wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunashukuru sana kwa majibu yako mengi na sahihi kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Temeke, aulize swali lake.

Na. 298

Udhibiti wa Uchafuzi wa Mito, Temeke

MHE. MARIAM N. KISANGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti viwanda vinavyomwaga maji machafu kwenye mito, Temeke?

MWENYEKITI: Majibu kwa Mheshimiwa yatasomwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti viwanda vinavyomwaga maji machafu kwenye mito, ikiwemo kufanya kaguzi za mara kwa mara katika viwanda vilivyopo Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo za kufanya ziara za mara kwa mara za kushtukiza, Serikali pia, imesimamia utekelezaji wa Sheria yetu ya Mazingira, Sura ya 191, pamoja na Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272, ikiwemo kutoa maagizo ya kurekebisha au kusimamisha kabisa shughuli za viwanda zinaosababisha uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha doria za mazingira, kufanya kaguzi za kushtukiza na kutoa elimu kwa wamiliki wa viwanda vilivyopo Temeke na maeneo mengine nchini. Sambamba na hilo, Serikali inakamilisha ufungaji wa mfumo wa kisasa wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira *(Tanzania Online Continuous Emission Monitoring System)* utakaowezesha kufuatilia viwango vya uchafuzi kwa wakati na

kuchukua hatua za haraka dhidi ya wanaokiuka Sheria. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mariam Kisangi, maswali ya nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, changamoto ya kutiririka kwa maji katika Mto Mpogo uliopo katika Jimbo la Temeke unaathiri Kata ya Sandali, Mitaa ya Mpogo, Kimbunga, Usalama, Kilakala, Makangarawe na Buza, maeneo haya yanafurika maji, ambayo yanakuwa na kemikali zinazotoka viwandani. Je, Serikali pamoja na majibu mazuri iliyotoa, iko tayari kutoa tamko kwa wenye viwanda kufuata utaratibu ambao umeelekezwa hapo mbele na Mheshimiwa Naibu Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, matatizo haya au changamoto hiyo imewakumba katika kata hizo, lakini hasa katika Kata ya Kilakala eneo la Yombo Reli, Bonde la Bongotonyo. Wananchi wako ndani ya maji ambayo yamejaa, wako mabondeni kwenye maji, ambayo yana kemikali na maji hayo hayatoki. Tunajitahidi kuyanyonya na nini, yaani yanafanyiwa kazi, lakini wananchi bado wenyewe wako katika maeneo hatarishi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kufuatana nami akaone hali halisi iliyopo katika eneo hilo la Bongotonyo na maeneo mengine ya Jimbo la Temeke?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali, kupitia *NEMC,* tumefanya ukaguzi wa viwanda Mkoa wa Dar es Salaam na hususan Jimbo la Mheshimiwa Mbunge kule Temeke, kupitia Ofisi zetu za Kanda. Tumefanya ukaguzi kwenye viwanda 158 na tumebaini mapungufu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanda vichache kweli vinatiririsha maji kuelekea kwenye makazi ya wananchi na vipo

viwanda ambavyo vinatiririsha maji machafu bila kuyatibu kabla ya kuyaruhusu kutoka nje ya kiwanda. Vilevile vipo viwanda ambavyo vinatiririsha maji hayo bila kuwa na vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu, vibali hivi vya kutiririsha maji vinatolewa na Ofisi za Mabonde, chini ya Wizara ya maji na vilevile kumekuwepo na uchafuzi wa viwanda hivyo bila kuzingatia Sheria zetu za Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Tumechukua hatua kwanza, mbali na kufanya ukaguzi huo, tumetoa elimu kwa wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua vilevile hatua za kisheria, ikiwa ni pamoja na kuwapiga *fine* na wakati mwingine imetulazimu kuzuia utiririshaji wa maji kwenye viwanda hivyo katika shughuli zao za uzalishaji. Ninachukua nafasi hii, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kuwaeleza Mameneja wetu wote wa Kanda mbalimbali nchini za *NEMC*, wasimamie utekelezaji wa Sheria kuhakikisha kwamba, wamiliki wa viwanda hawatiririshi maji kuelekea kwenye makazi ya wananchi na kuelekea kwenye mito yetu kusababisha uchafuzi wa mazingira. Si hivyo tu, ninawaomba sana wenye viwanda wazingatie matakwa ya Sheria na kuhakikisha kwamba, wananchi wanakuwa salama wakati wao wakiendelea na shughuli zao za kiuchumi za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kuelekea kwenye Kata hiyo ya Kilakala, kata ambayo Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba, wananchi wameathirika kwa maji haya machafu kuingia kwenye makazi yao. Kwa idhini ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Lucy Kombani.

MHE. LUCY D. S. KOMBANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Kumekuwa na uchafuzi mkubwa sana wa mazingira unaosababishwa na shughuli za uchimbaji wa madini unaoendelea katika Mito ya

Mvua na Mto Mfizigo, ambayo inapatikana Morogoro Vijijini. Je, Serikali inachukua hatua gani ya haraka na ya kudumu, ili kudhibiti uchafuzi huu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucy. Ninaelekeza, kama ambavyo nimetangulia kuelekeza kwenye swali la msingi na jibu la msingi; kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mameneja wetu wote wa Kanda ikiwemo Kanda ya Morogoro anakotokea Mheshimiwa Mbunge, wahakikishe kwanza wanaendelea na kaguzi hizi za mara kwa mara za kushtukiza. Vilevile wahakikishe uzalishaji wowote ule uwe ni kwenye viwanda au madini, uzingatie Sheria hizi mbili zinazotuongoza, Sheria ya Mazingira, Sura 191 na Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Sura 272.

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Hija.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba, viwanda vilivyofanya uchafuzi wa mazingira wamekuwa wakivipiga *fine*. Ni kwa nini Serikali haiagizi kwamba, viwanda hivyo vitoe fidia kwa wananchi wanaoathirika? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sijakusikia vizuri.

MWENYEKITI: Hebu rudia swali lako.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali haitoi agizo pale viwanda vinapoharibu mazingira kutoa fidia kwa wananchi ambao wanaathirika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi taratibu zote hizi tunazoziendesha za kuhakikisha mazingira yanalindwa, mazingira yanatunzwa dhidi ya uchafuzi unaotokana na uzalishaji ndani ya shughuli zetu za kiuchumi, tunaziendesha kisheria. Popote ambapo uchafuzi huu umefanyika, Sheria inatuongoza nini tufanye. Sisi tunaweka msisitizo zaidi katika kuzuia uchafuzi huu unaoweza kusababisha madhara kwa wananchi wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ninamwita sasa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 299

Wananchi wa Arusha Kunufaika na *AFCON 2027*

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Je, Serikali imewaandaaje Wananchi wa Mkoa wa Arusha kunufaika na uwepo wa Mashindano ya *AFCON 2027*?

MWENYEKITI: Majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa niaba yake, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa fursa nyingi zinazoambatana na mashindano ya *AFCON* 2027 na imedhamiria kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa hizo. Serikali imeunda Kamati za Kitaifa za Maandalizi na zile za mikoa wenyeji, ikiwemo Mkoa wa Arusha, Dar es Salaam na Mjini Magharibi. Majukumu ya Kamati hizi ni kusimamia maandalizi ya *AFCON* 2027 na kuhakikisha wananchi wanazijua na kujiandaa nazo ipasavyo, ili waweze kunufaika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inatekeleza mpango mkakati wa maandalizi na kutangaza fursa za mashindano haya kwa wadau wote kupitia majukwaa mbalimbali, kama vile makongamano, vikao kazi vya makundi mbalimbali ya wadau na kutumia vyombo vya habari. Mkoa wa Arusha umezindua kamati yake ya maandalizi na tayari ipo kazini. Ninatoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwenye miji ya mashindano kushirikiana na Kamati za Mikoa, ili kuhamasisha wananchi kuchangamkia fursa hizi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, maswali ya nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa *AFCON* na ni ukweli kwamba, mashindano haya ni fursa kubwa kwa wananchi wetu, hasa wajasiriamali wadogowadogo na wa kati wakiwemo mama lishe, baba lishe, madereva bajaji, madereva *taxi* na wafanyabiashara walioko sokoni. Je, kwa nini Serikali isitengeneze mpango wa muda mfupi wa kuwatambua, kuwapa mafunzo na kuwawezesha wafanyabiashara hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tumeshuhudia kwa nyakati tofauti Timu yetu ya Taifa kutokufanya vizuri katika mashindano mbalimbali. Je, kwa nini Serikali isiwe na mpango madhubuti wa kuandaa wachezaji wadogo na kuwapeleka kwenye shule mbalimbali za michezo, ili baadaye waje kuchezea Timu yetu ya Taifa?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninampongeza Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso kwa maswali mazuri na jinsi anavyoendelea kuwapigania Wakazi wa Mkoa wa Arusha. Kujibu

maswali yake, kwanza Serikali imetengeneza kamati mbalimbali za uratibu zikiwemo Kamati za Mikoa. Kamati hizi miongoni mwa hadidu rejea zake ni kuhakikisha zinaendesha semina, makongamano na warsha, ili kuwaelimisha wananchi wa maeneo husika kuhusiana na fursa zinazoletwa na *AFCON* na namna ya kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa mikoa ambayo ina kamati inayofanya vizuri sana, ninafikiri ni kwa sababu ya uanamichezo wa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa pale, *CPA,* Amos Makala, ambaye kamati yake imekuwa inafanya kazi nzuri sana. Kwa hivyo, miongoni mwa mambo ambayo Kamati ya Mkoa wa Arusha inayafanya ni pamoja na kuwakusanya wanufaika ambao tunaamini wanaweza kunufaika na Mashindano haya ya *AFCON,* wakiwemo mama lishe, watu wa bodaboda, watu wa utalii na kadhalika, ili kuhakikisha kwamba, inawaelimisha na kuwaonesha fursa ambazo zinaweza kuja na *AFCON*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, inatengeneza mfumo. Tuko katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba, tuna mfumo wa kuwasajili, kwa ajili ya kuhakikisha watoa huduma mbalimbali wanatambuliwa na wanasaidiwa kuhakikisha wanazifikia fursa ambazo zinakuja na *AFCON* na kufanya mashindano hayo yaweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili la kuhusiana na Timu ya Taifa; sasa hivi Kocha wa Timu yetu ya Taifa, Miguel Gamondi, anaendesha mazoezi mbalimbali ya kuhakikisha anapata timu bora, ikiwemo kutambua vipaji kuanzia ngazi za chini kabisa. Hili la Mheshimiwa Mbunge Cecilia Paresso alilolileta la kuhakikisha tunakusanya vijana na kuwapeleka kwenye *academy* za nje ya nchi; bado hatujalifikia, lakini ninaomba nilichukue kama wazo na tutaona namna ambavyo tunaweza kulifanyia kazi. Ahsante.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka kujua tu Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba,

wageni na watalii wanaotarajiwa kuja kwenye Masindano ya *AFCON* ambao wanakadiriwa kuwa zaidi ya laki tatu, wanaweza kugeuka na kutoa fursa halisi ya ajira, uwekezaji kwenye huduma za utalii na malazi kwa sababu, sasa hivi hoteli tulizonazo ni chache kuweza kupokea watu hao wanaokadiriwa. Pia, kwenye huduma za kitamaduni na kuongeza ukuaji halisia kwa Watanzania wa kada zote, kwa maana ya wale wafanyabiashara wa chini na wa kati badala ya kubaki tu kwa wawekezaji wakubwa wenye hoteli kubwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na kweli nilikuwa nina jibu refu, lakini ukweli ni kwamba, kwa sababu, kama ambavyo nimejibu wakati ninajibu swali la Mheshimiwa Paresso, moja ya mambo tunayoyafanya ni kutengeneza mfumo ambao utawasajili watoa huduma wote. Kwa mfano, hoteli zetu hazitoshi kwa idadi ya wageni tunaowatarajia, miongoni mwa mambo ambayo tunataka kuyafanya ni kuhakikisha makazi binafsi yanaweza kuandikishwa na yakatumika kama *Airbnb*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwa mama ntilie na waendesha bodaboda, tunatengeneza mfumo ambao utawasajili kama watoa huduma rasmi wa Mashindano ya *AFCON*. Kwa hivyo, tunalifanyia kazi jambo hili na ninamtoa wasiwasi Mheshimiwa Matiko kuhusiana na suala hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ninashukuru kwa majibu ya Serikali, kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri, na namna ambavyo wadau mbalimbali watashiriki katika *AFCON* 2027, lakini bado SIYOni ushiriki wa wahitimu wetu wanaomaliza vyuo na vyuo vikuu. Je, Serikali haioni kwamba, ni muda muafaka pia, wa kuandaa programu maalum itakayowaunganisha vijana wetu wanaomaliza vyuo na vyuo vikuu katika mashindano haya ya mpira wa miguu, ambayo pia, yana fursa nyingi za kiuchumi ndani yake? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

Hilo swali ungeleta kama swali la msingi aweze kujibu vizuri zaidi. Kwa kifupi, ni majibu yaleyale.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nimeisikia hoja ya Mheshimiwa Dkt. Regina Malima kuhusiana na ushiriki wa wahitimu wa vyuo na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema mbele ya Bunge lako Tukufu ya kwamba, fursa ambazo zinakuja na *AFCON* hazina ulazima wa kutoka kwa Serikali moja kwa moja. Bado tunachukua maoni mbalimbali wakiwemo wahitimu wa vyuo na vyuo vikuu kuhusiana na mambo ambayo wanaona wanaweza kufanya, kwa ajili ya kuhakikisha *AFCON,* ambayo sisi tunakwenda kuiandaa 2027, inakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, milango yetu iko wazi. Kama kuna jambo wahitimu wa vyuo na vyuo vikuu wanaona wanaweza kulifanya na likaleta tija kwa *AFCON* hii, tupo tayari kuwasikiliza na kuona namna ambavyo tunaweza kuliratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Ninamwita Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, aulize swali lake na swali hilo litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Emmanuel Khambay.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika.

MWENYEKITI: Ahaa! Mheshimiwa kumbe umerudi. *(Kicheko)*

MHE. EDWARD O. KISAU: Kwa niaba ya wananchi wa Kiteto tunaomba majibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa niliambiwa haupo.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa safarini sikujua kwamba ningewahi, lakini nimewahi.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. EDWARD O. KISAU: Kwa niaba ya wananchi wa Kiteto tunaomba majibu ya swali Na. 300.

Na. 300

Ukarabati wa Bwawa la Kijiji cha Asamwata - Kiteto

MHE. EDWARD O. KISAU aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukarabati Bwawa la muda mrefu la Kijiji cha Asamwata Kata ya Sunya – Kiteto.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa niaba ya Waziri, Mheshimiwa Andrea Mathew Kundo, Mheshimiwa endelea.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itafanya mapitio ya usanifu na tathmini ya Bwawa la Asamwata lililopo Kijiji cha Asamwata Kata ya Sunya Wilaya ya Kiteto, Mkoani Manyara. Lengo la kufanya kwa usanifu na tathmini ya bwawa hilo linalohudumia binadamu pamoja na mifugo ni pamoja na kubaini maeneo yanayohitaji ukarabati sambamba na fedha zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kazi hiyo kukamilika, Serikali itapeleka fedha za ukarabati wa bwawa hilo kulingana na kazi zitakazoelekezwa na fedha kadri zitakavyokuwa zikipatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Olelekaita, maswali ya nyongeza. Waheshimiwa ambao tumewasha visemeo kwa matumaini ya kupata maswali ya nyongeza, ninaomba tuzime, endelea.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili. Swali la kwanza; kutokana na hali ya Kiteto kuwa ni kame nini kauli ya Serikali kutupa kipaumbele kwa huko mbele kuhusu pesa za mabwawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari tutembelee hili Bwawa la Asamwata ambayo kwa kweli kwa miundombinu yake imechakaa sana, lini yuko tayari tutembelee hilo bwawa haraka sana? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa maswali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Wakili Msomi Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhusiana na utayari wa Serikali kwenda katika Jimbo la Kiteto kulitembelea hili Bwawa la Asamwata. Daima na kwa dhamira ya Serikali ya kuendelea kutekeleza miradi ya maji, sisi Serikali na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba tunafika katika maeneo yenye changamoto na kujionea ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari muda wowote hasa baada ya Bunge hili la bajeti kukamilika kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kujionea bwawa hili. Hata hivyo, nimtoe hofu Mbunge, wataalam wetu watakuwa wameshaanza kazi ya kufanya usanifu ili kuangalia maeneo ambayo yatakuwa yanahitaji kufanyiwa ukarabati ili fedha zitengwe kwa ajili ya kupelekwa na kutatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine tunatambua kwamba Jimbo la Kiteto ni kame sana na tunao mpango wa Serikali katika maeneo ambayo ni kame kuyapa kipaumbele cha kipekee ili kuhakikisha kwamba wasiwe wanapitia changamoto ya maji

wakati kuna fursa ya mitambo ambayo ilinunuliwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo itaweza kutumika kuchimba mabwawa hayo. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Josephine Kapoma.

MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Morogoro wanaishukuru sana Serikali kwa kusaini mkataba na Nchi ya Ufaransa kwa ajili ya upanuzi wa Bwawa wa Mindu zaidi ya bilioni 81, lakini sasa wanauliza imeshakuwa muda mrefu sana kuwalipa fidia wananchi waliopisha zoezi hili, wanataka kujua ni lini sasa Serikali inaweza ikaanza zoezi hili. Ahsante?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kifupi.

(Hapa kulitokea hitilafu ya kipaza sauti)

MWENYEKITI: Washa uzime tena, hebu jaribu kuwasha na kuzima.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro. Serikali inatambua umuhimu wa kulipa fidia wananchi wote ambao wako katika hifadhi ya Bwawa la Mindu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo makundi mawili, kundi la kwanza ni wale ambao walikuwepo katika mita 500 ambapo wanalipwa fidia zaidi za bilioni 4.8, lakini pia baada ya kuinua tuta na kupanua maeneo ya uhifadhi kuna mita 500 zingine zinaongezeka na wenyewe pia wako katika mpango huo. Tumeshakamilisha awamu ya kwanza na sasa Serikali inaendelea na awamu ya pili kuhakikisha kwamba wananchi wote ambao wanapisha mradi huo, waweze kunufaika kulingana na stahiki zilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kawamba, swali la nyongeza.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inazoendelea kufanya kwa kusimamia sekta ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuuliza swali langu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ndani ya Jimbo la Igalula tayari umeshafika katika Kata ya Kigwa na Serikali imejenga tanki la lita 500,000 katika Kata ya Kigwa, lakini imejenga tanki la lita 1,000,000 katika Kijiji cha Itundauhuru. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha na kuleta mabomba kwa ajili ya kuweza kumalizia kutandaza mabomba katika Kata nne ili wananchi wa Kata ya Nsololo, Kata ya Igalula, Kata ya Goweko na Kata ya Kigwa yenyewe waweze kupata maji safi na salama na kuweza kutimiza ndoto ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi umeyaongelea kwenye bajeti hayo masuala yote.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kawamba, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi uliopo katika Kata ya Kigwa ni mradi ambao ni maelekezo ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi na tunatambua kwamba matanki yameshajengwa na tunafahamu kwamba Mheshimiwa Mbunge anatupa ushirikiano mzuri sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kutoa maeneo kwa ajili ya kupitisha mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe habari njema Mheshimiwa Mbunge, tayari tunatarajia kupata gari 10 za mabomba na hivi sasa tayari tuna gari tatu zimeshafika Tabora na leo hii tunaweza tukapata gari tatu, lengo tufikie gari kumi ambazo zitakuwa na mabomba 48 kwa kila gari. Baada ya kuwa tumekamilisha bomba hizo sasa wataalam wetu wataweza ku-*issue certificate* kwa ajili ya malipo ambapo tunakadiria kama takribani 800,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya, sisi tutaendelea kumuunga mkono na fedha zitapelekwa baada ya mabomba kuwa yamefika yote kama ambavyo yatakuwa yamepangwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa haya tunaendelea, swali linalofuata nimwite Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 301

Mkakati wa Huduma ya Maji Safi – Mtwara

MHE. AGNES E. HOKORORO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Mkoa wa Mtwara unapata huduma ya maji safi na salama kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025-2030 inaitaka Serikali kuimarisha upatikanaji wa maji kwa wananchi wote nchini kwa miaka mitano ijayo. Hatua mojawapo ya kuweza kufikia lengo hilo ni pamoja na Serikali kuongeza idadi ya kaya vijijini na mijini kwa asilimia isiyopungua 90 zilizofikiwa na huduma ya maji safi na salama ikiwemo kaya za Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza azma hiyo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa na midogo 29 katika Mkoa wa Mtwara ikiwemo Mradi wa Makonde sambamba na Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma kwenda Mangaka Mtambaswala kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 123.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali na mpango wa miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2026/2027 ni kuhakikisha inatoa kipaumbele kwa miradi yote inayoendelea kwa kupeleka fedha za utekelezaji sambamba na kuisimamia kwa karibu ili iweze kukamilika kwa wakati na ubora stahiki kwa lengo la kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnes Hokororo.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mkoa wa Mtwara kwa sasa ni 72% ikibebwa na maeneo yaliyo karibu na Mijini, pamoja na mradi mkubwa uliotajwa wa Makonde ambao sasa umefikia 40%. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuharakisha upatikanaji wa fedha katika Miradi iliyotajwa kama Makonde na ile midogo 29? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inajenga mabwawa yaliyotajwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 likiwemo Bwawa la Lukuledi, Masasi ili kuwawezesha wananchi wa Kanda ya Magharibi Masasi waweze kupata huduma ya maji safi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge kutoka Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kabisa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa Mkoa wa Mtwara kwa sasa ni 72% kwa vijijini, lakini kwa mjini sasa ni 85% na tunatambua kwamba tunavyo vijiji zaidi ya 785 ambapo mpaka sasa ni vijiji 156 pekee ndiyo havina huduma rasmi ya utoaji huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba huu Mradi wa Makonde ni mradi wa kimkakati ambao Mheshimiwa Rais ameelekeza na kuwekeza zaidi ya shilingi 84,000,000,000 katika kuhakikisha kwamba mradi huu umekamilika. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge katika bajeti yetu ambayo wametupitishia moja ya kipaumbele ambacho tumekiweka namba moja ni kuhakikisha tunakwenda kutekeleza na kukamilisha miradi yote inayoendelea kabla ya kuanza mradi wowote mpya. Kwa hiyo na Mradi huu wa Makonde ni sehemu ya miradi ambayo inaendelea. Kwa hiyo nimtoe hofu na sasa mradi huu uko 40% na tutahakikisha kwamba tunaongeza nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Masasi miradi ambayo ilikuwa imeshaanza kutekelezwa katika bajeti za miaka ya nyuma tunaandaa utaratibu mzuri zaidi na maalum kuhakikisha kwamba tunakwenda kutumia mitambo ambayo Mheshimiwa Rais aliinunua ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ambayo ilikuwa imekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Esther Midimu.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mpindo na Kata ya Budeko, Wilaya ya Maswa kuna shida sana ya maji. Je, ni lini Serikali itachimba visima virefu katika kata hizo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana dada yangu kwa kazi nzuri anayoifanya na kuwatetea akinamama wa Mkoa ikiwemo Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu. Serikali inatambua kwamba Mkoa wa Simiyu hasa hususan katika Wilaya ya Maswa

ni kame na kwa muktadha huo tunaelekeza zaidi nguvu katika kuchimba mabwawa ili yaweze kutumika kama njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji chini ya ardhi kwa upande wa Maswa ni changamoto, lakini wataalam wetu wanaendelea kuhakikisha kwamba wanafanya tafiti za kutosha pale ambapo tunabaini kwamba tuna uwezo wa kupata maji yanayostahili na yenye ubora unaotakiwa, basi Serikali itaendelea kufanya hivyo. Lengo ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote 1,575 ambavyo bado havijaafikiwa na huduma rasmi ya majisafi na salama kufikia mwaka 2030 viwe vimepata maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata nimwite sasa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sita, Mbunge wa Urambo na swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Japhael Lufungija.

Na. 302

Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Urambo

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA auliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Kupeleka Maji Urambo kutoka Ziwa Victoria ili kuondoa changamoto ya maji?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo na limeulizwa na Mheshimiwa Lufungija, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kupeleka Maji Urambo, Sikonge na Kaliua Mkoani Tabora kutoka Ziwa Victoria ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Miji 28 kwa gharama ya shilingi 143,000,000,000. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja

na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 253 sambamba na ujenzi wa matanki tano yenye jumla ya lita 8,000,000 likiwemo tanki la lita 2,000,000 lililojengwa katika Kijiji cha Muungano Wilayani Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo umefikia wastani wa 76.5% za utekelezaji ambapo tayari umeanza kutoa huduma ya maji katika Mji wa Sikonge na maji pia yameanza kuingia kwenye tanki la Muungano Wilayani Urambo. Kwa mujibu wa mkataba, mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2026 na kunufaisha zaidi ya wananchi 490,926 waishio kwenye Miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua sambamba na vijiji 63 vya Wilaya hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lufungija, swali la nyongeza.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na majibu yaliyosheheni kwa maana ya kujitosheleza. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nini sasa kauli ya Serikali kwa wananchi wa Urambo kuhakikisha kwamba maji hayo sasa wataanza kuyatumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, swali la msingi linaonyesha mradi mkubwa wa kimkakati Wilaya ya Urambo, lakini Jimbo la Ulyankulu mradi wa kimkakati ni Bwawa la Ichemba, ninataka Waziri aniambie lini Mradi wa Bwawa la Ichemba utaanza kujengwa? Kwa sababu sasa hivi mkandarasi keshatoa vifaa vya uchimbaji sasa *speed* ya ujenzi ni ndogo. Je, ni lini mradi huu utaongeza kasi ya utekelezaji kuhakikisha kwamba wananchi wa Ulyankulu wanapata maji ya kutosha? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kifupi kauli ya Serikali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swali dogo la nyongeza limeulizwa na Mheshimiwa Lufungija Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba wananchi wajiandae kupata maji safi na salama kwa sababu mradi huo ambapo kwenye tanki la 2,000,000 maji tayari yameshaanza kuingia. Kwa hiyo kinachofuatia tu ni kuanza kuyasambaza na kufikiwa wananchi na iko katika asilimia nzuri kati ya 76%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; suala la Bwawa la Ichemba. Ninakiri kwamba tunayo changamoto na mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Ichemba na ni kweli kabisa kwamba mradi huu ni shilingi bilioni tatu na nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia amechangia kwenye bajeti ya maji akaongelea suala la Ichemba, lakini pia alifika kwenye Ofisi ya Waziri akaongelea Ichemba na leo kauliza swali la Ichemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kweli hatutoendelea kuvumilia wakandarasi ambao ni wazembe. Kwa sababu ameshalipwa milioni 500, lakini muda wake wa mkataba ukaisha lakini bado yupo 10%, tukamwongezea tena, kama unavyosikia Mheshimiwa Mwenyekiti mkandarasi ameondoa vifaa. Ninamwelekeza *DG* wa *RUWASA* ili aweze kumwita na kufikia makubaliano kwa maandishi ili tuone kama ameshindwa kazi, basi Serikali itafute mkandarasi mwingine aweze kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata asipotokea pia Serikali tutatumia sheria zetu ili kuhakikisha kwamba tunasitisha mkataba na mkandarasi huyo ili asiwe chanzo cha kuwafanya wananchi wa Ichemba – Ulyankulu wakose huduma ya maji safi na salama, kwenye hili tutakuwa makini nalo sana hatutaki watukwamishe kufikia azma ya Mheshimiwa Rais. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kutatua kero ya maji katika Tarafa ya Wanging'ombe ndani ya Jimbo la Wanging'ombe, lakini bado kuna baadhi ya maeneo kwenye Tarafa ya Wanging'ombe, changamoto hiyo bado

inaendelea. Ninataka kujua, ni lini Serikali itamaliza kabisa changamoto hiyo ya upatikanaji wa maji safi na salama ndani ya Tarafa ya Wanging'ombe, Jimbo la Wanging'ombe? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum Njombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana dada yangu kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kuwatetea akinamama na nimtoe hofu mwarobaini wa changamoto ya maji ni Mradi wa Miji 28 unaoendelea kutekelezwa katika Mkoa wa Njombe, ukianzia Njombe wenye *package* ya shilingi 40,000,000,000, ukija hapa Makambako shilingi 42,000,000,000, ukienda pale Wanging'ombe shilingi 43,000,000,000 ambao ni neema kubwa imeletwa na kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia, mradi huu ukikamilika, vijiji vyote ambavyo amevitaja, hasa Kata hii ya Wanging'ombe, Tarafa ya Wanging'ombe watapata huduma ya maji safi na salama. Kama kutakuwa na changamoto wataalam wetu wataendelea kufanya tathmini na kujiridhisha wapi bado kuna tatizo ili tukachukue hatua stahiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, aulize swali lake.

Na. 303

Ujenzi wa Jengo la Kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Muleba

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Muleba?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji haki katika ngazi mbalimbali. Mpango huu unahusisha ujenzi wa majengo mapya pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tunakamilisha kuandaa mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama awamu ya tatu. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Muleba utazingatiwa katika mpango huo kwa mwaka wa fedha 2027/2028.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali mazuri yanayotia moyo, kwamba Muleba itapata Mahakama ya kisasa. Maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pale Muleba kuna mdau wa maendeleo kwa jina maarufu la PR, Kata ya Ijumbi, alitoa majengo yake na ardhi yake kwa ajili ya kuanzisha Mahakama ya Mwanzo kwa ajili ya kuhudumia Kata ya Ijumbi. Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa kuchukua hilo jengo na kulikarabati na kutoa idhini ya kuanzisha Mahakama ya Mwanzo Kata ya Ijumbi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kata ya Kimwani wanatumia jengo la kukodi, lakini wana kiwanja. Je, Serikali haioni kuwa ni muda muafaka sasa kuanza ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kata ya Kimwani ambao wanahangaika na kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za Mahakama ya Mwanzo katika Jimbo la Muleba Kusini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kwamba upatikanaji wa haki katika jimbo lake unaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, kwamba mdau amepatikana na amejitolea majengo na ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo; ni kweli kabisa Mahakama inajenga au inajengewa Mahakama na Serikali, wadau wa maendeleo au kwa kutumia nguvu za wananchi. Mahakama haipokei majengo kutoka kwa watu binafsi na hasa kwa kuzingatia umuhimu wa uhuru wa Mahakama; na hasa pale yule mtu binafsi anapokuwa ametoa majengo au amejenga majengo, ametoa ardhi halafu na yeye akawa ana kesi; kunakuwa na mgongano wa maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna utaratibu mzuri ambao tunaweza tukaufuata. Ninaomba mimi na Mheshimiwa Mbunge tukutane tujadili ili tuone namna ambayo labda Serikali inaweza ikapokea majengo hayo kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kisha Serikali ikakabidhi kwa Mahakama kwa ajili ya kuyatumia, kuyaboresha na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili kuhusiana na ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Kimwani; Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana katika Mahakama katika uboreshaji wa majengo ya Mahakama; kwa kiwango cha shilingi bilioni 524.9 katika kipindi cha miaka mitano. Yaani kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022. Hadi sasa Serikali tayari imekwishajenga Mahakama hizi za Mwanzo kwenye kata mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu mpango huu wa pili wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama umefika mwisho na tayari sasa hivi umehusishwa kwa kuuanzisha mpango wa tatu. Katika mpango wa tatu wa ujenzi wa miundombinu hii ya

Mahakama tutazingatia pia kwa kuzingatia vigezo na vipaumbele mbalimbali ili Mahakama hii ya Mwanzo katika Kata ya kimwani iweze kujengwa wananchi waweze kupata majengo mazuri kwa ajili ya kupata huduma ya upatikanaji wa haki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga, swali fupi.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisimama mara kadhaa kuomba ujenzi wa Mahakama kwenye Tarafa, siyo kata, Tarafa ya Ikuwo ambayo ina umbali kuelekea Mashariki na Magharibi, zaidi ya kilometa 100 na wananchi wamekuwa wakikosa haki. Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama hii ya Mwanzo ili wananchi wapate haki yao? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri, kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Mahakama kujenga Mahakama za Mwanzo katika kila kata. Katika kata zote dhamira ya Mahakama ni kuhakikisha kwamba zinakuwa na Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama imekuwa ikitekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama, mpango wa pili kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022; na imetumia zaidi ya bilioni 524.9 kwa ajili kufanya maboresho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kuwa dhamira ni kufika katika kila kata; na kwa hivyo kadri fedha zinavyokuwa zinapatikana Mahakama inaendelea kuongeza majengo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu uhitaji mkubwa uliopo katika kata hii aliyoitaja, ya Ikuwo. Mahakama itafanya juu chini ili iweze kufika katika kata hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inajenga Mahakama ya Mwanzo.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nimwite Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini aulize swali lake.

Na. 304

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kigoma Mjini

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO auliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza migogoro mingi ya ardhi inayowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali ya Kigoma Mjini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kaspar Mmuya.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba nijibu swali namba 304 la Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi ni changamoto inayowakabili wananchi wengi nchini wakiwemo wa Mkoa wa Kigoma. Migogoro hii imekuwa ikisababishwa na mwingiliano wa matumizi ya ardhi, uuzwaji wa ardhi uSIYOzingatia sheria na mamlaka husika, uvamizi wa maeneo ya umma na mashamba makubwa. Pia, elimu ndogo ya wananchi kuhusu masuala ya ardhi na matangazo ya mipaka ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Kiserikali imeendelea kutatua migogoro hii kiutawala kupitia Ofisi za Makamishna wa Ardhi za Mikoa, Kliniki za Ardhi zinazoendelea nchi nzima na vikao na mikutano ya viongozi. Mathalani, katika Mkoa wa Kigoma jumla ya kliniki za ardhi tano zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 katika Mkoa wa Kigoma jumla ya migogoro 1,092 ilipokelewa na kusikilizwa; ambapo kati yake migogoro 1,046 ilitatuliwa kiutawala. Migogoro 46 iliyobakia ipo kwenye hatua mbalimbali za utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia migogoro hiyo, Serikali kwa kushirikiana na mamlaka ya Mkoa wa Kigoma imeendelea kuweka mikakati inayolenga kuhakikisha kuwa migogoro ya ardhi iliyopo katika Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine nchini inapungua na hatimaye kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati hiyo ni pamoja kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na kuisimamia, kuendesha programu ya kliniki za ardhi, kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya ardhi ili kuwaepusha wananchi kujiingiza katika migogoro ya ardhi inayoweza kuzuilika. Pia, kuandaa rejista ya migogoro ili kuepusha ushughulikiaji wa mgogoro mmoja zaidi ya mara moja na kusimamia nidhamu za watumishi wa sekta ya ardhi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Clayton Chipando.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, ninakiri kwamba tumeona wakipambana kutatua migogoro. Ninampongeza pia hata Mkuu wa Wilaya ya Kigoma Mjini, Mzee wangu Mheshimiwa Dkt. Chuachua, anapambana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kwamba, katika dunia hii kuna vitu vitatu peke yake ambavyo mtu anavyoweza kupambana kufa na kupona; fedha, ardhi na mapenzi. Hivi vitu ni vitu ambavyo binadamu anaweza kupambana kwa nguvu zake zote kwa ajili ya kutetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ardhi migogoro imekuwa ikijirudia mara kwa mara. Ni ule ule mgogoro ambao wameutatua mwaka mwaka jana mwaka huu unajirudia; na mingine inatengenezwa na wataalam wetu. Maeneo ya umma yanakuwa yanabadilishwa kiholela. Sehemu ilikuwa sehemu ya ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chipando maelezo yako yametosha, uliza swali.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaweka mizizi kidogo ya swali.

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. CLAYTON R. CHIPANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali inipe majibu. Je, ni lini itaweka sheria kali ya kuzuia kubadilisha matumizi ya maeneo ya umma kama *open space* na sehemu ambazo zimetengwa kwa ajili ya shule na zahanati na kliniki?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Chipando kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi. Mara nyingi alikuwa anawasiliana na sisi katika kujua hatua mbalimbali za migogoro hii. Ninawapongeza sana wananchi wa Kigoma Mjini kwa kumchagua Mbunge mahiri na mfuatiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na Bunge hili. Tukumbuke tuna Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, ambayo Serikali imeitunga. Pia, tuna Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 ya Toleo la mwaka 2023; vilevile tuna Sheria ya Mipango Miji, Sura 355. Licha ya hivyo, pia tuna kanuni ya sheria hii, kanuni ya mwaka 2018 na iliyofanyiwa maboresho mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya yamefanyika kwa sababu wanataka kusimamia sekta ya ardhi hususan kwenye kupanga, lakini kumilikisha na hata kusimamia matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa sheria hizi na sera hizi na kanuni ndiyo msingi mkubwa. Hapa kinachotakiwa ni kutoa tu angalizo kwa watu wote wanaopenda kutumia maeneo ya wazi bila kufuata utaratibu; maelekezo ya Waziri wa Ardhi yako wazi.

Tutakwenda kubomoa kuanzia hatua ya kupanga kuleta matofali yako, tukikukuta kwenye msingi, tukikukuta umejenga bila kujali gharama uliyotumia tutaenda kubomoa na kukuelekeza ufuate sheria zinazotakiwa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, muda wetu unakwenda haraka. Wizara ya Viwanda na Biashara, nimwite sasa Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, Mbunge wa Hanang aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Khambay.

Na. 305

Kuanzisha Kiwanda cha Kuchakata Saruji – Hanang'

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY K.n.y. MHE. ASIA A. HALAMGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kiwanda cha Kuchakata Saruji Hanang' kwa kuwa ipo malighafi ya zaidi ya miaka 100?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ninaomba nijibu swali namba 305 kutoka kwa Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utafiti na tathmini kwa kadri ya maelekezo ya Dira ya Maendeleo ya 2020 – 2050, Serikali ina majibu ya tafiti ambayo inaonyesha kwamba uwepo wa malighafi za *pozzolana* na *klinker* ambazo zinatumia katika kuzalisha saruji katika Wilaya ya Hanang. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na kiwanda cha kuzalisha saruji wilayani humo, Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 360 katika Kata ya Mogitu

katika Kijiji cha Mogitu, ambapo eneo lenye malighafi lina ukubwa wa ekari 300 na eneo la ujenzi lina ukubwa wa ekari 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kushirikisha wadau, sekta binafsi na taasisi za Serikali kuona kwamba wanawekeza katika eneo hilo la kiwanda. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khambay, kwa niaba.

MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Asia Halamga, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itakwenda katika maeneo hayo ya Hanang na kuweza kujiridhisha na kuanzisha kiwanda hicho kwa ajili ya manufaa ya watu wa Hanang?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, ni lini Serikali itaanzisha kongani ya viwanda katika Jimbo la Babati Mjini?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inavyoelekeza na Dira ya Maendeleo ya 2050 inavyoelekeza, kwamba tuwe na viwanda vya kimkakati kila mkoa. Kwa Mkoa wa Manyara tathmini tumeifanya, tunatambua kwamba katika Wilaya ya Hanang hususan Jimbo la Hanang kuna malighafi nyingi ambayo inaweza kuzalisha saruji, lakini pia, kuna malighafi nyingi ambazo zinaweza zikazalisha chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi Serikali iko katika kipindi cha kutafuta wawekezaji wa uhakika ambao wanaweza kwenda kuwekeza katika maeneo hayo ya uhakika. Pia, kwa upande wa kuongeza thamani. Tunatambua kuwa Hanang ni mzalishaji mkubwa pia ina hali ya hewa nzuri kwa ajili ya uzalishaji wa ngano; kwa hiyo, tunaendelea kutafuta wawekezaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na lini Serikali inaenda kuanzisha kongani katika Wilaya ya Babati; mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tunaenda kuongeza thamani ya bidhaa zetu. Kuanzisha kongani mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya nchi, pamoja na kuanzisha viwanda katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuongeza thamani ya mazao yetu na kuongeza uzalishaji pamoja na ku-*export* bidhaa zetu kwa wingi kwa kadri ya Dira ya Maendeleo ya 2050 inavyotuelekeza. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru.

Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho Wizara ya Ujenzi; nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, aulize swali lake.

Na. 306

Ukarabati wa Barabara ya Dar es Salaam – Lindi

MHE. DKT. YAHAYA E. NAWANDA aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa Barabara ya Dar es Salaam hadi Lindi kutokana na hali yake kuwa mbaya?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ukarabati wa Barabara ya Dar es Salaam – Lindi kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa kuanzia Serikali imeanza na upanuzi wa barabara hii kwa kipande cha Mbagala Rangi Tatu hadi

Kongowe yenye urefu wa kilometa 3.8; ambapo kazi ya upanuzi wa barabara hii imefikia 12%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja na makalavati yaliyoathiriwa na mvua za *El Nino* na Kimbunga Hidaya zilizonyesha katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2024, kwa lengo la kuunganisha mawasiliano ya kudumu kwenye barabara hii katika kipindi chote cha mwaka. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara kwa sehemu zilizobaki. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Nawanda, maswali ya nyongeza.

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja sasa ya kuijenga upya barabara hii kwa sababu hali yake ni mbaya sana na kwa kuzingatia kwamba kuna miradi mikubwa ya kimkakati, Mradi wa *LNG* pale Lindi, Mradi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa, Bandari ya Kisiwa Mgao ambayo inaendelea, lakini pia makaa ya mawe yanapita sana katika barabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; umejitokeza sasa hivi msongamano mkubwa sana kutoka Kongowe hadi Mkuranga. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kuongeza barabara nne ili kuondoa msongamano mkubwa sana ambao wananchi wa kusini wanapata adha kubwa kwa kutumia barabara hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

Ninamwona Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Ulega.

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Kasekenya kwa majibu mazuri ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; ninaomba nitumie fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Nawanda kwa kuuliza swali hili muhimu sana kwa watumiaji wote wa Barabara ya Kilwa mpaka Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango wa Serikali wa kuweza kuifanya barabara hii ya kiuchumi ambayo inabeba makaa ya mawe, inabeba *cement*, inabeba korosho, inabeba ufuta, inabeba mazao kadhaa ya chakula ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda kusoma bajeti yake hapa karibuni, Serikali imejipanga kuja na mpango wa kuwa na hatifungani *(bond)* ambayo tupo katika mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hii itakapokuwa tayari moja ya kazi yake kubwa ni kwenda kufanya marekebisho makubwa ya barabara zetu zote kuu ambazo tunasema ni *economic corridors* zote na hasa ukizingatia kwa sasa bandari zetu zinafanya vizuri sana ikiwa ni pamoja na barabara ya Kilwa. Hii tutakwenda kuifanyia marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo yameharibika sana, mfano, kutoka Muhoro kwenda mpaka Somanga na kadhalika yameharibika sana. Tunakwenda kuyasafisha na kuyaweka vizuri. Kwa hivyo Mheshimiwa Mbunge Nawanda na Wanakusini wote wawe na matumaini ya kwamba Serikali jambo hili tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni msongamano kutoka Mkuranga mpaka Kongowe. Nimshukuru tena kwa mara nyingine mtu bingwa kabisa huyu Mheshimiwa Dkt. Nawanda kwa kuwaulizia swali watu wa Mkuranga na watumiaji wengine wa barabara hii; ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kongowe Serikali inajenga *flyover*. Hivi sasa tayari kazi hiyo inaendelea, ambapo watu wanaotoka upande wa Kigamboni hawatakutana na watu wanaotoka njia ya *Kilwa Road*. Hiyo itakuwa ni sehemu ya

kwanza ya kuondosha ule msongamano, lakini matarajio yetu pia kutoka Kongowe mpaka Mkuranga tunakwenda kujenga barabara nne; mbili zinaingia na mbili zinatoka na katikati tunaweka barabara ya *BRT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kujibu hayo maswali, lakini tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa na utayari wa kujibu maswali.

Waheshimiwa, muda wetu wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Kuna matangazo machache, *actually* ni mengi.

Tangazo la kwanza kabisa, Waheshimiwa Wabunge tunakumbushwa wote tulioingia humu ndani, tunapoingia tu-*log in* kwenye *system* yetu ili tupate takwimu sahihi za Wabunge waliopo ndani ya Bunge. Wote tuwe tumesha-*log in* na wengi wame-*log in,* lakini kuna wengine hawaja-*log in* bado.

Tangazo la pili linahusiana na wageni waliopo ndani ya ukumbi wa Bunge na tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Afya na ni wafuatao: Dkt. Seif Shekalaghe, Katibu Mkuu Wizara ya Afya; Ndugu Emmanuel Tayari yeye ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya; na Dkt. Grace Magembe yeye ni Mganga Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Wengine ni Profesa Abel Makubi yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini Mkapa; Mheshimiwa Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya, yeye ni Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa *MOI*; Dkt. Delila Kimambo yeye ni Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; na Dkt. Peter Kisenge, yeye ni Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Tunao pia, Dkt. Irene Isaka yeye ni Mkurugenzi Mkuu Mfuko wa Taifa Bima ya Afya; Dkt. Adamu Fimbo yeye ni Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TMDA)*; Ndugu Phidelis Mafumiko, yeye ni Mkemia Mkuu wa Serikali; Dkt. Diwani Msemo,

yeye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani; Ndugu Tukai Mavere, yeye ni Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa *(MSD)*; Profesa Said Aboud, yeye ni Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu; na Ndugu Mark Schreiner yeye ni Mwenyekiti wa Wadau wa Maendeleo Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Wapo pia, Dkt. Alex Gasasira, yeye ni Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)*; Ndugu Edwin Swai, yeye ni Mwakilishi wa *WHO* Mkoa wa Dodoma; Ndugu, John George yeye ni Mwenyekiti Mfuko wa Afya wa Pamoja; Ndugu Damasco Peter, yeye ni Mkurugenzi wa Menejimenti ya Maendeleo ya Afya *(MDH)*; Ndugu Ophilia Kalumuna, yeye ni Mkuu wa Ofisi ya *UNICEF* Mkoa wa Dodoma; Ndugu Grace Nguma, yeye ni Meneja Mahusiano Serikali kutoka Benki ya Azania na Ndugu Diana Baliagati, yeye ni msimamizi wa biashara za Serikali Benki ya Azania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine wa Mheshimiwa Mchengerwa, ni marafiki zake kutoka jijini Dar es Salaam kama ifuatavyo: -

Tunaye Dkt. Seif Rashid, (sasa huyu sijui anakuwaje rafiki). Yeye ni Naibu Waziri wa Afya Mstaafu na Mbunge Mstaafu. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Ndugu, Jonathan Mabihya, , Ndugu Ally Nambungo, Ndugu Raymond Mbezi, Ndugu Rose Sanga, Ndugu David Luambano, Ndugu Mbaraka Said, Ndugu Richard Kasesela na *Major General* Hamisi Semfuko. Hawa wote ni marafiki wa karibu wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Wapo pia, Ndugu Rajabu Mbonde, yeye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rufiji; Ndugu Prudence Mugisha, yeye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Rufiji; na Ndugu Shafii Dauda, yeye ni Mkurugenzi wa Mahusiano ya Kimkakati *Clouds*. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Naibu Waziri wa Afya, huyu ni ndugu Sadock Mugendi, yeye ni...

(polepole, Waheshimiwa polepole). Yeye ni mume wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa.

Wageni wote niliowataja tunawakaribisha sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge.

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Mgeni wa Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ambaye ni ndugu Hamisi Msagama, yeye ni Mfamasia kutoa Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Lulu Mwacha, ambaye ni Ndugu Glory Silayo, dada yake kutoka Mkoa wa Arusha.

Mgeni wa Mheshimiwa Baraka Ulimboka Mwamengo ambaye ni Ndugu Israel Mwakibinga, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Naibu wetu Waziri wa TAMISEMI; hawa ni ndugu zake na jamaa zake kutoka Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, huyu ni Ndugu Muzne Mohamed, Mwandishi wa Habari kutoka Nchini Ujerumani. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, hawa ni wazee na viongozi mbalimbali kutoka Bariadi Vijijini wakiongozwa na Mzee Bulogo Susani na Mzee Bahati Magamla. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, hawa ni wanafunzi na wapiga kura kutoka Ludewa Mkoani Njombe, wapo pale. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, hawa ni kutoka Taasisi ya Thamini Uhai, wapo pale. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, hawa ni wanafunzi wanataaluma wa Sekta ya Afya kutoka Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni waliotutembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Mgeni wa kwanza ni Ndugu Geraldine Duwe, huyu ni Mjasiriamali kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Ndugu Caren Joseph na Sada Sakulo kutoka Chamwino Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Wanafunzi 36 wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kutoka Jijini Dodoma, wapo pale. Karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 146 na walimu 12 wa Shule ya Msingi *St. Marys* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Mgeni mwingine, Ndugu Milki Mussa na Ndugu Peter Mushi kutoka Jijini Dar es Salaam, naye alikuja kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Hayo yalikuwa ya wageni. Tuna wageni wengine saba wa Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, hawa ni timu ya kampeni na wapiga kura kutoka Wilayani Kilwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo mengine: la kwanza, ni la ukumbusho. Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kuwa leo siku ya Jumatatu, tarehe 11 Mei, 2026 kutakuwa na semina itakayotolewa na Wizara ya Uchukuzi kuhusu miradi itakayotekelezwa na Taasisi na Mamlaka za Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)*, Taasisi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*. Semina hii itafanyika saa saba mchana, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa tena kuwa Chama cha Mawakili wa

Serikali Tanzania *(TPBA)* kimeandaa mbio za *marathon* zinazojulikana kama *Wakili Marathon 2026*. Lengo la mbio hizo ni kukusanya rasilimali fedha ili kusogeza huduma za msaada wa kisheria karibu na wananchi kupitia mifumo ya kidijitali, hususan waliopo katika mazingira ya vijijini, pembezoni mwa miji, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na wagonjwa ambao hukosa fursa za kufikiwa na huduma hizo kwa urahisi.

Kaulimbiu ya mbio hizo ni "Kusogeza Huduma za Msaada wa Kisheria Karibu zaidi na Mtanzania" na zinatarajiwa kufanyika siku ya Jumapili tarehe 31 Mei, 2026 Jijini Dodoma. Usajili wa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge unaendelea kufanyika katika viwanja vya Bunge kwenye banda la usajili *(Gazebo)* lililopo nyuma ya ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote na Watumishi wa Bunge mnaombwa kushiriki mbio hizo muhimu ili kusogeza huduma za msaada wa kisheria karibu na wananchi.

Tangazo la mwisho kwa muda huu kutoka kwa Katibu wa Bunge: Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Wizara ya Afya imeandaa programu maalum ya kutoa huduma za afya katika viunga vya Bunge kwa Wabunge na watumishi.

Huduma hiyo imeanza kutolewa tangu tarehe 10 na inaendelea hadi kesho tarehe 12 Mei, 2026. Huduma hizo zinatolewa na wataalam wa afya kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani *Ocean Road*, Hospitali ya Rufaa Kanda ya Benjamini Mkapa, Hospitali ya Rufaa Kanda *KCMC*, Hospitali Maalum ya Taifa ya Afya ya Akili *(Mirembe)*, Hospitali Maalum ya Tiba ya Magonjwa Ambukizi (Kibong'oto), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando.

Aidha, huduma zinazotolewa ni uchunguzi na ushauri wa kitaalam kuhusu magonjwa ya moyo, mifupa, mgongo, afya ya wanawake na uzazi, macho, ngozi, magonjwa ya ndani, figo, afya ya akili, saratani, afya ya kinywa na meno pamoja na tiba asili.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutembelea mabanda hayo ili kupata huduma na ushauri wa kitaalam kwa faida yenu. Hayo ndiyo matangazo kwa sasa.

Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

MWENYEKITI: Hoja za Serikali, Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa ili aweze kutoa hotuba yake ya bajeti. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ninaomba kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2023, Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na muhtasari huu, ninaomba hotuba yangu yote yenye kurasa 287 iingie katika Kumbukumbu za Bunge lako Tukufu kama ilivyo katika kitabu kilichowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili. Kwa namna ya pekee, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inagusa uhai na ustawi wa kila Mtanzania bila kujali jinsia, umri, dini, kabila au hali ya

kiuchumi. Ninatambua dhamana hii kubwa na ninaahidi kuitekeleza kwa uadilifu, uzalendo na weledi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha diplomasia ya afya na ushirikiano wa Tanzania na nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na wadau wa maendeleo; hasa kipindi cha changamoto za ugharimiaji wa huduma za afya kutokana na mabadiliko ya sera za nje. Uongozi wake umehakikisha huduma za afya zitaendelea na zinaendelea kutolewa bila kuathiri misingi ya urafiki, heshima na maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, "Afya ya wananchi ni msingi wa maendeleo ya watu" na kwa mafunzo ya Nelson Mandela, "Heshima ya binadamu ni kiini cha Taifa huru." Hivyo huduma ya afya tunayoijenga ni huduma ya utu, haki na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili katika uchaguzi wa Oktoba 2025. Ushindi huo ni ishara ya imani ya wananchi kwa uongozi wake na Serikali yake kwa ujumla. Nitaendelea kuibeba ajenda yake ya kuimarisha huduma ya afya nchini kwa kutambua kuwa afya ni mali na afya ni mtaji na kwamba Taifa lenye watu wenye afya ndiyo Taifa lenye uwezo wa kuzalisha, kujitegemea na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Viongozi Wakuu wa Nchi kwa dhamana walizopewa: Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuchaguliwa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Ninaamini miongozo, maelekezo na busara zao zitaendelea kusaidia utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ikiwemo Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe na kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na

uongozi thabiti unaozingatia kanuni. Ninampongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa dhamana ya kuwawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Makamu Mwenyekiti kwa ushauri wao katika kuboresha utendaji wa Wizara. Wizara ya Afya itaendelea kupokea na kuzingatia ushauri wa Bunge katika kuboresha huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza vilevile Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Afya na Ndugu Emmanuel David Tayari, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia dawa na vifaa tiba. Ninawashukuru Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe, Katibu Mkuu; Dkt. Ismail Hassan Rumatila, Naibu Katibu Mkuu; Dkt. Grace Elias Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali; Menejimenti ya Wizara na watumishi wote wa sekta ya afya kwa uzalendo wao, kwa weledi wao na kujitoa kwao katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa shukrani kwa Wizara na taasisi za Serikali tunazoshirikiana nazo ikiwemo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI; Wizara ya Fedha; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Maji. Ushirikiano wao umechangia upatikanaji wa rasilimali watu, fedha, uratibu wa sekta mtambuka, usimamizi wa huduma za afya ya msingi na masuala ya kisheria, masuala ya afya na mazingira na masuala ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwemo Bohari ya Dawa (*MSD*), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*), Mamlaka ya

Dawa na Vifaatiba (*TMDA*), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Chakula na Lishe, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Maalum, Hospitali za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa, Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wafawidhi kwenye Halmashauri, vituo vyote vya afya, zahanati na maeneo mbalimbali, vyuo vya mafunzo, bodi na maabara, mabaraza ya kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia nchi rafiki, mashirika ya kimataifa, sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma na vyuo vya elimu kwa mchango wao katika kuimarisha huduma za afya hususan afya ya msingi, miradi ya maendeleo na afua mbalimbali za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Rufiji kwa imani yao na ushirikiano wao wanaonipatia. Ninawaahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii, kufanya kazi kwa uadilifu na uzalendo ili kutekeleza ahadi na vipaumbele tulivyokubaliana kwa maslahi ya Rufiji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nimshukuru Dkt. Seif Suleiman Rashid, Mbunge mstaafu wa Rufiji na Waziri wa Afya mstaafu na ninawashukuru Mawaziri wote wa afya wameongozana nami akiwemo Dkt. Hamis Kigwangala na wengine waliowahi kutangulia kupita sekta hii ya afya. Ninaishukuru pia familia kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano, dua na maombi yao wakati ninapotekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na rafiki na wananchi wote kwa kuondokewa na viongozi wetu wapendwa wakiwemo Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mheshimiwa Halima Idd Nassoro, Mhadhama *Polycarp* Kadinali Pengo, Mhashama Bernardin Francis Mfumbusa na viongozi wengine wa dini na madhehebu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pia pole kwa watumishi wa sekta ya afya waliopoteza wenza wao na Watanzania wote waliopoteza ndugu zao kutokana na magonjwa, kutokana na ajali na kutokana na majanga mbalimbali yanayoikumba nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitoe pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa na ajali ya boti tarehe 13 Machi, 2026, iliyosababisha sekta ya afya kupoteza watumishi saba wa kada za afya waliokuwa kazini wakitekeleza majukumu yao. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bajeti na utekelezaji wa majukumu ya sekta ya afya kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wizara imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya 2050, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya CCM ya Mwaka 2025, *HHSP* na mpango mkakati wa muda wa kati, *SDGs* 2030 pamoja na makubaliano ya kanda na kimataifa yenye lengo la kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara na taasisi zake zilikadiria kukusanya shilingi bilioni 819.98. Hadi kufikia Machi 2026, zilikusanya shilingi bilioni 593.85 sawa na 72.42% ya lengo. Kwa mwaka huu, Wizara iliidhinishiwa shilingi trilioni 1.76 na hadi Machi 2026, imepokea shilingi trilioni 1.11, sawa na 63%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida yaliyopokelewa ni 76% na miradi ya maendeleo ni 56%. Fedha za nje kutoka *Global Fund, GAVI*, Benki ya Dunia, *HBF, UNICEF, UNFPA* na wadau wengine zimeendelea kusaidia kudhibiti na mapambano dhidi ya UKIMWI, *TB*, *Malaria*, chanjo, lishe, damu salama na afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafanikio ya sekta ya afya katika Awamu ya Sita. Katika kipindi cha Awamu ya Sita upatikanaji wa huduma za afya umeongezeka kwa kasi. Vituo

vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka 10,153 Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 13,683 Machi 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake amejenga vituo vipya vya afya 3,530. Zahanati zimeongezeka kutoka 7,189 hadi 8,706, vituo vya afya 956 hadi 1,359, hospitali kutoka 404 hadi 475 na vituo vingine 1,604 hadi 3,143.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo mapya yameongezeka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Kanda ya *KCMC*, Mbeya, Benjamin Mkapa, Bugando, Hospitali Maalum ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali Maalum ya Kifua Kikuu na Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto, Hospitali za Kanda za Mtwara na Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imejenga hospitali 10 mpya za rufaa za mikoa, kukarabati hospitali kongwe 50, kukamilisha maboma 980 ya zahanati, kujenga vituo vya afya 390, kuongeza mitambo ya oksijeni kutoka 25 hadi 61 na kujenga nyumba za watumishi zenye kuhudumia familia 540.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za dharura zimeimarishwa kwa kuongeza majengo ya dharura kutoka saba hadi 125 kufikia Machi, 2026 na kuzifikisha kwa mara ya kwanza hadi ngazi ya msingi ambapo zaidi ya 80% ya Watanzania hupata huduma. Vitanda vya wagonjwa vimeongezeka kutoka 86,131 hadi 156,932 sawa na ongezeko la 82%. Vitanda vya *ICU*, vituo vya umma kutoka 258 hadi 1,647. Uwekezaji huu una maana ya kupokea wagonjwa kwa wakati, kupunguza msongamano na kuimarisha huduma kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya uzazi, mama na mtoto imeimarishwa kwa kuongeza wodi za watoto wachanga kutoka 80 hadi 438, vituo vya upasuaji wa dharura kutoka 445 hadi 630 na vituo vya uchunguzi wa awali vya saratani ya mlango wa kizazi kutoka 732 hadi 1,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya uzazi, mama na mtoto umefikia 85%. Mafanikio haya yamechangia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai laki moja mwaka 2016 hadi vifo 104 mwaka

2022. Hii imeifanya Tanzania kutambulika barani Afrika kupitia uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo hivi karibuni Umoja wa Afrika ulimtunuku kuwa *Champion* wa kupambana na vifo vya mama na watoto. Serikali imedhamiria kupunguza zaidi vifo hivyo kwa 50% ifikapo mwaka 2030 na kuvuka lengo la dunia la chini ya vifo 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchunguzi, matibabu na huduma za kibingwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 241.6. *MRI* zimeongezeka kutoka saba zilizokuwepo hapo awali hadi 13, *CT-Scan* 12 hadi 45, *Digital X-ray* 147 hadi 559, *ultrasound* 476 hadi 970, *Cath lab moja* hadi nne, mini angio *suit tano*, *fluoroscopy* 14 na *PET-CT scan moja*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zimeongezeka zikiwemo upandikizaji wa figo 170, uloto 57, vifaa vya usikivu 102, nyonga na magoti 3,037, upasuaji wa mgongo 1,688, upasuaji wa ubongo kwa kufungua kichwa 1,208, kuzibua mishipa ya moyo 2,074, tiba ya mionzi ya ndani 10,056, *immunotherapy* 4,024 na uchunguzi wa saratani *kwa PET-CT* kwa wagonjwa 731. Huduma hizi zimevutia wagonjwa 26,770 kutoka nchi jirani hivyo kuimarisha tiba ya utalii na diplomasia ya afya duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanjo zimeendelea kuwa imara. Watoto waliopata Penta-3 (*Pentavalent* dozi ya tatu) wameongezeka kutoka milioni 2,093,412 hadi milioni 3,186,979 sawa na ongezeko la 52.2%. Kiwango cha chanjo kimepanda kutoka 93% hadi 96% juu ya lengo la kimataifa la 90%. Serikali imeratibu ununuzi wa dozi milioni 161,499,930 za chanjo zenye thamani ya shilingi bilioni 439.9. Hadi Machi, 2026 kulikuwa na dozi milioni 20,268,820 ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya umeimarika. Serikali imetoa shilingi trilioni 1.4 kupitia *MSD*. Kati yake, shilingi bilioni 150 zililipia madeni na bilioni 141.9 zilitumika kugharamia dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI, malaria na kifua kikuu. Trilioni 1.1 kwa bidhaa za afya za vituo. Viwanda vipya 11 vya dawa na vifaatiba vimeanzishwa ikiwemo *KPI* Arusha kinafufuliwa ili kuzalisha dawa za *VVU* na lita milioni 1.45

za viadudu zenye thamani ya shilingi bilioni 17.5 zimesambazwa katika halmashauri 184. Upatikanaji wa bidhaa 382 umeongezeka kutoka 58% Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 88% Machi 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu zimeimarishwa kwa kuajiri wataalam 53,633 kuanzia mwaka 2021 hadi mwezi Machi 2026. Hii imefanya watumishi wa afya kufikia 182,430. Watumishi 9,039 wameajiriwa kwa mkataba wa muda mfupi kupitia mapato ya ndani. Kupitia *Samia Health Super Specialization Scholarship Program*, wataalam 2,982 wamepata mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi ikilinganishwa na 961 katika kipindi cha 2016/2017 hadi 2020/2021. Bima ya Afya kwa Wote nayo imeanza baada ya sheria kupitishwa na Bunge hili mwezi Novemba, 2023. Hadi mwezi Machi 2026, Serikali imetoa shilingi bilioni 48.8 kaya 172,297 zimefikiwa na wananchi 463,228 wamesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya si takwimu tu za majengo, vitanda, vifaa na huduma, mafanikio haya ni simulizi ya maisha yaliyookolewa ni matumaini yaliyorejeshwa na utu wa Mtanzania uliolindwa. Kama ambavyo Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamini maendeleo ya kweli ni maendeleo ya watu. Kama Nelson Mandela alivyotufundisha, kwa heshima ya binadamu ndiyo msingi wa Taifa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila zahanati iliyojengwa, kila hospitali iliyoboreshwa, kila mama aliyepata huduma salama na kila mgonjwa aliyepata huduma karibu na nyumbani ni ushahidi kuwa Tanzania inaendelea kujenga Taifa lenye afya, Tanzania inaendelea kujenga Taifa lenye usawa na inaendelea kujenga Taifa lenye utu na matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza mzigo wa wagonjwa umeongezeka kutoka shilingi 6,502,913 mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 6,874,308 mwezi Machi, 2026. Gharama kutoka shilingi trilioni 1.3 mwaka 2023 hadi shilingi trilioni 1.8 mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeanzisha kliniki 130 za wagonjwa wa kisukari na shinikizo la damu na kufanya jumla kufikia 168. Huduma za *dialysis* zimefikia vituo 74 na kuhudumia

wagonjwa 3,342. Huduma za saratani zimepanuliwa kutoka Mwongozo wa Bodi ya Saratani, uchunguzi katika hospitali za rufaa za mikoa, huduma zimepelekwa Mbeya, *KCMC*, Bugando, Mtwara, pamoja na uzalishaji wa dawa za uchunguzi wa matibabu ya saratani kupitia Saigitroni katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya ya akili zimefikia wateja 274,932, vituo 16 vya waghaibu vimehudumiwa wateja 17,807 na upatikanaji wa dawa za afya ya akili umefikia wastani wa 75%. Huduma za *sickle cell* zimepanuliwa, watoto 17,245 wamepimwa, 369 wamegundulika kuwa na ugonjwa na 250,000 kuwa na vinasaba, wagonjwa 42,564 wamehudumiwa na elimu imewafikia zaidi ya wananchi 29,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kinywa na meno zimeongezeka, viti 26 kufikia 900 na mashine za mionzi wakati huduma za macho katika mikoa 15, zimewafikia watu 51,000, wakiwemo 17,697 waliofanyiwa upasuaji, 17,715, waliopata tiba, tiba dawa 10,239 waliopata miwani na 6,289 na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magonjwa ya kuambukiza, watu 1,624,907 kati ya takriban 1,700,000 wanaoishi na *VVU* wanajua hali zao. Watu 1,609,078 wameanza dawa za *ARV* na 98.1% waliopimwa wamefubaza makali ya virusi. Wajawazito 2,080,819 walipimwa *VVU* kwa mara ya kwanza na 11,445 walibainika kuwa na maambukizi ya *VVU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto 23,023 kwenye miezi 18 walipimwa na 1,197 kuthibitika. Wajawazito 1,995,822 walipimwa na kaswende na 8598 kati ya 8,684 walibainika kuwa na kaswende na walianzishiwa matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, homa ya ini *B, TB* na ukoma vinaendelea kudhibitiwa ambapo watumishi wa afya 13,646 wamekamilisha chanjo ya homa ya ini B, visa 41,473 vya *TB* vimeibuliwa na visa 755 vya ukoma vimebainika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malaria inaendelea kudhibitiwa kupitia vyandarua 4,567,179, shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya viuadudu na pampu 16,000 pamoja na ununuzi wa *ALU, RDT, Artesunate SP* na *Primaquine* kwa lengo la *Zero Malaria* 2030. Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi 3,331,925 wamepata kinga tiba ya usubi, watoto 10,414,632 ya minyoo, watoto 6,176,203 ya kichocho na wagonjwa 1,775 wa mabusha pamoja na 3,125 wa trakoma walifanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kinga zimehusisha *Penta three* kwa watoto 2,361,701, *HPV* kwa wasichana 866,299, *Vitamin A* kwa watoto 9,115,501 na kampeni ya Mtu ni Afya kaya zenye vyoo bora 9,165,833, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,832 na kampeni ya zijue namba zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIMRI* imetekeleza miradi 119 kati ya 150 na *ALBSL* imeimarisha ufuatiliaji wa mlipuko kipindupindu kimedhibitiwa tangu tarehe 25 Februari, 2026. Wewe ni shahidi pamoja na mafuriko hayo makubwa hatujapata kesi ngumu za kipindupindu na visa 153 vya surua pamoja na 253 vya *Mpox* viliripotiwa bila kifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Public Health Emergency Operating Center* (Vituo vya Kuratibu Dharura za Afya) vimekamilika kuratibu dharura za afya. Wasafiri 10,829,732 wamechunguzwa mipakani, 233 wakipelekwa kwa uchunguzi zaidi; 17,734 wamepata chanjo ya homa ya manjano na ofisi mpya tatu za afya mipakani zimeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huduma za tiba, Mwaka wa Fedha 2025/2026, vituo vimeongezeka kutoka 12,846 hadi 13,683 sawa na 85% ya wananchi wanapata huduma ndani ya kilometa tano. Vitanda vimefika 156,932 na uwiano wa 2.3 kwa watu 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani wagonjwa 36,996,862 wamehudumiwa kote nchini kwa mwaka mmoja. 35,260,883 ni wagonjwa wa nje na 1,735,979 ni wagonjwa wa kulazwa.

Magonjwa yaliyoongoza ni mfumo wa hewa, *UTI*, *malaria*, kuharisha, ngozi, shinikizo la damu na *NCD* na magonjwa mengine. Tiba asili imeimarishwa, dawa 48 zimesajiliwa, sita zimepelekwa kwenye utafiti wa salama, mbili za kisukari zinafanyiwa utafiti wa ufanisi na wagonjwa 648 wamehudumiwa katika hospitali jumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ubingwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 zimewafikia wagonjwa 4,202,137, huduma kama *IVF*, upandikizaji wa figo, vifaa vya usikivu, puto tumboni, meno, goti au nyonga na uroto zimeokoa takribani shilingi bilioni 3.67 ambazo zingetumika nje. Madaktari Bingwa wa Mheshimiwa Dkt. Samia wamehudumia wagonjwa 55,300 katika halmashauri 184 na kujenga uwezo wa wataalam 5,585. Huduma Mkoba zimewafikia wagonjwa 77,118; tiba utalii wagonjwa 3,018; na huduma nje ya nchi wagonjwa 4,363.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuguzi na ukunga unaotoa takribani 80% ya huduma umeimarishwa kupitia mafunzo ya ukunga 1,850. Jumla ya waliopatiwa mafunzo ni 9,093 na vituo 5,884 vinatumia chati uchungu na huduma ya mama mwambata imefikia vituo 1,244. Uhakiki ubora umeimarishwa kupitia maandalizi ya taasisi ya ithibati, maabara zenye ithibati kuongezeka kutoka 90 hadi 102. Maabara tano za *BSL 3* kujengewa uwezo na *KCRI* kutambuliwa na Umoja wa Afrika wa vimelea hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, damu salama imeimarika kwa chupa 273,105 kukusanywa sawa na 82% ya lengo. Kanda sita zina ithibati, Mpango wa Taifa wa Damu Salama umepata *ISO* 17043 na *SANAS* na Maabara za Mkemia Mkuu zinaendelea kushikilia *ISO* 17025.2017. Serikali pia imetoa shilingi bilioni 242.7 kwa ununuzi wa dawa kupitia *MSD*, upatikanaji wa bidhaa 382 umefikia 88.8% na hatua za *PIAT* Mloganzila *Pharmaceutical and Medical Device Special Economic Zone*, *Bio-Equivalent Lab* na ushirikiano na *Sartorius* zinaweka misingi ya kujitosheleza kwa bidhaa za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya ya uzazi, mama, mtoto na vijana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 zimeimarika.

Wanawake 4,626,300 wamepata huduma za uzazi wa mpango; vituo vya upasuaji wa dharura vimefikia 630; wajawazito 2,218,640 walihudhuria *clinic* sawa na 98% ya waliojifungua vituoni; na mashine tiba joto 392 zimesambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika rasilimali watu Serikali imeajiri watumishi 5,000 na kufikisha jumla ya watumishi wa sekta ya afya 182,430. Wataalam 9,039 wameajiriwa kwa mikataba na *Samia Health Super Specialization Program* imefikisha jumla ya wanaofadhiliwa na Serikali kupitia programu hii ya Dkt. Samia 1,483.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika TEHAMA Wizara imetengeneza *health data universal (IPI)* ili mifumo ya afya ibadilishane taarifa na kutoa rufaa kidijitali. *EHMS* imetumika katika hospitali zote 28 za rufaa na mikoa *GOTHOMIS* katika 96% vya ngazi ya msingi na *computer* 2,758 vimesambazwa katika mikoa yote 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya kwa Wote imeanza kwa kaya zisizo na uwezo ambapo Serikali imetoa shilingi bilioni 48.8 kaya 172,297 zimefikiwa na wanufaika 463,228 wameanza kupata huduma. Mabaraza na bodi za kitaaluma yamesajili wataalam 14,310, maduka ya dawa 330, watarajali 3,004, vituo 3,643 vya kushughulikia mashauri 30, kutoa *CPD* kwa wataalam 102,066 na kukagua vituo binafsi 654.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ya maendeleo Wizara imefuatilia miradi 40 ya ujenzi; miradi 27 ipo katika hospitali za rufaa za mikoa na 13 katika hospitali ya Taifa, maalum na kanda. Miradi saba imefikia zaidi ya 90%, miradi nane wastani wa 70%, mradi mmoja 45% na miradi 25 ipo hatua za awali. Miradi hii inahusisha majengo ya huduma za mionzi, wagonjwa wa nje, damu salama, dharura, *ICU*, mama na mtoto pamoja na hospitali na huduma nyingine muhimu 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kubaini changamoto za uchakavu wa miundombinu, kutawanyika kwa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na mazingira yasiyoruhusu

maboresho ya kudumu ya huduma ya ubobezi na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano, Bunge la Kumi na Moja, Serikali ilianzisha mchakato wa ujenzi wa Muhimbili mpya ambapo Serikali inapanga kujenga Muhimbili mpya ndani ya miaka mitano kwa gharama ya shilingi trilioni 1.2 ambapo shilingi bilioni 908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali. Mchango huu wa Serikali ni kupitia maandalizi ya eneo lakini pia sehemu ya fedha hizi ni misamaha ya kodi, ushuru na tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganifu wa gharama na miradi 16 kutoka nchi 15 umeonesha kuwa Muhimbili mpya yenye eneo la meta za mraba 115,000 itagharimu Dola za Kimarekani 1,819 kwa mita za mraba, ikilinganishwa na dola 3,000 mpaka 7,000 kwa mita za mraba katika mataifa mengine kote duniani. Hivyo, Tanzania itapata hospitali kubwa kwa gharama nafuu. Chini ya wastani wa 42% ya hospitali hiyo itapanda kutoka ngazi ya tatu kwenda ngazi ya nne ya huduma kwa vigezo vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Muhimbili mpya si mradi wa afya pekee bali ni uwekezaji wa kimkakati katika uchumi wa kisasa. Utapunguza rufaa nje, utaongeza tiba utalii, utavutia wawekezaji, mashirika ya kimataifa na vipaji adimu na utaifanya Tanzania kuwa ni kitovu cha huduma za afya, biashara na uwekezaji wa kikanda. Kwa ujumla, utekelezaji huu unaonesha dhamira ya Serikali kujenga mfumo wa afya unaojali kinga, kujenga mfumo wa afya unaojali ubora, kujenga mfumo wa afya unaokwenda kuongeza upatikanaji wa huduma, kujitegemea kwa bidhaa za afya, matumizi ya teknolojia na ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha sehemu hii, mwelekeo wa sekta ya afya haujajengwa juu ya takwimu peke yake bali juu ya wajibu wa kulinda utu wa mwananchi. Tunapoongeza hospitali tunasogeza haki; tunapozalisha dawa nchini tunajenga uhuru wa afya; tunapounganisha mifumo ya

TEHAMA, tunaharakisha maamuzi ya kuokoa maisha; na tunaposisitiza ubora tunathibitisha kuwa kila Mtanzania anastahili kuhudumiwa kwa heshima. Hii ndiyo falsafa ya maendeleo ya watu ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliisimamia na ndiyo roho ya utu ambayo Nelson Mandela aliikumbusha dunia maeneo mahsusi ya msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wakati wa hotuba yake ya kuzindua Bunge hili, Wizara inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuweka mkazo katika maeneo mahsusi ambayo ni kuboresha mifumo ya ugharamiaji kwa huduma za afya, kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba na vitendanishi na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili iweze kusomana na kupunguza muda mrefu ambao mteja anatumia kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusaini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na usajili wa wanachama kuanza rasmi Januari, 2026, hatua inayoendelea ni maboresho ya mifumo ya utoaji wa huduma. Kuendelea kusajili wananchi waSIYO na uwezo kupitia kaya na kuendelea kutoa elimu ya bima ya afya kwa wananchi ili wawe na uelewa wa dhana ya bima ya afya na kujiunga na mifumo ya bima ya afya iliyopo nchini. Hatua hii ni mageuzi makubwa ya kihistoria yanayoweka bayana ukweli kuwa afya si fadhila, afya si bahati, afya si upendeleo bali ni haki ya msingi ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Bima ya Afya kwa Wote si mradi wa Wizara pekee bali ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa Taifa na wananchi wake, lakini pia ni ukumbusho wa misingi ya mapambano ya adui wa Taifa letu iliyotolewa na Baba wa Taifa kuhusu ujinga na maradhi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo la Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuimarisha uwezo wa nchi katika kuzalisha bidhaa za afya, ili kufika azma ya kujitosheleza kwa 80%, ifikapo mwaka 2030, Wizara itaendelea

kukiwezesha kikosi kazi maalum cha *Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce (PIAT)* kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vipya vya bidhaa za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuweka mazingira rafiki na wezeshi, ikiwemo upatikanaji wa ardhi na miundombinu muhimu ili kuwavutia wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya bidhaa za afya na kupunguza utegemezi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wizara tunaamini wakati ni sasa. Katika kuhakikisha suala la kuimarisha viwanda vya ndani na uwezeshaji wa uzalishaji wa ndani si maneno tu bali ni dhamira thabiti ya Serikali. Wizara imejipanga kuhakikisha *MSD* inanunua kwanza dawa zinazozalishwa ndani, zinazokidhi vigezo vya *TMDA* kabla ya kwenda kununua nje ya nchi. Lazima tuchukue hatua za ukweli na uwazi ili kuimarisha na kulinda uzalishaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili Wizara haita-*compromise* hata kidogo. Nitumie nafasi hii kuwaalika wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa hii ya kuwekeza katika viwanda vya bidhaa za afya ili kuunga mkono juhudi na maono ya Mheshimiwa Rais kwa kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya nje ya nchi, kwani dawa ni tiba, dawa ni ulinzi na dawa ni usalama wa wananchi na usalama wa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kuwa mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi. Ili kuhakikisha hilo Wizara itaendelea kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika sekta ya afya inasomana na kubadilishana taarifa pamoja na kuwezesha kutuma, kupokea na kutunza taarifa za wagonjwa katika hospitali za umma na binafsi, kutoa rufaa kidijitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo mingine inayohitaji taarifa muhimu. Kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuleta ufanisi ni kutafsiri kwa vitendo

maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kutaka mifumo ya Serikali kuwa ni michache na yenye kusomana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ipo kwenye hatua za awali ya uanzishwaji wa chombo cha kutoa ithibati ya ubora wa huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma ya umma na binafsi. Hatua hii itaimarisha ubora wa huduma za afya nchini kwa kuzingatia uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye vituo hivyo na kuwezesha huduma zinazotolewa katika vituo vyetu kutambulika kikanda na kutambulika kimataifa. Kupitia chombo hiki, Wizara imedhamiria kutoa huduma bara za afya kwa wananchi ikiwemo kupunguza muda wa mgonjwa wa kusubiri huduma na kuhakikisha matumizi ya lugha zenye staha kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ithibati vilevile zitakapotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya, zitawezesha kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na kuimarisha tiba utalii, malengo yetu ni kuhakikisha kwamba vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya rufaa, mkoa, hadi Taifa vinapata ithibati ya ubora ifikapo 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha eneo hili, maeneo mahsusi ya msisitizo yanaonesha wazi kuwa safari ya sekta ya afya katika kipindi kijacho haitajengwa tena kwa kuongeza huduma pekee, bali kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa ni huduma endelevu zenye ubora, zinazofikiwa na kila mwananchi na zinazolinda utu wa kila mgonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya kwa Wote inaleta usawa na inalinda familia dhidi ya umaskini unaotokana na gharama za matibabu, uzalishaji wa dawa na bidhaa za afya nchini unaleta kujitegemea, ajira na usalama wa Taifa. Mifumo ya TEHAMA inaleta ufanisi, inapunguza urasimu na inaharakisha maamuzi ya kitabibu na ithibati ya ubora inaleta heshima, uwajibikaji na ushindani wa huduma tunazozitoa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, falsafa inayotuongoza ni rahisi, lakini yenye maana kubwa. Afya ya mwananchi si gharama bali ni uwekezaji, dawa si bidhaa ya kawaida bali ni tiba, ulinzi na

usalama, taarifa za mgonjwa si makaratasi ni maisha yanayohitaji uamuzi wa haraka na ubora wa huduma si anasa ni haki ya msingi ya Mtanzania. Haya ndiyo mageuzi tunayoyasimamia leo, afya iwe haki, dawa zizalishwe nyumbani, huduma ziwe za kidijitali, vituo viwe na ubora unaotambulika na kila mgonjwa ahudumiwe kwa heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu si mpango wa kisekta, hii ni ahadi ya Taifa letu kwa watu wake kwamba, hakuna Mtanzania atakayeachwa nyuma katika kupata huduma bora za afya na kwamba Tanzania yenye afya bora ndiyo msingi wa Tanzania yenye uchumi imara, utu, matumaini na maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vipaumbele vya mpango wa bajeti, mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2026. Vipaumbele na mpango wa Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 umezingatia mipango ya kitaifa na kisekta ikiwemo: Dira ya Taifa 2050; Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi wa Mwaka wa Fedha 2025/2030; Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufungua Bunge lako Tukufu la Kumi na Tatu; Sera ya Afya na Mipango Mkakati ya Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa, Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza vipaumbele 11 vya kimkakati pamoja na afua zake zinazolenga kuleta maboresho makubwa katika sekta ya afya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Kuimarisha ubora wa huduma za afya ili kukidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa. Kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma, kufanya tathmini ya ubora na kupata ithibati, kuharakisha uanzishwaji wa taasisi za ndani ya ithibati, kusimamia maadili, usajili wa wataalam na ukaguzi shirikishi wa vyuo na vituo na kuimarisha huduma kwa mteja ikiwemo muda wa kusubiri, mfumo wa malalamiko na usalama wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kuimarisha mfumo wa ugharamiaji huduma za afya na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Kuimarisha ugharamiaji kwa kutumia vyanzo vya ndani, kusajili wananchi wa kaya zenye uwezo na zisizo na uwezo, kutoa elimu kwa jamii, ili wajiunge na bima, kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2025-2030 na Mpango Mkakati wa Muda wa Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuwezesha uwekezaji wa viwanda vya ndani, ili kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi kwa kujenga maabara ya kisasa ya utafiti wa dawa *(Bioequivalent Lab)*, kuwekeza katika uzalishaji wa dawa za UKIMWI katika Kiwanda cha *TPI* na kuvutia wawekezaji wengine. Kuboresha mifumo ya maoteo, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa, kuratibu majukwaa ya wawekezaji na kudhibiti usugu wa vimelea dhidi ya dawa na matumizi sahihi ya *antibiotics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara tayari imezindua *Mloganzila Pharmaceutical Hub* (Kongani ya Viwanda ya Mloganzila). Kulitaarifu Bunge lako kwamba, hivi nimesimama, tayari wawekezaji wanaendelea na ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Serikali imejipanga vizuri kwamba, leo hii uzalishaji wa dawa ni 16% tu. Ninalitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mikakati na mipango tuliyoiweka, ifikapo Mwaka 2030 Wizara imeamua kwamba, ni lazima Taifa letu liweze kuzalisha dawa lenyewe kwa 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA, ili kuhakikisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya. Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika vituo, ili iweze kusomana na kubadilishana taarifa, ikiwemo Afya Mtandao, *Teleradiology*, *Teleconsultation*, Kituo Kikuu cha Kuhifadhi Taarifa *(Central Data Repository)*, kuondokana na matumizi ya karatasi katika ukusanyaji wa takwimu na kuimarisha matumizi ya akili unde katika utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, pamoja na lishe na usafi wa mazingira. Kuhamasisha jamii kupima afya mapema, ambapo ninaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hivi karibuni Wizara imebuni Programu mpya inayotambulika kama "Ijue Namba Yako" imezinduliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko, kujenga miundombinu ya kuwatenga wahisiwa mipakani, kukamilisha vituo vya umahiri wa elimu ya afya kwa umma na kutekeleza mpango jumuishi wa huduma za afya ngazi ya jamii, ikiwemo nafasi 8,000 za ajira mpya. Kuboresha huduma za chanjo kwa mfumo wa kielektroniki, majokofu na vifaa vya kutilia jotoridi. Kutoa kinga, tiba ya trakoma, matende na mabusha katika halmashauri 19 pamoja na huduma za utengamao na kuendelea na afua za lishe za vyakula vilivyoongezwa virutubisho kupambana na utapiamlo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha utafiti wa matokeo ya tafiti za afya, ubunifu na teknolojia. Kuratibu utafiti katika vituo, taasisi na vyuo pamoja na kulenga changamoto za afya nchini. Kutoa huduma kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi. Kukamilisha tafiti zinazoendelea na kuanza tafiti mpya katika kinga, tiba, utengamano, mafunzo, dawa na mifumo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha huduma za ukunga, afya ya uzazi na mama na mtoto, ili kupunguza vifo vya watoto wachanga vitokanavyo na uzazi. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya ya uzazi, mama na mtoto, kuongeza vituo vya huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu. Vituo vya kujifungua na huduma rafiki kwa vijana, kuimarisha matumizi ya Chati Uchungu iliyoboreshwa pamoja na vyumba vya kujifungulia kwa huduma ya mapacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam wa Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi. Kuongeza programu za mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi kwa utaratibu wa muda mrefu wa

SETI. Kusimamia ubora wa mafunzo kwa wanafunzi wa vyuo vya umma na binafsi pamoja na mafunzo kwa vitendo. Kuendelea kuajiri watumishi wa ajira ya kudumu na mkataba na kuimarisha miradi ya ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, kuimarisha afua za tiba asili na tiba mbadala. Kuwajengea uwezo wataalam, kuongeza wigo wa huduma za tiba asili kwenye mfumo rasmi. Kuanzisha mashamba ya miti dawa kwa kila kanda kwa uzalishaji endelevu. Kununua eneo la kujenga kituo cha umahiri cha tiba asili Mkoani Dodoma. Kushirikiana na mataifa na taasisi za kimataifa zilizopiga hatua kwenye teknolojia ya tiba asili na tiba mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, kuimarisha huduma za tiba, ubingwa na ubingwa bobezi na kuvutia tiba utalii nchini. Kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali za rufaa za mkoa, kanda, maalum na Taifa. Kuanzisha huduma mpya za kibobezi, kupunguza rufaa nje ya nchi, kuendeleza kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya moyo na mishipa ya damu. Upandikizaji wa figo na uroto, kuanzisha kituo cha umahiri cha wagonjwa wa kinywa na meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza huduma za ubingwa katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka nane hadi 17 na huduma tano katika hospitali za halmashauri. Kuimarisha huduma za uchunguzi kwa vifaa na vitendanishi vya kisasa, damu salama, uhandisi na matengenezo ya vifaa tiba na kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma katika hospitali zote za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamano hususani kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu. Kuandaa mpango mkakati wa afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii utakaohusisha kinga, tiba na utengamano. Kuboresha mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Sekta ya Afya, ili kukuza usalama wa kazi na ustawi wa kiakili. Kuendelea kuimarisha huduma za afya ya akili, kisaikolojia, utengamano na huduma za wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa

Mwaka wa Fedha 2026/2027. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara na hospitali zilizo chini yake inakadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi 747,200,091,299.81. Kati ya fedha hizo, shilingi 76,195,850,735.53 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara, shilingi 165,804,149,264.47 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha shilingi 505,200,091,299.81 kutoka Taasisi, Hospitali ya Taifa Maalum na Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 652,236,871,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 36% ya bajeti iliyotengwa. Ambapo kiasi cha shilingi 516,323,356,000 ni mishahara ya watumishi wa Wizara, hospitali na taasisi zilizo chini yake na kiasi cha shilingi 135,913,515,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 1,148,025,187,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na 64% ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni kiasi cha shilingi 789,458,609,000 na fedha za nje ni shilingi 358,566,578,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni kiasi cha shilingi 1,800,262,058,000 ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele ilivyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba hii inapatikana pia, katika tovuti ya Wizara ya Afya, *www.moh.go.tz*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, hotuba yangu ina jumla ya kurasa 287. Ninakuomba uridhie Bunge lako Tukufu, sehemu ya hotuba katika yale ambayo sijayasema iwe ni sehemu ya Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, kwa heshima kubwa na kwa maamuzi rasmi ya kwenda kuhakikisha tunalinda utu wa Mtanzania, ninaomba kutoa hoja. Ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

11 MEI, 2026

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MHE. MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA I: UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** baada ya Bunge lako tukufu kupokea taarifa iliyochambua bajeti ya Wizara kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, naomba kwa mujibu wa **vifungu namba 118 hadi 123 vya kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2023**, kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,**kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa namna ya kipekee kabisa nachukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Wizara hii SIYO tu inagusa afya za kila mtanzania bali inagusa uhai wa watanzania wote bila kujalijinsi, umri, dini, kabila, tajiri au maskini. Ninatambua kuwa, nina deni na dhima kubwa kwa nchi yangu katika kutekeleza jukumu hili muhimu na ninamuahidi Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu pamoja na watanzania wote kuwa sitawaangusha.

3. **Mheshimiwa Spika,** namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kwa nchi, mashirika ya kimataifa, wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi licha ya changamoto za ugharamiaji wa huduma za afya zilizotokana na kubadilika kwa sera za nje. Katika kuhakikisha kuwa nchi inavuka salama katika kipindi hiki, Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha huduma za afya nchini zinaendelea kutolewa bila kuathiri uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na wadau mbalimbali uliodumu kwa muda mrefu tangu tulipopata uhuru. Mheshimiwa Rais amekuwa kinara wa kuimarisha uhusiano wa

diplomasia ya kimataifa na kutetea maslahi ya Taifa ili kujenga Tanzania yenye amani na uchumi imara.

4. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili kupitia uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Ushindi huo wa kishindo ni ishara kuwa wananchi wana imani na Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla. Nami namuahidi kuwa, kwa imani ile ile iliyooneshwa na watanzania, nitaibeba agenda yake ya kuimarisha huduma za afya nchini na kuwa chachu ya kukuza uchumi hasa ikizingatiwa kuwa Afya ni Mali na Afya ni Mtaji.

"Baba wa Taifa aliwahi kusema kuwa afya ya wananchi ni msingi wa maendeleo na Taifa haliwezi kuendelea ikiwa watu wake ni wagonjwa au dhaifu". "na kwa mafunzo ya Nelson Mandela, heshima ya binadamu ni kiini cha taifa huru. Hivyo, huduma ya afya tunayojenga ni huduma ya utu, haki na maendeleo" Nami nitaendelea kusimamia utekelezaji wa maono hayo ili kufikia azma na maono ya sekta ya afya yakujenga jamii yenye afyabora na ustawi itakayochangia katika kukuza uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja".

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,** kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Imani waliyopewa na wananchi kwa kuwachagua, ni ishara kuwa wananchi wana imani kubwa kwao katika kuendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kimahusiano, kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)**, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa miongozo, maelekezo, hekima na busara zake katika kusimamia shughuli za Serikali, zitanisaidia katika kutekeleza

majukumu yangu ya kila sikuya usimamizi waSekta ya afyakwa ufanisi mkubwa.

7. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi thabiti unaozingatia kanuni bila upendeleo katika kusimamia majadiliano na kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu. Aidha, nampongeza **Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)**, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Nitumie fursa hii pia, kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa ili kusimamia na kuishauri Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa.

8. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Johannes Lukumay (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na **Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid (Mb)** kuwa Makamu Mwenyekiti. Hakika miongozo yenu na ushauri kwa kushirikiana na wajumbe wa Kamati ni nguzo muhimu katika kuwezesha kuboresha utendaji wa majukumu ya Wizara ya Afya. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara ya Afya itaendelea kutoa ushirikiano kwa kuzingatia ushauri wenu katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa **Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard** na watumishi wa Bunge kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia. Niwahakikishie kuwa viongozi na watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utoaji wa huduma za afya.

9. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Florence George Samizi (Mb)**, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Afya. Ninaamini kuwa, taaluma na uzoefu wake katika Sekta ya Afya utasaidia kuleta mapinduzi yenye tija. Vilevile, nachukua nafasi hii kumpongeza **Ndugu. Emmanuel Tayari** kwa kuaminiwa na

kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya anayeshughulikia masuala ya dawa na vifaa tiba.

10. Mheshimiwa Spika, kipekee nachukua fursa hii kuwashukuru **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe**, Katibu Mkuu, **Ndugu. Ismail Hassan Rumatila**, Naibu Katibu Mkuu na **Dkt. Grace Elias Magembe**, Mganga Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Afya. Vilevile, naishukuru **Menejimenti ya Wizara ya Afya na watumishi wote wa Sekta ya Afya** kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, moyo wa uzalendo na imani thabiti kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Hakika mmekuwa nguzo muhimu kwa kipindi kifupi ambacho nimehudumu katika Wizara.

11. Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Wizara zote kwa namna tunavyoshirikiana kwa pamoja kuimarisha huduma za afya nchini. Kipekee naishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kuwezesha utekelezaji wa afua za afya mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa uratibu wa sekta mtambuka, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, kwa usimamizi wa huduma za afya ngazi yamsingi, Wizara ya Fedha kwa kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika masuala mbalimbali ya kisheria na Wizara ya Maji katika kuimarisha afua mbalimbali za afya kupitia upatikanaji wa maji safi na salama.

12. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambao ni **Bw. Mavere Tukai** (MSD), **Dkt. Irene Isaka** (NHIF), **Dkt. Adam Fimbo** (TMDA), **Prof. Said Shehe Aboud** (NIMR), **Dkt. Fidelice Mafumiko** (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali), **Dkt. Germana Leyna** (Taasisi ya Chakula na Lishe). Pia, nichukue fursa hii kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa,Maalum na Kanda ambao ni **Dkt. Delillah Kimambo** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Mheshimiwa. Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt. Peter Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Diwani Msemo** (Taasisi ya Saratani ya

Ocean Road), **Dkt. Leonard Subi** (Hospitali ya magonjwa ambukizi Kibong'oto), **Dkt. Innocent Mwombeki** (Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Makubi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Mawalla** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Herbert Massigati** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara), **Dkt. Sr. Alicia Massenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando), **Prof. Gileard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC) na **Bi. Brenda Msangi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda CCBRT).

13. Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa zote 28, Hospitali za Halmashauri, vituo vya afya, zahanati, wakuu wa vyuo vya mafunzo vilivyo chini ya Wizara, wasajili wa bodi na mabaraza ya kitaaluma. Aidha, kipekee nawashukuru watumishi na watendaji wa Sekta ya Afya wa ngazi zote kwa mchango wao katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa bidii, weledi na kujitoa usiku na mchana kuokoa maisha ya watanzania.

14. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi rafiki na mashirika ya kimataifa yanayochangia katika uboreshaji na utoaji wa huduma za afya nchini. Hivyo basi, nitumie wasaa huu kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Uingereza, Ireland, Uswisi, Korea Kusini na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNFPA na UNICEF kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususan afya ya msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za Ujerumani, Japan, India, Sweden, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uturuki, Marekani, Ufaransa, China, Cuba, Italia, Misri na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Sekta ya Afya kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi inayotekelelezwa na Serikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

15. Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa Sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kiraia,

vyama vya kitaaluma na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini. Wadauhao wamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo ya sekta ya afya. Baadhi ya wadau hao ni, Benjamin Mkapa Foundation, APHFTA, AMREF, AGOTA, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Foundation for Cancer Care in Tanzania, LHL International, MDM, COUNSENUTH, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, PST, TAPHATA, Good Samaritan Foundation, Aga Khan Foundation, NEST 360, EGPAF, JHPIEGO, JSI, FHI, AFRICARE, Abbott Fund Tanzania, Shirika la Msalaba Mwekundu, Plan International, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, Pathfinder, PATH, CHAI, AMERICARES, MELSAT, TARA, TAWOPHA, PASADA, NACOPHA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, MKUTA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, Tanzania Surgical Association, Association, SATA, TANESA, Tanzania THPS, Diabetic Tunajali, Tanzania Midwives Association, TAYOA, NACONGO, TDA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, CIHEB TANZANIA, Starlink Gulf Trading LTD, KIVULINI, WILDAF, Haydom Lutheran Hospital, GSM Foundation, MO Foundation, VODACOM Foundation, TCRF, FSDT, JAI, Touch Foundation pamoja na asasi nyingine zinazoshirikiana na Sekta ya Afya kwa namna moja au nyingine. Ushirikiano wao ni wa kupongezwa na unaendelea kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya afya nchini.

16. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa vyuo vya elimu ya juu vinavyoshirikiana na Sekta ya Afya katika kuimarisha huduma za afya nchini. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Kairuki, Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi, Chuo Kikuu cha KCMC, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, Chuo Kikuu cha Aga Khan, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala, Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Arusha, Taasisi yaTeknolojiaya Nelson Mandela, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mtakatifu Franscisco pamoja na

wadau wote wa vyuo vya kati vinavyotoa mafunzo ya afya na sayansi shirikishi.

17. Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako tukufu kuwashukuru kwa moyo wa dhati wananchi wote wa jimbo langu pendwa la Rufiji kwa namna wanavyoniamini na kunipa ushirikiano wa kiwango cha juu katika kipindi chote ninachowatumikia kama Mbunge wao. Kila ninapokumbuka Imani waliyonayo kwangu, ninajikuta mwenye nguvu na ari kubwa ya kuwatumikia wananchi wa jimbo langu. Ninawaahidi kuwa nitafanya kazi bila kuchoka ili kuhakikisha ahadi zangu kwao na vipaumbele tulivyopanga kwa pamoja jimboni ninavitekeleza SIYO tu kwa maslahi mapana ya wana Rufiji bali kwa maslahi ya Taifa kwa ujumla. Natambua imani yao ni deni kubwa kwangu na nimedhamiria kuzitekeleza ahadi zangu kwa uadilifu kama ilivyo desturi yetu wana Rufiji kuweka mbele uadilifu na uzalendo katika kuijenga Rufiji na Taifa letu kwa ujumla.

18. Mheshimiwa Spika, mwisho japo SIYO kwa umuhimu, kuishukuru nichukue nafasi hii familia yangu kwa kipekee upendo, uvumilivu, ushirikiano, dua na maombi yao wakati wote ninapokuwa natekeleza majukumu yangu. Hakika wamekuwa wa msaada na faraja kubwa kwangu wakati wote ninapokuwa katika wajibu wangu wa kuwatumikia watanzania.

19. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwako binafsi na Bunge lako tukufu, wanafamilia wote, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu; Mheshimiwa enista Joachim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Vilevile, nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), Muadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mhashamu Bernadin Francis Mfumbusa aliyekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Kondoa na viongozi wengine wa dini na madhehebu mbalimbali waliopoteza maisha.

20. Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwapoteza watumishi wenzao katika kipindi hiki na watanzania wote waliopoteza ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Kipekee nitoe salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa kwa ajali ya boti iliyotokea tarehe 13 Machi, 2026 na kusababisha Sekta ya Afya kupoteza watumishi saba (7) wa kada za afya waliokuwa kazini wakitekeleza majukumu yao. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

SEHEMU YA II: MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2026.

21. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo yangu ya awali, naomba sasa kutambua mafanikio ya Sekta ya Afya yaliyotokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu alipoingia madarakani kama ifuatavyo:-

Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya

22. Mheshimiwa Spika, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 10,153 mwaka 2021/22 na kufikia vituo 13,683 mwezi Machi 2026 sawa na ongezeko la vituo 3,530 vilivyojengwa katika kipindi cha Awamu ya Sita. Ongezeko hili linahusisha Zahanati 8,706 kutoka 7,189; Vituo vya Afya 1,359kutoka 956; Hospitali475kutoka 404 na Vituo vinginevyo 3,143 kutoka 1,604. Aidha, kuna ongezeko la majengo mapya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini –KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Hospitali ya Kanda Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga hospitali kumi (10) mpya za rufaa za mikoa ambapo hospitali tano (5) za mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu na Songwe hazikuwa na hospitali hizo na hospitali tano (5) za mikoa ya Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi zilihamishwa kutoka majengo ya zamani kwenda kwenye majengo yaliyojengwa katika maeneo mapya. Vilevile, Serikali imeongeza majengo katika hospitali za rufaa za mkoa za Ligula (Mtwara), Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa) na Kitete (Tabora). Hivyo, kwa sasa mikoa yote nchini ina hospitali za rufaa za mikoa na Wilaya zote zina hospitali katika ngazi ya halmashauri. Pia, Serikali imefanya ukarabati wa majengo ya zamani katika hospitali kongwe 50 za Halmashauri, ukamilishaji wa maboma ya zahanati 980, ujenzi wa vituo vya afya 390, ujenzi wa mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na wagonjwa wa dharura kutoka 25 hadi 61 na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya zenye uwezo wa kuhudumia kaya 540.

24. Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za dharura nchini, idadi ya majengo maalum ya kutolea huduma za dharura (Emergency Medicine Department – EMD) imeongezeka kutoka saba (7) yaliyokuwepo mwaka 2021/2022 katika ngazi ya rufaa pekee hadi kufikia 125 mwezi Machi 2026, yakijumuisha ngazi ya rufaa na msingi, sawa na ongezeko la majengo 118. Hii ni hatua ya kihistoria,kwani kwamara ya kwanza huduma hizi zimefikishwa hadi ngazi ya afya ya msingi, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hupata huduma. Uwekezaji huu umeimarisha upatikanaji wa huduma za dharura ndani ya muda muhimu wa saa moja ya kwanza (Golden Hour), ambao kitaalamu ni kipindi muhimu cha kuokoa maisha na kuzuia madhara makubwa kama ulemavu au kifo. Aidha,Wizarainaendelea kusimamia ubora wa huduma hizi, kwa kuwa ushahidi unaonesha kuwa huduma bora za dharura zinaweza kupunguza vifo kwa wastani wa asilimia 40 na hivyo kuokoa maisha ya wagonjwa wa dharura, ajali na majanga.

25. Mheshimiwa Spika, idadi ya vitanda vya wagonjwa imeongezeka kutoka 86,131 mwaka 2021/2022 hadi 156,932 mwezi Machi 2026 ikiwa ni ongezeko la vitanda 70,801 sawa na asilimia 82. Aidha, idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa

ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka 258 mwaka 2021/2022 hadi 1,647 mwezi Machi 2026 ikiwa ni ongezeko la vitanda 1,389. Ongezeko la vitanda hivyo limeboresha huduma kwa wagonjwa mahututi, wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum na wagonjwa wote wa kulazwa na kuwezesha kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika.

Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

26. Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano iliyopita Serikali imeimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kupitia diplomasia ya afya na kuwezesha kutekeleza miradi mbalimbali iliyogharimu kiasi cha Shilingi Trilioni 1.2 zilizowezesha kuongezeka kwa wodi maalum za watoto wachanga kutoka 49 mwaka 2021/2022 hadi 438 mwezi Machi 2026 na vituo vya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi katika ngazi ya msingi kutoka 732 mwaka 2021/2022 hadi 1,700 mwezi Machi 2026. Aidha, katika kipindi hicho kupitia mpango wa madaktari wa Dkt Samia, mafunzo kazini kwa watumishi 29,129 yametolewa na jumla ya watu 286,381 wamehudumiwa. Vilevile, Serikali imehakikisha upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa asilimia 85 zikiwemo bidhaa za uzazi wa mpango, dawa za kuzuia damu kuvuja kwa wingi wakati wa kujifungua (oxytocin na misoprostol), dawa za kutibu kifafa cha mimba (magnesium sulfate), dawa za kutibu kuharisha kwa Watoto (ORS/Zinc) na vidonge vya myeyuko vya kutibu nimonia kwa watoto (amoxycilline).

27. Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo yamechangia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104 mwaka 2022. Kushuka kwa vifo hivyo kumesababisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuchaguliwa kuwa kinara wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika bara la Afrika. Kutokana na heshima kubwa iliyopewa Tanzania, Serikali imedhamiria kwa dhati kuendelea kuwekeza katika afua za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza kwa asilimia 50 ya vifo 104 kwa takwimu za sasa ifikapo 2030. Lengo ni kuvuka Malengo Endelevu ya Dunia ya vifo vitokanavyo na uzazi kufikia chini ya 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo 2030.

"Nichukue fursa hii kuwafahamisha waheshimiwa wabunge na wananchi kuwa, Mheshimiwa Rais ameendelea kutambuliwa kama Rais wa mfano aliyefanya vizuri katika kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa kipindi cha muda mfupi tangu kuingia madarakani. Mafanikio hayo yametokana na dhamira yake ya dhati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na kuboresha huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha hakuna mwanamke anapoteza maisha wakati analeta uhai duniani".

Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa

28. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa tiba vya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 241.6 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya hospitali ya Taifa hadi ngazi ya afya ya msingi. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, MRI zimeongezeka kutoka saba (7) hadi 13, CT Scan 12 hadi 45, Mini Angio Suite tano (5), kipimo cha uchunguzi na tiba ya magonjwa ya mfumo wa chakula na mfumo wa uzazi (Fluoroscopy) 14, Digital X-ray 147 hadi 559, Ultrasound 476 hadi 970, huduma ya kutibu matatizo ya moyo ya dharura (CathLab) moja (1) hadi nne (4) na matibabu ya hali ya juu ya magonjwa ya saratani (PET CT SCAN) ambayo haikuwepo awali na sasa ipo moja (1). Aidha, kuongezeka kwa vifaa na vifaa tiba vya uchunguzi kumepunguza rufaa za ndani na nje ya nchi, kumewezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kusaidia kutoa matibabu sahihi zaidi na kupunguza muda wa kupata huduma. Tumeshuhudia siku za karibuni wananchi wengi wakijiuliza kwa nini magonjwa yameongezeka, pamoja na sababu nyingine za mtindo wa maisha na mabadiliko ya tabia nchi, uwezo wetu wa kugundua na kutambua magonjwa umeongezeka sana kufuatia uwekezaji huu mkubwa.

29. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha huduma bora za maabara zinapatikana nchini kwa kuendelea kuijengea uwezo Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ambapo mwaka 2025 Maabara hiyo imepata ithibati ya kimataifa ISO 17043:2022 ya

kuandaa, kusambaza, kusimamia na kupima ubora wa vipimo vya maabara ndani na nje ya nchi. Hatua hiyo imeongeza uwezo wa ndani wa usimamizi wa maabara, kupunguza utegemezi kwa maabara za nchi za nje katika uthibiti ubora wa maabara, kupunguza gharama, kulinda usalama wa nchi na kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wakati.

30. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma za uchunguziwa maabara nchini, Serikali imefanikiwa kuongeza maabara zilizopata ithibati ya ubora wa kimataifa kutoka Maabara 49 mwaka 2021/2022 hadi 102 Machi 2026. Aidha, Serikali imenunua na kusimika mashine za uchunguzi wa maabara 3,238 ambapo mashine 1,081 ni za hematolojia, mashine 1,334 za uchunguzi wa kemia, mashine 792 za uchunguzi wa mkojo na mashine 31 za kuotesha vimelea na kutambua dawa sahihiya kuua vimelea husika. Mashine hizo zimesimikwa kwenye vituo 900 vya kutolea huduma katika ngazi mbalimbali zikiwemo zahanati nane (8), vituo vya afya 686, hospitali za wilaya 121, hospitali teule za wilaya 39, hospitali za kijeshi 29 na hospitali 64 za ngazi ya rufaa. Vilevile, Serikali imefanikiwa kununua jumla ya makabati 15 ya usalama wa vimelea vya magonjwa ambayo hutumika kulinda afya za wataalam wa maabara dhidi ya vimelea hatarishi wakati wa kutimiza majukumu yao.

Huduma za Ubingwa na Ubingwa Bobezi

31. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika ngazi ya rufaa ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana ndani ya nchi. Baadhi ya huduma za ubingwa bobezi zilizotolewa kwa wagonjwa kuanzia mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026 ni pamoja na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 170, upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa 57, upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa wagonjwa 102, uwekaji wa puto tumboni kwa wagonjwa 200, kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi mshtuko kwa wagonjwa 510, upandikizaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 1,791, upasuaji wa mgongo kwa wagonjwa 1,688, upasuaji wa kibiongo kwa wagonjwa 98, upasuaji na urekebishaji wa mifupa ya kiuno kwa wagonjwa 647, upasuaji wa vichwa

vikubwa na mgongo wazi kwa wagonjwa 2,095, na upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu kwa wagonjwa 1,246.

32. Mheshimiwa Spika, huduma nyingine za ubobezi zilizotolewa katika miaka mitano ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ni pamoja na upasuaji wa ubongo kwa kufungua kichwa kwa wagonjwa 1,208, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 785, uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 1,347, upasuaji wa moyo (kwa kufungua kifua) kwa wagonjwa 73, kuzibua mishipa ya moyo kwa wagonjwa 2,074, upandikizaji wa kurekebisha mapigo ya moyo kwa wagonjwa 34, upasuaji wa macho kwa kutumia matundumadogo kwa wagonjwa 1,078, upasuaji wa ubongo kwa kutumia teknolojia ya mawimbi kwa wagonjwa 13, matibabu ya radiolojia kwa wagonjwa 1,680, matibabu ya mfumo wa chakula na ini wagonjwa 9,666, tiba mionzi bobezi kwa wagonjwa 1,651, tiba ya mionzi ya ndani kwa wagonjwa 10,056, tiba ya immunotherapy wagonjwa 4,024, huduma za upasuaji wa magonjwa ya saratani kwa wagonjwa 6,097 na wagonjwa 731 wa saratani walifanyiwa uchunguzi kwa kutumia PET-CT scan.

33. Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika huduma za ubingwa na ubingwa bobezi umewezesha watanzania wengi kupata huduma hizo ndani ya nchi na karibu na maeneo wanapoishi kwa gharama nafuu ambapo awali walikuwa wakizifuata huduma hizo nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huo haujawanufaisha watanzania pekee bali wagonjwa kutoka nchi za jirani nao wamevutiwa na huduma nzuri zinazotolewa na hospitali na taasisi zetu hali iliyopelekea kuhudumia jumla ya wagonjwa 26,770 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji, Kenya, Burundi, Angola, Rwanda, Sudani ya Kusini, Somalia na Uganda.

Hali ya Upatikanaji wa Chanjo Nchini

34. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo nchini ambapo idadi ya watoto waliopata chanjo ya Pentavalent dozi ya 3 imeongezeka kutoka watoto 2,093,412 hadi 2,361,701 na kufanya wastani wa watoto waliopata chanjo kuongezeka kutoka

asilimia 93 mwaka 2021/2022 hadi 94.3 Machi 2026 na hivyo kuendelea kuvuka lengo la kimataifa la asilimia 90. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara imeratibu ununuzi wa dozi 161,499,930 za chanjo zenye thamani ya Shilingi 439,889,990,420 zilizosambazwa nchi nzima na hadi kufikia Machi 2026 kulikuwa na jumla ya dozi 20,268,820 za chanjo mbalimbali katika maghala ya kuhifadhia chanjo. Hii inaonesha kuwa upatikanaji wa chanjo nchini ni wa kutosheleza na huduma za kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa 13 yanayozuilika kwa chanjo zimeendelea kupatikana bila malipo kwa wananchi kulingana na mahitaji.

35. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za chanjo ili kuhakikisha chanjo zinafika kwa walengwa kwa uboraunaostahili kwa kununua majokofu 3,980 yenye thamani ya Shilingi 31,486,129,515, boti saba (7) zenye thamani ya Shilingi 1,184,312,500 kwa ajili ya huduma za chanjo kwa halmashauriza Wilaya ya Kibiti, Kigoma, Muleba, Ukerewe, Nkasi na Zanzibar. Vilevile, magari 68 aina ya Hilux pickup double cabin, malori 28 na pikipiki 300 zimenunuliwa kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma za chanjo nchini. Aidha, Serikali imesambaza mfumo wa rejista ya kielektroniki kwenye vituo 1,487 vilivyopo katika halmashauri 33 za mikoa sita (6) pamoja na ugawaji wa vishikwambi 1,603 kwenye vituo vya serikali na binafsi kwa ajili ya huduma za chanjo.

Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya

36. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi, 2026, jumla ya Shilingi trilioni 1.4 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Aidha, kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi bilioni 150 zilitolewa kulipa madeni ya MSD na Shilingi bilioni 141.9 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa za UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Shilingi trilioni 1.1 zilitumika kwa manunuzi ya bidhaa za afya kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya. Pia, katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 11 vya dawa na vifaa tiba ambavyo ni viwanda viwili (2) vya kuzalisha maji tiba, viwanda vitatu (3) vya kuzalisha vitendanishi vya maabara, viwanda vitatu

(3) vya kuzalisha dawaza vidonge na maji na viwanda vitatu (3) vya kuzalisha vifaa tiba. Viwanda hivyo vitawezesha uwepo endelevu wa maji tiba, vitendanishi vya maabara, dawa za maji na za vidonge.

37. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeanza kufufua na kuwezesha kiwanda cha Tanzania Pharmacetical Industry (TPI) kilichopo Arusha ili kuzalisha dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI. Aidha, katika kuimarisha utendaji na uendelevu wa kiwanda cha viuadudu Kibaha, Serikaliimenunua lita milioni 1.45 za viua dudu zenye thamani ya Shilingi bilioni 17.5 zilizosambazwa kwenye halmashauri 184 nchini kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa malaria.

38. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi, 2026 hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu za kipaumbele 382 ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeimarika kutoka asilimia 58 mwaka 2021/2022 mpaka asilimia 88.8 Machi 2026 sawa na ongezeko la asilimia 30. Mchanganuo wa ongezeko hilo katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma ni kama ifuatavyo: zahanati kutoka asilimia 69 hadi 88, vituo vya afya asilimia 68 hadi 88, hospitali za wilaya asilimia 72 hadi 90, hospitali za rufaa za mikoa asilimia 83 hadi 91, hospitali za kanda, maalum na taifa asilimia 58 hadi 91.

39. Mheshimiwa Spika, Wizarakupitia Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeendelea kuimarisha utendaji na ubora wa huduma hivyo kuwezesha kuendelea kushikilia cheti cha utambuzi wa umahiri katika mifumo ya udhibiti ubora wa dawa kwa vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ngazi ya tatu (Maturity Level 3). Hii inamaanisha kuwa, wananchi wameendelea kupata bidhaa za afya kwa ubora unaokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

40. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 53,633 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi Machi 2026 na hivyo kufanya idadi ya watumishi katika Sekta

ya Afya kufikia 182,430. Aidha, watumishi 9,039 waliajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato vya vituo husika vya kutolea huduma.

41. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalam bingwa na bingwa bobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuanzisha **Programu ya Samia Health Super Specialization Scholarship** ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, jumla ya wataalam 2,982 wamepata mafunzo katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ikilinganishwa na wataalam 961 waliofadhiliwa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 sawa na ongezeko la wataalam 2,021.

Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote

42. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ilileta mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote mbele ya Bunge lako Tukufu na kupitishwa mwezi Novemba, 2023. Kupitishwa kwa sheria hiyo kunawahakikishia wananchi kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi watakapougua.

43. Mheshimiwa Spika, masuala muhimu yaliyokamilishwa baada ya sheria hiyo kupitishwa ni pamoja na kanuni za utekelezaji wa sheria, mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watuwaSIYO na uwezo, mwongozo wa utambuzi wa kaya maskini zitakazogharamiwa na Serikali, mwongozo wa rufaa wa huduma za afya na kitita cha mafao cha huduma muhimu kinachojumuisha huduma 372 kwa kiwango cha uchangiaji cha Shilingi 150,000 kwa kaya ya watu waSIYOzidi sita kwa mwaka. Vilevile,Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) zimefanya mapitio ya muundo na sheria zilizoanzisha taasisi hizo ili kuendana na utekelezaji wa sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

44. Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza rasmi usajili wa wanufaika wa Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya kwanza mnamo tarehe 26 Januari, 2026 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani yasiku 100tangu kuingia madarakani katika kipindi cha pili cha awamu ya sita. Hadi kufikia Machi 2026 Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi bilioni 48.8** kwa ajili ya kugharamia kaya zisizo na uwezo kwa awamu ya kwanza. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, kaya 172,297 zimefikiwa sawa na asilimia 62 ya lengo la kaya 276,004 na kufanya jumla ya wananchi waliosajiliwa kufikia 463,228 sawa na asilimia 38 ya lengo la kufikia wananchi 1,206,319 na zoezi hilo linaendelea.

45. Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha maboresho ya mfumo utakaowezesha usimamizi wa bima ya afya kwa ufanisi, udhibiti wa gharama katika ngazi zote na kuwezesha kuanza usajili wa awamu ya pili utakaohusisha wananchi kutoka katika kaya 589,772 zisizo na uwezo pamoja na wananchi wenye uwezo wa kujigharamia. Aidha, kabla ya kuanza uandikishaji wa wananchi kwa awamu ya pili kwenye kitita cha bima ya afya kwa wote, wananchi wenye uwezo kutoka sekta rasmi, binafsi na sekta isiyo rasmi wanaendelea kujiunga kwa utaratibu uliokuwepo.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya, kwa kutumia mkakati na nyenzo za mawasiliano zilizoandaliwa kufikia makundi yote. Jukumu hili endelevu linatekelezwa kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi zote, hususan Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao ni kiungo muhimu katika kufikisha ujumbe sahihi, kubadilisha mitazamo ya jamii, kuhamasisha ushiriki, na kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma. *Nipende kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2026, Serikali kupitia Wizara imefanya mikutano na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zote, Wahariri na Waandishi wa Vyombo vya Habari vyote nchini ili kuwawezesha kuelewa kwa kina malengo ya Serikali, mwelekeo wa kisera na dhana ya bima ya afya kwa wote ili wawe washirika wa maendeleo katika kuifikisha dhana hii kwa wananchi*.

"Ifahamike kuwa, Mafanikio haya ya Sekta ya Afya katika kipindi cha Awamu ya Sita si takwimu tu za majengo, vitanda, vifaa na

huduma zilizoongezeka; ni simulizi ya maisha yaliyookolewa, yaliyorejeshwa matumaini na utu wa Mtanzania uliolindwa. Kama ambavyo Mwalimu Nyerere aliamini kuwa maendeleo ya kweli ni maendeleo ya watu, kama Nelson Mandela alivyotufundisha kuwa heshima ya binadamu ndiyo msingi wa taifa huru, na kama Kwame Nkrumah alivyosisitiza kuwa uhuru lazima uambatane na uwezo wa kujijenga, Serikali imeonesha kwa vitendo kuwa afya bora ndiyo msingi wa maendeleo ya kweli. Hivyo, kila zahanati iliyojengwa, kila hospitali iliyoboreshwa, kila mama aliyepata huduma salama, na kila maisha yaliyookolewa ni Ushahidi kwamba Tanzania inaendelea kujenga taifa lenye afya, usawa, utu na matumaini kwa vizazi vya sasa na vijavyo".

SEHEMU YA III: MAENEO MAHSUSI YA MSISITIZO

47. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** wakati wa hotuba yake ya kuzindua Bunge hili, Wizara inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuweka mkazo katika maeneo mahsusi ambayo ni: kuboresha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili iweze kusomana na kupunguza muda mrefu ambao mteja anatumia kupata huduma.

48. Mheshimiwa Spika, baada ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kusaini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na usajili wa wanachama kuanza rasmi Januari 2026, hatua inayoendelea ni maboresho ya mifumo ya utoaji huduma, kuendelea kusajili wananchi waSIYO na uwezo kupitia kaya na kuendelea kutoa elimu ya Bima ya Afya kwa wananchi ilikuwa na uelewa wa dhana ya bima ya afya na kujiunga na mifumo ya Bima ya Afya iliyopo nchini. Hatua hii ni ya mageuzi makubwa ya kihistoria ambayo yanaweka bayana ukweli kuwa afya si fadhila, si bahati, si upendeleo bali ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. ***Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Bima ya Afya kwa Wote si mradi wa Wizara pekee bali ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa taifa na wananchi wote*.**

49. Mheshimiwa Spika, kufuatia agizo la **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** la kuimarisha uwezo wa nchi katika kuzalisha bidhaa za afya ili kufikia azma ya kujitosheleza kwa asilimia 80 ifikapo mwaka 2030, Wizara itaendelea kukiwezesha kikosi kazi maalum cha Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce (PIAT) kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vipya vya bidhaa za afya nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuwawekea mazingira rafiki na wezeshi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ardhi na miundombinu muhimu ili kuwavutia kuwekeza katika ujenzi wa viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi.

50. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha suala la kuimarisha viwanda vya ndani na suala la uwezeshaji wazalishaji wa ndani si maneno tu bali ni dhamira thabiti ya Serikali, Wizara imejipanga kuhakikisha MSD inanunua kwanza dawa zinazozalishwa ndani zilizokidhi vigezo vya TMDA kabla ya kwenda kununua nje ya nchi. Hatutarajii kuona dawa kama Paracetamol, metronidazole, ciprofloxacini, erythromycin za maji na vidonge, maji tiba na nyingine zinazozalishwa kwa utoshelevu nchini zinaagizwa kutoka nje. Lazima tuchukue hatua za ukweli na uwazi ili kuhamasisha na kulinda uzalishaji wa dawa nchini.

"Nitumie nafasi hii kuwaalika wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa hii ya kuwekeza katika viwanda vya bidhaa za afya ili kuunga mkono juhudi na maono ya Mheshimiwa Rais ya kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya kutoka nje ya nchi kwani dawa ni tiba, dawa ni ulinzi nadawani usalama kwawananchi na Taifa kwa ujumla".

51. Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuwa mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi. Ili kuhakikisha hilo, Wizara itaendelea kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika Sekta ya Afya inasomana na kubadilishana taarifa pamoja na kuwezesha kutuma, kupokea, kutunza taarifa za wagonjwa katika hospitaliza ummanabinafsi, kutoa rufaa kidigitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye

mifumo mingine inayohitaji taarifa mbalimbali. Kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuleta ufanisi ni kutafsiri kwa vitendo maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ya kutaka mifumo ya Serikali kuwa michache na yenye kusomana.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara ipo kwenye hatua za awali za uanzishaji wa chombo cha kutoa **ithibati ya ubora wa huduma** katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma na vya binafisi. Hatua hii itaimarisha ubora wa huduma za Afya nchini kwa kuzingatia uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye vituo na hivyo kuwezesha huduma zinazotolewa katika vituo vyetu kutambulika kikanda na kimataifa. Kupitia chombo hiki, Wizara imedhamiria kutoa huduma bora za afya kwa wananchi ikiwemo kuwapunguzia muda wa mgonjwa kusubiri huduma kwenye vituo pamoja na kuhakikisha matumizi ya lugha zenye staha kwa wagonjwa. Vilevile, kupitia ithibati zitakazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya zitawezesha kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na hivyo kuimarisha utekelezaji wa dhana ya tiba utalii. Malengo yetu kama Wizara ni kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya rufaa ya Mkoa hadi Taifa vinapata ithibati ya ubora ifikapo 2030.

53. Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha eneo hili, maeneo mahsusi ya msisitizo yanaonesha wazi kuwa safari ya Sekta ya Afya katika kipindi kijacho haitajengwa tena kwa kuongeza huduma pekee, bali kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa endelevu, zenye ubora, zinazofikiwa na kila mwananchi na zinazolinda utu wa kila mgonjwa. Bima ya Afya kwa Wote inaleta usawa na inalinda familia dhidi ya umaskini unaotokana na gharama za matibabu. Aidha, uzalishaji wa dawa na bidhaa za afya nchini unapelekea kujitegemea, kuongeza ajira na kuimarisha usalama wa Taifa. Vilevile, mifumo ya TEHAMA inaongeza ufanisi katika utendaji, inapunguza urasimu na inaharakisha maamuzi ya kitabibu. Pia, ithibati ya ubora inaleta heshima, uwajibikaji na ushindani wa huduma zetu kitaifa, kikanda na kimataifa. Falsafa inayotuongoza ni rahisi lakini yenye maana kubwa.

“Napenda kusisitiza kuwa, Afya ya mwananchi si gharama, ni uwekezaji; dawa si bidhaa ya kawaida, ni tiba, ulinzi na usalama; taarifa za mgonjwa si makaratasi, ni maisha yanayohitaji uamuzi waharaka; na ubora wahuduma si anasa, ni haki ya msingi ya Mtanzania. Hivyo, tunaposema tunaboresha sekta ya afya, tunamaanisha tunajenga mfumo unaolinda maisha, unaozuia umaskini, unaotumia teknolojia kuongeza ufanisi, unaoweka heshima ya mgonjwa katikati ya huduma, na unaoimarisha uwezo wa Taifa kujitegemea. Kwa maneno machache, haya ndiyo mageuzi tunayoyasimamia: afya iwe haki, dawa zizalishwe ndani ya nchi, huduma ziwe za kidigitali, vituo viwe na ubora unaotambulika, na kila mgonjwa ahudumiwe kwa heshima. Huu si mpango wa kawaida wa kisekta; ni ahadi ya Taifa kwa watu wake kwamba hakuna Mtanzania atakayeachwa nyuma katika kupata huduma bora za afya, na kwamba Tanzania yenye afya bora ndiyo msingi wa Tanzania yenye uchumi imara, utu, matumaini na maendeleo endelevu.”

SEHEMU YA IV: MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

54. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/2022– 2025/2026), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya - HSSP V (2021/2022 – 2025/2026), Mpango Mkakati wa muda wa kati wa Wizara wa mwaka (2021/2022 – 2025/2026), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs -2030) pamoja na makubaliano ya kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

55. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala za Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa;

iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;

iv. Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati;

v. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga;

vi. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;

vii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini;

viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;

ix. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko; na

x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 819,977,862,602.14** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 74,207,303,307.00** ni kutoka Makao Makuu ya Wizara (ikiwemo Hospitali za Kanda, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma), **Shilingi 153,792,696,693.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 591,977,862,602.14** ni kutoka Hospitali Maalum, Hospitali ya Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

57. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya kiasi cha **Shilingi 593,852,818,278.97** sawa na asilimia **72.42** ya lengo la kukusanya maduhuli ya **Shilingi 819,977,862,602.14**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 55,433,495,972.85** sawa na asilimia **74.70** ya makadirio kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha **Shilingi 111,089,490,230.85** sawa na asilimia **72.23** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha **Shilingi 427,329,832,075.27** sawa na asilimia **72.19** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/26 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,763,541,235,000.00** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 626,433,136,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (mishahara ni **Shilingi 475,418,119,000.00** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 151,015,017,000.00)** na **Shilingi 1,137,108,099,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 347,649,490,000.00**).

Mapokezi ya Fedha

59. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **Shilingi 1,107,155,251,269.36** kimepokelewa sawa na asilimia **63** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 473,128,037,804.21** ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia **76** (mishahara ni **Shilingi 368,072,592,445.00** sawa na asilimia **77** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 105,055,445,359.21** sawa na asilimia **70**) na kiasi cha **Shilingi 634,027,213,465.15** sawa na asilimia **56** ni kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi ya maendeleo (fedha za ndani ni **Shilingi 403,278,048,926.28** sawa na asilimia **51** na fedha za nje ni **Shilingi 230,749,164,538.87** sawa na asilimia **66**).

60. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, fedha za nje zilizopokelewa ni kutoka Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, GAVI kwa ajili ya huduma za utoaji chanjo nchini, Susan Thompson Buffet Foundation na Benki ya Dunia, kwa ajili ya uwekezaji wa afya ya mama na mtoto, Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF) kwa ajili ya uimarishaji huduma za afya ikiwemo huduma za damu salama, Shirika la Kimataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), Nutrition International na UNFPA kwa ajili ya huduma za lishe pamoja na huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, asasi zisizo za kiraia na wadau wengine.

SEHEMU YA V: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza

61. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na wadau mbalimbali inaendelea kuimarisha huduma za afya nchini ikiwemo udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza ambapo takwimu za magonjwa hayo zinaonesha kuwa kuna ongezeko la mzigo wa magonjwa yasiyoambukiza nchini, hali inayoendelea kuiweka Sekta ya Afya katika hitaji la kuimarisha afua za kinga, uchunguzi na matibabu. Kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya National HealthAccounts (NHA) ya mwaka 2024 imeonesha kuwa ugharamiaji wa magonjwa yasiyoambukiza umeongezeka kwa asilimia 38 kutoka **shilingi trilioni 1.3** mwaka 2023 hadi **shilingi trilioni 1.8** mwaka 2024.

Huduma za Kisukari na Shinikizo la Damu

62. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha uratibu na utekelezaji wa afua za magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kumeanzishwa kliniki mpya 130 za huduma za kisukari na shinikizo la damu na hivyo kufanya jumla ya kliniki hizo kufikia 168 kutoka 38 zilizokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kliniki hizo zilipatiwa dawa, vifaa tiba na mafunzo

kwa watumishi ili kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma. Aidha, huduma za kinga na uchunguzi ziliboreshwa kupitia upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza mahali pa kazi, utoaji wa elimu kwa jamii, matembezi ya Kitaifa ya kuhamasisha mazoezi, pamoja na kampeni za uelimishaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini.

63. Mheshimiwa Spika, uwezo wa rasilimali watu umeimarishwa kupitia mafunzo kazini kwa watoa huduma katika vituo vya afya na Hospitali za Wilaya, pamoja na mafunzo ya kitaalamu kwa madaktari bingwa na wauguzi kuhusu huduma za kisukari, ikiwemo matibabu ya vidonda vitokanavyo na ugonjwa wa kisukari. Watoa huduma wa ngazi ya jamii na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza pia walijengewa uwezo katika maeneo ya udhibiti wa magonjwa, lishe, mazoezi na kupunguza unyanyapaa. Katika kuimarisha matumizi ya takwimu, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu katika ngazi ya jamii.

Huduma za Figo

64. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za figo nchini kwa kupanua upatikanaji wa huduma za kuchuja damu ambapo jumla ya wagonjwa 3,342 wamehudumiwa. Aidha, katika kipindi hicho, hospitali tatu (3) zimeanza kutoa huduma ya kuchuja damu; hospitali hizo ni hospitali ya rufaa ya mkoa Mawenzi, hospitali ya rufaa ya kanda ya kusini Mtwara na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na kufanya jumla ya vituo vinavyotoa huduma hiyo kufikia 74. Kati ya vituo hivyo, vituo 28 ni vya umma na 46 ni vituo binafsi. Vituo vya umma vinavyotoa huduma za kuchuja damu ni Hospitali ya Taifa Muhimbili Upanga na Mloganzila, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, hospitali 16 za Rufaa za Mikoa, Kituo cha Afya UDOM, Hospitali ya Jeshi Lugalo na Hospitali ya Emilio Mzena.

65. Mheshimiwa Spika, uwezo wa kiufundi umeimarishwa kupitia mafunzo maalum kwa wahandisi wa vifaa tiba kutoka Hospitali 13. Mafunzo hayo yalilenga kuboresha matumizi, matengenezo na uendeshaji wa mashine za kusafisha damu, hivyo kuchangia

katika kuboresha huduma. Vilevile, Wizara imekamilisha na kuwasilisha waraka wa mapendekezo ya sheria ya huduma za damu na upandikizaji wa viungo vya binadamu katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi wa huduma za figo nchini.

Huduma za Saratani

66. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ubora wa **huduma za saratani**, Wizara imeandaa mwongozo wa Kitaifa wa taratibu sanifu za uendeshaji wa bodi za kitaalamu za saratani, hatua iliyolenga kuboresha maamuzi ya kitabibu nausimamizi wawagonjwa. Aidha, Wizara imepanua huduma za matibabu ya saratani ikijumuisha uchunguzi wa saratani kwenye hospitali zote za rufaa za mikoa, tiba dawa kwenye hospitali ya rufaa ya mkoa Mount Meru na kuendelea kutoa huduma za tiba mionzi na upasuaji katika hospitali za kanda pamoja na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya kitaifa ya matibabu ya saratani.

67. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kupanua huduma za Saratani nchini kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma hizo katika kanda za nyanda za juu kusini Mbeya, Kaskazini – KCMC, kanda ya ziwa Bugando na kanda ya Kusini – Mtwara ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi. Kupitia mtambo maalum wa kisasa ujulikanao kama Cyclotron, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road imeanza uzalishaji wa dawa za uchunguzi na kutibu saratani nchini. Aidha, uwepo wa mtambo huo na uzalishaji wa dawa nchini umewapunguzia wagonjwa muda wa kusubiri huduma.

68. Mheshimiwa Spika, Wizara imeimarisha uratibu na usimamizi wa rejesta za saratani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma na Mbeya kwa kufanya mafunzo ya ukusanyaji, uchakataji na uhakiki wa ubora wa takwimu, usahihishaji wa makosa ya usajili, pamoja na kuendelea na zoezi la kuoanisha mifumo ya CanReg5 na DHIS2. Uwezo wa wataalam wa rejesta umeimarishwa kupitia programu ya kimataifa ya GICR e-learning ambapo wasajili watano (5) walipata vyeti vya kitaalam vya kimataifa.

Huduma za Afya ya Akili

69. Mheshimiwa Spika, Huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii ziliendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi nchini, ambapo jumla ya wateja 254,932 walihudumiwa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026. Huduma hizo zilijumuisha matibabu ya kifafa, skizofrenia, matatizo ya tabia, pamoja na utegemezi wa pombe na dawa za kulevya. Aidha, katika kipindi hiki, vituo 16 vya matibabu ya waraibu wa dawa za kulevya vilitoa huduma kwa wateja 17,807 na upatikanaji wa dawa za afya ya akili katika vituo umefikia wastani wa asilimia 75.

70. Mheshimiwa Spika, mafunzo pia yalitolewa kwa wataalam wa afya ngazi ya jamii, yakihusisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii 50 na wahudumu wa Afya 10 kwa lengo la kuwawezesha kutambua na kutoa huduma kwa watu wenye changamoto za msongo wa mawazo na sonona katika jamii husika ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, wanajamii 1,709 wamepimwa na 1,362 wamegundulika kuwa na sonona na wapo kwenye tiba.

Vilevile, elimu kuhusu ugonjwa wa kifafa ilitolewa kwa jamii kupitia maadhimisho ya Sikuya kifafa Duniani Pamoja na mkutano wa EpiNA na kufikia watu 150. Mafunzo kwa watoa huduma za afya kuhusu tiba na usimamizi wa wagonjwa wa kifafa yalitolewa kwa washiriki 22 pamoja na kutumia vyombo vya habari mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu kifafa na magonjwa ya afya ya akili kwa ujumla. Hali kadhalika elimu ya afya ya akili kuhusu usonji imetolewa katika kilele cha sikuya usonjiduniani ambapo watu 247 walifikiwa.

"Nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi na kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya kupima magonjwa ya afya ya akili hususan hali ya msongo wa mawazo na sonona inayoonekana kuongezeka ili kuepusha madhara zaidi kwani hali hii inatibika".

Huduma za Sikoseli na Himofilia

71. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kupanua huduma za uchunguzi na matibabu ya ugonjwa wa sikoseli kutoka hospitali ya taifa hadi katika ngazi ya mkoa. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, watoto 17,245 walipimwa. Kati yao 369 waligundulika kuwa na ugonjwa wasikoseli na 2,500 walibainika kuwa na vinasaba vya ugonjwa huo. Aidha, jumla ya wagonjwa 42,564 walihudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, elimu ya sikoseli ilitolewa kwa wananchizaidiya 29,000 wakiwemo vijana, walimu, viongozi wa dini, waandishi wa habari na makundi maalum kama vijana waliopo kambini, hatua iliyochangia kuongeza uelewa na kupunguza unyanyapaa. Pia, usimamizi shirikishi ulifanyika katika mkoa wa Mwanza na Tabora kwa ajili ya kuangalia upimaji wa watoto chini ya miaka mitano kuhusu ya ugonjwa wa sikoseli ambapo jumla ya vituo 25 vilitembelewa.

Afya ya Kinywa na Meno

72. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za afya za kinywa na meno kwa kuratibu ununuzi na usambazaji wa viti maalum vya matibabu ya kinywa na meno 26 na kufanya jumla ya viti maalum vya matibabu ya kinywa na meno kufikia 900. Aidha, Wizara imenunua mashine kubwa za mionzi (2D-OPG) saba (7) na mashine ndogo za mionzi (Periapical X-ray) tisa(9) na kufanya jumla ya mashine ndogo za mionzi kufikia 396. Mashine hizo zilipelekwa katika hospitali ya kanda ya Benjamin Mkapa, hospitali za rufaa za mikoa za Mawenzi na Amana, Hospitali za Halmashauri za Itigi, Dodoma Jiji, Sengerema na Msalala, Vituo vya Afya vya Ilazo, Ihumwa, Ilolangulu na Uhuru, Muriet, Magugu, Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga, Hospitali ya Wilaya ya Itilima na Nanyumbu.

73. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Wagonjwa 680,995 walihudhuria kwenye vituo vinavyotoa matibabu ya kinywa na meno. Wagonjwa 459,238 walikuwa na tatizo la kuoza meno, wagonjwa 68,474 walikuwa na tatizo la magonjwa ya fizi, wagonjwa 17,294 walikuwa na tatizo la jino gego kunasa kwenye mfupa, wagonjwa 17,035 waligundulika na uvimbe wa kinywa na meno, wagonjwa 175 waligundulika na

saratani ya kinywa na wagonjwa 118,779 waligundulika kuwa na matatizo mengine ya kinywa na meno.

Aidha, wagonjwa wagonjwa 172,494 284,691 walizibwa meno, waling'olewa meno, wagonjwa 35,829 walifanyiwa matibabu ya kusafishwa meno, wagonjwa 14,946 walifanyiwa upasuaji mdogo wa magonjwa ya kinywa na meno, wagonjwa 914 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa magonjwa ya kinywa na 172,121 walipatiwa matibabu mengine.

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa mafunzo ya afya ya kinywa na meno kwa watoa huduma za afya 1,289 ambapo kati yao, wauguzi 140, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,010 na tabibu meno 139 katika mikoa ya Morogoro, Kagera, Ruvuma na Mwanza.

"Nitumie fursa hii kuwajulisha waheshimiwa wabunge wenzangu pamoja na wananchi wote kuwa, huduma za kinywa na meno zimeboreshwa sana nchini. Hivyo niwaombe kuwahi mapema katika vituo vinavyotoa huduma za afya ili kupata huduma inayostahili kwani dawa ya jino SIYO kung'oa pekee".

Huduma za Macho

75. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za macho nchini kupitia kambi za huduma za macho na huduma za upasuaji katika mikoa 15 na kutoa elimu kwa umma. Jumla ya watu 51,940 walifanyiwa uchunguzi wa afya ya macho, kati yao watu 17,697 walifanyiwa upasuaji, 17,715 walipatiwa tiba dawa na 10,239 walipewa miwani na 6,289 walipatiwa huduma nyingine za macho. Aidha, huduma hizo zimechangia kupunguza mzigo wa upofu unaozuilika na matatizo ya kuona yanayorekebishika kwa miwani.

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilinunua kifaa maalum kwa ajili ya uchunguzi wa mapema wa saratani ya macho kwa watoto chini ya miaka mitano, hatua iliyoboresha uwezo wa uchunguzi na rufaa kwa watoto chini ya miaka mitano.

Aidha, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Macho Duniani kitaifa yaliyoambatana na kampeni za uelimishaji zilizofanyika kupitia hospitali, shule na kambi za macho na kufikia zaidiya watu milionimbili.

Huduma za Utengamao, Wazee na Tiba Shufaa.

76. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekamilisha orodha ya kitaifa ya msingi ya kiteknolojia saidizi. Wizara imekamilisha ujumuishwaji wa mfumo wa ukusanyaji takwimu za utengamao (Rehab HMIS) na viashiria 17 vya kufuatilia utoaji wa huduma za afya kwa wazee kwenye mifumo ya kieletroniki ya Afya-eHMIS na GoTHOMIS inayotumika kukusanyia takwimu kwenye hospitali za rufaa za Mikoa na vituo vya afya ngazi ya msingi.

Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za tiba shufaa nchini, ambapo watumishi nane (8), wafamasia wawili (2), wauguzi wawili (2), madaktari wawili (2) na maafisa ustawi wa jamii wawili (2) kutoka hospitali mbili (2) za rufaa za mikoa wamepata mafunzo ya msingi ya utoaji wa huduma za tiba shufaa.

77. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watalaam ili kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya afya kwa wazee ambapo jumla ya watalaam 80 katika vituo vya afya ngazi ya msingi wamepata mafunzo namna ya kutoa huduma za afya kwa wazee. Aidha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeongeza klabu za afya za wazee kutoka 32 hadi 263; Tanga (64); Mwanza (40); Morogoro (128); Kigoma (18) na Shinyanga (13).

78. Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kupima usikivu kwa watoto wachanga 2,112. Kati yao, watoto 350 sikio moja au yote mawili yalikuwa na changamoto ya kupoteza usikivu. Aidha, katika Siku ya Kimataifa ya Masikio na Usikivu mwaka 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wadau iliweza kuwafikia wananchi 8,500 na kutoa elimu kuhusu masikio na usikivu. Jumla ya mashine za kutibia masikio 23 zimenunuliwa na kusambazwa katika hospitali 23 za

mikoa za Tumbi, Mt. Meru, Manyara, Mawenzi, Morogoro, Amana, Mwananyamala, Dodoma, Songwe, Mbeya, Sumbawanga, Singida, Maweni, Katavi, Kitete, Songea, Njombe, Ligula, Sokoine, Bukoba, Tanga na Hospitali za Kanda za Chato na Mbeya.

Aidha, mashine 15 za kupima usikivu zimenunuliwa na kusambazwa katika hospitali za rufaa za mikoa za Ligula, Sokoine, Morogoro, Amana, Mwananyamala, Mt.Meru, Manyara, Mawenzi, Songwe, Mbeya, Sumbawanga, Njombe, Katavi, Kitete pamoja na hospitali ya kanda ya Chato. Vilevile, jumla ya watalaam 50 kutoka vituo vya afya ya msingi wamepata mafunzo namna ya kuhudumia watoto wachanga na watoto wadogo wenye maambukizi ya masikio kwa kutumia uwiano kwa njia ya masafa.

"Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza yanahitaji si tiba tu, bali kinga, mabadiliko ya mtindo wa maisha na uelewa wa pamoja kwa jamii. Serikali itaendelea kuwekeza katika afua za kinga na uchunguzi wa mapema katika kudhibiti ukuaji wa magonjwa yasiyoambukiza ili kuepuka gharama kubwa za matibabu kwa wananchi na Serikali".

Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza

Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono.

79. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango Jumuishi wa kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini, imeendelea kutoa huduma za tiba na matunzo kwamagonjwa ya VVU/UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono pamoja na kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi.

Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI

80. Mheshimiwa Spika, Takwimu zinazokusanywa kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa huduma za matunzo na matibabu kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) zinaonesha kuwa, hadi kufikia Machi 2026, watu 1,624,907 kati ya 1,700,000 wanaokadiriwa kuishi na maambukizi

ya VVU walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ikiwa ni sawa na asilimia 95.7 ya watu wanaokadiriwa kuishi na Virusi vya UKIMWI nchini (95 ya kwanza). Watu 1,609,078 kati ya waliopima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, hii ikiwa ni sawa na asilimia 94.7 (95 ya pili).

Aidha, jumla ya WAVIU 1,343,112 wanaotumia dawa za ARV walifanya vipimo vya kujua wingi wa Virusi vya UKIMWI, ambapo WAVIU 1,317,593 sawa na asilimia 98.1 walifubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (95 ya tatu). Jedwali Na 1 linaonesha ufafanuzi huo.

Jedwali Na. 1: Mafanikio Kuelekea Kufikisha Malengo ya 95-95-95

a.	**Kiashiria**	**Julai 2024 hadi Machi 2025**	**Julai 2025 hadi Machi 2026**	**Hali ya 95-95-95**
	Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi (People Living with HIV/AIDS -PLHIV)	1,700,000	1,700,000	**95 ya kwanza**
	Wanaotambua hali zao za maambukizi	1,530,227	1,624,907	
	Asilimia ya wanaotambua hali zao (on care)	**90**	**95.7**	
	Wenye maambukizi na wameanza dawa	1,500,212	1,609,078	**95 ya pili**
	Asilimia ya walioanza dawa (on ART)	**98**	**94.7**	
	Idadi ya WAVIU waliofanya vipimo (VL test)	874,944	1,343,112	**95 ya tatu**

	Idadi WAVIU ambao makali ya VVU yamefubazwa	858,272	1,317,593	
	Asilimia ya waliofubazwa makali (VL<1000)	**98**	**98.1**	

81. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa huduma kwa WAVIU zinasogezwa karibu na jamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeendelea kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya kina uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo vimeongezeka kutoka 7,994 hadi 8,203 sawa na asilimia 74.4 ya vituo 11,030 vyenye huduma ya utambuzi wa VVU. Lengo ni kufikia asilimia 95 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya utambuzi kwa WAVIU ifikapo mwaka 2030.

Huduma ya Dawa Kinga kwa Makundi yaliyo kwenye Mazingira Hatarishi

82. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa kinga kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa au kuambukiza VVU ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya watu 121,957 walipewa dawa kinga. Makundi lengwa ni wanaume na vijana wa kike na kiume walio katika hatari zaidi ya maambukizi ikijumuisha wachimbaji madini, madereva wa masafa marefu, wavuvi, wanaojidunga, vijana walio katika mazingira hatarishi na wanaojihusisha na biashara haramu ya ngono. Aidha, mikakati mahsusi imepangwa kutekelezwa katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ambayo ina kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU. Baadhi ya mikakati hiyo ni; kuhakikisha uimarishaji wa afua ya tohara kwa wanaume, utoaji wa elimu ya kinga na maambukizi kwa vijana balehe na wajawazito.

Kuzuia Maambukizi ya Magonjwa ya Ngono na VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto

83. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha wajawazito wanapimwa maambukizi ya VVU wanapohudhuria kliniki na hata baada ya kujifungua, lengo likiwa ni kuhakikisha mtoto aliyeko tumboni anakingwa dhidi ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, ikiwa mama atakuwa ameambukizwa. Huduma hizo huenda sambamba na kupima na kutibu maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini aina B kwa wajawazito ili kuwakinga watoto dhidi ya maambukizi hayo kabla ya kuzaliwa.

84. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wajawazito 2,218,640 walihudhuria kliniki na kati yao 2,080,819 walipimwa maambukizi ya VVU kwa mara ya kwanza wakati wa hudhurio la kliniki na wajawazito 11,445 sawa na asilimia 0.6 walibainika kuwa na maambukizi. Aidha, watoto 23,023 wenye umri wa miezi 18 kati ya Watoto 24,998 waliotarajiwa, walipimwa maambukizi ya VVU na kati yao 1,197 walithibitika kuwa na maambukizi. Aidha, jumla ya wajawazito 1,995,822 sawa na asilimia 90 ya waliohudhuria kliniki walifanyiwa kipimo cha kaswende. Kati yao wajawazito 8,684 sawa na asilimia 0.4 walibainika kuwa na maambukizi ya kaswende na 8,598 sawa na asilimia 99 walianzishiwa matibabu.

"Kwa takwimu hizo nichukue nafasi hii kuwasihi wananchi kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki mara wanapojigundua kuwa wajawazito na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata huduma stahiki za kinga dhidi ya magonjwa ya ngono na maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kupata matibabu mapema".

Huduma za Magonjwa ya Homa ya Ini

85. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za kinga na tiba dhidi ya homa ya ini aina ya B kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa jumuishi na kutolewakatika ngazi ya afya ya msingi na rufaa. Huduma za chanjo zilianza kutolewa kwa watoto wote waliozaliwa mwaka 2002, hivyo nguvu kubwa imekuwa ikielekezwa kwa wananchi waliozaliwa kabla ya mwaka 2002 kwa kufanyiwa uchunguzi na kutoa chanjo kwa wanaokidhi vigezo na matibabu kwa wanaobainika kuwa na maambukizi.

86. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi wa afya ni sehemu ya kundi lililopo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya homa ya ini ainaya B, Serikaliimendelelea kuhakikisha watumishi wa afya wanapata chanjo hiyo ili kuwakinga. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya watumishi wa afya 13,646 sawa na asilimia 39.7 wamekamilisha chanjo zote tatu za homa ya ini aina ya B.

"Nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kufanya uchunguzi na kupata chanjo ya homa ya ini aina ya B pamoja na kuwaomba waheshimiwa wabunge kujitokeza na kuwahamasisha wananchi kupima, kupata chanjo kwa wanaokidhi vigezo na matibabu kwa watakaobainika kuwa na maambukizi".

87. Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea maoni na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na kamati ya kudumu ya afya na masuala ya UKIMWI kuhusu mapambano dhidi ya homa ya ini. Katika eneo hili, Mheshimiwa Erick Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa amekuwa mstari wa mbele kwenye kuhamasisha utoaji wa chanjo na tiba dhidi ya ugonjwa huu na Wizara inatambua jitihada na mchango wake na tunamhakikishia ushirikiano katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini.

Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma

88. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikisha kuibua jumla ya visa 41,473 vya kifua kikuu, ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya lengo la kuibua visa 48,792 kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ambapo visa 125 vilikuwa vya kifua kikuu sugu. Aidha, Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Manyara na Tabora imechangia wagonjwa wa Kifua Kikuu kwa asilimia 50 ya wagonjwa wote walioibuliwa nchini. Mikoa ya Katavi, Rukwa, Unguja, Kigoma na Pemba ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya wagonjwa walioibuliwa. Kwa upande wa kifua kikuu sugu, Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Tabora, Mbeya, Mwanza, Arusha, Kagera na Morogoro ilichangia asilimia 63 ya wagonjwa na Mikoa ya Songwe, Singida, Pemba, Rukwa na Pwani hawakuwa na wagonjwa wa kifua kikuu sugu.

89. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuchukua hatua za dhati ili kuongeza kasi ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu nchini kwa mikoa ambayo imeonesha kiwango kidogo cha kuibua wagonjwa ikilinganishwa na malengo ya uibuaji wa wagonjwa uliowekwa katika mikoa hiyo. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na; kuongeza hamasa ya uelewa na uthubutu wa wananchi kuchunguzwa na kupimwa vimelea vya ugonjwa huo katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na jamii kwa kutumia huduma mkoba za kifua kikuu na kupitia kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

90. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na huduma mkoba za kliniki tembezi zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya kifua kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi ya kuambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wagonjwa 77 waliibuliwa kupitia huduma za mkoba za kliniki tembezi.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya visa 755 vya ukoma viliibuliwa nchini sawa na asilimia 95.3 ya lengo la kuibua wagonjwa 792. Mikoa iliyoibua visa vingi ni pamoja na Morogoro, Lindi, Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Kigoma na Geita. Mikoa ambayo haikuwa na visa vipya vya wagonjwa ni Arusha, Iringa, Manyara na Njombe. Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa ukoma kwa kushirikisha jamii na wadau katika kuibua visa vipya na kutoa matibabu kwa wakati.

Mapambano Dhidi ya Malaria

92. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kufanya ugawaji wa vyandarua kwa awamu kwenye kaya kupitia kampeni katika mikoa yenye maambukizi ya juu na ya kati. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imesambaza jumla ya vyandarua 4,567,179 vyenye viuatilifu ambapo vyandarua 1,236,294 vimesambazwa kwenye kaya 454,595 za halmashauri saba (7) za Mkoa wa Pwani (Chalinze DC, Kibaha DC, Kibiti DC, Kisarawe DC, Rufiji DC, Mafia DC, na Mkuranga DC) na vyandarua 3,330,885

vilisambazwa kwa wajawazito na watoto wa umri chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya kutolea huduma za afya kwenye halmashauri zote 184 nchini.

93. Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa jumla ya Shilingi bilioni 5.5 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 1.5 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa lita 125,000 za viuadudu vya kibaiolojia kutoka katika kiwanda cha Tanzania Biotech Product Limited (TBPL) kilichopo wilayani Kibaha mkoani Pwani na Shilingi bilioni 4 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa pampu 16,000 kwa ajili ya kuziwezesha halmashauri kunyunyizia viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ili kuua mbu waenezao malaria na magonjwa mengine yaenezwayo na mbu. Wizara imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya mikoa na halmashauri ili kuwajengea uwezo wataalam wa ngazi hizo katika kutekeleza afua ya unyunyiziaji wa viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ya mbu.

94. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo ya "Zero Malaria ifikapo 2030" yanafikiwa, Wizara imenunua jumla ya dozi 1,262,490 za dawa mseto (ALu), vitepe 15,015,250 vya kupimia malaria, vichupa 1,063,327 vya dawa ya sindano ya Artesunate, vyandarua 2,089,473, vidonge 1,460,700 vya SP na vidonge 26,600 vya primaquine. Usambazaji wa bidhaa hizo unaendelea kufanyika kulingana na mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya na kwa kuzingatia afua zilizokusudiwa katika maeneo mbalimbali. Katika kuboresha uagizaji wa bidhaa za malaria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imeendelea kufuatilia na kutatua changamoto za kimfumo na kuwawezeshawatoa huduma kufanya uagizaji wa bidhaa hizo kwa kuzingatia idadi halisi ya watumiaji wa bidhaa. Aidha, katika kipindi hiki Serikali imeagiza jumla ya dozi 2,470,260 za ALu zitakazotosheleza matumizi ya miezi 7 na vichupa 500,000 vitakavyotosheleza matumizi ya miezi 17.

95. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya utafiti wa kuangalia kiwango cha maambukizi ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano na wanafunzi wa shule za msingi wa miaka mitano (5) hadi 16. Utafiti huo umefanyika katika halmashauri zote 184 nchini ambapo, jumla ya watoto 66,801 wa shule za msingi na watoto 8,828 wa umri chini ya miaka mitano walipimwa malaria kwa

kutumia kipimo cha haraka cha malaria ili kubaini kiwango cha maambukizi na wale waliokutwa na maambukizi walipatiwa matibabu kwa kutumia dawa ya ALu. Malengo ya utafiti huo ni kupima hali ya utekelezaji wa afua za malaria katika jamii na kujipima kama tumeweza kushusha kiwango cha maambukizi ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano. Taarifa ya awali ya utafiti huo inaonesha kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 8.1 ya mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 5.5 mwaka 2025.

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kutekeleza afua za kutokomeza Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs) kama vile matende, mabusha, trakoma, usubi, kichocho, na minyoo ya tumbo. Jitihada hizo zinalenga kufikia lengo la kimataifa na kitaifa la kutokomeza magonjwa hayo ifikapo 2030 kupitia ugawaji wa kinga tiba huduma za upasuaji na uimarishaji wa mifumo ya kidijitali.

97. Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za kingatiba na tiba dhidi ya magonjwa hayo, Wizara imetekeleza afua za moja kwa moja kwa wananchi kama ifuatavyo: Wananchi wapatao 3,331,925 (sawa na asilimia 69 ya walengwa) katika halmashauri 25 wamefikiwa na huduma ya kingatiba dhidi ya ugonjwa usubi. Aidha, watoto wenye umri wa kwenda shule (miaka 5 – 14) 10,414,632 kati ya 11,916,055 sawa na asilimia 87.4 katika halmashauri 119 wamepatiwa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa minyoo. Vilevile, watoto 6,176,203 kati ya 6,832,084 sawa na asilimia 90.4 ya walengwa katika halmashauri 147 wamepatiwa kingatiba dhidi ya kichocho. Huduma za upasuaji zimetolewa kwa wagonjwa1,775 wa mabusha kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, na Mbeya. Wagonjwa 3,125 wa trakoma walifanyiwa upasuaji mdogo wa kusawazisha kope ili kuzuia upofu wa kudumu kwa wananchi hao kutoka Halmashauri za Nanyumbu, Nanyamba, Ngorongoro, Nachingwea, Ruangwa, Masasi DC, Masasi MC, Newala TC, Newala DC, Momba, Bagamoyo na Kibaha.

98. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ilifanya tathmini ya kiwango cha maambukizi kwa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa halmashauri za Njombe TC,Njombe DC, Mufindi, na Morogoro DC maambukizi ya ugonjwa wa usubi yameshuka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2018 hadi asilimia 1.6 kwa mwaka 2026, isipokuwa halmashauri ya Morogoro DC ambapo kiwango cha maambukizi kimeongezeka kutoka asilimia 0.6 mwaka 2013 hadi asilimia 17.1 mwaka 2026. Kwa ugonjwa wa matende na mabusha, tathmini iliyofanyika katika halmashauri za Lindi MC, Mtwara Mikindani, na Mtama inaonesha kupungua kwa maambukizimapya kutoka asilimia 7.5 mwaka 2023 hadi asilimia 0.2 Machi 2026.

99. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo, tathmini katika halmashauri za Mbeya CC, Rungwe, Songwe, Ileje, na Sumbawanga inaonesha maambukizi ya minyoo yamepungua kutoka asilimia 50 kwa mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 5 Machi 2026; kadhalika maambukizi ya kichocho yameshuka kwenye halmashauri tajwa kutoka asilimia 50.3 hadi asilimia 10 isipokuwa halmashauri ya Sumbawanga DC ambapo maambukizi yamesalia kuwa asilimia 50. Kwa ugonjwa wa trakoma, tathmini iliyofanyika katika halmashauri za Kiteto, Simanjiro, Mpwapwa, na Kalambo ilionesha kupungua kwa maambukizi kutoka asilimia 14.6 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 5.6 Machi 2026, isipokuwa katika halmashauri ya Kiteto ambapo kiwango cha maambukizi ni asilimia 9.9.

Utoaji wa Huduma za Kinga

100. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma bora za kinga kwa kuhakikisha huduma za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana muda wote kulingana na mahitaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, umri chini ya miaka mitano, wajawazito, wasichana wenye umri wa miaka tisa (9), na makundi mengine yaliyo katika hatari ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati.

101. Mheshimiwa Spika, Wizaraimeendelea na uratibuwa ununuzina usambazajiwa chanjo za watoto kwa magonjwa 13 yanayozuilika kwa chanjo. Chanjo hizo ni: Rota kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara dozi 8,910,655; PCV - 13 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimonia dozi 8,532,600; chanjo za Surua Rubella 8,295,000; bOPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio) dozi 19,204,560; Pentavalenti kwa ajili ya kukinga Donda Koo Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza dozi 11,943,100; Td kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Pepo Punda dozi 5,600,000; BCG za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu dozi 12,700,000; HPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi dozi 588,740 na IPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio) dozi 6,838,400. Aidha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kulikuwa na jumla ya dozi za chanjo 17,239,640 nchi nzima katika maghala ya kuhifadhiachanjo na zinatosheleza mahitaji ya nchi kwa muda wa miezi mitatu (3) mpaka sita (6).

102. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilitoa chanjo ya Penta -3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo nchini kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja kwa watoto 2,361,701 sawa na asilimia 94.3 ya lengo la watoto 2,504,130. Aidha, katika kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka tisa (9) hadi 14 dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, wasichana 866,299 wamepatiwa chanjo ya HPV sawa na asilimia 98 ya walengwa.

103. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo, Wizara imenunua Boti saba (7) ambazo zimepelekwa katika maeneo ya Kigoma DC (1), Kibiti (1), Nkasi (1), Ukerewe (1), Muleba (1) na Zanzibar (2). Vilevile, Wizara imenunua Majokofu 237 ya kutunzia chanjo na vifaa 4,363 (RTM) na Fridge Tags 10,000 kwa ajili ya kufuatilia jotoridi la jokofu la chanjo kwa matumizi ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Huduma za Lishe

104. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha afua za lishe nchini, Wizara imeratibu utoaji wa matone ya vitamini A kwa watoto 9,115,501 walio chini ya umri wa miaka mitano sawa na asilimia

96.9 ya watoto 9,408,384 waliolengwa kupatiwa huduma hiyo. Aidha, Tanzania iliungana na mataifa mengine kuadhimisha wiki ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama duniani ambayo hufanyika kila mwaka kuanzia tarehe 1 hadi 7 Agosti na kaulimbiu ilikuwa "Thamini unyonyeshaji, weka mazingira wezeshi kwa mama na mtoto". Kupitia maadhimisho hayo, watoa huduma za afya 4,027 kutoka mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Dodoma, Katavi, Dar es Salaam, Manyara, Njombe, Rukwa, Songwe na Kigoma walijengewa uwezo wa kutoa huduma za lishe kwa makundi mbalimbali hususan kwa kina mama na watoto wachanga, watoto chini ya umri ya miaka mitano na vijana balehe.

105. Mheshimiwa Spika, Wizaraimeendelea na utekelezaji wa kanuni za uongezaji wa virutubishi kwenye chakula ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 imenunua vifaa (I-check iron Machine) 12 vya kufuatilia kiwango vya madini chuma kwenye unga wa ngano na mahindi ambavyo vimesambazwa katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Geita, Tabora, Arusha na Tanga.

106. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu ulaji unaofaa kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo; maadhimisho ya Siku ya Lishe Kitaifa yaliyofanyika tarehe 21 Novemba 2025 mkoani Ruvuma. Wizara ilitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wadaumbalimbali kwa kauli mbiu isemayo: "Afya ni mtaji wako, Zingatia Unachokula." Katika maadhimisho hayo shughuli mbalimbali zilifanyika katika halmashauri zote ikiwemo uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu ulaji unaofaa. Jumla ya wananchi 5,650,002 walifikiwa, na vipindi 970 vya elimu ya lishe vilitolewa kupitia redio,luninga na mitandao ya kijamii. Jumla ya mabango 3,624 ya hamasa ya lishe yaliwekwa shuleni na vyuoni ili kuongeza uelewa. Aidha, jumla ya miche 118,546 ya matunda ilipandwa kama hatua ya kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi.

Taasisi ya Chakula na Lishe

107. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imekamilisha utafiti unaobainisha gharama za athari za utapiamlo hasa lishe pungufu hapa nchini. Utafiti huo

ulianzishwa na Umoja wa Afrika kupitia mpango wa "The Cost of Hunger Study in Africa – COHA" na umeshafanyika pia katika nchi nyingi za Afrika. Utafiti huo umebainisha kuwa nchi yetu inapoteza hadi asilimia 2.03 ya pato ghafi la taifa (GDP) ambayo ni sawa na takribani Shilingi trilioni 3.47 (Dola za Marekani bilioni 1.5) kwa mwaka. Kiwango hiki kimetokana na uchambuzi wa athari za utapiamlo katika sekta ya afya, elimu na uzalishaji mali. Kiwango hiki ni kikwazo kwa taifa kuweza kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya pato ghafi la Dola za Marekani trilioni 1. Mikakati madhubuti ya kukabiliana na lishe duni inahitaji kuendelea kutekelezwa ili kupunguza/kuondoa upotevu huu kwa kujenga raslimali watu ambayo itashiriki kikamilifu katika kazi za ujenzi wa taifa na kuleta tija.

108. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa damu kwa vijana balehe, Taasisi imetengeneza asusa (snack bar) kwa kutumia maharage yaliyoongezwa virutubishi kibaiolojia (bio fortified beans). Bidhaa hii inatarajiwa kuzalishwa kwa wingi na kampuni ya BIVAC inayoongozwa na mjasiriamali Mtanzania kutoka Arusha kwa kushirikiana na taasisi, lengo likiwa ni kuzalisha tani 200,000 ili kuwafikia vijana balehe 2,000,000 kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Sambamba na hili, taasisi imetengeneza pia unga mchanganyiko kwa lengo la kukabiliana na tatizo la utapiamlo wa kadiri. Unga huu umethibitishwa kisayansi kuwa na uwezo wa kupunguza utapimlo wa kadiri kwa asilimia 66 na upungufu wa damu kwa asilimia 59 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

109. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maabara ya chakula, taasisi imefanya vipimo 18,000 kupitia maabara yake kwenye sampuli za damu, mkojo na vyakula zilizopokelewa kutoka katika nchi za Kenya, Ethiopia, Malawi, katika tafiti mbalimbali za lishe zinazoendelea nchini Tanzania kwa kushirikiana na taasisi zingine kama vile IITA, NI, Technoserve, GAIN na TARI. Maabara imeweza pia kufanya uchambuzi wa viashiria vya madini chuma, vitamin A, vitamin B12, madini joto na viashiria vya maambukizi ya magonjwa katika sampuli za utafiti wa Kitaifa wa Demorgraphic Health Survey (DHS). Idadi hii ya vipimo ni nyongeza ya asilimia 80 ya uchambuzi uliopangwa kufanyika katika kipindi hiki. Aidha, idadi hii ya watumiaji inapelekea nchi ambazo zinapata huduma

katika Maabara ya Taasisi kufikia 18 kutoka katika ukanda wa Afrika, Mashariki ya Kati, na Ulaya Mashariki. Katika kipindi hiki pia, maabara imeweza kuongeza idadi ya viashiria vinavyoweza kufanyiwa uchambuzi kutoka 9 hadi 12 pamoja na kununua mashine mpya ya kisasa yenye uwezo wa kupima vinasaba vinavyosababisha matatizo ya lishe.

*"**Taifa letu haliwezi kuwa na askari imara au wakulima wenye nguvu kama wanawake hawajui thamani ya chakula wanachopika. Jiko la mwanamke ndilo kiwanda cha kwanza cha kutengeneza afya ya watanzania". Bibi Titi Mohamed***

Afya Mazingira na Usafi

110. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za usafiwa mazingirana usafi binafsi kwa kuhamasisha na kusimamia ujenzi na matumizi ya vyoo bora katika ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya umma kwa lengo la kudhibiti magonjwa ya mlipuko hususan kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya kaya zilizojenga vyoo bora zimeongezeka kutoka 8,504,503 hadi 9,165,833 sawa na ongezeko la kaya 661,330 na kufanya nchi kuwa na asilimia 78.4 ya kaya zenye vyoo bora. Vilevile, kaya zenye vifaa vya maji tiririka na sabuni vya kunawia mikono zimeongezeka kutoka asilimia 45.6 hadi 47.6 katika kipindi hicho. Mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa kampeni ya Taifa ya Mtu ni Afya kwa kuzingatia afua saba (7) ikiwemo ujenzi na matumizi ya vyoo bora na unawaji wa mikono, pamoja na kuimarisha uhamasishaji kupitia mbinu ya mabadiliko ya tabia na ushiriki wa vyombo vya habari.

111. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhuisha miongozo inayolenga kuendelea kuimarisha usimamizi wa afua za usafi nchini ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa ikiwemo Mwongozo wa Ujenzi wa Vyoo Bora ngazi ya Kaya yaani "The National Guideline for Household Sanitation Options & Catalogue on Sanitation Options" na Mwongozo wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wakati wa majanga "National Guidelines on WASH During Emergency". Miongozo hii inalenga kutoa maelekezo kwa wataalam katika kusimamia na kuwezesha ujenzi wa aina

mbalimbali za vyoo bora ngazi ya kaya kwa usahihi. Aidha, Mwongozo wa WASH During Emergency unatoa maelezo ya hatua sahihi za kufuata wakati wa majanga.

112. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OWM TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya huduma endelevu za maji na usafi wa Mazingira kwa Sekta ya Afya inayotekelezwa katika Halmashauri 137 za Mikoa 25 ya Tanzania Bara. Programu hii inahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji, udhibiti wa taka hatarishi, ujenziwa vyoobora,vifaavya kunawia mikono na maboresho ya vyumba vya kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya, ambapo kwa awamu ya kwanza (2019 - 2025) jumla ya vituo 3,483 vimenufaika, ikiwa ni ongezeko la vituo 847 zaidi ya lengo la vituo 2,636.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ili kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa malengo ya kitaifa ya kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuimarisha utayari wa pamoja katika ngazi zote. Aidha, Wizara ilikamilisha uandaaji wa mchango wa taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa Sekta ya Afya inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Mpango wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya Afya wa mwaka 2018 - 2023, kwa lengo la kujumuisha masuala mapya ya kimkakati ya kukabiliana na athari za afya zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Mapitio hayo yamezingatia tathmini ya athari za kiafya zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi hususan kuongezeka kwa magonjwa ya milipuko. Tathmini hiyo imesaidia kuboresha nyenzo za kutathmini ubora wa huduma za afya ili kujumuisha viashiria vya ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi.

114. Mheshimiwa Spika, katika udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, Wizara ilitekeleza afua mbalimbali za udhibiti wa mazingira na taka. Wizara, ilikagua maeneo 145,566 yenye viashiria vya kelele na kubaini maeneo 41,456 kuwa na kelele na kati ya maeneo hayo, 4,632 yalibainika kuzidi kiwango kinachokubalika cha decibel 85 cha kelele. Vilevile, malalamiko 3,146 ya kelele yalipokelewa na kushughulikiwa, na hatua za kisheria zilichukuliwa

ikiwemo tozo ya faini na mashitaka kwa malalamiko 568. Aidha, katika udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya, jumla ya kilo 1,873,824 za taka ziliripotiwa kuzalishwa katika vituo vya kutolea huduma, ikiwemo taka hatarishi na zisizo hatarishi, hali inayoendelea kuhitaji uimarishaji wa mifumo ya usimamizi wa taka. Katika kutekeleza hili, jumla ya watumishi 120 wanaosimamia masuala ya afya mazingira kutoka katika Hospitali za Rufaa za Mikoa yote 26 na vituo 80 vya kutolea huduma ngazi ya msingi walipatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji shughuli za udhibiti taka zitokanazo na huduma za afya na matumizi sahihi ya viteketezi taka.

"Bila mazingira bora na afya imara, binadamu hawezi kuwa na tija" Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akizindua kampeni ya Kitaifa ya Elimu ya Afya kwa umma mwaka 1973.

Huduma za Afya na Usalama Kazini

115. Mheshimiwa Spika, Huduma za Afya na Usalama Kazini zina lengo la kuwajengea watumishi uwezo wa kutambua na kujikinga dhidi ya hatari za kiafya na kiusalama katika mazingira ya kazi, jambo linalochangia kuimarisha ufanisi wao na kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Kupitia huduma hizo, watumishi huwezeshwa kufanya kazi katika mazingira salama, bora na yenye afya.

116. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha mwongozo wa kitaifa wa kulinda afya, usalama na utu wa wafanyakazi wa usafi wa mazingira na kuandaa nyenzo za mafunzo. Hatua inayoendelea sasa ni kusambaza na kutoa mafunzo ya mwongozo katika mamlaka mbalimbali nchini.

117. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza mpango wa kimataifa wa "Beat the Heat", unaolenga kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya joto kali yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Tanzania imekuwa nchiya kwanza kutekeleza mpango huo kwa ngazi ya kitaifa kati ya nchi tatu wenyeji katika mashindano ya AFCON 2027. Moja ya utekelezaji wa afua ya mpango huo ni pamoja na

tathmini ya awali ya hatari na utayari wa kukabiliana na joto kali, ikiwemo tathmini ya miundombinu ya michezo iliyofanyika katika uwanja wa Benjamin Mkapa wakati wa mashindano ya CHAN mwezi Agosti 2025. Maeneo yenye hatari yalibainishwa na mapendekezo yaliwasilishwa katika kamati ya maandalizi ya AFCON 2027 kwa hatua za maboresho.

Elimu ya Afya Kwa Umma na Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

118. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kutoa elimu ya afya kwa umma na hamasa kwa jamii kuhusu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yanayoambukiza, na yale yasiyoambukiza hususan katika lishe bora, ulaji unaofaa, afya ya uzazi, mama na mtoto na wazee. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilitayarisha na kusambaza vielelezo mbalimbali vya elimu ya afya ambapo jumla ya video 518, vipeperushi vya mtandaoni 987, matangazo ya redio 53, matangazo ya televisheni 26, vipindi vya redio 512, na vipindi vya televisheni 172 vimerushwa kuwafikia wananchi. Vilevile, elimu ya afya kuhusu kinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko ilitolewa kwa kufanya uhamasishaji kupitia magari ya matangazo na vipaza sauti katika maeneo yenye mikusanyiko ambapo jumla ya kata 108, na maeneo ya mikusanyiko 3,900 yalifikiwa. Juhudi hizo kupitia magari ya matangazo na huduma ya nyumba kwa nyumba inayofanywa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii zimewezesha kuwafikia wananchi 7,570,000.

119. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya utoaji elimu ya msingi katika tiba, kinga, lishe na ustawi wa jamii ngazi ya jamii inaimarika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ambapo kupitia mpango huo jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,832 walipata mafunzo ya miezi 6 na kuwezeshwa vitendea kazi ikiwemo vishikwambikutoka katika mikoa 12 ambayo ni Pwani, Mbeya, Kagera, Njombe, Songwe, Lindi, Geita, Kigoma, Tabora, Dodoma, Tanga na Ruvuma.Hadi sasa jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii waliohitimu mafunzo hayo na kurejea kwenye jamii waliyotoka na kuanza kutekeleza majukumu yao ni 9,870 kutoka halmashauri 25.

120. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuboresha huduma za afya, Wizara imeendelea kuboresha kituo cha mawasiliano ya afya kwa umma (Afya Call Center) kwa kuanzisha jukwaa la "Ongea na Waziri". Kituo hicho kinatoa huduma za elimu, ushauri na mwongozo wa afya kwa njia ya simu namba 199 bila malipo kama hatua ya kimkakati inayotafsiri dhamira ya Serikali kwa vitendo na kuifanya Sekta ya Afya kuwa karibu na wananchi kwa kupokea maoni, pongezi, kusikiliza kero, malalamiko na kutatua kwa wakati. Katika kipindi hiki, jumla ya wananchi 4,269,045 walipiga simu na kuhudumiwa. Miongoni mwa masuala yaliyoulizwa kwa wingi ni Bima ya Afya asilimia 31, magonjwa ya mlipuko asilimia 21, magonjwa yasiyoambukiza asilimia 11, magonjwa ya kuambukiza asilimia 11 na afya ya akili asilimia 10. Kituo hiki kimeiwezeshaWizara kupata tuzo ya umahiri katika utoaji wa huduma za afya kidijitali iliyotolewa mwezi Agosti, 2025 katika kongamano la East Africa Youth Business and Investment Expo Zanzibar. Vilevile, Wizara imetumia fursa ya majukwaa mbalimbali ya kidijitali ambapo jukwaa la "Tukutane TikTok Live", limeanzishwa na kuwafikia wananchi zaidi ya 100,000 kupitia vipindi 39 vilivyoandaliwa.

121. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, Serikali kupitia Wizara ya Afya imezindua kampeni maalum na endelevu ijulikanayo kama **"Zijue Namba Zako."** Kampeni hiyo niliyoizindua mwezi Mei 2026 mkoani Mwanza, ina lengo la kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii na kuwapa fursa ya kufanya uchunguzi wa afya ili kubaini hali ya magonjwa ya shinikizo la juu la damu, kisukari, ongezeko la mafuta mwilini na uzito uliokithiri. Itawawezesha Aidha, wananchi kampeni hiyo kuchukua hatua stahiki mapema ikiwa ni pamoja na kupata matibabu kwa wale watakaobainika kuwa na magonjwa yasiyoakuambukiza au kuchukua hatua za kinga kwa wale ambao hawatakuwa na magonjwa hayo kwa kuzingatia ulaji unaofaa, kufanya mazoezi, kujiepusha na tabiabwete, kuepuka matumizi ya vilevi kama vile pombe na tumbaku.

122. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa elimu na hamasa katika masuala mbalimbali ya afya na lishe katika shule za msingi 4,800 na kuwafikia wanafunzi 279,000. Aidha, moduli za kufundishia walimu

kuhusu afya na lishe zimeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi ya Elimu Tanzania, na kuwekwa katika mfumo wa kidijitali ili kuwezesha matumizi kwa walimu. Hii itasaidia kuimarisha uelewa kwa walimu kuhusu afya na lishe na kutoa elimu kwa wanafunzi kwa usahihi hivyo kusaidia kudumisha nakuboresha afya ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla.

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

123. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1979 ikiwa na jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali kutoka katikaTaasisi za tafiti ndani na nje ya nchi, wanataaluma kutokakatika vyuo vikuu na watu wengine wenye nia ya kufanyautafiti katika eneo la afya. Taasisi kupitia Medical Research Coordination Committee imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yaleyanayokidhi vigezo hupatiwa kibali kwaajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Taasisi ilitoa vibali 513kati ya maombi 600 yaliyowasilishwa sawa na asilimia 86.

124. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utafiti, Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazolenga magonjwa ya kuambukiza yanayojitokeza (emerging and reemerging diseases) na magonjwa yasiyoambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya, kuelewa viashiria vya kijamii na mazingira vya afya, tiba asili na tafiti mtambuka za mabadiliko ya tabianchi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imetekeleza miradi ya tafiti 119 kati ya 150 iliyopangwa kwa mwaka 2025/2026 ambayo ni sawa na asilimia 79.3.

Huduma za Dharura na Majanga

125. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa

magonjwa ya mlipuko kupitia matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa Electronic Infectious Disease Surveillance and Response (eIDSR), ambao unawezesha ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa kwa wakati ili kuchukua hatua za haraka za kudhibiti kusambaa kwa magonjwa. Tangu tarehe 25 Februari, 2026 Wizara imefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu na jitihada za kuzuia mlipuko mwingine zinaendelea. Aidha, katika kipindi hicho visa 153 vya Surua katika mikoa 14 na visa 253 vya Mpox katika mikoa 18 viliripotiwa bila vifo.

126. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha kituo maalum cha kisasa cha kitaifa kilichopo katika jengo la Wizara ya Afya (Public Health Emergency Operations Center-PHEOC), ambacho kinaratibu taarifa mbalimbali za matukio ya dharura za afya na tetesi za magonjwa zinazoibuliwa katika jamii, vituo vinavyofuatilia afya mipakani na vituo vya kutoa huduma za afya nchini. Kituo hiki kimeboresha uratibu wa vituo vingine kama hivi vilivyoko ndani ya mikoa 20 nchini vinavyosaidia kuchakata taarifa hizo na kuchukua hatua na kutekeleza afua za kujilinda dhidi ya magonjwa ya mlipuko au majanga pamoja na kujiandaa, kukabiliana na kudhibiti milipuko hiyo endapo itatokea. Wizara inaendelea kuboresha uendeshaji wa vituo hivyo kwa kuwajengea uwezo wasimamizi wote kwa kupitia dhana ya afya moja kwa kushirikiana na sekta zingine.

127. Mheshimiwa Spika, Wizara imejenga uwezo wa rasilimali watu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 548 katika Halmashauri 11 za mikoa ya Katavi na Ruvuma iliyo katika hatari zaidi ya kupata magonjwa ya mlipuko. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha utambuzi, utoaji wa taarifa na udhibiti wa magonjwa hayo. Vilevile, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 5,070 katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Geita na Ruvuma walipatiwa mafunzo ya kutambua na kuripoti tetesi za magonjwa kwa kutumia simu za mkononi.

128. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya usimamizi shirikishi kuhusu ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za tetesi za magonjwa na matukio yenye athari za kiafya ya jamii kwa kutumia mfumo wa kidigitali wa kutoa taarifa za matukio ili waweze kutoa taarifa za tetesi za magonjwa kwa wakati. Aidha, Wizara imefanya mafunzo

kwa timu za utayari kwa wataalam 195 kutoka katika mikoa saba (7) ya kimkakati ambayo ni Kigoma, Katavi, Songwe, Dodoma, Kagera, Dar es Salaam na Mwanza. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa namna ya kushiriki kikamilifu katika kushughulikia dharura na kuibua matukio katika jamii kwa kushirikiana na watoa huduma ngazi ya jamii pamoja na wananchi.

129. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza afua za udhibiti wa magonjwaya mlipuko ikiwemo Mpox, Ebola na Homa ya Manjano katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu kwa kufanya uchunguzi wa awali wa afya kwa wasafiri wanaoingia na kutoka nchini. Jumla ya wasafiri 10,829,772 walifanyiwa uchunguzi, wakiwemo wasafiri wa kimataifa 2,840,876 na wasafiri wa ndani 7,988,896. Kati yao, wasafiri 233 walihisiwa kuwa na dalili za magonjwa ya mlipuko na kupelekwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi zaidi.

130. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo ya homa ya manjano kwa wasafiri wa kimataifa, ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya wasafiri 17,734 walipatiwa chanjo hiyo. Ili kuboresha utoaji wa huduma hizo, magari manne (4), pikipiki 10, majokofu 20 na vibebea chanjo 20 vilinunuliwa na kusambazwa katika ofisi za Afya Mipakani. Aidha, ofisi mpya tatu (3) za afya mipakanizilianzishwa katika bandari ya Wampembe na viwanja vya ndege vya Iringa na Tabora na watumishi wapya 56 waliajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi.

131. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya tathmini ya vihatarishi vya matukio ya dharura na kuandaa kalenda maalum ya dharura za afya na milipuko inayoweza kutokea kwa kipindi cha mwaka 2025 -2027 kwa ngazi ya taifa na katika baadhi ya mikoa ya Kagera, Dodoma na Tanga iliyopewa kipaumbele. Kalenda hiyo inatumika kupanga mipango na kujiandaa kuzuia na kukabiliana na dharura za afya. Utambuzi wa vihatarishi vya matukio ya dharura katika mkoa husika utawezesha kujiandaa na kukabiliana na hatari ya matukio husika yasitokee na endapo yakitokea yasilete madhara makubwa katika jamii.

132. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya tathmini ya utayari wa mikoa 11 ya Kigoma, Mwanza, Dar es Salam, Tanga, Ruvuma, Songwe, Katavi, Arusha, Kilimanjaro, Tabora na Rukwa iliyo katika hatari kubwa ya kupata mlipuko wa Ebola na Marburg. Lengo ni kuangalia utayari wa timu za maafa na dharura pamoja na vituo vya dharura na maafa kwa ngazi za mikoa na kuwajengea uwezo wa namna ya kujiandaa kukabiliana na Ebola na Marburg. Aidha, katika kukabiliana na shambulio la ugonjwa wa Ebola na Marburg ulioripotiwa nchini Kongo mwezi Agosti 2025, Wizara iliandaa mpango kazi na mwongozo wa kukabiliana na Ebola na Marburg na kufanikiwa kuzuia ugonjwa huo kuingia nchini.

133. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya mafunzo kwa vitendo na usimamizi shirikishi katika utoaji wa huduma za tiba za dharura na wagonjwa mahututi kwa mikoa 12 ya Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Manyara, Arusha, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Simiyu Mbeya na Mara katika idara za dharura zaidi ya 125 zilizojengwa katika ngazi ya msingi (86) na ngazi ya rufaa (39). Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watoa huduma kuhusu namna bora ya kuhudumia wagonjwa wa dharura pindi wafikapo katika vituo vya kutolea huduma.

134. Mheshimiwa Spika, Wizara imejenga vituo maalum na kuweka vifaa vya kisasa vya mafunzo ya huduma za dharura kwa vitendo vyenye thamani ya Shilingi 3,059,979,959 katika hospitali za kanda za Bugando na Mbeya, na kufanya idadi kuongezeka kutoka vituo vinne (4) hadi vituo sita (6) katika hospitali za Kanda nchini ambazo zinasaidia sana kuongeza ujuzi wa watoa huduma na kuwawezesha kutoa huduma bora katika maeneo ya wodi za wagonjwa mahututi, idara za dharura, wodi za uangalizi maalum na wodi za uangalizi maalumkwa watoto. Vituo vingine vimejengwa katika hospitali ya Benjamin Mkapa, hospitali ya taifa Muhimbili Upanga na Mloganzila na hospitali ya kanda ya kaskazini KCMC. Vituo hivyo pia vinatumika kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza kwa makundi maalum ikiwemo jeshi la polisi, jeshi la zimamoto na uokoaji na madereva ili kusaidia katika kutoa huduma kwa majeruhi wakati wa ajali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya watu 7,396 wamepata mafunzo ya huduma ya tiba ya dharura na huduma ya kwanza katika mikoa mbalimbali nchini.

135. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma za magari ya kubebea wagonjwa nchini, Wizara imefanya tathmini katika Mikoa 11 ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Lindi, Mtwara, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma na Manyara kwa lengo la kuangalia ubora wa magari hayo ili yenye mapungufu kuandaliwa mpango wa maboresho. Jumla ya magari 80 kati ya 473 sawa na asilimia 17 ya magari yaliyofanyiwa tathmini hayakuwa katika hali nzuri ya kutoa huduma ambapo mkoa wa Lindi uliongoza kwa kuwa na asilimia 33ya magari yakubebea wagonjwa yasiyo na hali ya kuridhisha. Hivyo, Serikali inaendelea kuelekeza vituo vya kutolea huduma kote nchini kuimarisha utunzaji wa magari hayo na kuyafanyia matengenezo kinga, kutoa mafunzo kwa madereva na watoa huduma wakati wa usafiri wa dharura.

"Mheshimiwa Spika, nasisitiza kwamba uwekezaji katika kinga na utayari dhidi ya dharura na majanga ni nafuu kuliko gharama itakayotumika wakati wa kupambana na dharura au majanga yanapotokea. Hivyo, Serikali itaendelea kuwekeza katika kujikinga na kuimarisha utayari katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko yanayovuka mipaka".

Utoaji wa Huduma za Tiba

Miundombinu na Huduma kwa Wagonjwa

136. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya nchini, Wizara imeendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma mbalimbali za tiba. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 12,846 hadi 13,683 sawa na ongezeko la vituo 837. Aidha, vituo vinavyomilikiwa na Sekta binafsi ni 4,368 sawa na asilimia 32, mashirikayadini1,092 sawa na asilimia8 na Serikali ni 8,223 sawa na asilimia 60. Kati ya Vituo vinavyomilikiwa na Serikali hospitali ni 248, vituo vya afya 1,042, zahanati 6,722, na vituo vingine 211. Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya nchini limewezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi ambapo wastani wa asilimia 85 wanapata huduma za afya ndani ya kilometa tano (5) na hivyo kupunguza changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Utoaji wa Huduma za Tiba kwa Wagonjwa

137. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa wananchi katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vitanda vimeongezeka kutoka 153,683 hadi kufikia vitanda 156,932. Hivyo kufanya uwiano wa vitanda 2.3 kwa kila watu 1,000 ukilinganisha na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaoelekeza kuwa na uwiano wa vitanda 2.5 kwa kila watu 1,000. Aidha, kati ya vitanda 156,932 vitanda 65,938 vipo katika ngazi ya Hospitali, 41,491 vipo katika Vituo vya Afya, 46,282 vipo katika Zahanati na vitanda 3,221 vinapatikana ngazi ya kliniki, kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2 hapa chini.

Jedwali Na.2 Mchanganuo wa Idadi ya Vitanda.

Vituo	Vinavyohitajika	Vilivyopo wodini	Vitanda vya kujifungu lia	Vitanda vya uchunguzi	Jumla ya Vitanda
Hospitali	74,654	58,589	2,019	5,330	65,938
Vituo vya Afya	42,136	32,261	3,766	5,456	41,491
Zahanati	43,531	23,506	8,986	13,790	46,282
Kliniki	3,329	1,534	189	1,498	3,221
Jumla	163,650	115,890	14,960	26,074	156,932

138. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi, ambapo jumla ya wagonjwa 36,996,862 walihudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kati yao, wagonjwa wa nje walikuwa 35,260,883 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,735,979. Aidha, wagonjwa 6,736,126 sawa naasilimia 18 walipata huduma katika hospitali za rufaa ngazi ya mkoa, kanda, maalum na taifa na wagonjwa 30,260,736 sawa na asilimia 82 walipata huduma katika ngazi ya msingi.

Jedwali Na.3: Idadi ya Wagonjwa waliohudhuria katika matibabu ya Wagonjwa wa nje (OPD) na Wagonjwa wa kulazwa (IPD)

katika Vituo vya kutolea huduma kwa kipindi Julai 2025 hadi Machi 2026.

AINA YA KITUO	Jumla OPD	%	Jumla IPD	%	Jumla Kuu	%
Hospitali ngazi ya Taifa, Hospitali Maalum, Kanda	1,989,698	5.6%	194,986	11.2%	2,184,684	5.9%
Hospitali ngazi ya za Rufaa za Mikoa	4,059,150	11.5%	492,292	28.4%	4,551,442	12.3%
Hospitali ngazi ya Halmashauri	5,585,976	15.8%	551,869	31.8%	6,137,845	16.6%
Vituo vya Afya	7,573,559	21.5%	474,674	27.3	8,048,233	21.8%
Zahanati	14,577,396	41.3%	15,158	0.9%	14,592,554	39.4%
Kliniki	1,418,370	4.0%	1,251	0.1%	1,419,621	3.8%
Maternity and Nursing Home	34,770	0.1%	-	0.0%	34,770	0.1%
Nyinginezo	21,964	0.1%	5,749	0.3%	27,713	0.1%
JUMLA	**35,260,883**		**1,735,979**		**36,996,862**	

Magonjwa Yaliyoongoza Kuwaathiri Wananchi – Wagonjwa wa Nje

139. Mheshimiwa Spika, Magonjwa yaliyoongoza katika kuwaathiri zaidi wananchi na kuwasababishia kwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu kwa wagonjwa wa nje chini ya miaka mitano (5) ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 36.8, kuharisha asilimia 8.2, malaria ni asilimia 7.2 na maambukizi katika njia ya mkojo ni asilimia 6.2. Katika kipindi hicho

	WAGONJWA WA NJE - CHINI YA MIAKA MITANO			WAGONJWA WA NJE - ZAIDI YA MIAKA MITANO		
NA	**AINA YA UGONJWA**	**IDADI**	**%**	**AINA YA UGONJWA**	**IDADI**	**%**

1	Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	4,465,725	36.8	Maambukizi katika mfumo wa hewa	3,465,266	16.2
2	Kuharisha pasipo kupungukiwa maji	993,626	8.2	Maambukizi katika njia ya mkojo	3,296,017	15.4
3	Malaria(BS +Ve, mRDT +Ve & Clinical)	870,330	7.2	Shinikizo la Juu la damu	1,519,187	7.1
4	Maambukizi katika Njia ya Mkojo	756,955	6.2	Malaria(BS+Ve, mRDT+Ve & Clinical)	1,032,952	4.8
5	Homa ya mapafu	726,628	6.0	Vidonda vya tumbo	942,630	4.4
6	Maambukizi kwenye damu	497,217	4.1	Kisukari	704,316	3.3
7	Kuoza kwa meno	459,020	3.8	Magonjwa ya mfumo wa chakula	615,652	2.9
8	Magonjwa yasiyo ya mfumo wa chakula	361,677	3.0	Homa ya mapafu	502,408	2.3
9	Kuharisha	296,282	2.4	Maambukizi kwenye damu	457,639	2.1
10	Maambukizi ya Ngozi - fungal	249,336	2.1	Kuchanika kwa misuli/ mishipa	447,329	2.1

140. magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje kwa wagonjwa wenye umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 16.2, maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 15.4 na shinikizo la juu la damu asilimia 7.1.

141. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la juu la damu, kisukari, magonjwa ya viungo (arthritis) na upungufu wa damu yanaongezeka kwa kasi hadi kufikia kuwemo katika orodha ya magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha watu kuhudhuria katika vituo vya

kutolea huduma za afya. Magonjwa hayo yanaweza kuzuilika kwa wananchi kubadili mitindo ya maisha isiyofaa kama kula kusikozingatia ulaji bora, unywaji wa pombe uliopitiliza, uvutaji wa sigara, tabia bwete na kutopumzika vya kutosha.

Jedwali Na. 4: Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje; katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026

	WAGONJWA WA NJE - CHINI YA MIAKA MITANO			WAGONJWA WA NJE - ZAIDI YA MIAKA MITANO		
NA	AINA YA UGONJWA	IDADI	%	AINA YA UGONJWA	IDADI	%
1	Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	4,465,725	36.8	Maambukizi katika mfumo wa hewa	3,465,266	16.2
2	Kuharisha pasipo kupungukiwa maji	993,626	8.2	Maambukizi katika njia ya mkojo	3,296,017	15.4
3	Malaria(BS +Ve, mRDT +Ve & Clinical)	870,330	7.2	Shinikizo la Juu la damu	1,519,187	7.1
4	Maambukizi katika Njia ya Mkojo	756,955	6.2	Malaria (BS+Ve, mRDT+Ve & Clinical)	1,032,952	4.8
5	Homaya mapafu	726,628	6.0	Vidonda vya tumbo	942,630	4.4
6	Maambukizi kwenye damu	497,217	4.1	Kisukari	704,316	3.3
7	Kuozakwa meno	459,020	3.8	Magonjwa ya mfumo wa chakula	615,652	2.9
8	Magonjwa yasiyo ya mfumo wa chakula	361,677	3.0	Homa ya mapafu	502,408	2.3
9	Kuharisha	296,282	2.4	Maambukizi kwenye damu	457,639	2.1
10	Maambukizi ya Ngozi - fungal	249,336	2.1	kuchanika kwa misuli/ mishipa	447,329	2.1

Chanzo: DHIS2

Magonjwa Yaliyoongoza Kuwaathiri Wananchi – Wagonjwa wa Kulazwa

142. Mheshimiwa Spika, magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa ndani kwa wagonjwa wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 55.5,

maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 9.4 na maambukizi ya ngozi asilimia 3.1. Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 19.7, maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 18.7na shinikizo lajuu la damu asilimia 8.6.

Jedwali Na. 5: Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa wagonjwa wa ndani; katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026

	WAGONJWA WA NDANI - CHINI YA MIAKA MITANO			**WAGONJWA WA NDANI - ZAIDI YA MIAKA MITANO**		
NA	**AINA YA UGONJWA**	**IDADI**	**%**	**AINA YA UGONJWA**	**IDADI**	**%**
1	Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	4,465,725	55.5	Maambukizi katika Mfumo wa Hewa	3,465,266	19.7
2	Maambukizi katika Njia ya Mkojo	756,955	9.4	Maambukizi katika Njia ya Mkojo	3,296,017	18.7
3	Maambukizi ya ngozi yasiyotokana na fangasi	451,947	5.6	Shinikizo la Juu la damu	1,519,187	8.6
4	Maambukizi ya ngozi ya fangasi	249,336	3.1	Vidonda vya tumbo	942,630	5.4
5	Minyoo ya tumbo	183,623	2.3	Kisukari	704,316	4.0
6	Magonjwa mengine ya mfumo wa upumuaji	180,027	2.2	kuchanika wa misuli/ mishipa	447,329	2.5
7	Upungufu wa damu wa kiwango kidogo	173,319	2.2	Upungufu wa damu wa kiwango kidogo	389,981	2.2
8	Magonjwa ya ngozi yasiyo ya maambukizi	130,860	1.6	Maumivu ya viungo	357,822	2.0
	Maambukizi ya sikio	116,785	1.5	Maambukizi ya ngozi ya fangasi	337,606	1.9
10	Maambukizi ya mirija ya hewa	114,523	1.4	Maambukizi ya ngozi yasiyotokana na fangasi	303,791	1.7

Chanzo: DHIS2

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

143. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini, Wizara ilikutana na wadau wote nchini kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja na kutatua changamoto zinazokabili utoaji wa huduma hizo. Aidha, Wizara imeendelea

kuratibu huduma za tiba asili na tiba mbadala ikiwa ni pamoja na huduma jumuishi za tiba asili zinazoendelea kutolewa katika hospitali za rufaa za mikoa 14 (Mbeya, Bombo, Sekou Toure, Singida, Simiyu,Temeke, Mwananyamala, Morogoro, Dodoma, Mt. Meru, Kitete, Bukoba, Sumbawanga na Njombe). Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya dawa 48 zimesajiliwa ambapo dawa sita (6) zimepelekwa kwenye utafiti wa usalama wa awali na kati ya hizo dawa mbili (2) za kisukari zinafanyiwa utafiti wa ufanisi ili ziweze kujumuishwa katikavituo vya kutolea huduma za afya.Vilevile, jumla ya wagonjwa 648 wamehudumiwa kwa dawa za tiba asili katika hospitali zote zinazotoa huduma jumuishi. Magonjwa yaliyotibiwa zaidi ni vidonda vya tumbo, pumu, mfumo wa upumuaji, homa ya matumbo, mvurugiko wa homoni kwa wanawake, maambukizi ya mfumo wa mkojo, bawasili, baridi yabisi (athritis), tezi dume na upungufu wa nguvu za kiume. Katika kuboresha upatikanaji wa huduma jumuishi za tiba asili nchini, Wizara ilifanya usimamizi shirikishi katika hospitali sita (6) za rufaa za mikoa (Singida, Morogoro, Tanga, Arusha, Mwananyamala na Temeke) na kiwanda cha NIMR – Mabibo.

"Tunapothibitisha tiba asili kwa sayansi, tunageuza urithi wa mababu zetu kuwa tiba salama ya leo, fursa ya uchumi wa kesho, na nguzo ya kujitegemea kwa Taifa".

Huduma za Matibabu ya Ubingwa na Ubingwa Bobezi

144. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa wananchi na kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia tiba utalii. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla wa wagonjwa 4,202,137 walipatiwa huduma katika hospitali ngazi za rufaa. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa wa nje walikuwa 3,709,432 na wa kulazwa walikuwa 492,705. Aidha, baadhi ya huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na kupandikiza mimba kwa wateja kumi (10), upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 24, upandikizaji wa vifaa vya usikivu wagonjwa 16, huduma ya kuweka puto tumboni kwa ajili ya kupunguza uzito kwa wagonjwa tisa (9), upandikizaji wa meno kwa wagonjwa 26,

kubadilisha goti au nyonga kwa wagonjwa 58 na upandikizaji uloto kwa wagonjwa nane (8). Kutolewa kwa huduma hizo za kibobezi nchini kumepelekea kuokoa takribani Shilingi bilioni 3.67 endapo wagonjwa hawa wangehudumiwa nje ya nchi.

145. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali za rufaa za mikoa zimeendelea kuimarisha huduma za ubingwa kwa kuanzisha huduma mpya za ubingwa katika fani za magonjwa ya macho, mfumo wa mkojo, afya ya akili, masikio, pua na koo, kuchuja damu, magonjwa ya ngozi, saratani, magonjwa ya mfumo wa chakula, upasuaji wa mifupa, radiolojia, huduma za dawa za usingizi na ganzi, patholojia na magonjwa ya dharura ambapo wagonjwa 17,409 walihudumiwa. Hospitali za rufaa za mikoa zilizoanzisha huduma mpya ni Geita, Katavi, Ligula, Maweni, Mawenzi, Mount Meru, Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere, Sekou Toure, Shinyanga, Songea, Songwe na Tumbi.

146. Mheshimiwa Spika, Wizarakupitia Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia imetoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wagonjwa 55,300 katika halmashauri zote 184 nchini. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizotolewa ni pamoja na magonjwa ya ndani, magonjwa ya wanawake na uzazi, huduma za watoto, huduma za upasuaji bingwa wa mifupa na majeruhi, huduma za kinywa na meno na huduma za upasuaji wa magonjwa mbalimbali. Baadhi ya wananchi wenye magonjwa ya muda mrefu waliweza kupata huduma za upasuaji karibu na makazi yao na hivyo kuwapunguzia adha na gharama, mfano mgonjwa aliyeondolewa uvimbe wa kilo 20 tumboni. Aidha, jumla ya wataalam 5,585 waliopo katika vituo vya kutolea huduma za afya wamejengewa uwezo wakati wa utoaji wa huduma kutoka kwa madaktari hao.

147. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum na taifa ilitoa huduma mkoba nchini zilizoweza kuwafikia jumla ya wagonjwa 77,118 na kati yao 6,807 walifanyiwa upasuaji. Aidha, kupitia tiba utalii jumla ya wagonjwa 3,018 raia wa kigeni walipatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Madaktari bingwa na bobezi kutoka hospitali za JKCI na Benjamin Mkapa walikwenda nje ya nchi na kutoa huduma kwa wagonjwa 4,363 katika nchi za Zambia, Comoro na Burundi kwa

lengo la kuendelea kutangaza huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zinazopatikana nchini, kuvutia tiba utalii na kukuza diplomasia ya afya.

"Huduma za kibingwa zinaposogezwa karibu na wananchi, Taifa haliponyi wagonjwa pekee; linapunguza hofu, linarejesha matumaini, linajenga uwezo wa wataalam, na linatangaza ubora wa Tanzania ndani na nje ya mipaka yake."

Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga

148. Mheshimiwa Spika, hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Upanga imetoa huduma kwa wagonjwa 373,176 kati ya wagonjwa hao wakulazwa ni 28,881 na wagonjwa wa nje ni 344,295. Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi kwa kutoa huduma za kupandikiza mimba ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya wateja kumi (10) walipata huduma hiyo. Aidha, huduma nyingine zilizoendelea kutolewa ni Pamoja na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa saba (7) hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 88 tangu huduma ilipoanzishwa mwaka 2017; upandikizaji wa vifaa vya usikivu wagonjwa 16, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 86 tangu huduma hiyo ilipo anzishwa mwaka 2017. Vilevile, katika kukuza tiba utalii nchini, jumla ya wagonjwa 833 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mauritiusna Zambia walipatiwa huduma.

149. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali ya Taifa Muhimbili imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 6,802,647,947 kwa wagonjwa 36,414 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 10,640,269,858 kwa wagonjwa 42,714 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na kuchuja damu, huduma za ICU, huduma za vipimo vya CT scan, MRI na huduma za dawa.

150. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuboresha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini, Serikali ilifanya tathmini ya utoaji wa huduma katika hospitali ya Taifa Muhimbili na kubaini mapungufu mbalimbali. Mapungufu hayo ni Pamoja na

uchakavu wa miundombinu na kutawanyika kwa mpangilio wa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na ukarabati wa mara kwa mara na mazingira yasiyoruhuru maboresho ya huduma za ubobezi na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Dhamira ya Serikali ni kufanya mapinduzi na kujenga Muhimbili mpya itakayotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ili kufikia viwango vya kimataifa na kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi na wageni kutoka nje ya nchi na hivyo kuimarisha tiba utalii.

151. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Muhimbili mpya utapunguza idadi ya rufaa za matibabu nje ya nchi, itaongeza maeneo ya kutolea huduma, itapunguza kero ya kusubiri huduma kwa muda mrefu, itaboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, itaingiza fedha za kigeni na kuimarisha uchumi wa nchi. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano (5) na kugharimu Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa majengo, mifumo, ununuzi wa vifaana vifaatiba. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali. Naomba nifafanue kwa kifupi kuwa mchango wa Serikali katika mradi huo kwa sehemu kubwa si fedha taslimu bali ni gharama za maandalizi ya eneo la ujenzi, msamaha wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa bidhaa na vifaa vitakavyoingizwa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

152. Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya ulinganifu wa gharama za ujenzi wa hospitali mpya ya Muhimbili kwa kulinganisha na miradi mingine 16 kutoka nchi 15 tofauti za barani Afrika, Ulaya na Asia kwa kuangalia ukubwa wa hospitali, gharama kwa mita za mraba, kiwango cha huduma zinazotarajiwa na mwaka wa ujenzi wa mradi. Matokeo ya ulinganifu huo yameonesha kuwa mradi wa ujenzi wa Muhimbili mpya una gharama nafuu ikilinganishwa na miradi kutoka nchi nyingine. Kati ya hospitali zote zilizolinganishwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili ina eneo kubwa la ujenzi kuliko miradi mingine (mita za mraba 115,000), na gharama za ujenzi katika nchi hizo zinakadiriwa kati ya Dola za Marekani 3,000 hadi 7,000 kwa mita za mraba wakati mradi wa Muhimbili mpya utagharimu Dola za Marekani 1,819 kwa mita za mraba. Kwa ulinganifu huu ina maana kwamba, wakati baadhi ya nchi zinalipa mara mbili au zaidi kwa kila mita za mraba, gharama kwa nchi yetu itakuwa chini kwa wastani wa asilimia 42. Tanzania

inakwenda kupata hospitali kubwa kwa gharama nafuu na huu si ushahidi wa matumizi mabaya bali ni uwekezaji wa busara na wa thamani nzuri ya fedha za umma.

Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila

153. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila iliendelea kushuhudia ongezeko la utoaji wa huduma ikilinganishwa na mwaka uliopita. Katika kipindi hiki, jumla ya wagonjwa 229,281 walihudumiwa.Kati yao, wagonjwa wa nje ni 215,295na wagonjwa 13,986ni wa kulazwa.

154. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi ambazo ni pamoja na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa tisa (9) na kufanya jumla ya wagonjwa 24 tangu huduma hii ilipoanzishwa mwaka 2023. Gharama ya upandikizaji wa figo kwa mgonjwa ni Shilingi 37,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 120,000,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma ya kuweka puto tumboni kwa wagonjwa tisa (9) hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliohudumiwa tangu huduma hiyo kuanza mwaka 2022 kufikia 192. Gharama ya huduma hiyo ni Shilingi 5,500,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shillingi 26,565,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi.

Hospitali imeendelea kutoa huduma ya upandikizaji wa meno kwa wagonjwa 26 na kufanya idadi ya wagonjwa kufikia 55 tangu huduma hii ilipoanzishwa mwaka 2024/2025. Vilevile, huduma za kubadilisha goti na nyonga zilitolewa kwa wagonjwa 58, upasuaji rekebishi wagonjwa wanne (4) na upasuaji wa kupunguza ukubwa wa tumbo la chakula kwa wagonjwa watatu (3).

155. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 43,705 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo, MRI 3,141, CT Scan 3,400, x-ray 16,441, Mammograph 231, Ultrasound 16,149 na x-ray maalum za uchunguzi wa magonjwa ya kinywa na meno 2,127. Pia, jumla ya vipimo vya maabara 456,918 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya

kisasa. Kwa ujumla, huduma za uchunguzi zimeendelea kutoa matokeo sahihi na ya wakati kwa ajili ya kusaidia matibabu.

156. Mheshimiwa Spika, hospitali imetoa huduma za mkoba katika hospitali ya rufaa ya Ndanda – Mtwara kwa wagonjwa 2,064 na kati yao 29 walifanyiwa upasuaji. Aidha, katika kutekeleza sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali ilitoa misamaha ya huduma yenye thamani ya Shilingi 3,499,697,791 kwa wagonjwa 12,350. Kwa upande wa Tiba Utalii, wagonjwa 240kutoka nchi jirani za Uganda, Sudan, Kenya, Comoro, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo walihudumiwa.

Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

157. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi2026, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imetoa huduma kwa wagonjwa 169,313 kati ya wagonjwa hao, waliolazwa ni 25,441 na wagonjwa wa nje ni 143,872. Taasisi imeweza kufanya huduma ya kuchunguza mishipa ya miguu kwa wagonjwa 59 na kuzibua mishipa ya miguu kwa wagonjwa 14. Kutibu shinikizo la juu sugu kupitia tundu dogo (Renal Denervation) kwa wagonjwa 6 pamoja na kutibu magonjwa ya moyo kwa njia ya Transcatheter Aortic Valve Implantation kwa mgonjwa mmoja (1). Huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 967, kufunga vifaa visaidizi vya moyo kwa wagonjwa 129, kuzibua mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 217, kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo kwa wagonjwa 37, kuziba matundu ya moyo kwa watoto wagonjwa 192 na kuchunguza matatizo ya moyo kwa watoto wagonjwa 111.

158. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu kwa wagonjwa 339 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 8,927 tangu kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2015. Gharama ya kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu ni wastani wa Shilingi

15,450,000 kwa mgonjwa mmoja ndani ya nchi ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 50,800,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Vilevile, Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 1,974 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 38,739 tangu huduma hizo zilipoanza kutolewa. Gharama ya kufanya upasuaji huo ni wastani wa Shilingi 6,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 20,000,000 kwamgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi.

159. Mheshimiwa Spika, Taasisi ilitoa msamaha kwa wagonjwa 880 waSIYO na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 1,350,858,947 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 825,762,214 kwa wagonjwa 710 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Huduma zilizoongoza kuolewa misamaha ni pamoja na vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi.

160. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya moyo ambapo vipimo vya ECHO vilikuwa 19,931 Holter vilikuwa 2,368, Stress ECG vilikuwa 2,971 Dobutamine vilikuwa 46, Stress ECHO vilikuwa 12 na Sparkle Traching ECHO vilikuwa 1,086, Transosophageal ECHO vilikuwa 26, X-Ray vilikuwa 18,066, Ultra Sound vilikuwa 17,854, ECG vilikuwa 17,699 Ultra Functional Test vilikuwa 281, Lung functional test vilikua 60 na ABP vilikuwa 1,980. Aidha, jumla ya vipimo vya maabara 512,066 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 405,258 kipindi kama hicho mwaka 2024/2025.

161. Mheshimiwa Spika, katika kutekelezaDkt. Samia Cardiac Outreach Program, Taasisi imeendelea kutoa huduma za mkoba katika Mikoa ya Dar es Salaa, Geita na Arusha ambapo jumla ya wagonjwa 6,870 walifikiwa na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma tangu taasisi imeanza kutoa huduma za mkoba mwaka 2015 kufikia 54,192. Jumla ya wagonjwa 14,119 walipatiwa vipimo vya ECHO na ECG kupitia huduma hizo za mkoba na wagonjwa wapya 4,602 sawa na asilimia 33 waligundulika kuwa na magonjwa ya moyo.

162. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 234 waliofika nchini na wagonjwa 3,163 walipatiwa huduma katika nchi za Comoro na Zambia na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliotibiwa kufikia 3,360. Wagonjwa waliotibiwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete walitoka nchi za Msumbiji, Misri, Comoro, Malawi, Zambia, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Vilevile, kutokana na kuimarika kwa huduma za ubingwa za upasuaji wa moyo, Taasisi imezijengea uwezo nchi za Malawi, Rwanda na Zambia.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

163. Mheshimiwa Spika, Taasisi imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 224,715 kati yao wagonjwa wa kulazwa ni 9,882 na wagonjwa wa nje ni 214,833. Aidha, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, Taasisi imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 5,169,995,385.26 kwa wagonjwa 19,190 na huduma zilizoongoza kwa msamaha ni pamoja na upasuaji, uchunguzi wa mionzi, kulazwa, vipimo vya maabara pamoja na dawa.

164. Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa huduma zinazotolewa, Taasisi imeanzisha huduma mpya zifuatazo; upasuaji upasuaji wa ubongo wa mgongo bila kufungua fuvu, kwa kufungua eneo dogo, upasuaji wa kunyoosha mgongo uliopinda, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo kupitia tundu la pua, huduma ya kutibu maumivu sugu ya mgongo, kuweka tiba sementi kwenyepingili za mgongo, upasuaji rekebishi wa viungo vilivyopooza,huduma ya upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu. Aidha, huduma zingine za ubingwa bobezizimendelea kutolewakwa jumla ya wagonjwa 5,836 walihudumiwa kwa mafanikio makubwa na kuwezesha Serikali kuokoa Shilingi bilioni 318 ambazo zingetumika iwapo wagonjwa hao wangepewa rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

165. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 74,809 vya radiolojia vilifanyika,Katiyahivyovipimovya MRI vilikuwa 12,070, CT scan vipimo 7,850, X-Ray vipimo 50,633 na ultrasound vipimo 4,256.

Aidha, jumla ya vipimo vya maabara 163,023 vilifanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

166. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutoa huduma mkoba, ambapo jumla ya wagonjwa 13,204 walihudumiwa, kati yao wagonjwa 1,245 walifanyiwa upasuaji. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 365 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Burundi, Sudani Kusini, Uganda na Rwanda. Wananchi wa mataifa mengine wamekuwa na imani kubwa na tiba zetu kutokana na kuimarika na kuaminika kwa huduma za ubingwa bobezi hapa nchini.

Taasisi ya Saratani Ocean Road

167. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 62,976 kati yao, wagonjwa wa nje ni 60,840 na wagonjwa wa kulazwa ni 2,136. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na tiba mionzi bobezi, tiba ya mionzi ya ndani (3D brachytherapy) natiba bobezi kupitia dawa za Immunotherapy. Jumla ya wagonjwa 396 walitibiwa kwa tiba ya mionzi bobezi, wagonjwa 4,978 walitibiwa kwa tiba mionzi ya ndani na jumla ya wagonjwa 2,132 walipata tiba za immunotherapy. Vilevile, Taasisi imekamilisha usimikaji wa mashine tatu (3) mpya za kisasa ikiwemo moja (1) ya Linear Accelerator - LINAC itakayowezesha utoaji wa huduma za tiba mionzi bobezi (Volumetric Arch Therapy na Stereotactic Body Radiotherapy) na mashine 2 za tiba mionzi za cobalt 60. Uwepo wa mashine hizo umepunguza kwa kiasi kikubwa muda wa wagonjwa kupata matibabu. Pia, huduma za upasuaji mdogo wa magonjwa ya saratani ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 3,249 walifanyiwa upasuaji.

168. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba mionzi (3D-CRT) ambapo kwa kipindi hiki, tiba mionzi 173,786 zimetolewa ikilinganishwa na tiba mionzi 151,946 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa 2024/2025. Tiba mionzi ya 3D-CRT ilianza mwaka 2019 ambapo hadi sasa jumla ya tiba mionzi 1,497,542 zimetolewa. Aidha, Taasisi imetoa tiba kemia 28,279 ikilinganishwa na tiba kemia 25,754 katika kipindi kama hicho

mwaka 2024/2025. Hadi sasa jumla ya tiba kemia 527,842 zimetolewa tangu kuanzishwa kwa huduma hii mwaka 2017. Pia, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba shufaa kwa wagonjwa 46,551 ikilinganishwa na wagonjwa 35,715 kwa mwaka 2024/2025.

169. Mheshimiwa Spika, Huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya vipimo vya maabara 192,294vimefanyika ikilinganishwa na vipimo 171,930 katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Kwa upande wa radiolojia, vipimo 20,053 vimefanyika ikilinganishwa na vipimo 18,694 vilivyofanyika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/2025. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 6,552 ni vya X-Ray, 7,722 vya ultrasound, 3,268 vya CT scan, 2,050 vya MRI, 193 vya mammograph na 268 Interventional Radiology.

170. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa PET - CT scan ambao ulihusisha ujenzi wa bunkers na ununuzi na usimikaji wa mashine za PET - CT scan na Cyclotron umekamilika na huduma zinaendelea kutolewa. Huduma za uchunguzi kwa PET – CT scan kwa kutumia kitendanishi cha Gallium zilianza kutolewa Julai 2024 na jumla ya wagonjwa 574 wamechunguzwa. Vilevile, Serikali imewezesha kupatikana kwa Shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya mafunzo ya wataalam na ununuzi wa malighafi za uzalishaji kitendanishi cha FluoroDeoxyGlucose (FDG). Mashine ya Cyclotron imeanza uzalishaji wa FDG - 18 mwezi Machi 2026 na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa wanaochunguzwa kupitia mashine ya PET -CT scan kutoka wagonjwa watano (5) hadi wagonjwa 20 kwa siku.

171. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha, wagonjwa 26,808 walipewa msamaha wa jumla ya Shilingi 13,461,853,093.86. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni tiba mionzi, tiba za kibaiolojia, dawa za tiba kemia, uchunguzi wa maabara, radiolojia na huduma za kulazwa. Aidha, Taasisi imetoa huduma mkoba katika mikoa saba (7) ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Geita, Mara, na Dodoma na kuhudumia jumla ya wateja 6,825. Huduma zilizotolewa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya matiti, saratani ya mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana, tezi dume na utoaji wa elimu.

172. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, jumla ya wagonjwa 533 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikilinganishwa na wagonjwa 607 waliopata huduma hiyo kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Malawi, Kenya, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Msumbiji, Sudani ya Kusini, Zambia, Marekani, Rwanda, Burundi na Uganda.

Hospitali ya Benjamin Mkapa

173. Mheshimiwa Spika, hospitali imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 224,645. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 11,061 na wagonjwa wa nje ni 213,584. Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi za upasuaji wa moyo kwa watu wazima na Watoto ambapo wagonjwa 12 wamenufaika. Gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja wa upasuaji wa moyo ni wastani wa Shilingi 70,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 210,000,000 iwapo matibabu hayo yangefanyika nje ya nchi.

174. Mheshimiwa Spika, huduma za ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa na hospitali ni pamoja na upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa tisa (9) na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia 30 toka huduma ilipoanzishwa mwaka 2023. Pia, hospitali imefanikiwa kupandikiza figo wagonjwa nane (8) na kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia wagonjwa 58 tangu kuanzishwa 2018. Hospitali ilifanikiwa kufanya huduma ya uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 173.

Huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 180, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 405 na upasuaji wa moyo na huduma zitolewazo kwa kutumia mtambo maalum wa cathlab kwa wagonjwa 252. Katika kuimarisha wigo wa huduma, hospitali imeanzisha huduma mpya ikiwemo kurefusha miguu kwa wagonjwa 11 pamoja na huduma ya upasuaji wa kifundo cha mguu kwa wagonjwa wawili (2).

175. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 75,059 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo MRI 4,841, CT scan vipimo 4,976, X-Ray vipimo 24,561, fluoroscopy 1,341, mammography 436 na ultrasound vipimo 38,904. Aidha, jumla ya vipimo vya maabara 398,296 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

176. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 448,917,605.50 kwa wagonjwa 1,894. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni pamoja na uchujaji damu, vipimo vya maabara, kitengo cha wagonjwa mahututi, huduma za upasuaji, kumuona daktari na dawa.

Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe

177. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kipimo cha umeme wa Ubongo EEG kilifanyika kwa wagonjwa 71, ECHO wagonjwa 615, ECG wagonjwa 684, X-Ray wagonjwa 3,159, na ultrasound wagonjwa 2,541. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya vipimo vya maabara 37,851 vimefanyikakwa kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile, hospitali ilitoa huduma mkoba zilizolenga huduma za afya ya akilina msaada wakisaikolojiakatika mikoa ya Dodoma, Manyara na Ruvuma ambapo jumla ya wateja 915 walihudumiwa.

178. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili kwa wananchi, mahabusu na wafungwa kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, hospitali inatoa huduma za matibabu kwa waraibu wa aina mbalimbali ikiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 64,868, kati yao wagonjwa wanje ni 63,195 na wagonjwa wa kulaza ni 1,673. Aidha wagonjwa 13,063 sawa na asilimia 20 ni wagonjwa wa akili na wagonjwa 51,805 sawa na asilimia 80 ni wagonjwa wa magonjwa mengine. Kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa akili wahalifu waliothibitishwa na vyombo vya kisheria wanaotibiwa sehemu ya Isanga, ambapo

jumla ya wagonjwa 474 walithibitishwa na wanaendelea na matibabu.

179. Mheshimiwa Spika,katika kutekelezasera ya msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya shilingi 571,868,514.7 kwa wagonjwa 8,976. Huduma zilizotolewa msamaha ni pamoja na matibabu, chakula, mavazi na malazi.

Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto

180. Mheshimiwa Spika, hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto imeendelea kutoa huduma za tiba, kinga na tafiti. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 21,242. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa, wagonjwa wa nje ni 20,484 na wagonjwa wa kulazwa ni 758. Aidha, kati ya wagonjwa 21,242 waliohudumiwa, wagonjwa wa kifua kikuu walikuwa 506 (kifua kikuu cha kawaida 408 na kifua kikuu sugu 98), wagonjwa wa UKIMWI 908 na magonjwa mengine 19,828.

181. Mheshimiwa Spika, kati ya wagonjwa wa kulazwa 758, wagonjwa waKifua Kikuu sugu walikuwa 98 ambao ni rufaa kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao hulazwa kwa muda wa wastani wa miezi sita (6) wakipatiwa matibabu, chakula, chakula dawa kwa wenye utapiamlomkali na mahitaji mengine muhimu ya kijamii. Idadi ya wagonjwa waaliolazwa kutokana na mapafu kuathirika na vumbi la silica kutoka maeneo ya migodini walikuwa 50 ambao wanakuwa tegemezi wa hewa tiba ya oksijeni maisha yao yote. Kwa wastani hospitali hutumia mitungi 60 kwa siku kuhudumia wagonjwa hao.

182. Mheshimiwa Spika, hospitali ina maabara ya Afya ya Jamii ya usalama wa kibaiolojia daraja la tatu yenye ithibati ya kimataifa ISO:15189 yenye vifaa vya kisasa vya uchunguzi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya vipimo vya uchunguzi wa maabara vilivyofanyika ni 33,286. Kati ya hivyo vipimo vya radiolojia 3,583 (X-Ray 2,444, Ultrasound 593, ECHO 388, Doppler Ultrasound 22 na CT scan vipimo 136). Aidha, katika kutekeleza sera ya msamaha, hospitali ilihudumia wagonjwa 1,147

kwa msamaha kwa gharama ya Shilingi 786,048,490. Huduma zinazoongoza kutolewa msamaha ni huduma ya hewa tiba hasa kwa wagonjwa wa silicosis, huduma za dawa, kumuona daktari, uchunguzi wa maabara na radiolojia.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando

183. Mheshimiwa Spika, hospitali imetoa huduma kwa wagonjwa 286,934. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 21,206 na wagonjwa wa nje ni 286,934. Hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, ambazo ni matibabu ya magonjwa ya figo, kisukari, damu, njia ya chakula, ngozi, watoto, saratani, mfumo wa upumuaji, afya ya akili, huduma za dharura na ajali na huduma ya tiba viungo na utengemano.

184. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi za upasuaji kwa wagonjwa 8,750 katika maeneo ya nyonga, magoti, kinywa na meno, mdomo sungura kwa watoto, macho, masikio, pua na koo, kifua, moyo, ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo, mfumo wa mkojo, upasuaji sanifu, upasuaji maalum wa watoto, upasuaji wa matundu madogo na huduma ya viungo tiba na vifaa tiba saidizi. Aidha, kati ya waliofanyiwa upasuaji wagonjwa 8,290 walifanyiwa upasuaji mkubwa na wagonjwa 460 walifanyiwa upasuaji mdogo.

185. Mheshimiwa Spika, wagonjwa 12,820 wamepatiwa huduma ya matibabu ya saratani kati yao, wagonjwa 12,072 ni wagonjwa wa nje 748 ni wagonjwa wa kulazwa, wagonjwa 6,913 walipatiwa tiba kemia ya saratani na wagonjwa 3,346 walipatiwa tiba kwa kutumia mionzi. Aidha, utoaji wa huduma hizo umepunguza adha ya wagonjwa kufuata huduma hizo katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

186. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi hiki vipimo 46,501 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI 2,236, CT-Scan 5,355, X-Ray 18,367, ultrasound 19,661, mammography 137, fluoroscopy 502 na Interventional radiology1,052. Katika kipindi hiki, jumla ya vipimo vya maabara 887,550 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

187. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za mkoba kwa vituo 19 ambapo wagonjwa 13,702 walipatiwa huduma na kati yao 157 walifanyiwa Upasuaji. Aidha, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 1,739,468,790 kwa wagonjwa 6,647. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na, mionzi tiba, utoaji wa dawa za mionzi, magonjwa ya akili, huduma za matibabu ya watoto wachanga, mama wajawazito, huduma ya kuchuja damu na huduma kwa wazee waSIYOjiweza. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia wagonjwa 82 raia wa nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya

188. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuhudumia jumla ya wagonjwa 193,823 ambapo kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 60,223 na wagonjwa wa nje ni 133,600. Aidha, huduma zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, matibabu ya mfumo wa chakula na ini, huduma ya mfumo wa upumuaji pamoja na huduma ya upasuaji kwa watoto wachanga. Jumla ya wagonjwa wapatao 1,644 wamepatiwa huduma za ubingwa bobezi.

189. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo jumla ya vipimo 55,547 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo MRI ni 590, CT scan 3,423, X-ray 13,921 fluoroscopy 12,702 na utrasound 24,911. Vipimo vya maabara 191,900 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa.

190. Mheshimiwa Spika, katika kutekelezasera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 1,111,678,330 kwa wagonjwa 31,766. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni pamoja na kumuona daktari, kulazwa pamoja na upasuaji kwa

wajawazito wa kumtoa mtoto tumboni. Katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 190 kutoka nchi za Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia na Msumbiji.

191. Mheshimiwa Spika, kwa kutumia wataalam wa ndani, Hospitali imebuni mfumo wa kudhibiti joto "automatic temperature control" katika chumba cha watoto wachanga na watoto njiti. Pia, mfumo wa e-Medical unaotumika katika shughuli mbalimbali za hospitali ikiwemo kuona wagonjwa umebuniwa na wataalam wetu na umefungwa katika baadhi ya hospitali za kanda, taifa na hospitali binafsi. Wabunifu hao wametambuliwa na kupewa hati za ufanyakazi hodari na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani mwaka 2025.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC

192. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 193,379. Kati ya hao wagonjwa wa nje ni 178,688 na wagonjwa wa ndani ni 14,691. Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi ambapo jumla ya wagonjwa 7,998 wamefanyiwa upasuaji katika fani za upasuaji wa ubongo, upasuaji wa ubingwa katika njia ya mkojo, upasuaji wa mgongo na uti wa mgongo, upasuaji wa ubingwa wa kinywa na meno, macho, masikio, pua na koo na upasuaji wa utumbo mpana.

193. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi ambapo wagonjwa 2,211 walifanyiwa kipimo cha MRI, CT scan 4,651, ultrasound 12,444, X-Ray 20,292, mamography 222. Kwa upande wa vipimo vya maabara, Taasisi ilifanya jumla ya vipimo 208,798. Aidha, Hospitali imetoa huduma za msamaha kwa wagonjwa 1,786wenye thamani ya Shilingi 1,897,185,255. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni matibabu ya Saratani, Dawa, Vipimo na Kulazwa. Vilevile, hospitali imeendelea kutoa huduma mkoba, katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ambapo zaidi ya wagonjwa 2,500 walipatiwa huduma za saratani, macho na VVU/UKIMWI

194. Mheshimiwa Spika, katika dhana ya kuendeleza tiba utalii nchini, hospitali imeimarisha ubora wa huduma kwa kuweka mikakati ya kuvutia wateja wa kimataifa. Katika kipindi hiki hospitali imehudumia wateja 399 kutoka nchi mbalimbali, zikiwemo za Afrika Mashariki (Kenya, Uganda, Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, na Sudan kusini) pamoja na raia wa mataifa nje ya Afrika. Huduma hizo zimechangia kuongeza mapato ya Shilingi 335,679,733. Aidha, katika hatua nyingine ya kuongeza vyanzo vya mapato na ubora wa huduma, hospitali imeanzisha huduma za kliniki binafsi ambapo hadi sasa imehudumia zaidi ya wagonjwa 1,466 tangu kuanzishwa kwake mwezi Oktoba 2025.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato

195. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 46,252 ikiwa wagonjwa wa nje ni 43,168 na wagonjwa wa kulazwa ni 3,084. Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika fani za mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu ambapo jumla ya wagonjwa 6,184 walihudumiwa. Aidha, hospitali imeanzisha kliniki ya ubingwa ya selimundu ambapo jumla ya wagonjwa 4,198 wamehudumiwa. Vilevile, hospitali inaendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za magonjwa ya moyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete ambapo kwa kipindi hiki jumla ya wagonjwa 8,324 wamehudumiwa.

196. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 13,669 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa 268, CT Scan 487, X-Ray 3,343, Dental X-Ray 149, ultrasound 4,674, ECHO 3,099 na ECG 1,649. Jumla ya vipimo vya maabara 44,586 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa.

197. Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 222,797,016 kwa wagonjwa 1,063. Katika kutekeleza

dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia wagonjwa 21 raia wa nchi za Uganda, Rwanda na Burundi.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara

198. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali rufaa ya kanda Mtwara ili kuiwezesha kuwa na uwezo wa kutoa huduma nyingi za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa 36,550. Kati yao, wagonjwawa nje ni 34,329 na wagonjwa wa kulazwa ni 2,221. Hospitali ilifanikiwa kutoa huduma za ubingwa kwa wagonjwa 20,706 katika fani za upasuaji, magonjwa ya moyo, magonjwa ya wanawake na uzazi, magonjwa ya ndani, magonjwa ya masikio pua na koo na magonjwa ya watoto.

199. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa ubingwa ambapo imefanikiwa kusimika mashine ya C-Arm kwa ajili ya uchunguzi wa radiolojia na kuanzisha kitengo cha uchunguzi wa vinasaba. Kwa upande wa vipimo vya radiolojia, wagonjwa 399 walifanyiwa kipimo cha MRI, CT-scanwagonjwa 681, ultrasound wagonjwa 4531, X-ray wagonjwa 4740 na vipimo vya maabara 68,061.

200. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa za mkoba katika mkoa wa Mtwara kwa ajili ya matibabu ya pua masikio na koo, macho, ngozi, Watoto na meno ambapo jumla ya wagonjwa 1,684 walipatiwa matibabu, kati yao 61 walifanyiwa upasuaji. Katika kutekeleza sera ya kutoa huduma ya msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu gharama za matibabu, hospitali imetoa msamaha wenye thamani ya Shilingi 25,116,331 kwa wagonjwa 308. Aidha, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 248 kutoka nchi za jirani.

Hospitali ya Kanda ya Mashariki – CCBRT

201. Mheshimiwa Spika, hospitali imeendelea kutoa huduma mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ambapo jumla ya wagonjwa 85,178 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 88,808 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kati yao wagonjwa wa nje ni 81,104 na wagonjwa wa ndani ni

4,074. Aidha, wagonjwa wenye ulemavu waliohudumiwa ni 10,672 ikilinganishwa na wagonjwa 9,557 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika fani za upasuaji rekebishi kwa wagonjwa 98, upasuaji kwa njia ya matundu madogo kwa wagonjwa 52, kutoa uvimbe kwenye tezi za uzazi kwa wagonjwa saba (7), kufunga mirija ya uzazi kama njia ya uzazi wa mpango wagonjwa 10, upasuaji wa ndani ya kizazi kwa njia ya kamera mgonjwa mmoja (1) na huduma ya uchunguzi kwa njia ya matundu madogo wagonjwa 14, kuweka lensi kwenye mboni wagonjwa 196 na upasuaji wa makengeza kwa watoto 20.

202. Mheshimiwa Spika, huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 5,233 walifanyiwa upasuaji wa macho, fistula itokanayo na uzazi, mifupa, mdomo sungura na miguu kifundo. Aidha, wagonjwa 747 walipata viungo saidizi. Vilevile, hospitali kupitia kituo cha huduma za utengemao kilichopo Moshi ilitoa huduma ya utengemao kwa wagonjwa 3,338 katika maeneo ya upasuaji wa macho, upasuaji wa mtoto wa jicho kwa njia ya vitundu vidogo, upasuaji wa pazia la jicho, makengeza na upasuaji wa nyonga na goti bandia. Huduma hizo zimeboresha maisha ya watu ambao wangeweza kuwa walemavu wa macho au viungo vingine.

203. Mheshimiwa Spika, hospitali imeimarisha huduma za uchunguzi zinazoendana na huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuimarisha utendaji wa vifaa vya maabara ambapo jumla ya vipimo 54,435 vilitolewa. Kwa upande wa vipimo vya radiolojia, wagonjwa 237 walifanyiwa kipimo cha CT -Scan, wagonjwa 4,742 ultrasound na wagonjwa 4,737 X-Ray. Pia, hospitali imenunua mashine ya kisasa ya ultrasound ya machokwa ajili ya upimaji wa kibobezi wa pazia la nyuma ya jicho.

204. Mheshimiwa Spika,katika kutekelezasera ya kutoa huduma ya msamaha kwa wagonjwa waSIYOweza kumudu gharama za matibabu, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 2,100,180,013.52 kwa wagonjwa 3,976. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma mkoba kwa wagonjwa 5,819 kupitia

vituo vya utengemao vilivyoko kwenye jamii na huduma za majumbani. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, hospitali imetoa huduma za matibabu ya afya ya macho, vifaa saidizi vya macho, mifupa na fistula ya uzazi kwa raia wa nchi Jirani ambapo jumla ya wagonjwa 374 walihudumiwa.

Hospitali za Rufaa za Mikoa

205. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 hospitali 28 za rufaa za mikoa zimehudumia wagonjwa 2,789,223kati yao wa kulazwa ni366,027na wa nje ni 2,423,196 ikilinganishwa na wagonjwa 2,628,784 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, katika kutekeleza sera ya msamaha kwa wagonjwa waSIYO na uwezo wa kumudu matibabu, hospitali zilitoa msamaha kwa wagonjwa 116,117 wenye thamani ya Shilingi 2,735,855,307 ikilinganishwa na misamaha ya Shilingi 2,630,043,203 kwa wagonjwa 134,145 iliyotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

206. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa hospitali zote za rufaa za mikoa zinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za ubingwa katika fani nane (8) ambapo kwa sasa hospitali 18 kati ya 28 zimeweza kufikisha lengo ikilinganishwa na hospitali 15 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Sanjari na lengo hilo, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kuongeza idadi ya fani za ubingwa kufikia 17 katika hospitali zote za rufaa za mikoa. Fani hizo ni magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, afya ya watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, afya ya macho, magonjwa ya ngozi, huduma za dharura, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi, radiolojia,magonjwa ya damu, magonjwa ya saratani na patholojia. Aidha, idadi ya madaktari bingwa imeongezeka katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka 402 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 hadi kufikia madaktari 497 Machi, 2026.

207. Mheshimiwa Spika, hospitali zimetoa huduma mkoba kwa wagonjwa 41,657 ambapo kati yao 2,259 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 68,058 waliohudumiwa na 5,121

waliofanyiwa upasuaji kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Huduma zilizotolewa ni magonjwa ya kinamama na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo,macho,ngozi, utoajiwa dawa za usingizi, ganzi na radiolojia. Uanzishwaji wa huduma mpya na utoaji wa huduma mkoba umewezesha wananchi kupata huduma kwa haraka katika mikoa yao, kupunguza gharama za matibabu na kupunguza msongamano katika hospitali za rufaa za kanda, maalum na taifa.

208. Mheshimiwa Spika, jumla ya vipimo vya radiolojia 410,797 vilifanyika. Kati ya hivyo CT scan 35,025, Ultra Sound 193,365 na X-ray 181,406. Aidha, jumla vya vipimo 2,317,017 vya maabara vilifanyika. Vilevile, katika kuendeleza dhana ya tiba utaliinchini, hospitali za rufaa za mikoa na hasa zilizopo pembezoni mwa mipaka ya nchi, zilihudumia wagonjwa 616 kutoka nchi jirani za Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda na Msumbiji.

Huduma za Uuguzi na Ukunga

209. Mheshimiwa Spika, uuguzi na ukunga umeendelea kuwa muhimili muhimu katika utoaji wa huduma bora za afya nchini ambapo asilimia 80 ya huduma hutolewa na kada hiyo. Kulingana na takwimu zilizopo zinaonesha kuwa sehemu kubwa ya vifo vya wajawazito hutokea wakati wa uchungu, kujifungua na baada ya kujifungua. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wauguzi na wakunga ili kuimarisha ufuatiliaji wa uchungu wa mama mjamzitowakati na baada ya kujifungua kwa kutumia chati uchungu iliyoboreshwa.

210. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya wakunga 1,850 kutoka mikoa saba (7) ya Mbeya, Njombe, Rukwa, Arusha, Morogoro, Pwani na Kilimanjaro walipatiwa mafunzo. Hii imeongeza idadi ya wakunga waliopatiwa mafunzo hayo kufikia 9,093 ikilinganishwa na 7,243 kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, hadi sasa, jumla ya vituo vya kutolea huduma 5,884 katika mikoa 22 vinatumia chati uchungu iliyoboreshwa pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi

90 wa vyuovya afya na kujumuisha maudhuiya chati uchungu kwenye mitaala ya vyuo vikuu mbalimbali ikiwemo Bugando, Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, KCMC, Mwanza University, Kairuki, St. John, Aga Khan na Chuo kikuu cha Dodoma.

211. Mheshimiwa Spika, jumla ya vituo vya kutolea huduma 1,244 vimeanza kutoa huduma ya mama mwambata (birth companionship) ikilinganishwa na vituo 847 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kupitia huduma hii mama mjamzito anaruhusiwa kuwa na mwenza au ndugu wa karibu aliyemchagua yeye wakati wa kujifungua. Hatua hii imechangia kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji wa akina mama wakati wa uchungu na baada ya kujifungua, pamoja na kuboresha huduma zinazotolewa.

212. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa kuzingatia utu, heshima na staha, Wizara imetengeneza bango kitita ili kuongoza watumishi kutoa huduma staha na mawasiliano madhubuti. Kupitia juhudi hizo wauguzi na wakunga 3,500 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Katavi, Kigoma, Songwe, na Mtwara wamejengewa uwezo na kufanya idadi yao kufikia 15,700 ikilinganishwa na wauguzi na wakunga 12,000 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Sanjari na mafunzo hayo, jumla ya vituo vya kutolea huduma 413 vimeanzisha madawati yahuduma kwamteja ilikuongeza ufanisi wa kushughulikia kero za wananchi yaliyosaidia kuimarisha mawasiliano kati yao na watoa huduma.

213. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia miongozo na kuimarisha ubora kwa kutekeleza zoezi la ukaguzi wa kimatibabu katika utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam vilifanyiwa ukaguzi wa kimatibabu. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuendelea kuimarika kwa ubora wa huduma za Uuguzi na Ukunga na kufikia wastani wa asilimia 68 ikilinganishwa na asilimia 60 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, katika kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji na kutoa huduma bora, Wizara imewajengea

uwezo wa kufanya ukaguzi wa ndani wauguzi na wakunga 456 kutoka halmashauri 162. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa ukaguzi unakuwa endelevu na sehemu ya utendaji wa kila siku wa watoa huduma.

214. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa ndani, Wizara imetoa mafunzo kwa wauguzi viongozi 67 kutoka hospitali za rufaa za mikoa 28 na hospitali 11 za binafsi zenye hadhi ya hospitali za rufaa za mikoa nchini kuhusu uwajibikaji na namna bora ya kusimamia huduma za uuguzi na ukunga. Aidha, wauguzi na wakunga 241 kutoka vituo 14 vya kutolea huduma wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya hewa tiba ya oksijeni, hivyo kufanya idadi ya wauguzi na wakunga waliopatiwa mafunzo kufikia 1,001. Vilevile, katika kuimarisha usimamizi wa ubora wa huduma, Wizara imeandaa viashiria 24 vya kupima utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga ambapo wauguzi viongozi 256 wamejengewa uwezo wa kufuatilia na kutumia viashiria hivyo.

"Muuguzi aliyefundishwa amekuwa moja ya baraka kuu za ubinadamu! Muuguzi anatoa faraja, huruma, na huduma". Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya

215. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya afya ili kukidhi mahitaji ya sasa, kukua kwa teknolojia, mipango ya kitaifa na kimataifa na Dira ya Taifa 2050. Katika kutekeleza hilo, Wizara inafanya mapitio ya Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ambapo pamoja na mambo mengine itaweka mkazo katika maboresho ya mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini hususan kwa makundi maalum na rasimu ya sera hiyo ipo katika hatua mbalimbali za maamuzi. Vilevile, maandalizi ya Sheria ya Afya yanaendelea ili kuweka msingi wa kisheria katika usimamizina utoaji wa huduma za afya ikiwemo; uvunaji na upandikizaji wa viungo, uanzishwaji wa taasisi ya udhibiti wa gharama na huduma za afya, Taasisi ya Ithibati, uanzishwaji wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali na Bodi za taaluma za afya na sayansi shirikishi.

216. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufuatilia na kuimarisha ubora wa huduma za afya kwa kutumia takwimu katika kufanya maamuzi na kuimarisha uwajibikaji katika ngazi zote za utoaji huduma ikiwemo kufanya uchambuzi wa takwimu kutoka mfumo wa kidijitali wa usimamizi shirikishi wa AfyaSS, unaotumika kufuatilia utekelezaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya uhakiki ubora wa maeneo ya upimaji VVU ili kuona kama yanakidhi viwango vya ubora katika maeneo 240 kutoka vituo 156 vya kutolea huduma katika mikoa mitatu (3) ambayo ni Mtwara, Morogoro na Lindi. Kati ya maeneo yaliyofikiwa, maeneo 209 sawa na asilimia 87 yalipata daraja la nne la ubora na hivyo kukidhi viwango vya ubora vya upimaji VVU.

217. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendesha zoezi la usimamizi shirikishi kwa kutumia mfumo wa kidijitali wa AfyaSS. Zoezi hilo lilihusisha ufuatiliaji wa ubora wa huduma za afya, usimamizi wa mnyororo wa dawa, tathmini ya ubora wa takwimu na tathmini ya uwepo na ufanisi wa timu za uimarishaji ubora pamoja na timu ya uchakataji wa taarifa za bidhaa za afya. Kazi hiiilitekelezwa katika mikoa nane (8) ambayo ni Kilimanjaro, Tabora, Arusha, Tanga, Dar es salaam, Pwani, Morogoro na Geita kwa dhumuni la kuimarisha matumizi ya mfumo wa usimamizi shirikishi katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli za ubora wa huduma katika ngazi ya mkoa na halmashauri, sambamba na kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali na huduma.

218. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na mchakato wa uanzishaji wa taasisi ya ithibati ya ubora wa huduma za afya ili kuwezesha usimamizi wa ubora wa huduma za Afya nchini. Aidha, hospitali zimeanza taratibu za kupata ithibati ya ubora wa huduma za kimataifa kama ISO, JCI, SafeCare na COHSASA. Jitihada hizi zinalenga kuhakikisha huduma zinazotolewa na Taasisi za afya nchini zinakuwa na viwango vinavyokubalika kimataifa. Wizara itatumia ithibati ya ubora katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha wananchi wanaojiunga na bima ya afya wanapokea huduma zinazostahili na zenye viwango vinavyoridhisha.

Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa

219. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwekeza kwenye maeneo makuu ya uchunguzi ambayo ni huduma za maabara, radiolojia, matengenezo ya vifaatibapamoja na Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Huduma za Maabara

220. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kuna ongezeko la maabara 12 zilizopata ithibati ya kimataifa na hivyo kufanya jumla ya maabara zenye ithibati kutoka 90 hadi kufikia 102. Kati ya maabara hizo, 72 ni za umma, 24 zinamilikiwa na mashirika ya dini na maabara sita (6) ni za binafsi. Kati ya maabara hizo, maabara tatu (3) ziko katika ngazi ya taifa, sita (6) katika ngazi ya hospitali maalum, saba (7) ngazi ya Kanda, 36 ngazi ya rufaa za mikoa, 37 ngazi ya wilaya, tisa (9) katika vituo vya afya na maabara nne (4) katika vituo vya tafiti.

221. Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza kujengea uwezo maabara tano (5) za usalama wa vimelea ngazi ya tatu (Biosafety level 3 – BSL 3). Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii - Kibong'oto, maabara kuu ya Kifua Kikuu Muhimbili (CTRL), maabara ya hospitali ya Kanda Mbeya, Maabara ya Tafiti Kilimanjaro (KCRI) na Wakala ya Maabara ya Magonjwa ya Wanyama (TVLA). Kufuatia kukidhi vigezo vya kimaabara katika ngazi ya tatu ya usalama kwa viwango vya kimataifa, Maabara ya Tafiti Kilimanjaro imetambuliwa na Umoja wa Afrika kama maabara yenye uwezo wa kufanya kazi na vimelea hatarishi. Utambuzi huu una maana kuwa maabara hiyo inakidhi viwango vya juu vya ubora wa huduma za uchunguzi, inalinda usalama wa watumishi na sampuli dhidi ya maambukizi, na inaongeza uaminifu wa matokeo ya vipimo kitaifa na kimataifa. Aidha, hadhi hii huwezesha nchi kushiriki tafiti za kimataifa, kubadilishana taarifa za kisayansi, na kuimarisha utayari wa kukabiliana na milipuko ya magonjwa hatarishi.

Huduma za Radiolojia

222. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imefanikisha upatikanaji wa huduma za radiolojia na radiolojia tiba, zikiwemo PET CT-Scan, MRI, CT-Scan na huduma nyingine za radiolojia katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, katika kipindi hiki Wizara imefanya usimamizi shirikishi pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya vipimo vya radiolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Vilevile, Wizara imewezesha wataalam 125 kupata mafunzo ya matumizi bora ya mashine ya ultrasound kutoka vituo vya kutolea huduma na vyuo vya radiografia/radiolojia pamoja na wataalam 46 wa ufundi wa vifaa tiba.

Matengenezo ya Vifaa Tiba

223. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za matengenezo ya vifaa na vifaa tiba, Wizara imeandaa miongozo ya usimamizi wa mitambo ya uzalishaji wa hewa tiba ya oksijen pamoja na kufanya usimamizi shirikishi kwa mitambo 25 ya uzalishaji wa hewa tiba ya oksijen katika vituo 25 vya kutolea huduma ya afya nchini. Vituo vilivyotembelewa ni Hospitali ya taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mtwara, Hospitali ya maalum ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tumbi, Mwananyamala, Temeke, Bombo, Mawenzi, Mt. Meru, Singida, Iringa, Bukoba pamoja na hospitali saba (7) za Halmashauri za Mafia, Ulanga, Ngara, Nzega, Mafinga, Ukerewe na Kahama.

224. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya matumizi, ukarabati na usimamizi wa vifaa tiba, mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni na mashine 125 za Utrasound zilizosimikwa katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na vyuo vya afya. Aidha, wataalam 125 wa ufundi wa vifaa tiba wamepatiwa mafunzo ya msingiya utunzaji na matengenezo ya mashine hizo.

Huduma za Damu Salama

225. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa damu salama ya kutosha nchini. Jumla ya chupa za damu 273,105 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 82 ya lengo la kukusanya chupa 332,747 kwa mwaka 2025/2026. Makusanyo hayo yamewezekana kutokana na uwekezaji katika uhamasishaji wa jamii kuhusu kuchangia damu kwa hiari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, madhehebu ya dini, timu za ukusanyaji damu za halmashauri pamoja na timu za hospitali za rufaa za kanda na mikoa. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ubora wa huduma za damu nchini ambapo kanda sita (6) za damu salama zimeendelea kushikilia ithibati za kimataifa, kanda mpya ya Dodoma imependekezwa kupatiwa ithibati baada ya kufanyiwa ukaguzi mwezi Februari 2026. Ithibati hizi zina maana kuwa huduma za damu zinakidhi viwango vya kimataifa vya ubora na usalama, hivyo kupunguza hatari ya maambukizi kupitia damu na kuongeza ufanisi wa huduma za afya. Vilevile, huongeza hadhi ya nchi kimataifa kwa kuonesha uwezo wa kutoa huduma salama na zinazoaminika, na kuvutia ushirikiano wa kitaalamu na uwekezaji katika sekta ya afya.

226. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kutoa huduma za damu salama nchini, Mpango wa taifa wa damu salama ulifanyiwa tathmini ya kipimo cha uhakiki ubora kwa mujibu wa kiwango cha kimataifa cha ISO 17043. Kupitia tathmini hiyo, Mpango wa taifa wa damu salama umefanikiwa kupata ithibati na cheti kutoka South Africa National Accreditation System – SANAS hatua inayothibitisha ubora na uaminifu wa huduma za maabara nchini. Hatua hizo zinaendelea kuimarisha mifumo ya ubora na usalama wa huduma za damu na hivyo kuongeza imani ya wananchi na wadau katika huduma hizo muhimu.

227. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama umefanikiwa kutengeneza mazao ya damu chupa 627 na kusambaza katika hospitali zinazotumia mazao hayo kama hospitali ya taifa, hospitali maalum na hospitali za kanda ikilinganishwa na chupa 614 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imefanikiwa kuandaa sampuli za kuhakiki ubora wa

upimaji wa makundi ya damu na kusambaza katika hospitali 302 ili kuhakiki ubora wa huduma za damu zinazotolewa.

"Damu haiwezi kutengenezwa, inapatikana tu kutoka kwa watu wenye moyo wa ukarimu. Huhitaji kuwa daktari ili kuokoa maisha bali hata kwa kuwa mchangiaji tu wa damu. Niwasihi wananchi wenzangu kujitokeza kwa wingi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wengi".

Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii

228. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Maabara imefanikiwa kupima jumla ya sampuli80,111 za magonjwa mbalimbali ya milipuko. Sampuli hizo zinahusisha uchunguzi wa magonjwa yakiwemo Mpox, murburg, mafua makali ya influenza, kipindupindu, surua, rubella, kimeta, dengue, kichaa cha mbwa, matende, rotavirus, Human Papilloma Virus, wingi wa virusi vyaUKIMWI, na utambuzi wa maambukizi ya VVU kwa watoto wachanga. Maabara hii inaendelea kuwa kituo cha taifa cha ufuatiliaji wa magonjwa pamoja na kuendelea kuwa kituo cha umahiri cha ufundishaji wa usalama, upimaji na udhibiti wa vimelea hatarishi vya magonjwa yanayoweza kusababisha mlipuko na majanga.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

229. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya, iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura 177 yenye majukumu makuu ya kufanya uchunguzi wa Kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo, utoaji ushahidi wa kitaalam mahakamani na usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani.

230. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la kufanya uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo nchini, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu iliendelea kutoa huduma ya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo ambapo jumla ya sampuli 152,130 zilipokelewa. Kati ya sampuli hizo, sampuli 142,085 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 73 ya lengo la kuchunguza sampuli

194,310. Mwelekeo wa sampuli zilizochunguzwa umeongezeka kutoka 132,737 hadi kufikia sampuli 142,085 sawa na ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Uchunguzi huo umeisaidia Serikali na mamlaka nyingine kufanya maamuzi stahiki katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki kwa wananchi na katika vyombo vya maamuzi.

231. Mheshimiwa Spika, maabara tano (5) za mamlaka zenye ithibati ya kimataifa ambazo ni maabara ya mazingira, chakula, maikrobaiolojia, vinasaba vya binadamu na sayansi jinai, zilifanyiwa ukaguzi wa umahiri wa uchunguzi wa kimaabara kwa mujibu wa matakwa ya ithibati (ISO 17025:2017) kutoka taasisi ya ithibati ya Southern African Development Community Accreditation Services (SADCAS) na kuendelea kushikilia hadhi hiyo. Aidha, ukaguzi wa umahiri wa uchunguzi kwa mara ya kwanza kwa Maabara ya Sayansi Jinai Kemia ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa (ISO 17025:2017) na kufanikiwa kupendekezwa kupewa ithibati ya kimataifa. Hii ina maana kuwa maabara hizi zina uwezo wa kutoa matokeo sahihi, ya kuaminika na yanayotambulika kimataifa. Ithibati hii ni muhimu katika kulinda afya ya wananchi kupitia uchunguzi sahihi wa chakula, mazingira na vinasaba, Pamoja na kuimarisha ushahidi wa kisayansi katika masuala ya kisheria (forensic). Aidha, huongeza uaminifu wa nchi katika biashara na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, kwani matokeo ya maabara yanatambulika kimataifa bila kuhitaji uthibitisho wa ziada.

232. Mheshimiwa Spika, katika kuchangia utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi Mamlaka ilitoa ushahidi wa kitaalam mahakamani kwa mashauri 621 sawa na asilimia 80 ya mashauri 778 yaliyopokelewa. Aidha, kulikuwa na kupungua kwa asilimia 23 ikilinganishwa na mashauri 811 yaliyotolewa ushahidi mahakamani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025.

233. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Mamlaka ilisajili wadau 1,301 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 52 ya lengo la kusajili wadau 2,496 kwa mwaka. Lengo la kusajili wadau haoni kuendelea na juhudiza kulinda afya, mazingira na usalama wa nchi dhidi ya kemikali hatarishi na bashirifu

zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya au silaha za kemikali. Pia, Mamlaka ilitoa mafunzo kuhusu usafirishaji salama wa kemikali nchini kwa wadau wa kemikali 1,914. Mafunzo hayo yamesaidia kuwapa uelewa wa namna bora ya kujilinda, kulinda afya ya watu wengine pamoja na kulinda mazingira wakati wa usafirishaji wa kemikali hizo. Aidha, Mamlaka ilitoa jumla ya vibali 68,885 sawa na asilimia 76 ya lengo la kutoa vibali 90,700 kwa mwaka. Vilevile, jumla ya maghala 2,804 ya kuhifadhi kemikali yalikaguliwa, sawa na asilimia 78 ya maghala 3,585 yaliyopangwa kukaguliwa kwa mwaka.

234. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha Mamlaka inakuwa na vifaa vya kutosha kulingana na mahitaji na teknolojia ya kisasa, Serikali imeiwezesha Mamlaka kununua na kusimika mtambo wa Seq Studio Genetic Analyser na fire suppresSIYOn system na kuanza kufanya kazi katika maabara ya vinasaba vya binadamu Dodoma, mtambo wa Real Time PCR katika maabara ya vinasaba vya binadamu Dar es Salaam na mitambo midogo 85 katika ofisi ya makao makuu na ofisi za kanda. Mitambo hiyo ya maabara imewezesha matokeoya uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa wakati baada ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

Huduma za Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

235. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya zenye ubora, ufanisi na zilizo salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kununua, kutunza na kusambaza aina mbalimbali za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaaza afya, Serikali imeendelea kutoa fedha za ruzuku kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya kupitia MSD, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 275 zimetolewa.

Hali ya Upatikanaji wa Dawa na Bidhaa Muhimu za Afya

236. Mheshimiwa Spika, Wizara imeimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo upatikanaji wa

bidhaa za afya za kipaumbele aina 382, umeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 88.8 katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na wastani wa asilimia 86.2 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Hali ya upatikanaji wa dawa kwenye zahanati ni asilimia 79.5, vituo vya afya asilimia 82.8, hospitali za halmashauri asilimia 83.8, hospitali za rufaa za mikoa asilimia 95.9 na hospitali za kanda, maalum na taifa asilimia 97.7. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu za kipaumbele 382 katika Bohari ya Dawa umeimarika kutoka wastani wa asilimia 68 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 73 mwezi Machi 2026.

237. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia MSD huagiza zaidiya asilimia 80 ya bidhaa zaafya kutoka nje ya nchi wakati chini ya asilimia 20 ya bidhaa za afya huzalishwa na viwanda vya ndani. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuchukua hatua za kimkakati ili kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya kutoka nje, kuimarisha usalama wa afya wa Taifa, kuongeza uzalishaji wa ndani, kukuza ajira na kujenga uwezo wa nchi kujibu dharura za kiafya bila kutegemea masoko ya nje. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeanzisha kikosi kazi maalum kiitwacho Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce (PIAT) chenye jukumu la kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji katika uzalishaji wa dawa, vifaa tiba na bidhaa nyingine za afya nchini. Kupitia kikosi kazi hicho, Wizara imefanya mikutano maalum minne (4) na wadau wa uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, ambapo wawekezaji 64 wameonesha nia ya kuwekeza nchini.

238. Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha uwekezaji huo, Serikali imetenga eneo lenye jumla ya ekari 400 lililopo Mloganzila kwa ajili ya uendelezaji wa Kongani Maalum ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba, yaani Mloganzila Pharmaceutical and Medical Devices Special Economic Zone. Aidha, tarehe 8 Mei, Serikali ilianza rasmi hatua za uendelezaji wa eneo hili maalum, ikiwa ni alama muhimu ya mageuzi ya sekta ya afya kutoka katika utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje, kuelekea uzalishaji wa ndani, uhamishaji wa teknolojia, utafiti, ubunifu na biashara ya bidhaa za afya ndani na nje ya nchi. Kongani hii itakuwa kitovu cha uzalishaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine muhimu za afya, na hivyo kuiwekaTanzania katika nafasi

boraya kuwa kituo cha kikanda cha uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za afya.

239. Mheshimiwa Spika, Serikali pia katika Bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya kujenga maabara yenye hadhi ya Bio-Equivalent Laboratory. Maabara hii ni muhimu sana kwa kuwa itawezesha kufanya tathmini za kisayansi za ubora, usalama na ufanisi wa dawa zinazozalishwa nchini pamoja na zile zinazoingizwa kutoka nje. Uwepo wa maabara hii utaimarisha uwezo wa nchi kuthibitisha kuwa dawa zinazozalishwa ndani zinafanya kazi kwa kiwango sawa na dawa rejea, hivyo kuongeza imani ya wananchi, wataalam, MSD na masoko ya kikanda katika bidhaa zinazozalishwa nchini. Aidha, maabara hii itapunguza utegemezi wa kufanya vipimo nje ya nchi, itapunguza gharama na muda wa usajili wa dawa, na itachochea ukuaji wa viwanda vya ndani kwa kuwawezesha wazalishaji kupata uthibitisho wa ubora ndani ya nchi.

240. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha dhamira hii inakwenda sambamba na teknolojia ya kisasa, Serikali imesaini makubaliano na kampuni ya Sartorius kutoka Ujerumani kuwa mbia wa teknolojia katika eneo la biopharmaceuticals. Ushirikiano huu utasaidia kujenga uwezo wa nchi katika uhamishaji wa teknolojia, mafunzo ya wataalam, uanzishaji wa miundombinu ya uzalishaji wa bidhaa za kibayoteknolojia, pamoja na kushirikiana na Serikali katika kuendeleza uzalishaji wa chanjo muhimu. Hatua hii ni ya kimkakati kwa sababu chanjo, dawa na bidhaa za kibayoteknolojia si bidhaa za kawaida; ni sehemu ya usalama wa afya, usalama wa Taifa na uwezo wa nchi kujilinda dhidi ya magonjwa ya mlipuko na majanga ya kiafya.

241. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hatua hizi zinaonesha kuwa Serikali haijengi viwanda vya dawa kwa mtazamo wa kibiashara pekee, bali inajenga msingi wa uhuru wa kiafya wa Taifa. Kupitia PIAT, Kongani Maalum ya Mloganzila, maabara ya Bio-Equivalent, na ushirikiano wa kimkakati na wabia wa teknolojia kama Sartorius, Tanzania inaweka misingi ya kujitosheleza kwa bidhaa za afya, kukuza uchumi wa viwanda, kuongeza ajira za wataalam, kuvutia uwekezaji na kulinda maisha ya wananchi. Huu ni mwelekeo mpya unaotafsiri kwa vitendo maono ya Serikali ya

kujenga Taifa lenye uwezo wa kuzalisha, kuthibitisha, kusambaza na kutumia bidhaa zake za afya kwa usalama, ubora na uhakika.

Mapambano ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa.

242. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya tathmini ya uanzishwaji wa timu za usimamizi na ufuatiliaji wa Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa (UVIDA) katika hospitali nane (8) Tanzania Bara ambapo vituo vinne (4) kati ya hivyo vilipata zaidi ya asilimia 50 ikionesha vinahitaji kuwezeshwa kwa kiasi kidogo ili kuanza kutekeleza afua za UVIDA. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Taifa ya Mapambano Dhidi ya UVIDA inayofanya kazi chini ya mwamvuli wa Afya Moja iliandaa maadhimisho ya Kanda ya Afrika yanayojulikana kama "Continental World Antimicrobial Resistance Awareness Week". Maadhimisho hayo yalifanyika nchini kuanzia tarehe 02 hadi 05 Desemba, 2025 yakiwa yamebeba ujumbe wa "Act Now, protect our present, Secure our future", yaani "Chukua hatua sasa, linda leo yetu, hakikisha kesho yetu". Maadhimisho hayo yalifanyika sambamba na Kongamano la Kisayansi lililolenga kushirikisha wadau mbalimbali katika kujadili utekelezaji wa afua za UVIDA nchini.

Bohari ya Dawa (MSD)

243. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa (MSD) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa Sheria ya Bohari ya Dawa Na.13 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021 ikiwa na majukumu manne (4); uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vinavyohudumiwa na MSD vimeongezeka na kufika vituo 8,893 kutoka vituo 8,619 mwezi Machi 2025 sawa na ongezeko la vituo 274.

244. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa huagiza zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa zaafya kutoka nje ya nchi ambapo bidhaa zenye mikataba, hutumia miezi mitatu (3) tangu uagizaji hadi upokeaji wa shehena na kwa bidhaa zisizo na mikataba hutumia hadi miezi

sita (6) au zaidi. Vilevile, kwa baadhi ya bidhaa ambazo huhitaji uzalishaji baada ya kuagiza, huweza kuchukua hadi miezi tisa (9) tangu uagizaji hadi upokeaji wa bidhaa hizi kutoka kwa wazalishaji.

245. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imeendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kuhakikisha uwepo wa mikataba ya muda mrefu ambapo mpaka sasa tuna mikataba 479 yenye jumla ya bidhaa 1,354 kati ya bidhaa 1,725 zinazopaswa kununuliwa, kutunzwa na kusambazwa na MSD kwa muda wote. Kwa upande wa bidhaa za afya za kipaumbele aina 382, bidhaa 361 sawa na asilimia 94.5 zina mikataba ya kudumu na bidhaa nyingine zilizosalia zipo katika hatua mbalimbali za zabuni. Vilevile, katika kulinda viwanda vya ndani, MSD imenunua bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi bilioni 62.5 ikiwemo maji tiba kutoka kwa wazalishaji wa ndani ili kuvutia wawekezaji na kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya.

246. Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele 382 kwenye maghala ya MSD umefikia asilimia 71 kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya mwezi mmoja na zaidi ikilinganishwa na asilimia 65 iliyorekodiwa mwezi Desemba, 2025. Aidha, upatikanaji wa bidhaa za dawa pekee umefika asilimia 72 ikilinganishwa na asilimia 64 iliyorekodiwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 kwa kiwango kinachokidhi mwezi mmoja na zaidi. Vilevile, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Miradi Msonge umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 81 mwaka 2024/2025 hadi kufikia asilimia 87 Machi, 2026. Pia, hali ya utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 83.

247. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo, mashine za mionzi kwa ajiliya kinywa na meno, mashine za usingizi, ultrasound, Digital X-Ray, majokofu ya kuhifadhia miili na jenereta vyenye thamani ya Shilingi bilioni 116.4.

248. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa inamiliki maghala yenye mita za mraba 48,254 sawa na asilimia 48 ya mahitaji yake ya miundombinu baada ya kukamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa katika kanda ya Dodoma na Mtwara yenye jumla ya mita ya mraba 12,000 yaliyogharimu kiasi cha Shilingi bilioni 42. Katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maghala, Bohari ya Dawa imekodi mita za mraba 20,605 kutoka taasisi binafsi, hivyo kufikisha jumla ya mita za mraba 68,859 sawa na asilimia 68.9 ya mahitaji kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa za afya. Pamoja na jitihada za kukodi kutoka Sekta binafsi, bado maghala hayo hayakidhi viwango vya uhifadhi kwa kuzingatia nafasi na uhifadhi salama wa bidhaa husika hivyo kuhatarisha ubora na usalama wa bidhaa husika. Aidha, mahitaji halisi ya kutosheleza utunzaji wa bidhaa za afya ni mita za mraba 100,000 zinazoendana na kasi ya uwekezaji wa Serikali katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na ongezeko la idadi ya watu nchini. Kwa sasa Bohari ya Dawa inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ghala katika Mkoa wa Geita – Chato uliofikia asilimia 40 ya utekelezaji na hadi kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Shilingi bilioni 19.

249. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, uhakiki mali umefanyika kwa Kanda zote na bidhaa za afya zipo sawa kama ilivyo kwenye mfumo wa ERP epicor10. Kiasi cha bidhaa za afya za kundi la kawaida ilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 235.7, bidhaa za miradi msonge Shilingi bilioni 313.1, na bidhaa maalum Shillingi bilioni 13.1. Kwa Bohari ya Dawa kuwa na bidhaa za thamani hii kunatoa uhakika wa usalama wa afya katika kipindi cha kawaida na pale ambapo majanga yakitokea.

250. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kutekeleza mpango wa usambazaji wa mizunguko sita kwa mwaka, ambapo vituo hupatiwa bidhaa kila baada ya miezi miwili, tofauti na mfumo wa awali wa mizunguko minne kwa mwaka. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Bohari ya Dawa imefanikiwa kusambaza bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi bilioni 317 nchi nzima. Aidha, utekelezaji wa usambazaji huo ulifanyika kwa kuzingatia muda uliopangwa kwa wastani wa asilimia 98, hatua iliyochangia

kwa kiasi kikubwa kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya wakati wote. Katika kipindi hiki, Taasisi imefanya usambazaji wa vifaa tiba katika maeneo yote muhimu ikiwa ni pamoja na vifaa vya huduma za mama na mtoto, mashine za kuchuja damu na huduma za kinywa na meno.

251. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha afya ya mama na mtoto Bohari ya Dawa ilipokea mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9 kupitia mradi wa Safer Birth Bundle of Care (SBBC) PLUS kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa bidhaa za uzazi salama kwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya. Hadi kufikia Machi 2026, bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.5 zilikuwa tayari zimesambazwa sawa na utekelezaji wa asilimia 83.1.

Kwa vituo vilivyo chini ya OWM-TAMISEMI, Bohari ya Dawa ilipokea mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.3 ambapo bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 7.9 sawa na asilimia 77 zilikuwa tayari zimenunuliwa na kusambazwa. Aidha, hadi kufikia Machi 2026, kwa upande wa huduma za dharura kwa akinamama na watoto wachanga (CEmONC) vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 27.1 kati ya mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 27.9 sawa na asilimia 97.3 vimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

252. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa ajili ya huduma ya kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo zinakuwepo kwa gharama nafuu ambapo kwa sasa gharama ya mzunguko mmoja imepungua kutoka shilingi 250,000.00 hadi 150,000.00. Kwa kipindi hiki Bohari ya Dawa imesambaza jumla ya mashine 145 za kuchuja damu katika hospitali 16, ambapo hospitali 13 kati ya hizo tayari zinaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa. Aidha, kwa sasa Bohari ya Dawa ina mashine 19 za kuchuja damu, viti 22 vya kuchuja damu na mashine 21 za kuchanganya dawa kiautomatiki zilizopo kwenye maghala.

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)

253. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilianzishwa kupitia Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 ikiwa na jukumu kuu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine.

254. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa na vipukusi, kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 917 ya usajili wa dawa za binadamu, ambapo maombi 826 sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini. Aidha, maombi 643 sawa na asilimia 78 ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na kusajiliwa. Vilevile, maombi 179 ya usajili wa dawa za mifugo yalipokelewa, ambapo maombi 169 sawa na asilimia 94 yalifanyiwa tathmini kati ya hayo maombi 67 sawa na asilimia 40 yalikidhi vigezo na kusajiliwa.

255. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipokea maombi 605 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na dawa na vipukusi ambapo maombi 463 sawa na asilimia 77 yalifanyiwa tathmini na maombi 453kati ya hayo sawa na asilimia 98 yalikidhi vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara. Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda 80 (76 vya nje ya nchi na vinne (4) vya ndani ya nchi) na matokeo ni kwamba, viwanda 41 vya nje ya nchi na vitatu vya ndani ya nchi vilikidhi vigezo na kiwanda kimoja (1) cha ndani ya nchi na viwanda 35 vya nje ya nchi havikukidhi vigezo kutokana na mapungufu mbalimbali. Vilevile, maeneo 8,058 ya biashara ya dawa na vipukusi yalikaguliwa ambapo maeneo 7,066 sawa na asilimia 88 yalikidhi vigezo.

256. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilipokea jumla maombi ya vibali 3,441 vya dawa, vipukusi na malighafi za bidhaa hizo vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi ambapo maombi 3,334 ni ya kuingiza nchini na 107 ni ya kusafirisha nje ya nchi. Kati ya vibali vilivyoombwa, vibali 3,281 vilitolewa kati ya hivyo 3,186 ni vya kuingiza bidhaa nchini na 95 ni vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Kati ya vibali 3,281 vilivyotolewa, vibali 2,519 vilikaguliwa katika vituo vya forodha ambapo vibali 2,487 ni vya kuingiza bidhaa nchini na 32 ni vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Vilevile, jumla ya tani 257.7 za dawa zenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 15.2

ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

257. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi, Mamlaka imepokea jumla ya maombi 531 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi (Vifaa tiba 347 na vitendanishi 184), kati ya hayo maombi 488 (Vifaa tiba 314 na vitendanishi 174) sawa na asilimia 92 yalifanyiwa tathmini na maombi 217 (vifaa tiba 135 na vitendanishi 82) yaliidhinishwa. Aidha, maombi 489 ya usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi yalifanyiwa tathminina maeneo 465sawa na asilimia 95 yalikidhi vigezo na kusajiliwa.

258. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilikagua viwanda 41 (34 vya nje ya nchi na saba (7) vya ndani ya nchi) na maeneo 901 yanayojihusisha na biashara za vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 886 sawa na asilimia 98 na viwanda saba (7) vya ndani ya nchi vilikidhi vigezo. Pia, viwanda vya nje vitano (5) vilikidhi vigezo na viwanda vya nje 29 havikukidhi vigezo kutokana na upungufu mbalimbali.

259. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Mamlaka ilipokea maombi5,166 ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi vifaa tiba, vitendanishi na malighafi za vifaa tiba, ambapo vibali 4,762 vilitolewa. Aidha, jumla ya tani 180 za vifaa tiba na vitendanishi zenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 15 ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama na hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu. Vilevile, jumla ya sampuli 415 za bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi vilichunguzwa na vilikidhi vigezo. Hii inaashiria uwepo wa ubora na usalama wa bidhaa ambazo zimedhibitiwa na Mamlaka katika soko.

Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

260. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na vijana ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wanawake 4,626,300 sawa na asilimia 40 ya walengwa walipatiwa huduma za kisasa za uzazi wa mpango, kati yao 856,488 walipatiwa huduma hiyo

baada ya kujifungua. Vilevile, watoa huduma 219 kutoka mikoa 11 ya Lindi, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Shinyanga, Geita, Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam walipata mafunzo ya uzazi wa mpango. Aidha,jumla ya vituo 53vya kutolea huduma za afya vimeboreshwa kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni na kufikia idadi ya vituo 630 ikilinganishwa na 577 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

261. Mheshimiwa Spika, jumla ya kinamama wajawazito 2,218,640walihudhuria kliniki na kupatiwahuduma za afyawakati waujauzito na kati yao asilimia 73.3 walihudhuria angalau mara nne. Aidha, kinamama 1,892,998 walijifungua na kati yao asilimia 98 walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma zaafya nawaliojifungua kwa njia ya upasuaji ni asilimia 11. Kutokana na matokeo ya tafiti mbalimbali duniani asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea baada ya kujifungua.

Katika jitihada za kupunguza vifo hivyo, jumla ya kinamama 1,758,507 sawa na asilimia 93 ya walengwa na watoto wachanga 1,764,093 sawa na asilimia 93 ya walengwa, walipata huduma ndani ya saa 24 baada ya kujifungua. Aidha, jumla ya vizazi hai 1,917,647 vilitolewa taarifa kutoka vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Takwimu zinaonesha kuwa watoto wachanga 112,336 sawa asilimia 5.9 walizaliwa na uzito pungufu. Aidha, asilimia 94.8 ya Watoto hawa walianza kunyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa.

262. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, vifo vya Watoto wachanga vinaweza kupungua kwa zaidi ya asilimia 50 ikiwa kila halmashauri itaanzisha wodi maalumu kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu (Neonatal Care Unit -NCU). Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya NCU 76 zimeanzishwa na kufikia 438 ikilinganishwa na 362 kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa NCU kubwa na ya kisasa katika hospitali ya Wilaya ya Kwimba na imeanza ujenzi wa NCU nyingine kubwa za kisasa 35 (15 ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa na 20 hospitali za wilaya). Aidha, vifaa mbalimbali kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu vimenunuliwa na kusambazwa;

vikiwemo CPAP 1,350, Phototherapy mashine 182, Radiant warmer 495 na mashine ya kuzalisha oksijeni 252.

263. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imenunua na kusambaza bidhaa za afya ya uzazi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, bidhaa hizo ni; depo provera dozi 1,766,340 sawa na asilimia 85 ya lengo, vidonge vya uzazi wa mpango 1,643,623 sawa na asilimia 84 ya lengo, vipandikizi aina ya implanon NXT 358,084 sawa na asilimia 79 ya lengo, vitanzi aina ya copper T 123,377 sawana asilimia 83 ya lengo.Aidha, bidhaa nyingine ni; dawa ya sindano ya oxytocin ya kuzuia kupoteakwa damu baada ya kujifungua chupa 3,148,130 sawa na asilimia 97 ya lengo, sindano ya magnesium sulphate ya kuzuia na kutibu kifafa cha mimba chupa 234,170 sawa na asilimia 94 ya lengo, vidonge vya misoprostol 340,083 sawa na asilimia 93 ya lengo. Vilevile, dawa za watoto; vidonge myeyuko vya amoxycilin 41,039,930 kwa matibabu ya homa ya mapafu (nimonia) sawa na asilimia 96 ya lengo, pakiti za ORS na zinki zilizofungashwa pamoja 650,690 kwa matibabu ya kuharisha sawa na asilimia 87 ya lengo.

264. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma rafiki ya uzazi kwa vijana, vituo 69 vya kutoa huduma rafikiya afya ya uzazi kwa vijana vimeongezeka na kufikia 1,630 ikilinganishwa 1,561 vilivyokuwepo kipindi kama hiki 2024/2025. Lengo ni kupunguza mimba katika umri mdogo, maambukizi ya VVU na kuimarisha huduma za masuala ya jinsia. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya vituo jumuishi 15 vya kutoa huduma kwa waathirika wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto vimeongezeka na kufikia vituo 46. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya waathirika 137,146 walipatiwa huduma na kati yao asilimia 13 walikuwa wamefanyiwa ukatili wa kingono, asilimia 35 walikuwa wamefanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 27 ya waathirika walikuwa ni watoto.

265. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, vituo vya uchunguzi wa matiti vimeongezeka kufikia 1,700 kutoka 1,375 sawa na asilimia 23. Aidha, jumla ya wanawake 2,443,392 walifanyiwa uchunguzi wa matiti na kati yao asilimia 0.3 walibainika kuwa na dalili za awali za saratani ya matiti na

kupewa rufaa kwa ajili ya matibabu zaidi. Vilevile, jumla ya wanawake 501,615 walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi na kati yao asilimia 2.5 walihisiwa kuwa na saratani ya mlango wa kizazi, asilimia 1.1 walikuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wakizazi na walipatiwa matibabu. Katika kuimarisha huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi, Wizara imenunua na kusambaza mashine tiba joto 392 za kutibu mabadiliko ya saratani ya mlango wa kizazi.

266. Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuimarisha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto nchini, kikao cha Marais wa Umoja wa Afrika kilichofanyika mwezi Februari 2026, kilimpa heshima na kumtambua **Mheshimiwa Dkt. SamiaSuluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kama kinara wa kuongoza juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto barani Afrika.

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

267. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya, kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 5,000 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na kufanya jumla ya watumishi katika sekta ya afya kufikia 182,430. Kati ya watumishi hao, 142,794 sawa na asilimia 78 wapo katika ngazi ya afya ya msingi na 34,047 sawa na asilimia 19 wanafanya kazi katika ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum na taifa. Watumishi 5,589 wapo kwenye mashirika, vyuo vya mafunzo, wakala na idara zilizopo chini ya Wizara ya Afya sawa na asilimia 3.0. Vilevile, jumla ya wataalam 9,039 waliajiriwa kwa utaratibu wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani. Kati yao, watumishi 3,717 wameajiriwa kwenye hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum na hospitali ya taifa Muhimbili na watumishi 5,322 wameajiriwa ngazi ya afya ya msingi.

268. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji wa mafunzo

katika vyuo vya afya vya umma, binafsi na vinavyomilikiwa na taasisi za dini ili kuhakikisha vinazalisha wataalam mahiri na wenye weledi. Kwa mwaka wa masomo 2025/2026, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi lilifanya uchaguzi wa wanafunzi 39,698 sawa na asilimia 88.7 ya waombaji 44,760 waliotuma maombi ya kujiunga na programu mbalimbali za kada za kati za afya. Kati ya waliochaguliwa, wanafunzi 5,057 sawa na asilimia 12.7 walipangiwa vyuo vya Serikali, na wanafunzi 34,641 sawa na asilimia 87.3 walipangiwa vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za dini.

269. Mheshimiwa Spika, Wizara iliratibu mitihani ya kitaifa ya muhula wa pili kwa kada za kati za afya na jumla ya wanafunzi 85,959 kutoka vyuo vyenye programu za mafunzo ya afya ngazi ya kati walishiriki kwenye mitihani hiyo. Kati yao, wanafunzi 42,511 sawa na asilimia 49.5 walifaulu mitihani ambapo kati ya waliofaulu, wanafunzi 14,401 walikuwa wa programu za Stashahada (NTA Level 6) wakiwa ni asilimia 89.6 ya wanafunzi wote wa ngazi hiyo. Aidha, katika kuimarisha uwezo wa wakufunzi wa vyuo vya afya katika mbinuza ufundishaji na upimaji wa wanafunzi, Wizara iliratibu na kufanikisha mafunzo mahsusi kwa wakufunzi 33 kutoka vyuo vya mafunzo ya kada za kati. Vilevile, ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mafunzo katika vyuo vya afya vya umma, Wizara iliratibu uendeshashaji wa mafunzo ya uongozi na usimamizi ambayo yalihusisha washiriki 60 wakiwemo wakuu wa vyuo na makamu wakuu wa vyuo vya afya.

270. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia ufadhili wa masomo wa Samia Health Super-Specialization Program umewezesha ufadhili wa masomo kwa wataalam wapya wa Sekta ya Afya 498 na kufanya jumla ya wataalam wanaofadhiliwa kusomea fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kufikia 1,483. Kati ya wataalam wapya waliopata ufadhili, 442 wamepata ufadhili wa kusoma vyuo vikuu vya ndani na watalaamu 56 wamepata ufadhili wa kusoma nje ya nchi. Aidha, hospitali na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya zimeweza kutoa ufadhili wa masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi kwa jumla ya watumishi 132 kwa kutumia mapato yao ya ndani.

271. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mabaraza ya Kitaaluma imeendelea kuhakikisha mafunzo endelevu kwa watumishi wa Sekta ya Afya yanatolewa kwa wataalam wanaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Jumla ya watumishi 84,351 walifanikiwa kukamilisha mafunzo na kutunukiwa vyeti. Haya ni matokeo chanya kutokana na Wizara kuendelea kuimarisha na kusisitiza matumizi ya mfumo maalum wa mafunzo kwa njia ya kielektroniki unaojulikana kama National e-Learning Platform for Health. Aidha, katika kipindi hiki watumiaji wapya waliosajiliwa kwenye mfumo ni 12,088 hivyo kufanya jumla ya watumishi waliosajiliwa hadi sasa kufikia 143,156.

"Hakuna mfumo wa afya unaoweza kufanya kazi bila wataalam waliopata mafunzo, wenye motisha na wanaopata stahiki zao ipasavyo". Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Matumizi ya TEHAMA

272. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo la **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** la kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika Sekta ya Afya inakuwa michache na inayosomana, Wizara inaendelea na maboresho ya mifumo ya TEHAMA na kuiunganisha na mifumo mingine ya Serikali. Hatua hiyo ni nguzo muhimu kwa ufanisi wa utoaji wa huduma, hususan wakati huu Wizara inapoendelea kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote. Wizara imeweka eneo hili kuwa kipaumbele cha kimkakati, ambapo mapitio ya mifumo yote iliyopo yanafanyika ili kuwezesha kuwa na mfumo wa kitaifa wa afya unaosomana (end-to-end health care management system) utakaotumika katika ngazi zote. Mfumo huo utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa wakati, kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa gharama za matibabu, kuzuia udanganyifu na mianya ya upotevu wa mapato, kusaidia kuthibitisha kwa ushahidi huduma zilizotolewa, kupanga na kufanya maamuzi ya kimkakati.

273. Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya mapitio ya sera, kanuni na sheria ili kuhakikisha matumizi ya mfumo huu ni ya lazima, dawa zote zitaandikwa kwa njia ya kielektroniki (e-prescription),

madai na malipo kufanyika kupitia mfumo huo. Hatua hizi ni muhimu ili kulinda uendelevu wa Bima ya Afya kwa Wote na kuimarisha ubora wa huduma kwa wananchi kwa kuhakikisha dawa zinazoandikwa zinapatikana ndani ya vituo vya kutolea huduma, kupunguza gharama kwa wagonjwa, kuondoa marudio ya vipimo vilivyofanyika na kuwezesha wataalam kuona taarifa za mgonjwa na mwendelezo wa matibabu yake kutoka kituo kimoja hadi kingine alichohudumiwa.

274. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa sasa imefanikiwa kutengeneza mfumo wa "Health Data Universal Application Programming Interface (HDU API)" ambao utawezesha kupokea, kutuma, kutunza kutoa rufaa kidigitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo mingine inayohitaji taarifa za wagonjwa kutoka hospitali za umma na binafsi. Mfumo huo utaunganisha mifumo mingine ya Afya eHMS, GOTHOMIS, mfumo wa dharura za Afya (NEMS), mfumo jumuishi wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii (UCS), Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Sekta ya Afya (HRHIS), Mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha ngazi ya Kituo (FFARS), Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE), Mfumo wa taarifa za usajili wa wataalam wa kada za afya (HPRS), mfumo wa taarifa za chanjo (VIMS), mfumo wa taarifa za utoaji wa huduma za afya (DHIS2) na Mfumo wa taarifa za wanaopata huduma za chanjo (TIMR). Aidha, kufikia Machi, 2026 mfumo wa Afya eHMS unatumika katika hospitali zote 28 za rufaa za mikoa na mfumo wa GOTHOMIS unatumika katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi kwa asilimia 96.

275. Mheshimiwa Spika, uunganishaji huo utawezesha wagonjwa kufungua jalada kwa njia ya mtandao, kupata namba ya malipo ya huduma zote za awali bila kulazimika kufika katika kituo cha kutolea huduma na kuandikiwa cheti cha dawa cha kidigitali baada ya kupata huduma. Kukamilika kwa mfumo huo kutapunguza msongamano, matumizi ya karatasi, muda wa kusubiri huduma na kuongeza ufanisi wa vituo vya kutolea huduma ikiwemo kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

Ufuatiliaji na Tathmini

276. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuandaa na kutoa takwimu mbalimbali za Sekta ya Afya kwa wakati ambazo hutumika kwa ajili ya kuandaa mipango na kufanya maamuzi. Katika kipindi hiki, Wizara imekamilisha taarifa nne (4) muhimu za kitakwimu ambazo ni Annual Health Statistical Bulletin Second Edition, *Annual Health Sector Performance Profile, Health Statistical Table and Figure, National Health Facility Atlas na Health Facility's Annual Mortality Statistics Report*. Taarifa hizi zinapatikana katika tovuti ya Wizara na tovuti ya Ofisiya MtakwimuMkuu wa Serikali – NBS.

277. Mheshimiwa Spika, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya kompyuta 2,758 katika mikoa yote 26 nchini kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa takwimu zenye ubora na kwa wakati katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kompyuta hizo zitawezesha vituo vya kutolea huduma za afya kufanya uchambuzi wa takwimu kwa kutumia mifumo ya kidigitali badala ya matumizi ya sasa ya karatasi, hivyo kupunguza nguvu kubwa na muda mrefu katika uchambuzi.

278. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu kwa kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ndani ya Sekta ya Afya. Katika kuhakikisha taaluma ya ufuatiliaji na tathmini inawafikia wataalam wengi zaidi nchini katika Sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na chuo cha CEDHA imeandaa mtaala maalum wa muda mfupi wa ufuatiliaji na tathmini katika Sekta ya Afya na kuanzisha mafunzo.

279. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya wataalam wa afya 756 wamepata mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kupitia mtaala huo, ikijumuisha baadhi ya waganga wakuu wa mikoa, halmashauri, timu za uendeshaji wa huduma za afya za mikoa na halmashauri na watumishi kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Wakurugenzi na wataalam kutoka katika Taasisi za Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Hospitali ya kanda ya ziwa Bugando, Hospitali maalum ya Taifa ya Afya ya Akili - Mirembe pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) wamepata mafunzo hayo. Vilevile, hospitali za

rufaa za mikoa nane (8) zilifikiwa na mafunzo ambazo ni hospitali ya rufaa ya mkoa ya Ligula, Tumbi, Mwananyamala, Dodoma, Manyara, Maweni, Geita na Hospitali ya Kumbukukumbu ya Mwalimu Nyerere – Mara.

Ugharamiaji wa Huduma za Afya

280. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora za afya kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini na kuhakikisha mpango wa bima ya afya kwa wote unatekelezwa kwa ufanisi.

281. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha Shilingi trilioni 3.1 kimetengwa kwa ajili ya kugharamia vipaumbele mbalimbali katika Sekta ya Afya ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, stahiki za watumishi na kuendelea kugharamia mafunzo ya wataalam katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi trilioni 2.54 kilichotengwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 22.

282. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya sera za kimataifa katika ufadhili wa huduma za afya, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini, ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya kugharamia bidhaa za afya imeongezeka hadi kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 398.2 kutoka Shilingi bilioni 200 zilizotengwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 99. Ongezeko hili limewezesha ununuzi na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) pamoja na dawa nyingine muhimu nchini, ambapo hadi kufikia Machi 2026 kiasi cha Shilingi bilioni 275 sawa na asilimia 69 ya fedha zilizotengwa kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo.

283. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** ya kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima

ya Afya kwa Wote kwa Awamu. Awamu ya kwanza ya utekelezaji ilianza rasmi tarehe 26 Januari, 2026 ambayo imehusisha usajili wa kaya 276,004 zisizo na uwezo ikiwa ni pamoja na wazee 235 na watoto 255 wanaoishi katika makazi maalum yanayomilikiwa na Serikali. Wanufaika wote katika awamu hii watagharamiwa na Serikali ambapo tayari kiasi cha Shilingi bilioni 48.8 kimetolewa. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya kaya 172,297 kati ya 276,004 sawa na asilimia 62 zimefikiwa na kufanya idadi ya wanufaika kuwa 463,228 sawa na asilimia 38 ya lengo la kusajili wananchi 1,206,319 ambapo kwa sasa wanufaika wameanza kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, katika zoezi la uhakiki na usajili ilibainika kuwa wananchi 15,747 walipoteza sifa za kugharamiwa bima ya afya na Serikali kutokana na sababu za kuimarika kiuchumi au kufariki na wananchi 192,208 hawakujitokeza wakati zoezi linatekelezwa. Kwa muktadha huo, jumla ya wananchi 671,183 sawa na asilimia 55 wamefikiwa kwa lengo la usajili wa wananchi 1,206,319 na usajili unaendelea ili kufikia wananchi 535,136 waliobaki.

284. Mheshimiwa Spika, katika zoezi la usajili wa makundi maalumu, kati ya wazee 235, wazee 141 wamepatiwa kadi za bima ya afya, 16 wamefariki, 33 hawakuwepo katika vituo vya kulelea wazee na 45 taarifa zao zilikosewa. Aidha, kwa upande wa watoto, kati ya watoto 255, watoto 205 wamekutwa wana kadi za bima ya afya zilizo hai, 49 hawakuwepo katika vituo vya kulelea watoto na mtoto mmoja (1) taarifa yake ilikosewa. Marekebisho ya taarifa zilizokosewa yanaendelea kufanyika ili wahusika waweze kusajiliwa na kupatiwa kadi za bima. Aidha wananchi wote ambao wamesajiliwa na kupatiwa kadi, wanaendelea kupata huduma.

285. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inaendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuhamasisha kuhusu umuhimu wa bima ya afya. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 makundi ya kimkakati yaliyofikiwa ni pamoja na viongozi wa ngazi za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo vyote nchini. Dhamira ya Wizara kufikia makundi hayo kwanza ni kujenga uelewa wa pamoja,

kuwawezesha kuelewa kwa kina malengo ya Serikali, mwelekeo wa kisera na dhana ya bima ya afya kwa wote, ili wawe washirika wa maendeleo katika kuifikisha sera hii kwa wananchi.

Vilevile, jumla ya vipindi 10 vya televisheni, 108 vya redio za kitaifa, 20 vya redio jamii na makala tano (5) kwenye magazeti matano (5) na mitandao ya kijamii zimetolewa. Aidha, jukumu la kuelimisha wananchi ni endelevu lenye lengo la kufikia wananchi wote ikiwa ni pamoja na kubadilisha fikra, mtazamo na tabia za wananchi ambao wengi wao hawana uelewa mzuri wa dhana ya bima ya afya.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

286. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa umma na wategemezi wao kupitia bima ya afya. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya ya mwaka 2009, Mfuko unajumuisha watumishi katika sekta ya umma, wafanyakazi kutoka katika sekta binafsi na makundi mbalimbali katika sekta zisizo rasmi. Majukumu ya kisheria ya Mfuko ni pamoja na kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuitunza, kusajili watoa huduma na kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma, kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa umma.

287. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umesajili wanachama 763,793 sawa na asilimia 68 ya lengo la kusajili wanachama 1,129,929. Asilimia 92 ya wanachama waliosajiliwa ni kutoka sekta binafsi na asilima 8 ni kutoka sekta ya umma. Idadi ya wanachama waliosajiliwa imewezesha Mfuko kuwa na wanachama 1,640,646 wenye jumla ya wanufaika 6,904,539 sawa na asilimia 10.5 ya watanzania wote. Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kuendelea kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

288. Mheshimiwa Spika, Mfuko umekusanya mapato jumla ya Shilingi bilioni 697.4 sawa na asilimia 74.3 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha zilizokusanywa, kiasi cha Shilingi bilioni 625.6 kimetokana na michango ya wanachama, kiasi cha Shilingi bilioni 66.4 kimetokana na mapato yatokanayo na uwekezaji na kiasi cha Shilingi bilioni 5.4 kimetokana na mapato kutoka vyanzo vingine kama vile maombi ya mikopo, usajili wa vituo na usimamizi wa huduma za ziada.

289. Mheshimiwa Spika, Mfuko umechakata jumla ya madai 47,502 na jumla ya Shilingi bilioni 399.3 zimelipwa sawa na asilimia 90 ya madai yaliyowasilishwa. Madai hayo yalichakatwa kwa wastani wa siku 51 ikilinganishwa na siku 58 kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Vilevile, asilimia 40 ya malipo yalilipwa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma vya Serikali na asilimia 60 kwenda vituo vya kutolea huduma vya binafsi na vituo vinavyomilikiwa namashirika ya dini. Aidha, Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanziaJulai 2025 hadi Machi, 2026 Mfuko umesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 2,259. Kati ya vituo hivyo, vituo 420 ni usajili wa mara ya kwanza na vituo 1,839 ilikuwa ni kwa sababu nyingine zikiwemo kuhuisha usajili, kubadilishiwa hadhi, kuongeza huduma, kubadilishiwa umiliki pamoja na kubadilisha eneo.

290. Mheshimiwa Spika, Mfuko umeendelea kupambana na kudhibiti udanganyifu kutoka kwa watoa huduma, waajiri binafsi, wanufaika wa huduma na watumishi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo imelenga kudhibiti na kuibua vitendo vya udanganyifu kutoka kwa watoa huduma na wanufaika, kuibua maeneno yenye upungufu katika shughuli za uendeshaji na kuchukua hatua stahiki. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umefanikiwa kufanya chunguzi 115 ambapo kufuatia chunguzi hizo kiasi cha Shilingi bilioni 2.1 kilibainishwa kwa ajili ya kurejeshwa.

291. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza kiwango cha kuridhishwa na huduma za Mfuko kwa wateja, mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa huduma imefanyika ikiwemo Mfuko

kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja kwa ajili ya kuhakikisha wanachama wanapata msaada wakati wote. Katika kipindi husika, kituo cha huduma kwa wateja kilishughulikia simu 206,351 kati ya 283,536 zilizopigwa sawa na asilimia 73. Aidha, asilimia 97 ya malalamiko yaliyowasilishwa kwa njia ya barua pepe na masanduku ya maoni yalijibiwa na kupatiwa ufumbuzi na kupandisha kiwango cha wateja kuridhika na huduma kufikia asilimia 94.

292. Mheshimiwa Spika, Mfuko umeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima ya afya na kuimarisha mahusiano na wadau kwa njia mbalimbali kama vile runinga, redio, mitandao ya kijamii, maonesho, majukwaa mbalimbali na tovuti ya Mfuko. Aidha, elimu kuhusu Vifurushi vya NHIF, elimu ya Bima ya Afya kwa Wote na mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa/udanganyifu pamoja na matumizi ya Self Service Portal ilitolewa.

293. Mheshimiwa Spika, Mfuko umeendelea kusisitiza matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake hususan kuwezesha mchakato wa ulipaji madai kwa kutumia mifumo inayojiendesha (inayotumia akili unde - AI); kuboresha mfumo wa usajili wa wanachama kwa kuunganisha pamoja na mifumo ya Serikali kwa ajili ya utambuzi mfano: TASAF; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Wizara ya Afya; Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA); kuboresha mfumo wa uandikishaji na kumwezesha mwanachama kujiandikisha na kujihudumia bila kulazimika kufika katika ofisi za Mfuko.

Utekelezaji wa Majukumu ya Mabaraza na Bodi za Kitaaluma

294. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya katika vituo vya kutolea huduma nchini. Katika kutekeleza ilo, mabaraza ya kitaaluma na bodi za usajili wa vituo binafsi ziliundwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kusimamia maadili ya kitaaluma, kusajili wataalam na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wataalam wa kada mbalimbali za afya.

295. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jumla ya mabaraza ya kitaaluma nane (8) na bodi za usajili mbili (2), ambazo ni pamoja n a; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria), Baraza la Wataalam wa Radiolojia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi.

296. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, mabaraza ya kitaaluma yalisajili jumla ya watalaam 14,310, usajili wa maduka ya dawa 330, usajili wa watarajali 3,004, mashauri ya kinidhamu yaliyofanyiwa kazi ni 30, mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) yametolewa kwa watalaam 102,066 (84,351 kupitia mfumo wa National e-Learning Platform for Health na 17,715 nje ya mfumo), ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya 654 na usajili wa vituo vya kutolea huduma 3,643. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma yametekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)

297. Mheshimiwa Spika, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lina mamlaka ya kisheria ya kusimamia taaluma na wanataaluma wa uuguzi na ukunga Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wauguzina wakunga 4,658walisajiliwa sawa na asilimia 77.6 ya lengo lakusajili wataalam 6,000 kwa mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na wataalam 4,506 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Idadi hiyo inafanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 59,257. Aidha, wauguzi na wakunga 741 wamepewa usajili wa awali na wanaendelea na mafunzo ya utarajali katika vituo 37 zikiwemo hospitali ya taifa, hospitali za rufaa za kanda na hospitali za rufaa za mikoa. Aidha, jumla ya wauguzi na wakunga 4,382 waliohitimu mafunzo yao kwa ngazi mbalimbali walifanya mtihani wa usajili na leseni. Idadi hiyo ilijumuisha watahiniwa 673 sawa na asilimia 15 ngazi ya shahada, watahiniwa 3,683 sawa na asilimia 84 ngazi ya stashahada na watahiniwa 26 sawa na asilimia 1 ngazi ya astashahada. Katika kipindi hiki, vyuo viwili (2) vimesajiliwa

kuendesha mafunzo ya stashahada ya uuguzi na ukunga. Vilevile, Baraza lilipokea na kuhakiki jumla ya maombi 485 ya wanafunzi waliodahiliwa vyuoni ambao waliomba usajili wa awali.

298. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kuimarisha uendelezaji wa wataalam ambapo jumla ya moduli 20 za mafunzo ya kujiendeleza zenye maudhui mbalimbali zilipokelewa, kuhakikiwa na kupewa ithibati. Vilevile, jumla ya mashauri 12 ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa kutoka Mkoa wa Tabora, Arusha na Dodoma ambapo ufuatiliaji wa awali umefanyika. Kati ya hayo, mashauri 10 yamekamilika na kuwasilishwa kwenye kikao cha 225 cha Baraza na kujadiliwa ambapo wauguzi na wakunga 17 walihusishwa. Aidha, maamuzi kwa tuhuma zilizosikilizwa yalikuwa kama ifuatavyo; wauguzi watano (5) walipewa onyo, sita (6) walisimamishwa kutoa huduma mwaka mmoja kwa kila mtaaluma, wawili (2) walisimamishwa kutoa huduma miezi sita, watatu (3) walisimamishwa kutoa huduma miezi mitatu (3) na mmoja (1) hakukutwa na hatia.

Baraza la Madaktari Tanganyika

299. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, majukumu ya msingi yaliyoendelea kutekelezwa na Baraza kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ni pamoja na kusimamia usajili, utendaji na maadili ya wataalam na taaluma ya udaktari. Katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 2,252 walisajiliwa ikilinganishwa na wataalam 3,794 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na kufanya jumla ya wataalam wote waliosajiliwa mpaka sasa kufikia 43,405. Aidha, jumla ya wataalam 1,978 wamepatiwa leseni kwa mara ya kwanza na wataalam 5,561 wamehuisha leseni zao na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliopatiwa leseni na kuhuisha leseni kufikia 7,539.

300. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya maombi ya mtihani wa kabla ya utarajali yaliyopokelewa yalikuwa 1,510 ambapo watahiniwa wa udaktari walikuwa 1,324, udaktari wa meno walikuwa 57, fiziotherapia walikuwa 69 na wataalam wa tiba ya chakula na lishe 60. Aidha, kwa mitihani ya baada ya mafunzo ya utarajali iliyofanyika

Desemba, 2025 jumla ya maombi yaliyopokelewa yalikuwa 1,425 kati ya hayo watahiniwa wa udaktari walikuwa 1,290, udaktari wa meno 59, fiziotherapia 41 na wataalam wa tiba ya chakula na lishe 35.

301. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko mapya 14 yalipokelewa. Kati ya hayo malalamiko sita (6) yamechunguzwa na Kamati ya Uchunguzi wa Mashauri ya Kimaadili. Uchunguzi wa awali unaendelea dhidi ya malalamiko nane (8). Aidha, mashauri 11 yaliyokuwa yamechunguzwa kipindi cha 2024/2025 dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya kitaaluma yalisikilizwa na Baraza. Maamuzi ya mashauri hayo yalihusisha madaktari 11 ni pamoja na madaktari wawili (2) kupewa onyo; watatu (3) kupewa onyo kali; mmoja (1) kufungiwa leseni ya kutoa huduma kwa muda wa miezi sita (6); wawili (2) kufungiwa leseni ya kutoa huduma kwa muda wa mwaka mmoja (1); mmoja (1) kufutiwa leseni ya kutoa huduma na wawili (2) hawakukutwa na hatia hivyo kuachiwa huru.

302. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kusimamia mafunzo endelevu kwa wanataaluma ambapo kwa kipindi hiki, Baraza limetoa ithibati kwa watoa mafunzo endelevu 79 na kozi za mafunzo endelevu 290. Aidha, Baraza limefanya usimamizi shirikishi kwenye vituovitano (5)vyakutolea mafunzo endelvu, pia limejengea uwezo hospitali za wilaya na vituo vya afya 25 ili kuweza kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma. Vilevile, limefanya uhamasishaji unaohusu mafunzo endelevu, weledi na maadili ya kitaaluma katika mikutano mitatu (3) ya vyama vya kitaaluma ambavyo ni Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto, Chama cha Fiziotherapia Tanzania na Chama cha Viungo Tiba na Vifaa Saidizi Tanzania.

Baraza la Famasi

303. Mheshimiwa Spika, Baraza la Famasi lina majukumu ya kusimamia taaluma na wataalam wa dawa, utendaji wake pamoja na usajili na kutoa vibali katika maeneo yanayotoa huduma za dawa na kuelimisha jamiijuu ya matumizi sahihiya

dawa. Baraza limesajili jumla ya wafamasia 216, fundi sanifu dawa1,001 wameandikishwa na fundi sanifu dawa wasaidizi 30 wameorodheshwa na kufikisha jumla ya wanataaluma 15,943 wanaotambuliwa hadi sasa. Kati ya hao, wafamasia ni 4,256; fundi sanifu dawa ni 10,512 na fundi dawa wasaidizi ni 1,175.
304. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi hiki, majengo ya biashara ya famasi 487 yamesajiliwa kutoa huduma ya dawa nchini, hivyo kufanya jumla ya majengo ya biashara ya famasi kuwa 3,718. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wafamasia 3,159, fundi dawa sanifu 5,305 na fundi dawa wasaidizi 324 wamefanya mafunzo endelevu na moduli 17 za mafunzo hayo zimeidhinishwa.

Baraza la Wataalam wa Radiolojia

305. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Baraza lilipitia maombi ya usajili wa wataalam wa radiolojia kwa kada mbalimbali na kufanya usajili wa awali, usajili wa kudumu, usajili wa muda, uandikishaji na uorodheshaji kwa wataalam waliokidhi vigezo. Katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 258 wamesajiliwa, kuorodheshwa na kuandikishwa, hivyo kufikia jumla ya wataalam2,473 waliosajiliwa hadi sasa. Aidha, jumla ya wataalam 1,554 wamehuisha leseni zao kati ya wataalam 2,083 wanaotegemewa kuhuisha leseni kwa mwaka 2025/2026 ikiwa ni sawa na asilimia 74.6.

306. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kusimamia watarajali wa kada za radiolojia nchini ambapo jumla ya watarajali 94 walipewa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili na kupangiwa vituo vya utarajali kwa njia ya mfumo. Aidha, katika kipindi hiki, Baraza lilitoa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili kwa wataalam wapatao 450 katika makongamano ya wanataaluma wa radiolojia. Vilevile, Baraza limepokea Shauri moja (1) la uvunjifu wa maadili ya taaluma ambalo limejadiliwa kwenye kikao cha baraza na kwa sasa lipo hatua ya ofisi ya mwanasheria kwa hatua zaidi.

Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria)

307. Mheshimiwa Spika, Baraza lina jukumu la usimamizi na udhibiti wa wataalam wa kada ya optometria, kliniki za optometria, wasambazaji wa vifaa na miwani na kuhakikisha kliniki zote zinazotoa huduma za optometria zinasajiliwa na kupatiwa leseni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Baraza limesajili jumla ya wataalam 80 kwa usajili wa kudumu ikilinganishwa na wataalam 40 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kwa usajili wa kudumu kufikia 520. Vilevile, jumla ya wahitimu 40 ngazi ya stahashada ya optometria kutoka vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi wamepewa usajili wa awali na kupangiwa vituo vya mafunzo chini ya usimamizi wa wataalam wazoefu kwa muda wa mwaka mmoja (1), ambapo mara baada ya mafunzo hayo watapewa usajili wa kudumu. Baraza limefanikiwa kusajili kliniki ishirini na mbili (22) zinazotoa huduma za optometria na kuwapangia watarajali wanne (4)kwa ajili yakupata mafunzo kwa vitendo.

308. Mheshimiwa Spika, Wataalam wa huduma za optometria takribani 342 wamefanya mafunzo ya kujiendeleza (CPD) kwa njia tofauti tofauti ikiwemo kwa njia ya mtandao, semina mbalimbali za kujengewa uwezo, na tafiti mbalimbali. Aidha, Baraza lilifanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za optometria katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Pwani, Songwe, Iringa, Mbeya na Njombe kwa lengo la kuwajengea uwezo waratibu ngazi ya mikoa (RHMTs) na halmashauri (CHMTs) ili wataalam na wamiliki wa vituo hivyo viweze kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo. Kati ya vituo 116 vilivyokaguliwa, vituo 51 vilibainika kuwa na changamoto mbalimbali na baadhi vilishauriwa namna bora ya kuendesha huduma za optometria, na vingine vilichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ya optometria ya mwaka 2007.

309. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Baraza lilifanya ukaguzi wa vyuo vitatu (3) vinavyotoa elimu ya optometria ambavyo ni Chuo cha Sayansi Kishiriki Mvumi, Hospitali ya CCBRT na Chuo cha City ndaki ya Mwanza ambapo Taasisi ya CCBRT inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya kada ya optometria ngazi ya stashahada. Aidha, Baraza lilifanya tathmini ya majaribio kwa wataalam wenye usajili wa awali wenye lengo

la kutambua uwezo wa wataalam hao katika vituo vyao vya kujifunzia. Katika zoezi hilo jumla ya wataalam 25 ngazi ya stashahada na watarajali watano (5) walitembelewa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

Baraza la Wataalam wa Maabara

310. Mheshimiwa Spika, Baraza lina jukumu la kuhakikisha wataalam wa maabara wamesajiliwa, wameandikishwa, kufuata miiko na maadili ya taaluma ya Maabara Pamoja na kusimamia utekelezaji wa mitaala ya mafunzo ya maabara ya afya. Katika kipindi hiki cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Baraza limesajili wataalam 1,987 ikilinganishwa na Wataalam 1,221 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Kati yao, wataalam 787 walisajiliwa kwa usajili wa kudumu, wataalam 75 walipata usajili wa kuandikishwa na wataalam 1,127 walipata usajili wa awali na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa kufikia 17,390. Wataalam walioweza kuhuisha leseni zao kwa kipindi hiki walikuwa 9,354. Aidha, jumla ya leseni 313 zimetolewa kwa wapimaji wa VVU waSIYO wataalam wa maabara. Vilevile, katika kipindi hiki mashauri mawili (2) ya kimaadili yalishughulikiwa na hatua za ufuatiliaji wa awali zinaendelea.

311. Mheshimiwa Spika, Baraza liliendesha mitihani ya usajili kwa kada ya maabara ngazi ya astashahada, stashahada na shahada, ambapo jumla ya wataalam 2004 walifanya mitihani na waliopata alama ya ufaulu walikuwa 1,424 sawa na asilimia 71.1. Katika kipindi hiki, Baraza liliendelea kuwasimamia watarajali wa maabara 436 katika vituo 25 vya kutolea mafunzo. Vilevile, Baraza limetoa mafunzo endelevu kwa wataalam wa maabara 7,766 ambao walipata alama.

312. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Baraza lilifanya ukaguzi wa maabara ya hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Njombe, Katavi, Songwe na Kagera kwa ajili ya kupatiwa watarajali wa maabara. Kati ya maabara hizo, maabara ya hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Katavi na Kagera zilifikia vigezo. Vilevile, Baraza limefanya ukaguzi katika chuo cha "Military College of Heath Lugalo" na Chuo cha Teofili Kisanji, University mkoani Mbeya kwa ajili kuanzisha kozi ya maabara. Pia, Baraza liliweza kufanya usimamizi shirikishi katika

mikoa tisa (9) ambayo ni Rukwa, Mbeya, Songwe, Iringa, Ruvuma, Njombe, Singida, Dodoma na Arusha. Jumla ya wataalam waliofikiwa katika zoezi hili walikuwa 667 ambapo kati yao, 656 sawa na asilimia 98.8 walikuwa na usajili wa Baraza.

Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira

313. Mheshimiwa Spika, Baraza linasimamia usajili wa wataalam wa afya mazingira ili kulinda na kusimamia nidhamu na maadili katika taaluma ya afya mazingira. Katika kipindi cha Julai, 2025hadi Machi2026, idadi ya wataalam wapya waliosajiliwa na Baraza la Afya Mazingira ni 730 ikilinganishwa na wataalam 448 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/25 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kufikia 5,599, kati ya hao, wenye usajili kamili ni 2,159, usajili wa kuorodheshwa ni 2,677, usajili wa kuandikishwa ni 581 na usajili wa muda ni 182. Aidha, Baraza linaendelea na utaratibu wa kusajili wataalam kwa njia ya kielektroniki (hprs.moh.go.tz) ambapo jumla ya wataalam 4,735 wamesajiliwa kupitia mfumo huo.

314. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Baraza liliendelea kuratibu mafunzo ya utarajali ambapo, jumla ya watarajali 181 wanaendelea na mafunzo katika mikoa 26ya Tanzania Bara na vyuo sita (6) vinavyotoa mafunzo ya afya mazingira ngazi ya stashahada ambapo watarajali 144 wamehitimu mafunzo hayo katika kipindi hiki. Aidha, ufuatiliaji wa usajili, uhuishaji wa leseni na watarajali umefanyika katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Ruvuma, Lindi, Kigoma, Njombe, Mbeya, Kilimanjaro, Morogoro na Mwanza na katika vyuo vya afya mazingira vya Mpwapwa na MUHAS. Vilevile, Baraza linaendelea kuhamasisha na kufanya ufuatiliaji kwa wanataaluma wote kujisajili na kuhuisha leseni ili kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

315. Mheshimiwa Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala lilianzishwa kwa lengo la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza shughuli za tiba asili na tiba mbadala nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya waganga, wasaidizi wa waganga, wauza dawa wa tiba asili na tiba mbadala wapatao 3,098 wamesajiliwa sawa na asilimia 69 ya lengo la kusajili

wataalam 4,500 ikilinganishwa na wataalam 6,713 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 67,783. Vilevile, Baraza limesajili vituo vya tiba asili sita (6) na kufanya kuwa na jumla ya vituo 154 vinavyotambulika kisheria.

316. Mheshimiwa Spika, Baraza linaendelea na utoaji wa elimu, usajili wa wauza dawa na wamiliki wa maduka ya tiba asili katika Mkoa wa Dar es salaam ambapo hadi kufikia Machi 2026 limesajili wataalam 529 kwa mchanganuo ufuatao: wataalam wa tiba mbadala wawili (2); waganga 147; wasaidizi wa waganga 20; wasaidizi tiba mbadala watatu (3); vilinge vitatu (3); vituo vya masaji vitatu (3); kliniki tiba asili56; maduka ya dawa 66; wauza dawa 104; na kuhuisha waganga 125.

Bodi ya Maabara Binafsi za Afya

317. Mheshimiwa Spika, Bodi hii ina jukumu la kusajili, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma bora za maabarabinafsi hapa nchini zinatolewa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya (zahanati, vituo vya afya, hospitali Pamoja na maabara zote zinazojitegemea). Katika kipindi Julai 2025 hadi Machi, 2026, Bodi ilisajili vituo 287 ikilinganishwa na vituo 317 vilivyosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kati ya vituo hivyo, vituo 127 vinajitegemea na 160 vipo ndani ya vituo vya kutolea huduma za afya na kufanya jumla ya maabara binafsi nchini kufikia 4,640.

318. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi hiki, Bodi imefanya ufuatiliaji wa huduma zitolewazo kwenye maabara binafsi za afya 1,117 katika Mikoa10 yaKagera, Shinyanga, Simiyu, Morogoro, Dar es Salaam, Singida, Dodoma, Mwanza, Geita na Tabora. Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha maabara zinazingatia vigezo vya mfumo wa udhibiti ubora ambapo uhakiki wa ubora wa ndani wa vipimo (IQC) uliongezeka kutoka asilimia 55 hadi 58 na matengenezo kinga ya mashine yalipanda kutoka asilimia 45 hadi 47.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

319. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ina jukumu la msingi la kusajili na kusimamia vituo vyote vya kutolea huduma za afya binafsi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Bodi imesajili jumla ya vituo 3,653. Aidha, kati ya vituo hivyo, vituo vinavyofanya kazi ni 3,422, Vituo vilivyofungwa moja kwa moja ni 98 na vituo 133 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Pia, kati ya vituo hivyo, hospitali ni 231, vituo vya afya 324, zahanati 2,146, kliniki 278, polyclinics 396, kliniki za kusafisha damu 25 na vituo vya uchunguzi ni 22.

320. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, jumla ya vituo binafsi 191 vilisajiliwa, kati ya vituo hivyo, 151 vilikuwa vituo vipya, 27 vilikuwa vituo vinavyoomba kubadilishwa Daraja na vituo 21 vilikuwa vituo vinavyohuisha usajili. Vilevile, jumla ya vituo 300 viliwasilisha maombi ya usajili, kati ya vituo hivyo, 191 sawa na asilimia 64 vilikidhi vigezo vya kusajiliwa, na vituo 109 sawa na asilima 36 vilikuwa na mapungufu mbalimbali yaliyohitaji kuboreshwa. Kati ya vituo 191 vilivyosajiliwa, hospitali ngazi ya mkoa tatu (3), hospitali ngazi ya wilaya tisa (9) na hospitali ngazi ya kanda moja (1), vituo vya afya 12, zahanati 103 na kliniki 63.

321. Mheshimiwa Spika, Bodi kwa kushirikiana na waratibu ngazi za mikoa na wilaya ilifanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya binafsi katika mikoa 13 ya Mwanza, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Songwe, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Njombe, Manyara, Mtwara, Ruvuma na Dar es Salaam, ambapo baadhi ya vituo vilikutwa na mapungufu mbalimbali kama vile, uhaba wa watumishi, miundombinu chakavu na kutozingatia miongozo ya kukinga na kudhibiti maambukizi. Vilevile, baadhi ya vituo havikuwa na usajili na vingine vilikuwa vimeacha kutoa huduma.

Miradi ya Maendeleo

322. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususani katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara pamoja na

kuendelea na ujenzi lakini pia imefanya ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi 40 ambapo, kati yake, miradi 27 inatekelezwa katika hospitali za rufaa za mikoa, miradi 13 inatekelezwa katika hospitali ya taifa, maalum na kanda. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali mathalani miradi saba (7) imefikia zaidi ya asilimia 90 ikiwemo ujenzi wa jengo la huduma za mionzi, wagonjwa wa nje, damu salama, ujenzi wa jengo la dharura na wagonjwa mahututi katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Manyara; ujenzi wa hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kwangwa - Mara awamu ya nne; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje awamu ya kwanza katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Kigoma - Maweni; ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Kilimanjaro – Mawenzi; ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Simiyu; na ujenzi wa jengo la huduma ya tiba ya mionzi katika hospitali ya kanda ya KCMC. Aidha, miradi nane (8) imefikia wastani wa asilimia 70, mradi mmoja (1) umefikia wastani wa asilimia 45 na miradi 24 iko hatua za awali.

323. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Mifupa Muhimbili imeendelea na ujenzi wa jengo jipya la kuhudumia wagonjwa wa nje ili kupunguza msongamano kwa wagonjwa ambapo utekelezajiwake umefikia asilimia 54 na ukarabati wa kituo cha kliniki ya Tumaini ambao umefikia asilimia 99. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Saratani Ocean Road imeendelea na ujenzi wa jengo la huduma jumuishi za saratani ambao umefikia asilimia 37pamoja na ujenzi wakituochaSarataniMbeyauliofikiawastani wa asilimia 40 ya utekelezaji. Wizara imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ikiwemo maabara ya kisasa, ujenzi wa kituo cha utengamao kwa ajili ya waraibu wa dawa za kulevya. Vilevile, Wizara inaendelea kufanya ukarabati wa jengo la utawala katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong’oto ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 80.

324. Mheshimiwa Spika, Wizaraimeendelea na ukarabati wa jengo lakliniki ya wagonjwa wa nje lenye jumla ya vyumba 30 ambalo litatumika katika kuboresha huduma za matibabu na kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la kutolea mafunzo ya huduma za dharura na majanga ambalo limeanza kutoa

huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda Bugando. Aidha, Wizara kupitia hospitali ya kanda KCMC, imeendelea na ujenziwa jengo la upasuaji uliofikia wastani wa asilimia 89, mabweni ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani ambao umefikia wastani wa asilimia 94, maabara jumuishi umefikia asilimia 90 na jengo la huduma ya magonjwa ya moyo umefikia asilimia 55.

325. Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya utoaji wa huduma katika hospitali ya Taifa Muhimbili na kubaini mapungufu ya uchakavu wa miundombinu, kutawanyika kwa mpangilio wa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na ukarabati wa mara kwa mara na mazingira yasiyoruhusu maboresho ya huduma za ubobezi na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa, Serikali inakusudia kujenga Muhimbili mpya ambayo itapunguza idadi ya rufaa za matibabu nje ya nchi, itaongeza maeneo ya kutolea huduma, itapunguza kero ya kusubiri huduma kwa muda mrefu, itaboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na ndugu wa wagonjwa, itaingiza fedha za kigeni na kuimarisha huduma za ubobezi nchini.

326. Mheshimiwa Spika, mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano (5) na kugharimu Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa majengo, mifumo, ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali. Naomba nifafanue kwa kifupi kuwa mchango wa Serikali katika mradi huo kwa sehemu kubwa si fedha taslimu bali ni gharama za maandalizi ya eneo la ujenzi, msamaha wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa bidhaa na vifaa vitakavyoingizwa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

327. Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya ulinganifu wa gharama za ujenzi wa hospitali mpya ya Muhimbili kwa kulinganisha na miradi mingine 16 kutoka nchi 15 tofauti za barani Afrika, Ulaya na Asia kwa kuangalia ukubwa wa hospitali, gharama kwa mita za mraba, kiwango cha huduma zinazotarajiwa na mwaka wa ujenzi wa mradi. Matokeo ya ulinganifu huo yameonesha kuwa mradi wa ujenzi wa Muhimbili mpya una gharama nafuu ikilinganishwa na miradi kutoka nchi nyingine. Kati ya hospitali zote zilizolinganishwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili ina eneo kubwa la

ujenzi kuliko miradi mingine (mita za mraba 115,000) na gharama za ujenzi katika nchi hizo zinakadiriwa kati ya Dola za Marekani 3,000 hadi 7,000 kwa mita za mraba wakati mradi wa Muhimbili mpya utagharimu Dola za Marekani 1,819 kwa mita za mraba. Kwa ulinganifu huu ina maana kwamba, wakati baadhi ya nchi zinalipa mara mbili au zaidi kwa kila mita za mraba, gharama kwa nchi yetu itakuwa chini kwa wastani wa asilimia 42. Tanzania inakwenda kupata hospitali kubwa kwa gharama nafuu na huu si ushahidi wa matumizi mabaya bali ni uwekezaji wa busara na wa thamani nzuri ya fedha za umma. Maboresho hayo yatawezesha hospitali ya taifa Muhimbili kutoka ngazi ya tatu kwenda ngazi ya nne ya utoaji wa huduma za afya kulingana na vigezo vya kimataifa.

328. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali ya taifa ya kisasa si uwekezaji wa sekta ya afya pekee, bali ni uwekezaji wa kimkakati katika uchumiwa nchi. Katika ushindani wa kuvutia Makao Makuu ya Mashirika ya Kimataifa, kampuni za kimataifa, taasisi kubwa za kikanda, ubora wa huduma za afya ni moja ya vigezo muhimu vinavyozingatiwa. Wakati mwingine nchi yetu inaweza kukosa kuchaguliwa kuwa makao makuu au kituo cha kikanda cha taasisi na kampuni hizo kwa sababu nchi jirani zina hospitali za kisasa zaidi zinazotoa uhakika wa huduma bora, za haraka na za kibobezi kwa watumishi, familia zao na wageni wa kimataifa. Hivyo, kuwa na hospitali ya taifa ya kiwango cha juu kama Muhimbili mpya kutajenga Imani kwa wawekezaji na mashirika ya kimataifa, kutasaidia upanuzi wa biashara na kufunguliwa kwa ofisi za kikanda nchini, kutapunguza hitaji la rufaa za matibabu nje ya nchi, na kunaweza pia kuchangia kupunguza gharama za bima na malipo ya hatari kwa mashirika hayo. Aidha, uwepo wa huduma za afya za kibobezi na teknolojia ya kisasa utaifanya Tanzania kuwa eneo lenye ushindani zaidi katika kuvutia vipaji adimu vya kitaalamu vinavyohitajika kusaidia sekta mbalimbali za uchumi wetu, zikiwemo viwanda, madini, nishati, fedha, utalii, teknolojia na huduma za kitaalamu. Kwa msingi huo, mradi wa Muhimbili mpya ni sehemu ya miundombinu ya msingi ya uchumi wa kisasa na kichocheo muhimu cha kuongeza nafasi ya Tanzania kama kitovu cha biashara, uwekezaji na huduma za kimataifa na kikanda.

SEHEMU YA VI: VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI, MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO VYA WIZARA YA AFYA, KWA MWAKA 2026/2027.

329. Mheshimiwa Spika, vipaumbele na mpango wa Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027 vimezingatia mipango ya kitaifa na kisekta ikiwemo, Dira 2050, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Awamu ya Nne, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025-2030, hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera ya Afya na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya.

330. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa, Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza Vipaumbele 11 vya kimkakati pamoja na afua zake zinazolenga kuleta maboresho makubwa katika Sekta ya Afya kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha ubora wa huduma za afya zinazotolewa ili kukidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo: -

   a. Kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya wa kufanya tathmini ya ubora wa huduma zinazotolewa kwa lengo la kufikia viwango na kupata ithibati za taasisi za ndani na nje ya nchi.

   b. Kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa taasisi ya ndani ya kutoa ithibati ya ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.

   c. Kuhakikisha huduma bora zenye staha na utu zinatolewa kwa wananchi kwa kuendelea kusimamia maadili, usajili wa wataalam, mashauri ya kinidhamu na kitaaluma, ukaguzi na usimamizi shirikishi wa vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya.

   d. Kuimarisha huduma kwa mteja ikiwemo kupunguza muda wa kusubiri huduma husika, lugha ya mawasiliano, haki na wajibu wa mteja, mfumo wa

kushughulikia malalamiko na kutoa mrejesho pamoja na usalama wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

ii. Kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuimarisha ugharamiaji wa huduma za afya nchini kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani.

b. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili wananchi kutoka kaya zisizo na uwezo na zenye uwezo.

c. Kuendelea kutoa elimu kwajamiiili wajiunge na bima ya afya.

d. Kuimarisha ushirikiano na Sekta binafsi katika kugharamia huduma za afya nchini.

e. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Ilani ya Chama Tawala (CCM mwaka 2025-2030), Mpango Mkakati wa Muda wa Kati, mipango ya mwaka, programu na miradi kwa kuzingatia Mipango wa kitaifa, majukumu ya Wizara ili kuweka mipango ya ugharamiaji wa huduma za afya inayotekelezeka.

iii. Kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vya ndani ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Ujenziwa maabaraya kisasa ya Utafiti wa Dawa naununuziwa vifaakwa ajili ya uwekezaji katika viwanda vya dawa nchini.

b. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kufubaza makali yavirusi vya UKIMWI kwa kuwekeza katika uzalishaji wa

dawa katika kiwanda cha TPI pamoja na kuvutia wawekezaji wengine wa viwanda vya dawa.

c. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kuboresha mifumo ya maoteo, ugharamiaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na bidhaa nyingine katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

d. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine itaendelea kuratibu uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini ikiwemo kuandaa majukwaa mbalimbali na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

e. Kuimarisha ufuatiliaji, uratibu na udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kusimamia uingizaji wa dawa nchini na matumizi sahihi ya antibiotics.

iv. Kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuendelea kuimarisha mifumo katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuweza kusomana na kubadilishana taarifa.

b. Kuimarisha afya mtandao ikiwemo teleradiology, teleconsultation na elimu ya afya kwa umma.

c. Kuhakikisha mifumo inayotumika katika Sekta ya Afya inapeleka taarifa kwenye kituo kikuu cha kukusanyia na kuhifadhi taarifa (Central Data Repository).

d. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuondokana na matumizi ya karatasi katika kukusanya, kuchakata, kusambaza na kutumia takwimu ili kuwa na taarifa zenye ubora zitakazosaidia kuweka mipango ya kisera yenye uhalisia.

e. Kuimarisha matumizi ya akili unde (AI) katika utoaji wa huduma za afya nchini.

v. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, pamoja na kuimarisha afua za lishe na usafi wa mazingira kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuhamasisha jamii kupima na kutambua mapema hali za afya zao na kuchukua hatua stahiki.

b. Kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na utoaji wa taarifa kwa wakati kabla hayajasambaa na kusababisha madhara makubwa.

c. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha Umahiri wa Elimu ya afya kwa Umma na kusimika mitambo ya kisasa ya TEHAMA na uchapaji ili kuboresha utoaji wa elimu na hamasa za afya kwa umma.

d. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Jumuishiwa Wahudumuwa afya ngazi ya Jamii ikiwemo kuwajengea uwezo na kutoa nafasi 8,000 za ajira mpya nchini.

e. Kuendelea kuboresha na kuhamasisha utoaji wa huduma za chanjo kwa kuweka mfumo wa kielektroniki katika vituo vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa majokofu na ufungaji wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa jotoridi kwenye majokofu ya kuhifadhia chanjo.

f. Kuimarisha huduma za kinga tiba dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Halmashauri 19 kwa ugonjwa wa trakoma, matende na mabusha pamoja na kutoa huduma za utengamao kwa walioathirika.

g. Kuendelea kutekeleza afua za lishe kwa kuelimisha wananchi kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubishi ili kupambana na utapiamlo.

h. Kuimarisha huduma ya udhibiti wa magonjwa mipakani kwa kujenga miundombinu ya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko.

vi. Kuimarisha tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti za afya, ubunifu na teknolojia kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuratibu tafiti katika vituo vya kutolea huduma za afya, taasisi, Pamoja na vyuo kufanya tafiti zinazolenga kutatua changamoto za afya nchini.

b. Kutoa huduma za afya kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti.

c. Kukamilisha tafiti zinazoendelea na kuanza tafiti mpya katika maeneo ya huduma za kinga, tiba, utengamao, mafunzo, huduma za dawa na mifumo ya afya.

vii. Kuimarisha huduma za ukunga, afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya watoto wachanga na vitokanavyo na uzazi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kuchochea juhudi za Serikali za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga.

b. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu, vituo vya huduma za kujifungua na vituo vya huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana.

c. Kuendelea kuimarisha huduma za ukunga kwa kusisitiza na kusimamia matumizi ya chati uchungu iliyoboreshwa sambamba na kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuwezesha huduma ya mwambata.

viii. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuongeza programu za mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika kada mbalimbali za afya kwenye maeneo ya kipaumbele kwa utaratibu wa mafunzo ya muda mrefu na SETI kwa kuzingatia seraza kitaifa zautoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi.

b. Kusimamia ubora wa mafunzo kwa wanafunzi katika vyuo vya afya vya umma na binafsi pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa watarajali.

c. Kuendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya.

d. Kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya katika Sekta ya Afya kwa ajira ya kudumu na mkataba.

e. Kuendelea na uimarishaji na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya afya.

ix. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa afua za tiba asili na tiba mbadala kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuwajengea uwezo wataalam wa kada za afya ili kuimarisha utoaji wa huduma jumuishi za tiba asili katika vituo vya kutolea huduma za afya.
b. Kuongeza wigo wa huduma za tiba asili ikiwemo kujumuisha dawa na huduma nyingine kwenye mfumo rasmi wa afya.

c. Kuanzisha na kuendeleza mashamba ya miti dawa kwa kila kanda ili kuhamasisha uzalishaji endelevu wa dawa za tiba asili.

d. Kununua eneo la kujenga miundombinu ya kituo cha umahiri wa huduma na mafunzo ya tiba asili mkoani Dodoma.

e. Kuendelea kushirikiana na Mataifa na Taasisi nyingine za kimataifa zilizopiga hatua kwenye matumizi ya teknolojia na tiba asili na mbadala.

x. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa na kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi na kuvutia tiba utalii nchini kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali ngazi ya rufaa ya mkoa, kanda, maalum na taifa.

b. Kuanzisha huduma mpya za kibobezi katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda, maalum na taifa ili kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia tiba utalii.

c. Kuendeleza kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, upandikizaji figo, upandikizaji wa uloto na kuanzisha kituo cha umahiri chamatibabuya magonjwa ya kinywa na meno.

d. Kuongeza idadi ya huduma za ubingwa katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka nane (8) hadi 17 na kuanzisha huduma tano (5) za ubingwa kwenye hospitali za Halmashauri.

e. Kuimarisha huduma za uchunguzi kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa Pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa kada za uchunguzi.

f. Kuimarisha huduma za damu salama ikiwemo ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuwajengea uwezo watumishi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi

kuhusu umuhimu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha.

g. Kuimarisha huduma za uhandisi na matengenezo ya vifaa tiba kwa kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wataalam wa fani hizo.

h. Kuendelea na uimarishaji wa miundombinu ya utoaji huduma katika hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, hospitali maalum na hospitali ya Taifa.

xi. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuandaa mpango mkakati wa afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii utakaotoa mwelekeo wa utoaji huduma za afya ya akili katika eneo la kinga, tiba na utengamao.

b. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Afya ili kukuza usalama wa kazi na ustawi wa kiakili kwa watumishi wa afya.

c. Kuendelea kuimarisha huduma za afya ya akili na huduma za kisaikolojia nchini.

d. Kuimarisha huduma za utengamao na huduma za wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya.

SEHEMU YA VII: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

331. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara, Taasisi na hospitali zilizo chini yake inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 747,200,091,299.81.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 76,195,850,735.53** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya

ndani vya Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 165,804,149,264.47** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha **Shilingi 505,200,091,299.81** kutoka Taasisi, Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda.

Matumizi ya Kawaida

332. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha **2026/2027,** Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 652,236,871,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 36 ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha **Shilingi 516,323,356,000.00** ni mishahara ya watumishi wa Wizara, hospitali na taasisi zilizo chini yake na kiasi cha **Shilingi 135,913,515,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Miradi ya Maendeleo

333. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha **2026/2027,** Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 1,148,025,187,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia **64** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni kiasi cha **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni kiasi cha **Shilingi 358,566,578,000.00.**

334. Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni kiasi cha **Shilingi 1,800,262,058,000.00** ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele ilivyojiwekea.

Na	Fungu	Matumizi ya Kawaida	Miradi ya Maendeleo	Jumla
1	52	652,236,871,000.00	1,148,025,187,000.00	1,800,262,058,000.00

335. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya *www.moh.go.tz*.

336. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana, hoja imeungwa mkono. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ili aweze kuja kutoa taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Dkt. Zeyana Abdallah Hamid.

MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninaomba taarifa hii yote iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu – 52) kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo wa Taarifa. Sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia Masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu, ambazo ni:-

(a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii;

(b) Sehemu ya Pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(c) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni, Ushauri, Hitimisho na Shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi na Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kabla ya kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu umeiwezesha kamati kupata uzoefu wa mwaka uliopita, kubaini maeneo yanayohitaji kuongezewa nguvu na kujenga msingi madhubuti wa ushauri unaotolewa kwenye Taarifa hii. Aidha, uchambuzi uliofanyika, unaliwezesha Bunge kutoa ushauri wa kibajeti na kuimarisha uwajibikaji wa Serikali katika matumizi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Afya. Jumla ya miradi sita ilitembelewa na kukaguliwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. Miradi hiyo ni ifuatayo: -

(a) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana (Mradi Namba 5411);
(b) Uimarishaji wa Taasisi ya Saratani *Ocean Road* (Mradi Namba 5412);

(c) Ujenzi na ununuzi wa vifaa tiba vya upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (Mradi Namba 5419);

(d) Ukarabati wa Jengo la Wagonjwa wa Nje *(Out-Patient Department)* katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo *(Muhimbili Orthopaedic Institute-MOI)* (Mradi Namba 5491);

(e) Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Mradi Namba 5487);

(f) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke (Mradi Namba 5411); na

(g) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala (Mradi Namba 5411).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, imeiwezesha Kamati kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa, kiwango cha matumizi ya fedha za umma, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi. Kupitia ufuatiliaji huu, Kamati imebaini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoathiri utekelezaji wa miradi, na maeneo yanayohitaji uboreshaji wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi iliyokaguliwa, ipo miradi ambayo haijakamilika lakini utekelezaji wake umeanza na miradi ambayo utekelezaji wake haujaanza. Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama vile kutokutolewa kabisa kwa fedha au kucheleweshwa kutolewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya miradi mikubwa na ya kimkakati kwa Taifa ambayo haijaanza kutekelezwa ni Mradi Namba 5487 unaohusu Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili *(New Muhimbili)*. Ikiwa mradi huu utakamilika, utasaidia nchi kuimarika kwa kiwango kikubwa katika utoaji wa huduma za afya za ubingwa wa juu na kuiweka Hospitali ya Taifa Muhimbili katika nafasi ya juu kama kituo bora cha mafunzo ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki. Aidha, Hospitali ya Taifa Muhimbili itakuwa kwenye nafasi bora ya kupata Ithibati ya Kimataifa, itakayosaidia kutambulika duniani na kuimarisha Tiba Utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo wa ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili unatarajia kuanza kutekelezwa mara baada ya kukamilika kwa taratibu za michoro na usanifu wa jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na ziara za ukaguzi wa miradi. Kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, yamebainika mambo yafuatayo: -

(a) Uwekezaji mkubwa wa Mitambo, Mashine na Vifaa Tiba katika hospitali zote zilizokaguliwa;

(b) Fedha za miradi kutokutolewa au kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(c) Upungufu wa Wataalam wa Afya, mfano; Wataalam wa Tiba Mionzi na Madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi;

(d) Uwepo wa idadi kubwa ya watumishi wa mkataba katika maeneo yaliyotembelewa;

(e) Ufinyu wa maeneo ya hospitali unaoathiri uendelezaji wa miundombinu hususani ujenzi wa majengo mapya;

(f) Changamoto ya manunuzi ya vifaa tiba na dawa kwa gharama kubwa kuliko uhalisia kwa vifaa tiba pamoja na dawa maalum ambazo hazimo kwenye mfumo wa manunuzi wa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* hasa kwenye Taasisi au Hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na bobezi; na

(g) Changamoto ya ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa unategemea upatikanaji wa fedha. Katika miradi ambayo Kamati imetembelea, kunahitajika jitihada za ziada za kupata fedha, ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kufikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Afya yaliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni shilingi bilioni 819.9, hadi kufikia mwezi Februari 2026, zilikusanywa shilingi bilioni 494.6 sawa na 60% ya makusanyo yote. Kielelezo Namba Moja, kinaonyesha mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizokadiriwa kukusanywa na fedha zilizokusanywa kwa kila chanzo hadi mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imechambua vyanzo vyote vitatu vya makusanyo ya maduhuli ili kubaini maeneo yaliyofanya vizuri na yale ambayo hayakufanya vizuri kama yanavyoonekana katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya makusanyo ya maduhuli ni ya wastani, kwani inategemea hadi kumaliza robo ya tatu ya mwaka mwezi Machi 2026, makusanyo yawe yamefikia angalau 70%. Hivyo, ipo haja ya kuhakikisha makusanyo yote yanapatikana hasa kwa maeneo ambayo hayakufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha /2026 Wizara ya Afya, Fungu 52, iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.7 kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 626.4 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo mishahara ni shilingi bilioni 475.4 na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 151.01. Upande wa fedha za miradi ya maendeleo, ziliidhinishwa shilingi trilioni 1.1 ambayo kati yake fedha za ndani ni shilingi bilioni 789.4 na fedha za nje ni shilingi bilioni 347.6

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, hali ya utolewaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni ya kuridhisha, kwani fedha zimetolewa kiasi cha shilingi bilioni 417.3, sawa na 67% ya fedha zote za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hali ya upatikanaji wa fedha ni ya wastani, kwani kimetolewa kiasi cha shilingi bilioni 590.6, sawa na 59% ya fedha

zote zilizoinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilizopokelewa ni shilingi bilioni 360.5, sawa na 46% na fedha za nje zilizopokelewa ni shilingi bilioni 230.09, sawa na 66%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa unapatikana katika Kielelezo Namba Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika kuwa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha za ndani ni miradi 58. Kati ya miradi hiyo, miradi 17 sawa na 29% imepokea fedha. Miradi 41, sawa na 71% haikupokea kiasi chochote cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo. Kwa upande wa fedha za nje za miradi ya maendeleo, ziliidhinishwa katika miradi 21, kati ya miradi hiyo, miradi 12 sawa na 57% imepokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa Serikali ihakikishe fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 kwisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni shilingi bilioni 747.2. Kielelezo Namba Tatu kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo kutoka katika kila chanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebainisha kupungua kwa kiasi cha makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kiasi kilichopungua ni shilingi bilioni 72.7 sawa na upungufu wa asilimia tisa ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichokadiriwa kukusanywa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Upungufu huu uko katika chanzo cha makusanyo ya taasisi, ambapo baadhi ya taasisi zimekadiriwa kukusanya kiasi kidogo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makadirio ya makusanyo kutoka vyanzo vya Makao Makuu ya Wizara na Hospitali za Rufaa za Mikoa yameongezeka. Kielelezo Namba Nne kinaonyesha mchanganuo na ulinganisho wa fedha za makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Afya imetengewa shilingi trilioni 1.8, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 652.2 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 135.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 516.3 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 1.1. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 789.4 na fedha za nje ni shilingi bilioni 358.5 kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba Tano kinachoonyesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebainika kuwa fedha zinazoombwa kuidhinishwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya Wizara ya Afya, Fungu 52, zimeongezeka kwa shilingi bilioni 36.7, sawa na ongezeko la asilimia mbili, ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili la asilimia mbili ya fedha zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 lipo katika fedha za mishahara ambazo zimeongezeka kwa asilimia tisa na fedha za nje za miradi ya maendeleo ambazo zimeongezeka kwa asilimia tatu, kama inavyoonekana katika Kielelezo Namba Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine muhimu kuhusu Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Bohari kuu ya Dawa *(MSD)*. Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati mwezi Machi, 2026, Kamati imejulishwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ili kuinusuru *MSD,* ikiwa ni pamoja na

kujenga maghala makubwa mawili yaliyogharimu jumla ya shilingi bilioni 42.3, katika Mkoa wa Dodoma na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza vilevile deni la bidhaa za miradi misonge kwa kulipa kiasi cha shilingi 50,000,000,000. Changamoto ambazo zimekuwa zinaikabili Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ni ukosefu wa mtaji na madeni inayoidai Serikali. Madeni hayo yamegawanyika katika makundi mawili na yamekuwa yakiongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la kwanza ni bidhaa zinazotolewa kwa vituo vya kutolewa huduma za afya nchini, kwa matarajio ya kulipwa pindi vituo vitakapokuwa na fedha. Kundi la pili ni gharama za utunzaji na usambazaji wa bidhaa za miradi misonge, ambapo Serikali iliingia makubaliano ya kuchangia gharama. Jumla ya madeni yote ni takriban shilingi bilioni 302.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa madeni ya bidhaa zilizosambazwa unaonesha kuwa, vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo chini ya Wizara ya Afya, vinadaiwa shilingi bilioni 46.4 na vituo vilivyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI vinadaiwa shilingi bilioni 83.1. Kwa upande wa bidhaa za afya za miradi misonge, Serikali inadaiwa shilingi bilioni 172.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaji unaoombwa ni shilingi bilioni 300 kwa mchanganuo wa shilingi 150,000,000,000 kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa dawa. Shilingi 110,000,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni ya washtiri, shilingi 24,000,000,000, kwa ajili ya ujenzi wa maghala, shilingi bilioni 15.4, kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. Lengo la mtaji huo unaoombwa, ni kuongeza ufanisi wa Bohari Kuu ya Dawa ili itekeleze vyema majukumu yake ambayo ni uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema, Serikali ikaipa kipaumbele *MSD* kwa kuipa mtaji, kwani ikiwa kiasi kinachoombwa cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, madeni yote ya Serikali yanayodaiwa, yatafutiwe ufumbuzi ili kuinusuru ustahimilivu wa Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya. Uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini, ni eneo la kimkakati linalolenga kuimarisha sekta ya afya, kutoa ajira, kupunguza utegemezi wa uingizaji wa dawa kutoka nje na kukuza uchumi wa viwanda, pamoja na kuiweka Tanzania kwenye ramani ya uzalishaji wa bidhaa za afya Barani Afrika na Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni azma ya Serikali kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2025 - 2030 kwamba, kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji au sekta binafsi, kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaatiba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa ya Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata mwaliko wa kushiriki katika Mkutano wa tarehe 19 Januari, 2026, ambapo Waziri wa Afya aliitisha mkutano mkubwa wa wawekezaji wa viwanda vya dawa na vifaatiba. Lengo likiwa ni kuifanya Tanzania kuongeza uzalishaji, kufikia asilimia zaidi ya 60% na kuwa kitovu cha uzalishaji kikanda ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono hatua hii kubwa na ya muhimu, ni vyema sasa Serikali ikahakikisha kunakuwepo na mazingira rafiki na wezeshi, ambayo yatavutia uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuondoa urasimu, kutoa vivutio vya kodi na kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati, kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa, hatua kubwa iliyofikiwa katika maboresho ya huduma za afya nchini, inatokana na dhamira ya kweli ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujali afya kwa watu wake. Serikali inastahili pongezi kwa juhudi kubwa ya kuboresha huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijuilisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa huduma za afya na kuboresha Sekta hii muhimu kwa Taifa kwa kufanya mambo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanza awamu ya kwanza ya majaribio ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, kuwa na maono ya ujenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili au New Muhimbili, kuimarisha miundombinu ya hospitali za rufaa za Mikoa na kununua vifaatiba vya kisasa, katika hospitali za rufaa za Mikoa, Kanda Maalum na Taifa. Mfano, ununuzi wa Mashine ya *PET*-CT scan, *MRI* ambayo ni *Magnetic Resonance Imaging, Angio Suite, Mammography* na *Hyperbaric Chamber*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati pamoja na maoni hayo kuhusu azma ya Serikali, ushauri unaotolewa na Kamati unachochewa na miongozo mbalimbali, kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Pia Mpango wa maendeleo ya Taifa ya mwaka mmoja 2026/2027, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 - 2030, Mpango wa Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya *(HSSPV)* 2021/2026, Mpango Mkakati wa Wizara 2020/2021 hadi 2025/2026 na Malengo ya Maendeleo Endelevu *(Sustainable Development Goals)* ya 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Upungufu wa rasilimali watu. Kutokana na upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya, hususan kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vinavyosimamiwa na Wizara ya afya.

(i) Serikali iendelee kutoa vibali vya ajira kwa kada zinazokabilika na upungufu katika vituo vya kutolea huduma za afya.

(ii) Serikali iendelee kutoa ufadhili wa masomo kwa wataalam wa afya ili kupata mafunzo ikiwemo mafunzo ya huduma za kibingwa na ubingwa wa bobezi katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi.

(iii) Vibali vya ajira vitolewe kwa kuzingatia ikama ya taasisi husika na kipaumbele kiwe kwa wataalam

wanaojitolea, kutoa huduma za afya katika hospitali mbalimbali nchini.

(b) Mwenendo uSIYOridhisha wa utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026, kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyokusudiwa ikakamilike mapema na kuwanufaisha wananchi.

(c) Mwenendo hafifu wa makusanyo ya maduhuli. Serikali iendelee kuzijengea uwezo taasisi zake katika mifumo, utoaji wa huduma bora na ukusanyaji wa maduhuli ili kuwepo na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wote.

(d) Kasi ndogo ya ukamilishaji wa miradi ya hospitali za rufaa za Mikoa. Serikali iweke kipaumbele cha kutoa fedha katika miradi ambayo imeanza muda mrefu ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaatiba ili kuleta tija kwa jamii.

(e) Ukosefu wa mtaji Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*. Serikali itoe mtaji wa shilingi 300,000,000,000 kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*, ili kuongeza ufanisi na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha. Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

(f) Madeni ya Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* kwa Serikali. Serikali ilipe deni linalodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*, lenye thamani ya shilingi 302,000,000,000 kwa mchanganuo wa shilingi bilioni 46.4, kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma, vilivyopo chini ya Wizara ya Afya, shilingi bilioni 83.1 kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na shilingi bilioni 172.7 za Miradi Misonge. Ni muhimu sana madeni haya yakalipwa, ili kuendelea kulinda mnyororo wa ugavi na kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa utoshelevu.

(g) Uimarishaji wa viwanda vya ndani vya kuzalisha bidhaa za afya. Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi na rafiki

yatakayovutia wawekezaji wengi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini.

(h) Uimarishaji wa huduma za kinga. Serikali iimarishe huduma za kinga kwa kuwekeza zaidi kwenye kinga, kwani ndiyo msingi muhimu wa afya. Ikiwa huduma za kinga zitaimarishwa zaidi, zitasaidia sana kupunguza gharama za matibabu na kuokoa maisha. Hivyo, kuwa na jamii yenye afya bora na yenye nguvu kazi ya kutosha kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hitimisho; afya ni msingi wa Taifa lolote duniani unaobeba sekta zote nchini, hakuna maendeleo ya kweli bila uwekezaji wa kutosha katika huduma za afya, hivyo Serikali ina wajibu wa kuendelea kuimarisha huduma za afya, kwa kuwekeza na kununua mitambo ya matibabu na kuongeza huduma za kibingwa ikiwa kichocheo cha maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kukupongeza na kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa namna mnavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Abdallah Shekalage, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ismail Rumatila pamoja na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika na masuala ya dawa na vifaa tiba, Ndugu Emmanuel Tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninamshukuru Mganga Mkuu wa Serikali, Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote inapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wanatupa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema na kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA AFYA (FUNGU 52) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

11 MEI, 2026

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

(a) Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii;

(b) Sehemu ya Pili inayobainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027; na

(c) Sehemu ya Tatu inayobainisha Maoni, Ushauri, Hitimisho na Shukrani.

1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi

1.3.1 Msingi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kamati kuchambua bajeti unatokana na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ambacho kimeainisha moja ya majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ni kushughulikia Bajeti ya Wizara inayoisimamia. Aidha, Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaoisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka unaofuata kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Bunge. Baada ya hatua hiyo, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

1.3.2 Mbinu Zilizotumika

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inabainisha mbinu zilizotumika kufanyia kazi hoja hii kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145(a)(iii) ya Kanuni za Bunge. Lengo ni kujenga msingi wa kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali za uchambuzi zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa mawasilisho ya Wizara na majibu kwa hoja mbalimbali ulifanyika kwa njia ya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Matokeo ya kufanya hivyo, ni kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi.

1.3.3 Wigo na Mipaka ya Taarifa

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madhumuni ya Taarifa hii Bungeni, maudhui yake yanagusa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ufafanuzi unaotolewa

unahusu uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge linapitisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha. Eneo lingine ni makadirio ya maduhuli kwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ulinganisho wa bajeti na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Mambo hayo kwa ujumla wake, yanahusika katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi. Kamati hii ambayo ni tegemeo la Bunge katika kuisimamia, kuifuatilia na kuishauri Serikali kuhusu Afya, ilifanyia kazi maeneo hayo. Mazingatio makubwa yaliwekwa kwenye lengo Kuu la Serikali lililoelezwakwenye Ibara ya 8 (1 (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, ambalo, ni ustawi wa wananchi.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo wa Taarifa za Kamati, sehemu hii inaeleza kwa kina mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Maelezo yanayotolewa yamegawanyika katika maeneo makuu mawili makuu ambayo ni:

(a) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, unaolenga kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mapato na matumizi, kubaini changamoto zilizojitokeza pamoja na kushauri hatua stahiki; na

(b) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, unaolenga kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kwa kuzingatia uhalisia wa

mapato, vipaumbele vya kitaifa na ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Mpangilio huu unalisaidia Bunge kupata mtazamo jumuishi wa mwenendo wa utekelezaji wa bajeti iliyopita na mwelekeo wa bajeti inayopendekezwa, na hivyo kuimarisha uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kabla ya kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Lengo la kufanya hivyo, ni kupata taswira halisi ya mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali, kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza, pamoja na kupima kiwango cha ufanisi katika utekelezaji wa mipango iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi huu umeiwezesha Kamati kupata uzoefu wa mwaka uliopita, kubaini maeneo yanayohitaji kuongezewa nguvu na kujenga msingi madhubuti wa ushauri unaotolewa kwenye Taarifa hii. Aidha, uchambuzi uliofanyika, unaliwezesha Bunge kutoa ushauri wa kibajeti na kuimarisha uwajibikaji wa Serikali katika matumizi ya rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilichambua mambo matano (5) mahususi ambayo ni:

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Ukusanyaji wa Maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge;

(iii) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(iv) Utekelezaji wa kazi zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(v) Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa mambo hayo umewezesha tathmini jumuishi ya ufanisi wa utekelezaji wa bajeti. Aidha, maeneo hayo ni muhimu katika kuonesha mwenendo wa mapato, matumizi na utekelezaji wa mipango ya Serikali. Hali hiyo inasaidia kubaini mafanikio, changamoto na kutoa ushauri wenye tija. Kwa ujumla uchambuzi huu, unaliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa.

2.2.1 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kwa Mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Afya. Jumla ya miradi sita (6) ilitembelewa na kukaguliwa katika mkoa wa Dar es Salaam. Miradi hiyo ni ifuatayo: -

(a) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana (Mradi Namba 5411);

(b) Uimarishaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (Mradi Namba 5412);

(c) Ujenzi na Ununuzi wa Vifaa Tiba vya Upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (Mradi Namba 5419);

(d) Ukarabati wa Jengo la Wagonjwa wa Nje *(Out-Patient Department)* katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo *(Muhimbili Orthopaedic Institute-MOI)* (Mradi Namba 5491);

(e) Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (Mradi Namba 5487);

(f) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Temeke (Mradi Namba 5411); na

(g) Uimarishaji wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mwananyamala (Mradi Namba 5411).

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, imeiwezesha Kamati kujiridhisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa, kiwango cha matumizi ya fedha za umma, pamoja na maendeleo yaliyofikiwa katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi. Kupitia ufuatiliaji huu, Kamati imebaini mafanikio yaliyopatikana, changamoto zinazoathiri utekelezaji wa miradi, na maeneo yanayohitaji uboreshaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, Katika miradi iliyokaguliwa, ipo miradi ambayo haijakamilika lakini utekelezaji wake umeanza na miradi ambayo utekelezaji wake haujaanza. Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama vile kutokutolewa kabisa kwa fedha au kucheleweshwa kutolewa fedha.

Mheshimiwa Spika, Moja ya miradi mikubwa na ya kimkakati kwa Taifa ambao hauaanza kutekelezwa ni mradi namba 5487 unaohusu Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili *(New Muhimbili)*. Mradi huu utakamilika, utasaidia nchi kuimarika kwa kiwango kikubwa katika utoaji wa huduma za afya za ubingwa wa juu na kuiweka Hospitali ya Taifa Muhimbili katika nafasi ya juu kama kituo bora cha mafunzo ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki. Aidha, Hospitali ya Taifa Muhimbili itakua kwenye nafasi bora ya kupata ithibati ya Kimataifa, itakayosaidia kutambulika Kimataifa na kuimarisha Tiba Utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Mradi huo wa Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili unatarajia kuanza kutekelezwa mara baada ya kukamilika kwa taratibu za michoro na usanifu wa jengo.

Mheshimiwa Spika, Mfano wa mradi mwingine ambao ulitembelewa na kuonekana uwezekano wa kutokamilika kwa wakati ni mradi namba 5491 unaohusu Ujenzi wa Jengo la Kuhudumia Wagonjwa wa Nje katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI). Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Septemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2026

ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi mwezi Machi, 2026 ni asilimia 34 ya fedha imetolewa.

Yatokanayo na Ziara za Ukaguzi wa Miradi

Mheshimiwa Spika, kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, yamebainika mambo yafuatayo: -

(a) Uwekezaji mkubwa wa Mitambo, Mashine na Vifaa Tiba katika hospitali zote zilizokaguliwa;

(b) Fedha za miradi kutokutolewa au kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(c) Upungufu wa Wataalam wa Afya, Mfano; Wataalamu wa Tiba Mionzi na Madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi;

(d) Uwepo wa idadi kubwa ya watumishi wa mkataba katika maeneo yaliyotembelewa;

(e) Ufinyu wa maeneo ya hospitali unaoathiri uendelezaji wa miundombinu hususan ujenzi wa majengo mapya;

(f) Changamoto ya manunuzi ya vifaa tiba na dawa kwa gharama kubwa kuliko uhalisia kwa vifaa tiba na dawa maalum ambazo hazimo kwenye mfumo wa manunuzi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) hasa kwenye Taasisi/Hospitali zinazotoa huduma za kibingwa na bobezi; na

(g) Changamoto ya ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa unategemea upatikanaji wa fedha. Katika miradi ambayo Kamati imetembelea, kunahitajika jitihada za ziada za kupata fedha ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuyafikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora.

2.2.2 Utekelezaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Wakati Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo kumi na mbili (12). Taarifa ya Wizara imeonesha kwamba, kwa kiasi, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na inaendelea kutekeleza kwa yale ambayo bado hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliotolewa na Kamati ambao bado upo katika hatua ya mchakato wa utekelezaji ni kuhusu Sheria ya Kusimamia Huduma ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa Binadamu.
Kamati ilishauri Serikali ikamilishe mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria hiyo na Taarifa imeonesha kuwa Maandalizi yameanza na kufikia hatua ya ukamilishaji wa andiko la mapendekezo ya kutungwa kwa sheria hiyo. Kamati itaendelea kusisitiza kuwa Serikali iendelee kuzingatia ushauri kwa maeneo yote kama ilivyokuwa imeshauriwa.

2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Afya yaliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni **Shilingi 819,977,862,602.14.** Makusanyo haya yanatokana na vyanzo vitatu vya makusanyo ambavyo ni Makao Makuu, Hospitali ya Rufaa za Mikoa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya.

Kielelezo Namba 1, kinaonesha mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizokadiriwa kukusanywa na fedha zilizokusanywa kwa kila chanzo hadi mwezi Februari 2026.

Kielelezo Namba 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli Julai, 2025 hadi Februari, 2026

NA	CHANZO CHA MAKUSANYO	KIASI KILICHOIDHINISHWA KUKUSANYWA	KIASI KILICHOKUSANYWA HADI FEBRUARI 2026	ASILIMIA (%)
1.	Makao Makuu ya Wizara	74,207,303,307.00	45,968,268,378.59	62
2.	Hospitali za Rufaa za Mikoa	153,792,696,693.00	96,421,235,048.31	63
3.	Taasisi zilizo chini ya Wizara	591,977,862,602.14	352,269,409,839.43	59
JUMLA		**819,977,862,602.14**	**494,658,913,266.33**	**60**

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua vyanzo vyote vitatu vya makusanyo ya maduhuli ili kubaini maeneo yaliyofanya vizuri na yale ambayo hayakufanya vizuri. Katika chanzo cha makao makuu, uchambuzi umebaini kuwa baraza la radiolojia limeongoza kwa makusanyo ya asilimia 116.94 ikifuatiwa na usajili wa wanafunzi na ada za mitihani asilimia 110. Aidha, maeneo ambayo hayakufanya vizuri kwenye makusanyo ni pamoja na Baraza la Afya ya Mazingira (25%), Baraza la Optometria (34%) na Baraza la Tiba Asili (45%). Maabara ya Taifa (3%), Elimu ya Afya kwa Umma (9%) na Hospitali ya Kanda Mbeya (43%).

Mheshimiwa Spika, Katika chanzo cha Hospitali za Rufaa za Mikoa, imebainika kati ya Hospitali za Rufaa 28, Hospitali za Rufaa za Mikoa tisa (9) zimefanya vizuri kwenye makusanyo kwa kukusanya zaidi ya asilimia sabini (70%) hadi mwezi Februari, 2026. Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi (86%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro (78%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida (77%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi (85%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma - Maweni (82%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe (79%), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita (83%) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu (76%). Aidha, Hospitali kumi na tisa (19) hazikufanya vizuri kwenye makusanyo ya maduhuli. Baadhi ya Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songea (39%),

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara - Ligula (48%) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara (52%).

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Makusanyo ya Mapato yatokanayo na Utoaji wa Huduma kwa Taasisi, hadi kufika mwezi Februari, 2026 kati ya Taasisi 16, ni Taasisi tatu (3) tu ndiyo zimebainika kufanya vizuri. Taasisi hizo ni Kilimanjaro Christian Medical Centre -KCMC (77%), Hospitali ya Taifa Muhimbili (70%) na Taasisi ya Chakula na Lishe TFNC (84%). Baadhi ya Taasisi ambazo hazijafanya vizuri ni Taasisi ya Saratani Ocean Road (49%) na Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania - CCBRT (41%).

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla hali ya makusanyo ya maduhuli ni ya wastani, kwani inategemewa hadi kumaliza robo ya tatu ya mwaka mwezi Machi, 2026, makusanyo yawe yamefika angalau asilimia sabini (70%). Hivyo ipo haja ya kuhakikisha makusanyo yote yanapatikana hasa kwa maeneo ambayo hayakufanya vizuri.

2.2.4 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2025/2026

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,763,541,235,000.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 626,433,136,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 475,418,119,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 151,015,017,000.00.** Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo ziliidhinishwa **Shilingi 1,137,108,099,000.00** ambapo kati yake fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 347,649,490,000.00**.

Mheshimiwa Spika, Kupitia uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2026 hali ya utolewaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ni ya kuridhisha kwani fedha zimetolewa kiasi cha **Shilingi 417,383,266,085.48** sawa na **asilimia 67** ya fedha zote za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hali ya upatikanaji wa fedha ni ya wastani kwani

kimetolewa kiasi cha **Shilingi 590,628,476,490.18** sawa na **asilimia 59** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi 360,535,476,951.31** sawa na **asilimia 46**; na fedha za nje zilizopokelewa ni **Shilingi 230,092,999,538.87** sawa na **asilimia 66**.

Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa unapatikana katika katika kielelezo Namba 2.

Kielelezo Namba 2: Fedha zilizoidhinishwa 2025/2026 na Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2026



	Mshahara	Matumizi Mengineyo	Fedha za Miradi Maendeleo za Ndani	Fedha za Miradi ya Maendeleo za Nje
Fedha zilizoidhinishwa 2025/2026	475,418,119,000.00	151,015,017,000.00	789,458,609,000.00	347,649,490,000.00
Fedha zilizotolewa hadi Februari 2026	326,087,395,811.70	91,295,870,273.78	360,535,476,951.31	230,092,999,538.87
Asilimia	69	61	46	66

Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 iliyowasilishwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, Imebainika kuwa, miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha za ndani ni miradi hamsini na nane (58). Kati ya miradi hiyo, miradi kumi na saba (17) sawa na asilimia 29 imepokea fedha. Baadhi ya miradi iliyopokea fedha za ndani za maendeleo ni Taasisi ya Saratani Ocean Road, Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Kuambukiza, Uimarishaji wa Huduma za

Chanjo, Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko, Dawa na Bidhaa za Afya na Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto hospitali ya rufaa ya mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, Miradi arobaini na moja (41) sawa na asilimia 71 haikupokea kiasi chochote cha fedha za ndani zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo. Baadhi ya miradi ambayo haikupewa kiasi chochote licha ya kutengewa fedha za ndani ni pamoja na Udhibiti wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza (NCDS), Ujenzi wa Hospitali ya Mama na Mtoto Dodoma, Ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Matibabu ya Magonjwa ya Mlipuko Kagera na Kisopwa *(Isolation Centre)*, Ujenzi wa Hospitali Maalum ya Huduma za Utengamano katika Mkoa wa Tabora, Ujenzi wa huduma za Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga-Bombo, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Burigi, Chato,Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro- Mawenzi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu, Ujenzi wa jengo la kuifadhia maiti na uzio hospitali ya Rufaa ya Mkoa Dodoma, Ujenzi wa jengo la OPD na Mama na Mtoto Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi Wing A na B, Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara-Ligula, Ujenzi wa EMD ICU,OPD Utawala na jengo la Mionzi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara, Ujenzi wa OPD Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya,Ujenzi wa jengo la OPD hospitali ya Rufaa ya Arusha-Mount Meru,Ujenzi wa jengo la OPD Complex hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza-Sekou Toure na Ujenzi wa jengo la OPD awamu ya tatu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi-Sokoine.

Mheshimiwa Spika, Fedha za nje za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa katika miradi ishirini na moja (21). Kati ya miradi hiyo, miradi kumi na mbili (12) sawa na asilimia 57 imepokea fedha. Baadhi ya miradi hiyo iliyopokea fedha ni mradi wa udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na kuambukiza, mradi wa uimarishaji wa huduma za chanjo, mradi wa uimarishaji wa huduma za lishe, mipango ya afya na uendeshaji na mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria. Aidha, baadhi ya miradi ambayo haikupata fedha za nje zilizoidhinishiwa hadi mwezi Februari 2026 ni program ya maendeleo ya sekta ya afya, mradi wa ujenzi wa hospitali ya mama na mtoto Dodoma, mradi wa ujenzi wa kituo cha umahiri

cha matibabu ya magonjwa ya mlipuko Kagera na mradi wa ujenzi wa jengo la mionzi pamoja na ununuzi wa vifaa tiba hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwenendo huu wa utoaji fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wakuridhisha. Hivyo, ni muhimu sasa, Serikali ihakikishe fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2025/2026 kuisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

2.3 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ikizingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi huo ulifanyika kwa kujielekeza kwenye maeneo makuu mawili ambayo ni: -

(a) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(b) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa maeneo hayo mahususi unalenga kuhakikisha kuwa makadirio ya mapato yanazingatia uhalisia wa ukusanyaji uliopatikana, na kwamba makadirio ya matumizi yanaendana na uwezo halisi wa upatikanaji wa fedha. Hivyo, kuliwezesha Bunge kupima uhalali, utekelezekaji na ufanisi wa bajeti inayopendekezwa. Kwa msingi huo, uchambuzi huu ndio unaoliwezesha Bunge kufanya uamuzi sahihi na wenye kuzingatia nidhamu ya fedha za umma.

2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni **Shilingi 747,200,091,299.81.** Kielelezo Namba 3 kinaonesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo kutoka katika kila chanzo.

Kielelezo Na: 2 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Fungu 52 kwa Mwaka 2026/2027

CHANZO CHA MAKUSANYO	KIASI
Makao Makuu ya Wizara	76,195,850,735.53
Hospitali za Rufaa za Mikoa	165,804,149,264.47
Taasisi, Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda	505,200,091,299.81
JUMLA	**747,200,091,299.81**

Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umebainisha kupungua kwa kiasi cha makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2026/2027. Kiasi kilichopungua ni **Shilingi 72,777,771,302.33** sawa na upungufu wa asilimia tisa **(9%)** ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichokadiriwa kukusanywa mwaka 2025/2026. Upungufu huu upo katika chanzo cha makusanyo ya Taasisi ambapo baadhi ya Taasisi zimekadiriwa kukusanya kiasi kidogo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Baadhi ya Taasisi zilizopunguziwa makadirio ya makusanyo ni pamoja na Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasi, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu-NIMR na Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania-CCBRT.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Namba 4, kinaonesha mchanganuo wa ulinganisho wa fedha za makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 na 2026/2027.

Kielelezo namba 3: Ulinganisho wa Fedha za Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026 na 2026/2027

Maelezo	Makadirio ya Makusanyo 2025/2026	Makadirio ya Makusanyo 2026/2027	Kiasi Ongezeko	Ongezeko au Pungufu (%)

Makao Makuu	74,207,303,307.00	76,195,850,735.53	1,988,547,428.53	**+3**
Hosp za Rufaa za Mikoa	153,792,696,693.00	165,804,149,264.47	12,011,452,571.47	**+8**
Taasisi	591,977,862,602.14	505,200,091,299.81	86,777,771,302.33	**-15**
JUMLA KUU	**819,977,862,602.14**	**747,200,091,299.81**	**72,777,771,302.33**	**-9**

Chanzo; *Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi unaonesha makadirio ya makusanyo kutoka vyanzo vya makao makuu ya Wizara na hospitali za rufaa za Mikoa yameongezeka wakati chanzo cha makusanyo kutoka katika Taasisi yamepungua. Hata hivyo, ili kuhakikisha makusanyo yanayokadiriwa yanapatikana kwa uhakika, ni vema Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2026/2027 Wizara ya Afya imetengewa **Shilingi 1,800,262,058,000.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 652,236,871,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 135,913,515,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 516,323,356,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Fedha zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni **Shilingi 1,148,025,187,000.00**. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 358,566,578,000.00.** Kielelezo Namba 5 kinaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwa kuidhinishwa.

Kielelezo namba 5: Mchanganuo wa Fedha zinazoombwa Kuidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027



Chanzo: *Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, Imebainika kuwa fedha zinazoombwa kuidhinishwa mwaka 2026/2027 kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) zimeongezeka kwa **Shilingi 36,720,823,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 2** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026.
Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya mwaka hadi mwaka. Aidha, ongezeko hili la **asilimia 2** ya fedha zinazoombwa kwa mwaka 2026/2027 lipo katika fedha za mishahara ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 9** na fedha za nje za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 3**.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Namba 6 kinaonesha mchanganuo wa ongezeko la fedha kwa ulinganisho wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na 2026/2027.

Kielelezo namba 6: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa Mwaka 2025/2026 na Fedha zinazoombwa kuidhinishwa Mwaka 2026/2027

MAELEZO	2025/2026 (Shilingi)	2026/2027 (Shilingi)	Ongezeko/ Pungufu	Ongezeko/ Pungufu
Mishahara	475,418,119,000.00	516,323,356,000.00	+40,905,237,000.00	+9%
Matumizi Mengineyo	151,015,017,000.00	135,913,515,000.00	-15,101,502,000.00	-10%

JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	**626,433,136,000.00**	**652,236,871,000.00**	**+25,803,735,000.00**	**+48%**
Fedha Maendeleo (Ndani)	789,458,609,000.00	789,458,609,000.00	0	0%
Fedha za Maendeleo (Nje)	347,649,490,000.00	358,566,578,000.00	+10,917,088,000.00	+3%
JUMLA YA MIRADI YA MAENDELEO	**1,137,108,099,000.00**	**1,148,025,187,000.00**	**+10,917,088,000.00**	**+1%**
JUMLA KUU YA BAJETI	**1,763,541,235,000.00**	**1,800,262,058,000.00**	**+36,720,823,000.00**	**+2%**

Chanzo: *Randama ya Wizara ya Afya 2026/2027 iliyowasilishwa kwenye Kamati*

Mheshimiwa Spika, Ni imani ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kuongeza fedha kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuongeza kasi ya kuboresha sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila Mtanzania. Aidha, ni muhimu kwa fedha zote zinazoidhinishwa kutolewa kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

2.4 Masuala Mengine Muhimu kuhusu Mpango wa Wizara kwa Mwaka wa fedha 2026/2027

2.4.1 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati mwezi Machi, 2026, Kamati imejulishwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ili kuinusuru MSD ikiwa ni pamoja na kujenga maghala makubwa mawili yaliyogharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 42.3** katika Mkoa wa Dodoma na Mtwara. Vilevile, kupunguza deni la bidhaa za miradi misonge kwa kulipa kiasi cha **Shilingi bilioni 50**.

Mheshimiwa Spika, Changamoto ambazo zimekuwa zinaikabili Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ni ukosefu wa mtaji na madeni inayoidai Serikali. Madeni hayo yamegawanyika katika makundi mawili na yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Kundi la kwanza

ni bidhaa zinazotolewa kwa vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa matarajio ya kulipwa pindi vituo vitakapokuwa na fedha.
Kundi la pili ni gharama za Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Miradi Misonge ambapo Serikali iliingia makubaliano ya kuchangia gharama. Jumla ya madeni yote ni takribani **Shilingi bilioni 302.2.**

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa madeni ya bidhaa zilizosambazwa unaonesha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo chini ya Wizara ya Afya vinadaiwa **Shilingi bilioni 46.4** na vituo vilivyopo chini ya OWM-TAMISEMI vinadaiwa **Shilingi bilioni 83.1**. Kwa upande wa bidhaa za afya za miradi misonge, Serikali inadaiwa **Shilingi bilioni 172.7.**

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa changamoto ya mtaji katika mwaka wa fedha 2022/2023, ombi la kupewa mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya. Lengo la mtaji huo unaoombwa ni kuongeza ufanisi wa Bohari Kuu ya Dawa ili itekeleze vema majukumu yake ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya.

Mheshimiwa Spika, Mtaji unaoombwa ni **Shilingi bilioni 300** kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 150** kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa dawa, **Shilingi bilioni 110** kwa ajili ya kulipa madeni ya washitiri, **Shilingi bilioni 24.1** kwa ajili ya ujenzi wa Maghala, **Shilingi bilioni 15.4** kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda.

Mheshimiwa Spika, Ni vema Serikali ikaipa kipaumbele MSD kwa kuipa mtaji kwani, ikiwa kiasi kinachoombwa cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, madeni yote Serikali inayodaiwa yatafutiwe ufumbuzi ili kunusuru ustahimlivu wa Bohari Kuu ya Dawa.

2.4.2 Uwekezaji wa Viwanda vya Kuzalisha Bidhaa za Afya

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini ni eneo la kimkakati linalolenga kuimarisha

sekta ya afya, kutoa ajira, kupunguza utegemezi wa uagizaji wa dawa kutoka nje, na kukuza uchumi wa viwanda pamoja na kuiweka Tanzania kwenye ramani ya uzalishaji wa bidhaa za afya barani Afrika na duniani.
Hii ni azma ya Serikali kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025 – 2030, kwamba kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata mwaliko wa kushiriki katika Mkutano wa tarehe 19 Januari 2026 ambapo Waziri wa Afya aliitisha Mkutano mkubwa wa wawekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba lengo likiwa ni kuifanya Tanzania kuongeza uzalishaji kufikia zaidi ya asilimia sitini (60%) na kuwa kitovu cha uzalishaji kikanda ifikapo 2030.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani wa viwanda vya dawa, Ni vema kuhakikisha kunakuwepo mazingira rafiki na wezeshi ambayo yatavutia uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuondoa urasimu, kutoa vivutio vya kodi na kuboresha miundombinu.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI
3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa, hatua kubwa iliyofikiwa katika maboresho ya huduma za afya nchini, inatokana na dhamira ya kweli ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujali afya kwa watu wake. Serikali inastahili pongezi kwa juhudi kubwa ya kuboresha huduma za afya nchini. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa huduma za afya na kuiboresha Sekta hii muhimu kwa Taifa kwa kufanya mambo mbalimbali kama : -

(i) Kuanza awamu ya kwanza ya majaribio ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;

(ii) Kuwa na maono ya Ujenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili *(New Muhimbili)*;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa; na

(iv) Kununua vifaa tiba vya kisasa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa. Mfano ununuzi wa mashine ya PET CT SCAN, MRI (Magnetic Resonance Imaging), Angio Suite, Mammography na Hyperbaric Chamber.

3.2 Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni hayo kuhusu azma ya Serikali, ushauri unaotolewa na Kamati unachochewa na miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka Mmoja (2026/27), Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 - 2030, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (HSSP-V 2021-2026), Mpango Mkakati wa Wizara 2020/2021-2025/2026 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030).

Kwa msingi huo, Kamati inatoa ushauri ufuataao: -

(a) Upungufu wa Rasilimali Watu

Kutokana na upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya hususan kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vinavyosimamiwa na Wizara ya Afya, Serikali –

(i) Iendelee kutoa vibali vya ajira kwa kada zinazokabiliwa na upungufu katika vituo vya kutolea huduma za afya;

(ii) Iendelee kutoa ufadhili wa masomo kwa wataalam wa afya ili kupata mafunzo ikiwemo mafunzo ya huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi; na

(iii) Vibali vya ajira vitolewe kwa kuzingatia ikama ya Taasisi husika na kipaumbele kiwe kwa wataalam wanaojitolea kutoa huduma za afya katika hospitali mbalimbali nchini.

(b) Mwenendo USIYOridhisha wa Utolewaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa mwaka 2025/2026 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyokusudiwa ikamilike mapema na kuwanufaisha wananchi.

(c) Mwenendo hafifu wa Makusanyo ya Maduhuli

Serikali iendelee kuzijengea uwezo Taasisi zake katika mifumo, utoaji wa huduma bora na ukusanyaji wa maduhuli ili kuwepo na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wote.

(d) Kasi ndogo ya Ukamilishaji wa Miradi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa

Serikali iweke kipaumbele cha kutoa fedha katika miradi ambayo imeanza muda mrefu ili ikamilike na kuanza kutoa huduma. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaa tiba ili kuleta tija kwa jamii.

(e) Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 300** kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ili kuongeza ufanisi na kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha. Kukosekana kwa mtaji huo kunasababisha Bohari Kuu ya Dawa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

(f) Madeni ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa Serikali

Serikali ilipe deni linalodaiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) lenye thamani ya **Shilingi bilioni 302.2**, kwa mchanganuo wa **Shilingi bilioni 46.4** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo

chini ya Wizara ya afya, Shilingi **bilioni 83.1** kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma vilivyopo chini ya OWM- TAMISEMI na **Shilingi bilioni 172.7** za miradi Misonge. Ni muhimu sana madeni haya yakalipwa ili kuendelea kuulinda mnyororo wa ugavi na kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa wakati na kwa utoshelevu.

(g) Uimarishaji wa Viwanda vya Ndani vya Kuzalisha Bidhaa za Afya

Serikali iendelee kuweka mazingira wezeshi na rafiki yatakayovutia wawekezaji wengi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini.

(h) Uimarishaji wa Huduma za Kinga

Serikali iimarishe huduma za kinga kwa kuwekeza zaidi kwenye kinga kwani ndio msingi muhimu wa afya. Ikiwa huduma za kinga zitaimarishwa zaidi, zitasaidia sana hupunguza gharama za matibabu na kuokoa maisha hivyo kuwa na jamii yenye afya bora na yenye nguvu kazi ya kutosha kwa maendeleo ya Taifa.

Hitimisho

Mheshimiwa Spika, Afya ni msingi wa Taifa lolote Duniani unaobeba Sekta zote nchini. Hakuna maendeleo ya kweli bila uwekezaji wa kutosha katika huduma za afya. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kuendelea kuimarisha huduma za afya kwa kuwekeza kwa kununua mitambo ya matibabu na kuongeza huduma za kibingwa ikiwa ni kichocheo cha maendeleo ya Uchumi na Ustawi wa Jamii.

3.3 Shukrani

Mheshimiwa Spika, Napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kipekee nawashukuru sana Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)-Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi (Mb)-Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Abdallah Shekalage, Naibu Katibu Mkuu Ndugu. Ismail Rumatila pamoja na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulika na masula ya dawa na vifaa tiba Ndugu. Emmanuel Tayari. Vilevile, namshukuru Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Elias Magembe pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote inapotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika kujadili na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Dkt. Johannes Lembulung Lukumay, Mb -**MWENYEKITI**
2. Mhe. Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, Mb –**M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Jacqueline Kainja Andrew, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Adonis Alfred Bitegeko, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Janeth Peter Pinda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Juma Mustafa Kawamba, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Japhael Masanja Lufungija, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Husnain Gulamabbas Dewji, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Muhsin Haji Ussi, Mb -Mjumbe
14. Mhe. Nadra Ghulam Rashid, Mb -Mjumbe
15. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb -Mjumbe
16. Mhe. Eric James Shigongo, Mb -Mjumbe
17. Mhe. Yagi Maulid Kiaratu, Mb -Mjumbe

18. Mhe. Jamila Mahmoud Juma, Mb -Mjumbe
19. Mhe. Neema William Mgaya, Mb -Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Baraka I. Leonard kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema na kwa wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Johannes L. Lukumay (Mb),
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI
11 Mei, 2025

MWENYEKITI: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI.

Waheshimiwa Wabunge tuwatambue kwa haraka wageni wengine ambao tunao ndani ya ukumbi wetu wa Bunge.

Tuna wageni 126 wa Mheshimiwa Spika, hawa ni Umoja wa Madiwani wa CCM Tanzania (UAMA). Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Waziri Mohamed Omary Mchengerwa na huyu tumtambue kwa namna ya pekee. Huyu ni Mbunge Mstaafu na Waziri wa Afya Mstaafu Daktari Hamis Kigwangalla. *(Makofi)*

Ahsanteni. Ahsante sana. Karibu sana Dkt. Kigwangalla, Mbunge wa Bunge la Kumi na Mbili, Bunge lililopita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri ana wageni wengine ambao nao tuwatambue kwa ujumla wao. Hawa ni

Wakurugenzi mbalimbali ndani ya Wizara ya Afya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa; na Wadau mbalimbali wa Sekta ya Afya. Wako pale. Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Tunao pia viongozi kutoka vyama vya kitaaluma, ninaamini nao wako pale. Tuna taasisi za kifedha, Azania Benki na *NMB* wamewakilishwa ndani ya ukumbi wetu wako pale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna watumishi kutoka Wizara ya Afya, wale ambao pengine hawakutajwa lakini wamo ndani ya ukumbi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Viongozi kutoka Taasisi za Kidini ambao wako ndani ya ukumbi huu. Tunawakaribisha. *(Makofi)*

Tuna Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Rufiji; Madiwani kutoka Rufiji wakiongozwa na Ndugu Abdul Bakari ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Wilaya ya Rufiji; na Makatibu kutoka Wilaya ya Rufiji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge, Mheshimiwa Johannes Lukumay. Hawa ni wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali ya Mitaa Hombolo. Wako pale juu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo, tunaanza uchangiaji. Tutachangia kwa dakika 10, tutaanza na Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na Mheshimiwa Jacqueline Andrew Kainja ajiandae.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya afya. Awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu na kuweza kujadili hoja hii ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Taifa letu, ya

kuhakikisha kwamba analeta maendeleo mbalimbali; na vilevile katika masuala ya afya yeye pamoja na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niipongeze Wizara ya Afya kwa maana ya Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu wa Afya kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba wanatimiza ndoto za Rais wetu mpendwa katika suala zima la kuhakikisha kwamba anaipigania afya ya Mtanzania. Hongera sana kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Nchi inasema kwamba ifikapo mwaka 2050 tuhakikishe kwamba Tanzania inakuwa kitovu cha utalii tiba Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza Wizara kwa mikakati mbalimbali ambayo imeanza kufanya ili kuweza kutimiza azma hiyo. Wizara imeanza na Mradi wa Ujenzi na Uboreshwaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Niwapongeze sana. Kwa sababu katika suala zima la utalii tiba linaanza na miundombinu. Miundombinu ya Hospitali yetu ya Taifa ni lazima iendane na miundombinu ya hospitali zingine huko za kimataifa ndipo tutakapoweza ku-*qualify* kuwa sehemu ya utalii tiba Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa Muhimbili, *redevelopment* ya Muhimbili unagharamia takribani dola za Kimarekani 468,469,000; ni sawa na trilioni 1.2. Mradi huu ukiuangalia vizuri ni mradi wa mkopo nafuu. Kwa nini ninasema hivyo? Kwenye mradi huu Tanzania itakwenda kuchangia dola za Kimarekani 104,572,000. Katika hizi 104,572,000 dola 91,500,000 tutakwenda kuchangia kwa kupitia misamaha ya kodi ya vifaa ambavyo vitakuja kutengeneza hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, shilingi milioni 10 itakwenda kwenye maandalizi ya mradi. Kuna maandalizi mengi sana ambayo yatafanyika pale Muhimbili pamoja na kutengeneza barabara ambayo itasaidia shughuli za hospitali ziendelee kama kawaida na upande mwingine huo ndiyo utakuwa unafanya shughuli za ujenzi wa hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dola za Kimarekani 2,620,000, hizi zitakwenda kwenye usimamizi wa mradi; na dola 60,900,000 itatoka kwenye dola milioni 363 ya mradi ambayo tutapewa na Serikali ya Korea Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimetoa takwimu hizo? Ukiangalia thamani ya mradi ambao unakwenda kujengwa *per square metre,* Mheshimiwa Waziri hapa, amesema ni dola 1,819, lakini kiuhalisia sasa hivi mtaani Tanzania hapa *estimate construction cost ya per square metre* moja ni sawasawa na dola 2,300 hadi dola 2,500. Hivyo basi, ninawaomba wenzangu tuwaunge mkono kutokana na mradi huu tunaokwenda kuutekeleza kwa bei nafuu. Vilevile ni mradi ambao utakwenda kusaidia nchi yetu kwenda kuingia kwenye sifa ya kuwa na utalii tiba; kwa sababu utalii tiba unaanza na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaweza wakawa na wasiwasi kwamba, hizi fedha tutakuja kurudisha vipi? Ninaomba niwaambie Wabunge wenzangu; *return on investment* ya mradi huu tutakwenda kuipata kwenye utalii tiba. Tusiwe na shaka. Ukiangalia takwimu za wagonjwa wanaotibiwa kutoka nchi mbalimbali kuja hapa Tanzania kuanzia mwaka 2022 tumekuwa na wagonjwa takribani 5,700 na idadi hii imekwenda kuongezeka hadi kufikia wagonjwa 23,000 ilipofika mwezi Februari, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza tukaona kwamba *trend* ya wagonjwa ambao wanakuja kutibiwa Tanzania tayari kabisa hii inatupa imani kwamba mradi huu utakuwa na tija katika kuhakikisha kwamba Tanzania yetu na ule mkakati wetu wa kuhakikisha kwanza mwaka 2050 tutakuwa kitovu cha utalii tiba tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachilia mbali hiyo *return investment* ya mradi huu, tuna faida kubwa; tutapunguza *referrals* za wagonjwa kupeleka nje. Pia tutaongeza mapato; kwa maana ya kwamba wagonjwa watakaokuja kutibiwa ndani ya nchi yetu, mapato yatasaidia kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri; nilimwona juzi akiweka jiwe la msingi la kongani ya ujenzi

wa viwanda vya dawa na vifaa tiba. Kwa namna hii unaweza ukaona kwamba mipango ya Wizara ya Afya ni mipango ambayo inaendana. Lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba inataka kwenda kufanya afya ya Mtanzania na vilevile suala la afya ndani ya Tanzania liwe la kimataifa. Kwa nini? Umeona huku wanaboresha Hospitali ya Muhimbili; lengo likiwa ni kufikia kwenye utalii tiba. Vilevile hatuwezi kufikia utalii tiba tusipokuwa na dawa za kutosha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze; viwanda hivi vitazalisha dawa, wananchi wetu watapata dawa kwa bei nafuu na vifaa tiba kwa bei nafuu. Kwa hiyo, tutatibiwa kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ambavyo vitazalisha dawa na vifaa tiba ndani ya Tanzania yetu vilevile vitasaidia kupunguza gharama zaidi katika Hospitali yetu ya Taifa na sisi itatufanya tuweze ku-*compete* vizuri na nchi za jirani katika suala la utalii tiba. Watu wengi watavutiwa kuja kwetu kutibiwa, kwa sababu kwanza tutakuwa tuna miundombinu mizuri, tutakuwa na Madaktari Bingwa Wabobezi, pamoja na uhakika wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya vizuri kwenye hili suala la viwanda vya dawa na vifaa tiba tunaweza kuuza mpaka kwenye nchi ambazo zinatuzunguka. Tunaweza tukateka soko la *East Africa* na *SADC* kwa ujumla. Niwapongeze kwa mikakati hii mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye suala la *redevelopment* ya Muhimbili; tunawaomba, pamoja na kuwa tumepata mkopo wa bei nafuu, kwenye usimamizi wahakikishe kwamba wanasimamia mradi ule ili tupate matokeo mazuri; kwa maana ya *quality* ya mradi. Kwa sababu hiyo *square metre* moja yenye gharama ya dola 1,819 ina maana inajumuisha ujenzi, vifaa, pamoja na mifumo; *full furnished*. Kwa hiyo tunawaomba wahakikishe kwamba tunapata *quality* nzuri ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi pia uishe kwa wakati sahihi. Yaani kusiwe na muda mrefu wa kutekeleza mradi huo ili tuanze sasa kupata faida za mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia bima ya afya. Takwimu za Sensa ya mwaka 2022 zinaonyesha kwamba kaya maskini Tanzania ni kaya 3,900,000; lakini Serikali mpaka dakika hii imeshazitambua kaya maskini 931,000. Niwapongeze Wizara ya Afya, tayari wamekwishakwenda kuanza utekelezaji wa bima ya afya kwa kaya 276,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba wakati wanaendelea awamu ya pili na awamu nyingine waweze kuzitambua zile kaya milioni tatu ambazo bado hawajazitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bima ya afya ni suala ambalo linatakiwa Wizara zote ziweze kushirikiana kwa maana ya kwamba waweze...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. NEEMA W. MGAYA: ...kutambua makundi mbalimbali; kwa mfano vikundi vya madini, *AMCOS* waweze kuchangia kwenye bima hii ya afya ili tuweze kuwa na Mfuko himilivu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kwa kumalizia...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. NEEMA W. MGAYA: ...nilikuwa ninaiomba kuishauri Serikali kwa maana Wizara ya Afya wahakikishe kwamba wanaboresha upatikanaji wa dawa, wanaboresha huduma bora, lugha nzuri kwa wagonjwa, siyo tena mtu amekwenda pale; ah! huyu bwana ana bima tumuweke pembeni; Hapana. Vilevile aboreshe mifumo isomane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kikubwa zaidi *NIMR* waendelee kufanya *research* katika suala la *health care finance;* kwa maana

ya kwamba waangalie nchi nyingine katika suala la bima ya afya wamefanyaje; wamefanikiwa vipi; na wale wenzetu ambao hawakufanikiwa ni mambo gani ambayo yamewafanya wasiweze kufanikiwa...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Neema, muda wako umekwisha.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Nilimwita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Andrew Kainja.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa awali kabisa wa Wizara hii muhimu kwa ajili ya maendeleo na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi huwa nina kawaida ninapenda sana utendaji wenye matokeo. Ninayasema haya kwa sababu sisi Wabunge ambao tunawakilisha wananchi humu kwenye jumba hili ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba zile sauti za walipakodi walioko nje ya Bunge zinasemewa ipasavyo hapa; na kuhakikisha kwamba yale wanayoyatarajia kutoka kwetu yanapatikana kwa sisi Wabunge kuwa sauti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema hayo ninataka ku-*refer* kwanza kabisa; Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, ninataka niseme

kwa dhati ya moyo wangu, kwamba sisimami hapa kwa sababu yuko humu ndani; ninasimama hapa kwa sababu yeye ni Waziri wa matokeo, yeye na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemfuatilia, tumekaa pamoja, tumeanza Bunge mimi na yeye; pamoja kila Wizara anakokwenda, kwa dhati ya moyo wangu; kila Wizara anakokwenda anaacha alama. Nimesema Waziri yeyote anayesaidia kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi huyo ni

rafiki yangu; na Waziri yeyote ambaye hataonekana anatekeleza ilani, tutamsema hapa mchana kweupe bila kupepesa macho kwa maslahi ya Watanzania waliotutuma huko nje. Mheshimiwa Mchengerwa ni Waziri wa vitendo na anayeangalia matokeo. Kwa hilo ninampongeza kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa dhati, ana watendaji wazuri. Mimi nimeshatumikia hiyo Kamati kama Mwenyekiti. Ana Katibu Mkuu mwadilifu na mchapakazi, Shekalaghe na Manaibu wake wote wawili, akiwemo huyo Naibu aliyeteuliwa hivi karibuni, mwanangu Ima; ni watu wazalendo wanaotaka kuona nchi inakwenda mbele. Vilevile wa *CMO* mchapakazi na mcha Mungu, dada yangu Grace Magembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *dream* tuliyonayo ni kuhakikisha kuwa ndoto za Rais Dkt. Samia katika sekta ya afya zinatekelezwa; na Mheshimiwa Mchengerwa ameanza. Ninaomba uchukue kalamu na karatasi nitoe ushauri wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Bunge la Kumi na Mbili tumetunga sheria ya *universal health coverage* kwa nchi nzima. Kwa dhamira safi ya Bunge hili, Wabunge hawa waliangalia maslahi ya umma kwa pamoja wakakubaliana ndani ya Bunge hili; tukatunga sheria ya kuhakikisha kuwa wafugaji, wakulima, wavuvi, wafanyabiashara na wafanyakazi wa Taifa hili wanapata huduma ya afya nchi nzima bila kubaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie kaka yangu Mwanyika, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama huyu tumpe haki yake alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha tulipotunga sheria hii kwa ujasiri mkubwa na uzalendo, mama yetu Rais wetu akaisaini, Muswada ule ukasainiwa ukawa sheria tayari kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imeiweka Serikali hii madarakani imetekeleza kwa vitendo ujenzi wa zahanati zaidi ya maelfu huko kwenye majimbo yetu. Pia, kumejengwa vituo vya afya zaidi ya maelfu huko kwenye majimbo yetu na

zimeimarishwa hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, hospitali za kanda, rufaa na hadi Taifa na kuhakikisha ya kwamba vifaa tiba vinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu la msingi, Rais wetu anataka kuwaacha Watanzania wakiwa na afya. Mheshimiwa Mchengerwa, kaka yangu ni Waziri wa matokeo ambaye ninamtaja hapa na dunia ijue na Taifa lijue. Kwenye hili ninaomba asiniangushe ili kauli yangu isiende kusutwa huko na watu mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri, tumeshatunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, tunampaje Mama Samia tabasamu kuhakikisha kwamba Bima ya Afya kwa Wote inakuwa *financed* na vyanzo vinavyoeleweka vya mapato ili tuwasaidie Watanzania maskini na watu waSIYO na kipato cha kutosha waweze kupata Bima ya Afya kwa Wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kwa dhati ya moyo wangu hotuba ya Mheshimiwa Mchengerwa imenigusa. Amesema kwa uzalendo na ujasiri mkubwa kwamba mambo ya afya siyo mambo ya anasa wala siyo mambo ya ku-*compromise*, ni mambo yanayogusa ustawi wa Taifa letu katika masuala mazima ya kuwa na *productive nation* ya watu wenye afya wanaoweza kuzalisha na kuleta tija ya kimaendeleo na kiuchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu ni kwamba nimefanya *statistics* kupitia Mamlaka ya Mawasiliano na kusoma ripoti za *BOT*. Tanzania kwa mwaka mmoja inarekodi *transaction* bilioni 6.3 za watu wanaofanya *transaction* katika mitandao ya simu na katika *transaction* zingine. Nimefanya mahesabu, wastani kwa mtu mmoja anafanya *transaction* mara 100 kwa mwaka na fedha zinazopita kwenye *transaction* hizi kwa mwaka ni shilingi trilioni 158.4 zinazoonekana kwenye *transaction* kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kuna swali sisi Watanzania tunajiuliza; Bunge hili tumekaa hapa kwa maslahi ya watu huko nje? Hivi Wizara wanasubiri nini kuja na *platform* kwenye nchi; siyo waende kuleta tozo mpya zitakazowapa Watanzania mzigo, hapana, lakini ninakuja na mawazo; njooni na *coding system*

ambayo itatumia teknolojia ya kisasa wahakikishe sisi Watanzania na sisi tunawasemea kwa niaba ya Watanzania kwamba Watanzania wako tayari ku-*finance* Bima ya Afya kwa Wote. Wanachosubiri Watanzania ni kupewa *directives* na sisi Wabunge na Serikali ili watu wetu waweze kupata Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu akifanya *transaction* ya shilingi 3,000,000, kuna Mtanzania gani ukimwambia achangie shilingi 10 au shilingi 30 kwa ajili ya Bima ya Afya ya nchi yake katika kila *transaction* anayofanya kwa mwaka? Ninataka nimhakikishie kwa hesabu hizi wanaweza wakakusanya shilingi 4,000,000,000,000 waka-*finance* Bima ya Afya kwa Wote ili Watanzania wakienda Hospitali wasiambiwe dawa kanunue duka fulani, Watanzania wakienda Hospitali wakute madaktari wamejaa wakiwahudumia Watanzania na Watanzania wakienda Hospitali wakute mitambo ya kuwapima magonjwa yao ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa, hili ninamwambia na kwa kweli asipokuja na majibu nitambana kwenye shilingi ya Wizara yake. Kwa nini wasitekeleze *platform* hii ya kuhakikisha wanachukua shilingi tano

tano? Leo akinikata shilingi 10 nikapata afya bora mimi na watoto wangu watakuwa wamenisaidia kuwa na afya bora itakayoniwezesha kwenda kuwekeza na kuzalisha uchumi katika Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mawazo yangu watumie *platform* hii ya hizi *transaction*. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Mchengerwa wapo vijana wa Kitanzania wako tayari kuwaletea teknolojia wakawapa *platform* waka-*monitor* ile na hili Mchengerwa wasilifanye *blindly*. Wawaite *MNOs* (*Mobile Network Operators)* wote kwenye nchi hii wawakalishe na Mheshimiwa Rais wa Nchi wamweleweshe Rais Samia ni msikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa watakuwa wamemsaidia Mheshimiwa Rais kupata *fund* ya ku-*finance* Bima ya Afya kwa Wote na Mheshimiwa Mchengerwa kaka yangu ninamwambia atakuwa ameacha *legacy* kwenye Taifa hili, atasababisha Rais

aache *legacy* kwenye Taifa hili, atasababisha Wizara yake iache *legacy* na Watanzania watamkumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie wakienda kutekeleza jambo hili, kama kuna mahali wanafikiri wanakwamishwa, aje atuambie Wabunge ni wajibu wetu kama kuna Wizara inataka kukwamisha utekelezaji wa Ilani tutakuja hapa kuwaambia mchana kweupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya, ninafurahi Naibu Waziri wa Fedha yuko hapa. Tunawaomba Wizara ya Fedha na Wizara zingine wakasaidie Wizara ya Afya waweze kuanzisha hii *platform*. Tena Mheshimiwa Mchengerwa ninakwambia ikaanze kesho na si kesho kutwa. Bima ya Afya tutakapokuja Bunge lijalo watuambie wafugaji wa Mheshimiwa Dkt. Bashiru wangapi wameingia kupitia *transaction* hii na *platform* hii ninayoiongelea.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, ahsante muda wako umekwisha.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo la pili ninataka nizungumzie jambo la kuwekeza kwenye viwanda vya Afya, ninakwenda kuanza kuandika, ninaleta mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimwita Mheshimiwa Jacqueline Andrew Kainja.

MHE. JACQUELINE K. ANDREW: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Afya. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri, na Naibu Waziri kwa kazi ambazo wanafanya na watendaji wote wa Wizara hii ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwa kuendelea kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze sana

Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya uwekezaji mkubwa wa miundombinu, vifaa tiba pamoja na upatikanaji wa dawa katika Sekta hii ya Afya ambayo ni Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kutoa pongezi za Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anapigana katika janga kubwa la kupambana na vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua. Tayari ameweza kupewa u-*champion* katika kikao kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi (*AU)* na kuwa *champion* kinara wa kutokomeza vifo vya mama wajawazito wakati wa kujifungua na nchi zingine zitakuja kujifunza kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2015/2016 takwimu zinasema takriban akina mama 556 walikuwa wanafariki kwa tatizo la mama mjamzito wakati wa kujifungua. Kufikia mwaka wa fedha 2021/2022 akina mama waliokuwa wanafariki kwa tatizo hilo ni 104 sawa na 80% ambayo Mheshimiwa Rais amejitahidi sana kuhakikisha anatokomeza janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulichobakiza ni 20%. Nina uhakika kabisa Wizara wakijipanga vizuri katika mipango ya kuhakikisha mama huyu mjamzito anasaidiwa wanaweza kabisa Mheshimiwa Rais anapomaliza miaka yake mitano anamaliza na vifo vyote vya mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa 20% zilizobaki ambayo ndiyo ilikuwa kiu yake ya kutokomeza na kupata asilimia sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kabisa Wizara imeshaandaa michoro kwa ajili ya majengo mapya ya leba kwa ajili ya akina mama kujifungua. Michoro ile iweze kufanyika hata katika uboreshaji wa leba zingine ili kuwe kuna *privacy* ya mama anapojifungua waweze kuhimizwa kwenda na waume zao au ndugu zao wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa hatuna manesi na wahudumu wa kutosha, lakini mama anayejifungua anapokuwa kwenye *private room* yake anasindikizwa, inapotokea changamoto yoyote ndugu yake atatoa taarifa haraka kwa nesi na nesi atakuja kumsaidia. Kwa hiyo, niwaombe

sana hiyo michoro iweze kufanyiwa maboresho siyo kwamba kwa ujenzi wa majengo mapya tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kupongeza huduma nzuri inayofanyika kwa ajili *ya Pre-Mature Babies Ward (Neonatal Ward*) ambayo tumeiona Muhimbili. Sisi kama wanakamati wa Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI tumeona huduma nzuri. Sasa hivi hata mtoto mwenye gramu 500 anapata matibabu na ana uwezo wa kuishi. Niombe sana huduma hizi ziendelee kuimarishwa hadi ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa dawa ambazo ni muhimu sana kwa ajili ya watoto hawa ambao ni *premature babies*. Mfano *surfactant* ambayo ilikuwa inauzwa shilingi milioni 1.5 ambayo sasa hivi ni shilingi 700,000 ambayo ile inasaidia kukomaza mapafu ya mtoto. Vilevile, *caffeine* ambayo ilikuwa inauzwa shilingi 300,000 kwa dozi, hiyo ninaongelea ambayo sasa hivi ni shilingi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuna imani kabisa Mama yetu kipenzi, Mama Samia Suluhu Hassan anapenda akina mama wote, lakini pia watoto wote. Hili jambo linawezekana kabisa zikapatikana bure dawa hizi kwa ajili ya kuokoa watoto hao ambao wanakuja kabla ya umri na kwa gramu ambazo ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweze kuongelea suala zima la *NHIF*. Ninaipongeza sana Serikali na Wizara kwa pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Samia ambaye amekuwa akisimamia kila jambo analolipanga anahakikisha anaondoka akiwa amelikamilisha bila deni kwa Watanzania. Mama huyu anahitaji pongezi nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua ni awamu ya kwanza ambayo imepita kuhakiki kaya maskini na wameweza kuzipatia kadi kaya 276,000, kati ya kaya ambazo walikuwa wamegundua 1,206,000. Katika hizo, tayari wale waliokuwa na changamoto ya matibabu wamekwishapatiwa matibabu wananchi 18,000 katika hii awamu ya kwanza. Si kwamba kila anayepatiwa kadi ni mgonjwa ila wale waliokuwa wana shida ya ugonjwa

wameshapatiwa. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala *NHIF* ninaomba ku-*declare interest* kuwa mimi ni mfamasia na ni mmiliki wa biashara za *pharmacy*. Mheshimiwa Waziri, Wizara au Serikali tumekuwa bado hatuna uhusiano mmoja wa wafanyabiashara wa *community pharmacy* pamoja na Serikali. Sera zimekuwa zikitoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera ambayo imetoka ya *prescription* zisitoke nje ya Hospitali, lakini huko nyuma tulikuwa tuna *form 2C* ambayo mgonjwa akikosa dawa Hospitali ataipata popote. Anakuwa na wigo mpana wa kupata kile anachokihitaji na sicho anachotakiwa kupewa hapo kwa wakati huo, lakini wakaondoa. Kama kulikuwa kuna changamoto tulitakiwa tu-*deal* na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria na Kanuni tunazo wanaokiuka taratibu sheria ifuate mkondo lakini mmekuja kwenye suala hadi la *prescription*. Haya sera nyingine inahitaji hakuna dawa ambazo ni za cheti zisitolewe bila cheti *(antibiotics* sana). Huwezi ukakuta duka lolote la dawa ambalo linauza dawa ambazo hakuna *antibiotics* na tayari Mheshimiwa Waziri tuna changamoto ya *antimicrobial resistance* ambayo tunatakiwa tupambane nayo kama Taifa. Hili litakuwa ni janga kubwa sana. Kwa hiyo tunapoweka sera tuangalie hizi sera tunaenda kumsaidia nani? Tunamsaidia mwananchi au tunazidi kumuumiza? Hii *private sector (community pharmacy)* siyo maadui wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitengeneze tukaona kwamba hawa *community pharmacy* ni wafanyabiashara; wale ni watoa huduma ndiyo maana tuna kanuni hatutakiwi kufanya matangazo ya biashara. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. Ninajua yeye ni msikivu na usikivu wake hauishii mezani, unakwenda kufanya kazi. Nimwombe sana alisimamie hilo na atakapokuja kusimama hapo, atuambie sisi wafanyabiashara wa *pharmacy* tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema vijana tujiajiri, vijana wanajiajiri, wazazi wanasomesha watoto *School of Pharmacy* ili wakajiajiri, lakini changamoto inakuja kwenye soko la ajira. Changamoto ni ngumu tunawaajiri vijana wengi lakini bado *barriers* ni nyingi sana. Mheshimiwa Waziri tunaomba alibebe hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea vilevile ku-*declare interest* mimi ni mfamasia. Ninaomba niongelee suala ambalo Mheshimiwa Waziri tarehe 2, Aprili alikuwa na kikao cha watendaji pamoja na wadau wa *Medical Store Department* ambacho kilifanyika Keko *MSD*. Katika kikao hicho Waziri aulishauri kuhusiana na suala zima la kurugenzi za *pharmacy* kwamba wafamasia waweze kuingia kwenye *management*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri yuko sahihi, lakini jambo lile haliwezi kuongelewa kwenye majukwaa likaisha, tunahitaji kanuni. Aliliongea akiwa anajua kabisa umuhimu wa mfamasia katika Taifa na umuhimu wa mfamasia katika Hospitali zetu. 50% ya bajeti ya Hospitali yoyote ile iko chini ya mfamasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitengo kita-*order* kitu bila mfamasia kupitisha au yeye ndio kwenda kufuatilia *MSD*. Tukiachana na vifaa vikubwa kama ambavyo wanafanya *order* watu wa *procurement* lakini vilivyobaki vyote dawa na vifaa tiba lazima vitoke kwa idara ya *pharmacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inashindikana nini mfamasia huyu kuingia kwenye meza ya maamuzi mpaka awasilishwe au awakilishwe na Mkurugenzi? Haiwezekani, hawezi kuandaa wanapokwenda kufanya maamuzi ya kupunguza hiki kitoke, hiki kitoke; lazima mfamasia awepo ili na yeye aweze kushiriki. tunaomba Mheshimiwa Waziri alisimamie hilo na atakapokuja kuongea hapa aweze kutueleza wafamasia wote nchini tunataka kusikia kwamba liingie kwenye kanuni na lisiishie kwenye majukwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie jambo la Muhimbili Mpya. Ninaunga mkono na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kama Taifa na kama nchi Hospitali yetu ya

Muhimbili iko Dar es Salaam tunahitaji jengo linaloonekana. Ukiingia Muhimbili pale kwa mtu ambaye ni mgonjwa *JKCI* inaonekana, *MOI* inaonekana, lakini Muhimbili ni vitu vidogo vidogo pale *reception* unaweza ukashindwa kusema hapa ndiyo sehemu ya udobi au ndio penyewe? Ila unakuta tu umeambiwa mapokezi unajua ndiyo hapa, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia nchi za jirani zilizotuzunguka; je zina Hospitali ya Taifa? Je ni muhimu na sisi kama Taifa tuweze kutengeneza Hospitali yetu ya Muhimbili iendane na hadhi? Nikakuta ni kweli Kenya wana Hospitali ya Taifa; Uganda, nchi zote hizo kwa ajili ya muda sitaweza kuzitaja. Hata hivyo, *South Africa* wao hawana Hospitali ya Taifa ila wameboresha Hospitali zao nyingi kwa *level* ya huduma ya juu ambayo sisi kama Taifa ndiko tunakoelekea. Tuna Hospitali hizi za Kanda, tunaomba tuwekeze wataalamu wa kutosha huduma ziwe nzuri ili tufikie *level* ya huduma za Afya *South Africa*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. JACQUELINE K. ANDREW: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaunga mkono hoja lakini suala la Hospitali za Kanda Mheshimiwa Waziri tuna Kanda ya Magharibi bado kwa maana Tabora, Kigoma na Katavi na wameanza michakato, lakini Hospitali hiyo wameipeleka Kigoma. Hii kweli ni Kanda ya Magharibi au wanataka Tabora tuendelee kuja Kanda ya Kati. Tunaomba waturahisishie kwa kuangalia tu wakae mezani waangalie Kanda ya Magharibi na jiografia yake wanatusaidiaje wananchi wa Katavi pamoja na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tuna dakika kama tano zimebaki. Mheshimiwa Yagi Kiaratu unaweza kufanya kwa dakika sita?

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajitahidi.

MWENYEKITI: Haya endelea.

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwa nafasi hii adhimu ya kuchangia katika Bunge hili Tukufu. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa huruma zake kwetu na mapenzi yake makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya katika kutoa huduma kwa wananchi wa Tanzania. Nipongeze sana usimamizi wa uongozi wa Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Waziri bingwa kabisa mchapakazi, muadilifu na mwenye nia ya dhati ya kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemwona namna ambavyo anahangaika kutekeleza majukumu ya Wizara. Leo tumemwona anashughulika na kongani za viwanda. Amekuwa mgeni rasmi katika kukabidhi ekari 400 pale Mloganzila lakini yeye huyo huyo unamkuta yuko mstari wa mbele kuhamasisha kinga na tiba kwa magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa yanayoambukiza, lakini na magonjwa mlipuko na amekuja na *slogan* nzuri ya zijue namba zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zijue namba zako maana yake pima mapema na ujue uzito wako, ujue *pressure* yako, ujue *cholesterol* yako, lakini ujue sukari yako ili kuchukua tahadhari mapema kwa ajili ya magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ni kinara wa uzazi salama na staha na hii imetuletea heshima katika nchi yetu. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo tunaona ni namna gani tumepata Waziri sahihi kwa wakati sahihi kuelekea mageuzi makubwa ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Naibu Waziri dada yangu Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi kwa utulivu wake, umakini

wake na taaluma yake, amekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Wizara. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomwongelea Katibu Mkuu wa Wizara. Kaka mwenye hekima zake, mchapakazi lakini mwenye uzoefu mkubwa. Waswahili wanasema wali wa kushiba huonekana kwenye sahani. Tuiangalie taarifa kubwa ya Wizara ya Afya yenye kurasa takriban 287 namna ilivyoandaliwa kwa umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo ni kubwa na imesheheni maeneo mbalimbali, lakini kote kumesheheni takwimu, malengo, tumefikia wapi lakini kwa asilimia ngapi? Huyo ndiyo Dkt. Seif Shekalaghe, Katibu Mkuu wa Wizara, anaonyesha umakini mkubwa na uwezo mkubwa katika kuongoza utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye anasaidiwa na Manaibu wake wawili, ninawapongeza Wakurugenzi wote wa Wizara ya Afya na Daktari Mkuu dada yangu Magembe anafanya vizuri. Watumishi wote wote ninawapongeza na Mungu awasaidie waendelee kutumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote pia yanasimamiwa na kinara wetu, kiranja wa Mawaziri, Waziri wetu Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba. Tumemwona na yeye namna ambavyo suala zima la afya ni kipaumbele chake na Mheshimiwa Rais wetu yeye ndiyo chachu ya haya yote, amekuwa mstari wa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tuna historia ya wapi tumetoka katika huduma za afya. Kwa kipindi hiki kichache tumedumisha, tumejenga na tumeboresha miundombinu ya afya kutoka ngazi ya msingi mpaka Taifa. Tumejenga zahanati za kutosha, vituo vya afya vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila halmashauri ina Hospitali ya Wilaya. Tuna Hospitali nzuri za rufaa za mikoa zinazotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Pia, tuna Hospitali nzuri za Kanda, Hospitali maalum na tuna Hospitali yetu ya Taifa ya Muhimbili. Hapa niseme na mimi niungane na wenzangu kuunga hoja ya kuwa na Muhimbili mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muhimbili mpya itatuletea heshima na hadhi kama Watanzania kwa sababu ndiyo Hospitali yetu moja tu ya Taifa. Hospitali yetu ya Taifa inatoa huduma nzuri za kibingwa na ubingwa bobezi na hii imesababisha kuwa na tiba utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kutoka Comoro, Msumbiji, Zambia, Malawi, Rwanda, Burundi, Uganda, Sudani, Ghana na hata Ulaya (tumepata watu kutoka *Poland* kuja kutibiwa Tanzania na wakasifu huduma nzuri zinazotolewa hapa). Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuitengeneza Hospitali yetu kwa maana ya kuipa hadhi ya kukidhi ithibati ya kimataifa, lakini kuweka utaratibu mzuri wa mpango mkakati wa kuipanga pale Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema msemaji mmoja unaweza kwenda pale ukapotea. Unatoka maabara hujui uende wapi ukitoka kwa daktari unakwenda mwendo mrefu kwenda kupima. Kwa hiyo, ni vyema Hospitali hiyo ikapangwa vizuri ikawa na majengo mazuri yanayotoa huduma kwa mahali pamoja na hii itapunguza usumbufu kwa wagonjwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mama Samia amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na viwanda vya dawa kwa ajili ya uwekezaji mzuri lakini hii itatupunguzia sisi utegemezi kutoka nje na kutujengea uwezo wa kupata dawa safi na salama kwenye nchi yetu, kukuza uchumi wetu na kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninataka kuongelea ni Bima ya Afya. Hii sasa ni mwarobaini na tiba kwa Watanzania wote kuwa na wananchi wenye Afya kuelekea utekelezaji wa Dira ya 2050. Tutakuwa na Taifa zuri lenye watu wanaokuwa na Afya nzuri na wenye uwezo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania watakuwa na nafasi ya kupata tiba bora kwa wakati wote, lakini kwa gharama nafuu na vilevile tutazijengea uwezo Hospitali zetu za kuendelea kufanya kazi vizuri. Nitoe tu mfano sasa hivi Mheshimiwa Rais hataki mtu asitibiwe. Kwa hiyo, hospitali zinakuwa zinatoa msamaha mkubwa wa mabilioni ya shilingi. Kwa hivyo

tunazinyima uwezo wa kuendelea kufanya kazi, lakini tukianzisha Bima ya Afya maana yake Mfuko utalipa gharama za matibabu na hivyo Hospitali zetu zitakuwa na nguvu na uwezo wa kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu tuendelee kuimarisha huduma hii vizuri kwa kuendelea kuweka miundombinu mizuri, lakini vilevile tutoe elimu kwa wananchi. Wote tushirikiane; Serikali na sisi wanasiasa ndiyo tunajua zaidi. Sisi tunaamka tunajua watu wanaumwa kiasi gani na wanakosa matibabu kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la mifumo; ni lazima tuimarishe mifumo yetu kwa namna mbili. Namna ya kwanza mifumo hii ya matibabu lazima isomane kuanzia ngazi ya msingi mpaka Taifa. Vilevile lazima kuwe na mifumo mizuri ya kudhibiti *fraud* katika utekelezaji wa Bima ya Afya. Tumeona mtu anadanganya anatibiwa mwingine na mwenye bima mwingine. Kwa hiyo, lazima uwekwe mfumo mzuri wa kuhakikisha anayetibiwa ndiyo mnufaika wa ile Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa pia kuendelea kutoa huduma za Afya vizuri, wataalam wetu wasomeshwe vizuri na vilevile maslahi ya Watumishi wa Afya yaangaliwe kwa maana ya kuwapa motisha ili waendelee kutoa huduma nzuri ikiwemo *customer care* nzuri kwa wagonjwa. Bima ya Afya ni suala la sisi wote kama wamesema wasemaji wenzangu na hivyo tuwaombe wote tushirikiane; wa kuhamasisha wahamasishe, wa kuboresha miundombinu kama umeme, maji, barabara wafanye mambo yao; lakini vilevile tutenge fedha za kutosha kwa ajili ya yale makundi yanayohitaji kulipiwa na Serikali ili tusije tukamwacha mtu nyuma katika kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka Singida, ninaomba nikiri maslahi. Nishukuru sana Serikali Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida kwa kweli inafanya vizuri na kwa sasa hivi imeanza kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Tulikuwa hatufanyi *dialysis* lakini leo mashine zinafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Singida walikuwa wanasafiri umbali mrefu kuja Benjamin kufanya *dialysis*. Hii iliwagharimu sana na wengi walikata tamaa na kubaki nyumbani. Vilevile tuna mashine nzuri za afya *CT-SCAN,* tuna wataalam wa kutosha, lakini upo ujenzi unaoendelea kwa sababu hospitali ile ni kama mpya. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aendelee kupeleka fedha pale, majengo yale yakamilike ili huduma ziendelee kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Singida ni hospitali mpya, ina eneo kubwa la zaidi ya ekari 100. Niwaombe Wizara waitumie vizuri nafasi hiyo. Wanaweza kutumia eneo hilo kwa ajili ya kufungua Chuo cha Afya lakini vilevile wanaweza wakafungua pale Hospitali ya Kanda. Baada ya Benjamin kuwa Hospitali Maalum, basi Singida ni mahali sahihi kwa sababu iko katikati na miundombinu ya barabara ni mizuri. Niwaombe sana waliangalie hilo, lakini wananchi wa Singida wako tayari kutoa ushirikiano ili haya yote yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho niombe Wizara ya Afya ifikirie kujenga jengo la magonjwa ya afya ya akili pale Singida Hospitali ya Mkoa, kwa sababu hili tatizo linaendelea kukua, basi wapate faragha na matibabu mazuri. Nia ni kuona kwamba kila Mtanzania anapata huduma na anarudi kuijenga nchi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi hiki cha uchangiaji. Tutakaporejea tutaendelea na watakaoanza ni Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa George Natany Malima; kisha watafuata Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mheshimiwa Asha Juma Feruz na wengine tutawataja kadri muda unavyokwenda.

Kwa haraka tuwatambue baadhi ya wageni wachache. Kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Waziri wa Afya, hawa ni wawakilishi wa makampuni

au kampuni ya utengenezaji wa chanjo na bidhaa za Afya za kibaiolojia kutoka Ujerumani. Ninashukuru, wako pale karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tuna wafanyabiashara kutoka Malta, Dar es Salaam na Zanzibar. Karibuni sana ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Waheshimiwa Wabunge tunawakumbusha semina ya uchukuzi itakayoendelea mara baada ya kuahirishwa kikao hiki sasa hivi, kwenye ukumbi wetu wa kawaida wa Msekwa.

Baada ya hayo machache, ninaomba nisitishe Kikao cha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.06 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae. Katibu.

NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya. Sasa ninaomba kumwita Mheshimiwa Nadra Ghulam Rashid na Mheshimiwa George Natany Malima ajiandae.

MHE. NADRA GHULAM RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia katika bajeti hii muhimu ya nchi yetu ya Wizara ya Afya. Awali ya yote,

ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia afya kusimama hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu, ninaomba unipe ruhusa nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama, kwa kulirejesha jina langu ili niwe mgombea wa Ubunge Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee ninawashukuru wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, kwa imani kubwa walionionesha nami kunifanya kuwa mwakilishi wao kusimama katika Bunge hili Tukufu. Haikuwa rahisi, lakini analolipanga Mwenyezi Mungu, hakika mja hawezi kulipangua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoibeba Ajenda ya Afya, sote tumekuwa mashuhuda, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa kinara katika afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee nimeisikiliza bajeti hii kwa umakini mkubwa, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mohamed Mchengerwa, kwa wasilisho zuri lililobeba vipaumbele vya msingi ambavyo vitaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri Florence Samizi kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwa maarifa na weledi mkubwa. Kama unavyojua, afya ni msingi wa mwanadamu kwa maana unaweza kumiliki kila kitu lakini bila afya madhubuti ni kazi bure. Ndiyo sababu Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, huweka mkazo madhubuti kwenye Sekta ya Afya. Nyote mtakuwa mashuhuda, tokea Mheshimiwa Rais kuingia madarakani, ameweza kupunguza vifo vya akina mama na watoto kufikia 556 hadi 104. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo sababu iliyopelekea Shirika la *Gates Foundation* kumtunuku Mheshimiwa Rais wetu tuzo ya *Goalkeeper Award* kwa kutambua mchango wake wa kupunguza vifo vya akina mama kwa 80%. Sambamba na jitihada za Serikali, tunaikumbusha Serikali yetu juu ya kuendelea kusimamia mipango ya upatikanaji wa huduma bora kutoka kwa wahudumu wa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, tunaweza tukawa na kila kitu, lakini bila ya huduma bora ya afya, inakuwa ni kazi bure. Kwa hiyo ninawaomba watumishi wa afya nchini kote kuendelea kuonesha tabasamu kwa wagonjwa wetu kwani kufanya hivyo, nayo pia ni ibada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitimisha kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuibeba Ajenda ya Afya mabegani mwake na kuendelea kusimamia mikakati ya Bima ya Afya kwa wote, ujenzi wa miundombinu ya Muhimbili mpya na utekelezaji wa Sera kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa George Natany Malima na ajiandae Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii ya Afya. Kwanza ninaanza na kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutupa afya na nguvu wote tumeendelea kuhudhuria na kufanya shughuli zetu kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia, kwa kazi nyingi na nzuri ambazo anaendelea kuzifanya katika sekta mbalimbali na hasa katika Sekta hii ya Afya. Tumeona katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anazungumzia mafanikio mengi ambayo yamefanyika katika kipindi cha utawala wa Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande huu wa afya, amezungumzia jinsi ambavyo Vituo vya Afya vimeongezeka kutoka Vituo vya Afya zaidi ya 10,000 mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 13,000. Tumepunguza vifo vinavyotokana na uzazi kutoka vifo 556 kila uzazi 100,000 mpaka kufikia 104, haya ni mafanikio makubwa sana, ninamwombea Mungu aendelee kumjalia ili kazi hii iendelee kufanyika vizuri kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuchangia mambo machache katika eneo hili au katika Wizara hii ya Afya. La kwanza ninaanza na kuzungumzia habari ya au Mpango wa Bima ya Afya kwa Watu Wote. Ninaipongeza Serikali sana kwa kuanza na kaya za watu maskini 1,206. Idadi hii ukiangalia na idadi ya watu katika nchi yetu, utaona bado ni ndogo sana, lakini ninaamini Serikali itaendelea kufanya vizuri. Ambacho ninataka kutahadharisha hapa ni kwamba, zoezi la kutambua kaya maskini ni zoezi mtambuka, ni lazima Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawe waangalifu sana pia, tunao uzoefu wa kutosha kuhusu suala hili la kutambua watu wenye kaya maskini. Inaweza ikatokea tusipokuwa waangalifu, wale ambao siyo maskini sana wakapata huduma hii ya afya kwa watu wote halafu wale maskini kabisa wakaachwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kazi hii ni muhimu sana, lazima wasaidizi wako mpaka kule chini wanaokusaidia kutambua kaya maskini ili waingie kwenye mpango huu, wawe makini, lakini wawe waadilifu waweze kutambua kaya maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana umesema katika hotuba yako kwamba afya ni mtaji na afya siyo starehe. Kwa hiyo, kama unatambua afya ni mtaji, lazima tuangalie sana wale watu ambao kweli kaya zao ni maskini, hawawezi kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona katika mpango huu, kule vijijini watu bado wanashindwa kutofautisha kati ya kifurushi kile ambacho tulikuwa nacho cha shilingi 30,000 na hiki kipya cha shilingi 150,000. Hawaoni tofauti,

wanadhani ile huduma waliyokuwa wanaipata kwenye kifurushi cha shilingi 30,000 ndiyo ileile itapatikana kwenye kifurushi cha shilingi 150,000, kwa hiyo hawaoni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inatakiwa itoe elimu sana kwamba kifurushi kile kilikuwa na huduma chache, ni kama huduma ya mwanzo lakini hii ya shilingi 150,000 inakwenda kukomboa wananchi, inakwenda kuwa na *package* kubwa kuliko ile ya shilingi 30,000. Kwa hiyo, elimu itolewe watu waelewe, hii itasaidia watu wengi wawe na uelewa lakini pia watajiunga kwa wingi. Na kwa kufanya hivyo tutakuwa tumesaidia wananchi wetu na hasa wale wa kaya maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba Wizara inapoendelea kufanya shughuli zake iliangalie kwa karibu sana, bado tuna baadhi ya watendaji au wafanyakazi katika maeneo yetu ya kutolea afya au kutibu wananchi, ambao wanafanya kazi kinyume na maadili ya kazi zao. Kwenye hospitali wapo baadhi ya wafanyakazi wanatumia lugha mbaya kwa wagonjwa, wako wanaendeleza wizi wa dawa, lakini wako ambao wanafanya vibaya katika kazi zao. Hili tatizo ni kubwa katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali kupitia Wizara hii ya Afya, iendelee kufanya bidii, iende kwenye maeneo yote, vituo vya afya, iende kwenye zahanati, kwenye hospitali za wilaya, mikoa, iangalie, itafute hao watu ambao wanachafua *image* nzuri ya nchi yetu. Mama anakusudia kuwasaidia watu wote wa Tanzania kupata matibabu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma bora haiwezi kuja kama kuna baadhi ya wafanyakazi wanaendelea kueneza au kuendeleza rushwa katika hospitali, wanaendeleza lugha chafu kwa wagonjwa, wazembe, watoro. Hao wote lazima wizara hii iwe makini sana, iwaangalie kwa karibu ili tuweze kupata huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo bado tunalo kwenye hospitali zetu, ni upungufu wa dawa. Hata tulipokuwa tunatumia kifurushi hiki cha shilingi 30,000, watu wanakwenda

hospitali, amekata bima, akishaandikiwa dawa na daktari anaambiwa aende

akanunue duka ambalo lipo nje ya hospitali, jirani na ile hospitali. Tabia hii imefanya watu wanakuwa hawaelewi bima maana yake nini. Ana bima lakini hawezi kupata dawa. Kwa hiyo, upungufu wa dawa pia ni jambo ambalo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti ya Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba upatikanaji wa dawa uko vizuri sana na sisi tunaona, lakini dawa zile zikifika hospitali zinaibiwa ama zinapelekwa mahali pengine. Kwa hiyo, masuala ya dili kwenye dawa lazima jambo hili alichukulie kwa uzito mkubwa sana. Maeneo mengi kuna upungufu wa dawa, bima hii ya shilingi 150,000 inachukua *package* kubwa, hatutarajii kuona mtu ana bima hii ya shilingi 150,000 anakwenda hospitali halafu anaambiwa dawa hakuna atoke nje kwenye duka la jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa tulizonazo, dawa hizi ndizo zile zinazotoka mle ndani, zinaibiwa na baadhi ya wafanyakazi ambao siyo waaminifu, zinatolewa nje zinaenda kuuzwa kwa ajili yao. Tatizo hili ni kubwa karibu kila sehemu katika nchi yetu. Kwa hiyo, ninaomba sana jambo hili tuliangalie kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema tumeongeza vituo vingi, nami ninakubaliana na hayo, lakini bado kwa ukubwa wa nchi yetu, kuna maeneo mengi sana vituo vya afya vinahitajika. Wananchi wetu wanasafiri mwendo mrefu kwenda kutafuta dawa kwenye vituo vya afya. Bado kuna maeneo mengi, hata kule ninakotoka kwenye Jimbo la Mpwapwa, nina vituo, *I mean* nina kata za kimkakati hazina Vituo vya Afya. Kwa hiyo, ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu ili bima hii iwasaidie, lazima tuwe na maeneo ya jirani ambapo wanaweza kwenda na bima zao wakaenda kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali pia kwa kuongeza wingi wa zahanati. Zahanati zimeongezeka kwa wingi sana, ninampongeza Rais, Mheshimiwa Samia na Mheshimiwa Waziri na

Mheshimiwa Naibu Waziri wake, kwamba haya waliyoyasema kwenye maandiko kwenye hotuba yao, tumeviona na tunakiri kwamba wamefanya kazi kubwa sana. Hata hivyo, kwa ukubwa wa nchi yetu, bado tuna kazi, bado tuna mwendo, tukazane tuweze kuongeza zahanati kwa wingi. Maboma yapo mengi kwenye maeneo yetu, tuhakikishe tunamalizia maboma ya zahanati, wananchi waendelee kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhakikishe pia kwamba, kila kata inakuwa na kituo cha afya, hapo ndipo tutakuwa tumewakomboa Watanzania. Na spidi ya Mpango huo wa Bima ya Afya, mimi ninaomba iongezwe. Idadi hii ambayo tumeanza nayo ni ndogo, ninaomba tuongeze spidi ili baada ya muda mfupi, wananchi wengi wawe na Bima ya Afya ile ya shilingi 150,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, ajiandae Mheshimiwa Asha Juma Feruz.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uhai. Ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana aliyoifanya kuanzia ameshika madaraka mpaka sasa katika Sekta ya Afya. Hospitali kubwa zimejengwa, vituo vya afya na zahanati lukuki katika kila pande ya nchi hii zimejengwa kwa msukumo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Mohamed Mchengerwa na Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutuletea andiko hili la bajeti ambalo kwa kweli lina matumaini makubwa sana ya kuboresha afya za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja kama tatu hivi ninaomba kuziweka Mezani kwao. kwanza kabisa, ninaomba kuongelea kuhusiana na matibabu ya wazee pamoja na watoto walio chini ya miaka mitano na wazee ambao wana miaka 60 na kuendelea. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 Ukurasa wa 19, imeandikwa kwamba watoto chini ya miaka mitano na wazee wa zaidi ya miaka sitini, hawa wanapaswa kupewa matibabu ya afya bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee hawa ninaowataja hapa, ni wazee wote wanaozidi miaka 60, lakini ninasisitiza sana kwa wazee wale ambao walikuwa wajasiriamali, walikuwa wafanyabiashara, wakulima ambao sasa hawana nguvu tena ya kufanya hizo kazi, sasa hawawezi tena kutumia nguvu kuweza kufanya kazi. Wana afadhali wale waliokuwa watumishi, ambao labda wanapata pensheni, lakini hao niliowataja hawapati pensheni. Ninadhani, hii Sera itekelezwe ipasavyo; kwa sababu katika hali halisi mtaani, tunasema Sera inasema matibabu yatakuwa bure, lakini hali halisi haiko hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba uko utaratibu wa kuwahudumia wazee hawa, lakini hali halisi ilivyo ni kwamba wazee wengi na watoto mwisho wa chini ya miaka mitano, wanalipa na kwa kweli wakati mwingine wanapoteza maisha kwa sababu tu hawana uwezo. Kwa hiyo, ninadhani Sera hii iendelee kusisitizwa na kwa kuwa sasa tupo kwenye Bima ya Afya kwa Wote, basi Sera ya Bima ya Afya pamoja na Sera hii ya Afya ya 2007 ishirikiane kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba huduma bora za afya zinatolewa kwa watu wote hasahasa watoto chini ya miaka mitano na wazee wa zaidi ya miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninasema kuhusiana na vituo vya afya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli vituo vya afya vimejengwa vingi sana nchini. Kwa mujibu wa Sera yetu ya Afya ya Mwaka 2007 ambayo ipo kwenye ukurasa wa 22, inatamkwa wazi kabisa kwamba kila kata inapaswa kuwa na kituo cha afya, lakini ninaamini kutokana na bajeti, kwa kweli siyo kila kata ambayo ina kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza tu kwamba Serikali iendelee kujenga Vituo vya Afya kwa nguvu zote. Ninafahamu vituo vya afya viko chini ya TAMISEMI, lakini kwa kuwa Wizara ya Afya ndiyo inayotunga Sera na kuzisimamia, vituo vya afya viimarishwe kwa sababu viko kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema hapa kwa hapa katika Jiji la Dodoma, kuna Kituo cha Afya cha Chang'ombe: Kituo cha Afya cha Chang'ombe na labda niseme tu, Kata ya Chang'ombe ni kata yenye watu wengi katika Jiji la Dodoma, inafuatiwa na Nzuguni: Nzuguni inatangulia lakini inafuata Chang'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya kile kilichopo hakina uzio, ninaomba Mheshimiwa Waziri, ninajua hili suala la TAMISEMI, lakini ninamwomba ashughulike ili hiki Kituo cha Afya kiweze kupata fensi pamoja na kisima cha maji ili wagonjwa waweze kupata huduma stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kidogo kuhusiana na Hospitali ya *General* ambayo ni Hospitali ya Rufaa hapa Dodoma, ni hospitali ambayo kwa kweli inatoa msaada mkubwa sana kwa wakazi wa Dodoma. Hospitali hii ina changamoto kadhaa, ikiwemo ukosefu na upungufu mkubwa wa baadhi ya wataalam. Ninavyoongea sasa, kuna upungufu wauguzi 420 na madaktari 56. Ninaomba hawa wataalam wapatikane ili kuboresha huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mirembe ambayo ni hospitali ya wenzetu ambao wana shida ya afya ya akili. Hospitali ina changamoto kadhaa, kubwa zaidi ni watumishi. Watumishi wengi wakipangwa pale Mirembe wanakimbia kwa sababu ya hali halisi ya unyanyapaa wa wagonjwa wenye shida ya akili. Ninaomba sana hospitali hii ifikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri tu, ajira za watumishi hawa zitolewe kwa tangazo maalum ili wale wenye wito wa kusaidia ambao wana shida ya afya ya akili, waweze kuwasaidia ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; Hospitali yetu ya Muhimbili ni kweli hospitali inakarabatiwa inajengwa upya ni jambo jema, ni hospitali ya kihistoria, na ni hospitali ambayo ina wataalam wengi. Ninaomba nipendekeze tu kwamba nchi inazidi kuwa na watu wengi na Muhimbili inaweza ikaji-*reflect* katika mikoa yote na ninaomba nipendekeze na Mheshimiwa Waziri anaweza kunisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma wakati Muhimbili inajengwa watu walikuwa wachache sasa wamekuwa wengi na juzi kwenye semina nimesikia wazo kutoka kwa baadhi ya wachangiaji kwamba Shule ya Azania na hata Jangwani ziondolewe ili Muhimbili ipanuliwe, inaweza kuwa wazo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme hivi Wizara ihakikishe kwamba inapata maeneo nchi nzima. Mheshimiwa Waziri atafute maeneo, aelekeze *RMOs* watafute maeneo makubwa. Leo hii Watanzania tuko 65,000,000 huenda baada ya miaka 50 tukawa wengi zaidi, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atenge maeneo kila Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atenge maeneo makubwa kwa sababu baada ya miaka 50 tutakuwa sisi wote hatupo, lakini Bunge litakuwa na watu, ninaomba atenge maeneo, atafute hati miliki ili maeneo haya yawepo, watakaokuwepo watakuja kuwaza nini cha kufanya na hayo maeneo vinginevyo tutakuwa kama Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunawaza kubomoa Azania, tubomoe na Jangwani siyo jambo sahihi ni muhimu sana ninashauri tutafute maeneo ya kutosha katika nchi hii tuyapatie hati ili wanaokuja watajua nini cha kufanya ili kuimarisha afya ya Watanzania... *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ninakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Juma Feruz, ajiandae Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba.

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuchangia Hotuba iliyopo Mezani ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Afya. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote leo kuweza kupata fursa ya kuchangia na kusikiliza Hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza Hotuba hii na ukaisoma utaona nia thabiti ya Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo inakwenda kuwekeza pesa nyingi kwa ajili ya kuboresha afya za wananchi. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais tangu mwaka 2021 – 2025 na hata Hotuba imeonesha mpaka 2026 amefanya mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vimejengwa vituo vya afya 3,530. Hivi ni vituo vipya ambavyo havikuwepo, lakini zimejengwa zahanati 403 katika maeneo yetu, hospitali zimejengwa 71 na nikizungumzia hospitali 71 hapa tunaongeza Hospitali ya Mkoa wa Katavi ambayo haikuwepo, Hospitali ya Mkoa wa Njombe, Hospitali ya Geita, Hospitali ya Simiyu na Hospitali ya Songwe. Hakika Mheshimiwa Rais wetu tuna kila sababu ya kumuunga mkono katika jitihada za kuboresha afya za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais baada ya kuapa katika siku zake 100 za utendaji wa kazi ametoa kibali cha Watumishi wa Kada ya Afya 5,000. Ni ukweli bado tuna upungufu mkubwa wa Watumishi, lakini kitendo cha Mheshimiwa Rais, mama mwenye huruma kuweza kutoa kibali cha kuajiri watu 5,000 siyo jambo dogo. Ameona ni mujibu kujibana ili wananchi wake waendelee kupata ustawi kwenye eneo la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niuelekeze mchango wangu katika eneo la utoaji huduma katika ngazi ya msingi. Kama tunavyofahamu wananchi wetu wanaopata huduma wengi wanapata huduma katika eneo la zahanati na vituo vya afya na

huko ndiko wananchi waliko tofauti na Hospitali za Rufaa ambazo zinachukua 20% au 15% iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI iboreshe na iendelee kuongeza vituo vya afya katika kata zetu. Nchi yetu ina kata 3,960 lakini kata hizi 3,960 kata ambazo zina vituo vya afya ni 1,055 ambayo ni sawa na 27%. Tuna upungufu wa vituo vya afya kwenye kata zetu 2,905 ambayo ni sawa ni 83%, tuna vijiji 12,345, vijiji vyenye zahanati kama Sera inavyosema kila kijiji kuwe na zahanati, ni vijiji 6,556 ambayo ni sawa na 53%, 47% ya vijiji haina zahanati ambayo ni sawa na zahanati 5,789.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ninataka kusema? Wananchi wetu wanapata huduma za afya za msingi kwenye zahanati na kwenye vituo vya afya. Tukumbuke kwamba vipo vijiji ambavyo kutoka eneo la kijiji mpaka kuifikia kata ni umbali mrefu lakini kwenye vijiji hivi na kata hizi ambazo angalau zina vituo vya afya wapo watumishi wachache. Tuangalie tunapoajiri tuyalenge yale maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopeleka watumishi hawa niwaombe Wizara kuangalia namna watakavyoweza kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi ya watumishi hawa ili kuondoa ile adha ya mtumishi kaajiriwa leo na kesho anaomba uhamisho kuondoka kulingana na mazingira ya kazi yalivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya kwa Wote itakwenda kusaidia kundi kubwa ambalo linapata huduma kwenye hii afya ya msingi kwa maana ya zahanati na vituo vya afya. Kwa hiyo, tunayo sababu kubwa ya kuhakikisha tunaboresha mazingira ya utendaji kazi ya watumishi hawa, lakini pia tunaboresha huduma kwenye mazingira haya ya afya ya msingi na huu ndiyo mwelekeo wa Dira ya Taifa ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia kuchangia kwenye eneo la huduma ya mama na mtoto, lakini na kwa wazee, wamesema wachangiaji waliopita. Sera inasema mtoto chini ya miaka mitano apatiwe huduma bila gharama yoyote na mzee pia, lakini ni ukweli bado kuna maeneo watu hawa wanatozwa

pesa, tuangalie usimamizi. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote huku juu wanafanya kazi vizuri sana shida ipo kule tunapopata huduma za msingi niwaombe ufuatiliaji katika utendaji kazi, tuangalie changamoto iko wapi? Kwa nini tunaendelea kupata hiyo changamoto hali ya kuwa Serikali imejipanga vizuri, dawa zinashuka nini kinapelekea haya? Binafsi ninaona ni kama kuna eneo watu hawafanyi wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuipongeza Wizara, imechukua hatua kubwa tumeona kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, sasa wanakwenda kuimarisha mifumo kusomana, mifumo ya afya. Nimeona kuna Mfumo wa *eHMS GOTHOMIS*, Mfumo wa Dharura za Afya (*NEMS)*, Mfumo wa Jumuishi wa Wahudumu na mifumo mingine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, ilikuwa mgonjwa akipewa Rufaa kutoka Hospitali ya Wilaya kwenda Hospitali ya Mkoa akifika pale anaanza vipimo upya, ni gharama Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, akitoka Mkoa akapewa Rufaa kwenda Muhimbili au Benjamini akifika pale anaanza upya tena amejikusanya ametafuta nauli, amejikusanya aone ni namna gani anaweza kuji-*accommodate* kwenye maisha, anafika pale mifumo haijasomana anaanza upya tena vipimo vya milioni au laki. Mwananchi huyu wa kawaida tunakuwa tunamuumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze sana kwa hatua hii kubwa waliyoona sasa mifumo inakwenda kusomana na wamesema mpaka sasa 90% ya hospitali zetu za Rufaa mifumo inasomana. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na tunawatakia heri tuko hapa kuwapa ushirikiano. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba; wajiandae Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa na Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo.

MHE. JUMA M. KAWAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Hotuba ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kwanza ninanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejalia afya njema na ametujalia Wabunge wote kuhudhuria Kikao hiki jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nipeleke shukrani zangu za dhati na pongezi zangu za dhati kwa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazofanya na kuendelea kudumisha amani na utulivu ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri ya kusimamia sekta ya afya nchini. Sote tunakubaliana hapa Waheshimiwa Wabunge afya ndiyo msingi wa maendeleo, Taifa lenye afya bora litazalisha vizuri kwenye sekta ya kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, sekta hii ya afya inatakiwa ipewe kipaumbele kikubwa sana ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, lakini bado kuna changamoto mbalimbali zinaikabili sekta hii hasa kwa mimi Mbunge ambaye ninatokea maeneo ya vijijini. Ndani ya Jimbo langu la Igalula bado kuna upungufu wa dawa, bado kuna upungufu wa watumishi wa afya, lakini bado kuna upungufu wa vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya japokuwa yapo chini ya TAMISEMI, lakini ninafahamu hii ndiyo Wizara mama. Ninaamini Mheshimiwa Waziri amesema hapa, inatakiwa tupambane kwa ajili ya kuweza kuipigania sekta afya hii nchini, lakini ndani ya Jimbo langu la Igalula bado mama anatembea kutoka Kijiji cha Magulyati kuja Kijiji cha Tura kilomita 45 kwa ajili ya kufuata huduma za kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mama anatembea karibia kilometa 50 kutoka Kijiji cha Nkongwa kuja Kijiji cha Tura kwa ajili ya kufuata huduma za uzazi. Tunafahamu Sera ya Chama Cha Mapinduzi 2025 - 2030 inatuelekeza vizuri inatakiwa tupunguze vifo

vya mama na mtoto kutoka 0.06% mpaka 0.02% itakapofika 2030. Ninaiomba sana Wizara ya Afya twendeni tukamuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha, tunapambana kuweza kuzuia wananchi wetu wasitembee umbali mrefu kufuata huduma za afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambazo Wizara ya Afya inafanya, lakini Mkoa wangu wa Tabora bado unapitia changamoto mbalimbali. Tuna upungufu wa Watumishi wa Sekta ya Ganzi, Watumishi wa Radiolojia lakini tuna upungufu wa Wataalam wa Kinywa na Meno. Mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeajiri watumishi 305; mwaka wa fedha 2025/2026, watumishi 315. Tunaipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri ambazo inaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa Madaktari Bingwa sisi kama Mkoa tunatakiwa tuwe na Madaktari Bingwa 78 lakini tuna Madaktari Bingwa 12 tu, tuna upungufu wa Madaktari Bingwa 66. Hii ni sawasawa na 64% ya upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inamaanisha nini? Kwamba Hospitali yetu ya Mkoa wa Tabora kuna huduma zingine za kibingwa hazitolewi pale na hii ni rai yangu kwa Wizara ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* Bajeti yake ya Wizara ya Afya atuambie sasa, sisi kama Mkoa wa Tabora ni lini hospitali yetu itakamilisha kutoa zile huduma za kibingwa ambazo zilitakiwa zitolewe lakini sasa hivi hazitolewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niongelee masuala ya magonjwa yasiyoambukiza. Serikali imeendelea kupambana na magonjwa yanayoambukiza kama vile kifua kikuu, UKIMWI na malaria, lakini bado Taifa linatafunwa na magonjwa yasiyoambukiza. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara inaonesha takribani ya vifo 33% vinatokana na magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa za *WHO* 2020 zinaonesha kwamba watu 41,000,000 kila mwaka wanapoteza maisha kwa magonjwa yasiyoambukiza na sawasawa na 71%. Hii inatuonesha nini? Serikali inatakiwa ichukue hatua za haraka kupambana na magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu inayowekeza katika magonjwa yanayoambukiza hivyo hivyo iwekeze kwenye magonjwa yasiyoambukiza na haya magonjwa yasiyoambukiza yanatula sisi kimyakimya. Magonjwa yenyewe ni kama vile shinikizo la damu, saratani, kisukari, presha na yanatokana kwa ulaji uSIYOfaa, unywaji wa pombe na kuvuta sigara uliopitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali nguvu inazotumia kuwekeza kwenye magonjwa yanayoambukiza hivyo hivyo iwekeze kwenye magonjwa yasiyoambukiza. Ninaiomba Serikali, wagonjwa wengi ambao wanaonekana wanapata *HIV* wengi wanaangukia kupata magonjwa yasiyoambukiza. Sasa ninaiomba Serikali iunganishe nguvu za kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, iunganishe nguvu vilevile pamoja na kupambana na *HIV* nchini. Magonjwa haya ipambane nayo kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nichangie suala la miradi ya afya nchini. Kwanza kabisa ninapenda kumpongeza sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa ambao anawekeza kwenye sekta hii afya, kila mwaka anatoa trilioni 6.3 kwenye kuwekeza kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwenye Hotuba yake vizuri kwamba tuna miradi mingi, hilo ni suala la kujisifia sisi kama Taifa, lakini sijasikia kwamba hii; miradi kwa mfano tunajenga majengo mengi ndani ya nchi yetu sijaona fungu ambalo limetengwa kwa ajili ya wakandarasi wanaokagua miradi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri tunapoanzisha mradi wowote na tutenge fungu kwa ajili ya wakandarasi wa kukagua miradi yetu hii. Kwanza itasaidia tuweze kupata miradi iliyo bora, lakini miradi iweze kukamilika kwa wakati. Kuendesha miradi mikubwa kama tunaona Mradi wetu huu Muhimbili una trilioni 1.2, mradi huu unakwenda kuwekeza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania (walipakodi) wanataka waone hospitali hii imekamilika iendane na thamani ya fedha iliyowekwa. Sasa thamani hii itakamilikaje? Itakamilika kwa kuhakikisha kwamba kabla hatuja-*raise certificate* yoyote ya kuweza kumlipa huyu mkandarasi atakuwa anaendesha hapa. Lazima sisi wakandarasi wetu wa ndani ya Wizara wakague waone kwamba kazi imefanyika vizuri ndiyo mkandarasi aweze ku-*raise certificate* na fedha ziweze kulipwa na haya yote hayawezi kwenda kwa kutegemea *OC,* lazima tutenge bajeti maalum kwa ajili ya ku-*support* wakandarasi hawa ndani ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie suala la vifaa tiba nchini. Tunaiona Serikali inawekeza fedha nyingi kwenye suala la vifaa tiba nchini, lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, tumezunguka sehemu nyingi, tumekuta Mheshimiwa Rais amewekeza fedha nyingi kwenye sekta ya vifaa tiba nchini, lakini tumekwenda tumekuta Serikali inanunua mashine mpaka za shilingi 10,000,000,000, shilingi 15,000,000,000 mpaka shilingi 20,000,000,000. Mheshimiwa Rais anatoa fedha ananunua mashine hizi kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara sasa ije na mpango mkakati mzuri wa kuhakikisha tuna-*train* watu wetu hapa hapa kwa ajili ya kufanyia *service* mashine hizi na kuzitunza kwa ajili ziweze kudumu kwa muda mrefu kwa sababu lazima twende tukasimamie fedha ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uwekezaji wa viwanda nchini. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumchagua Katibu Mkuu ambaye ata-*deal* na suala la viwanda vya dawa nchini. Suala hili ni suala bora lakini ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri tunapokwenda kuanzisha viwanda hivi twende tukaruhusu ushindani wa masoko, tusije tukafungua tu viwanda vyetu tukafungia viwanda vya nje hatutokuwa tumewasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Wanaigalula tunataka tuone kwamba faida ya kuwekeza viwanda nchini ni kweli imewasaidia wananchi wetu. Bibi yangu kule Igalula, babu yangu kule Igalula apate dawa za sukari na presha bila kuuza jogoo wake, bila kuuza kuku wake, dawa hizi azipate bila shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa; wajiandae Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo na Mheshimiwa Eric James Shigongo.

MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Afya. Kipekee napenda kumshukuru sana Mungu aliyetujalia afya njema na tumeweza kufika hapa, ili kuweza kuchangia katika bajeti hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mohamed Mchengerwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Florence Samizi, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Afya kwa kazi njema wanayoifanya. Mungu awabariki sana maana ni kazi ya wito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninachukua nafasi hii pia, kumshukuru sana Mganga Mfawidhi wa Hospitali yetu ya Mkoa wa Kagera, Dkt. Museleta Nyakiroto na Katibu wa Hospitali yetu Bwana Faustin Pamba, Watumishi wote wa Wizara ya Afya, wa Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera na Watumishi wote katika Mkoa wetu wa Kagera ambao wana-*deal* na afya. Mungu awabariki sana kwa kazi njema wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi na mapinduzi makubwa sana aliyoyaleta katika Wizara hii ya Afya. Tulikokuwa, tulipo na tutakapokuwa kesho ni tofauti sana. Kwa hiyo, shukrani

za pekee zimfikie, lakini ziwafikie na watendaji kwa kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya ndiyo Wizara mama kwa kila jambo. Bila afya hatuwezi kufanya jambo lolote. Hata sisi hapa afya ikitetereka kesho hatuwezi kuwepo kwa hiyo, ni jukumu moja ambalo inabidi walibebe, ili waweze kuhakikisha afya ya Watanzania inatengemaa, kuwalinda na kuwakinga na magonjwa yote ambukizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamefanywa na Serikali, mengi sana. Wameongeza vifaatiba, wamejenga hospitali za rufaa na mkoa, wamefanya kila jambo, ni jambo jema sana. Kujenga na kufanya ni jambo lingine tofauti, ninawaomba sana Wizara, tuendelee kusimamia yale yote ambayo yako kwenye misingi, ili tuweze kuwatibu Watanzania magonjwa wanayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza sana kwenye ushauri. Kila Wizara ina kinga au kidhibiti baada ya kuwa imetengeneza kitu au imefanya jambo. Wizara ya Afya inabidi tuwe na kitengo cha kingatiba. Maana yangu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna magonjwa mengi tunayapata ambayo gharama ya kuyatibu ni kubwa sana, lakini unaweza ukakuta gharama ya kuyalinda, ili tusiyapate inaweza ikawa ndogo sana kuliko gharama ambayo mtu anatumia kutibiwa. Kwa hiyo, ni bora tunavyojenga hospitali zetu za rufaa au za mikoa, tuwe na kitengo cha kingatiba, ambako tuwe na wataalam wenye kushauri wananchi; wanafika pale kupima na kujua anasumbuliwa na nini au ana upungufu gani, ili apate kinga kabla ya kupata ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye barabara, wakijenga barabara ni lazima waweke mzani, mzani unaenda kulinda barabara kwa hiyo, tujitahidi sana kwenye Wizara yetu ya Afya tuwe na kitengo ambacho kitawahimiza wananchi kwenda kucheki afya zao kabla hawajaumwa. Hiki kitasaidia sana kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia gharama ya *dialysis* ni kubwa sana, gharama ya kutibu *cancer* ni kubwa sana. Je, tunaweza kufanyaje? Kwa sasa mtu anaweza akamshauri mtu, lakini huyo daktari atamshauri huyu kwamba, asile kitu na atamshauri na mwingine. Tuwe na kitengo mahususi cha kingatiba, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaishukuru sana Serikali kwa kuanzisha bima ya afya kwa wote. Hili jambo ni la kitume, hili jambo wameenda kuokoa maisha ya watu wengi sana, aliyeleta hili jambo na wazo hili Mungu ambariki sana. Wameanza na watu wa *TASAF,* lakini tuna wagonjwa ambao wanaumwa magonjwa wamelala nyumbani hawajiwezi na siyo *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wazee wetu ambao wamezeeka hawajiwezi na hawawezi kukidhi gharama ya matibabu na siyo *TASAF* kwa hiyo, katika awamu hii ya kwanza na hao watu ambao wana magonjwa sugu wamelazwa au wako majumbani mwao gharama hawaziwezi na wenyewe tungewafanyia takwimu tujue ni wangapi na Serikali inaweza ikawasaidiaje, hasa wazee. Wazee wengi SIYO *TASAF,* lakini unakuta uwezo wa kutafuta umepungua na gharama za matibabu hawezi kukidhi kwa hiyo, ninaomba sana katika hii awamu tuangalie na hiyo kwenye bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa ninajikita katika Mkoa wetu wa Kagera. Kwanza ninakushukuru sana Waziri, juzi wakati yuko Mwanza amesema neno moja ambalo limewafurahisha sana watu wa Kagera na Mungu ambariki kwa maono hayo. Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao uko pembezoni sana; kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, mgonjwa akiumwa, kutoka Murongo Kituo cha Afya Wilaya ya Kyerwa, kuja Bukoba Mjini kwenye hospitali ya rufaa ya mkoa ni kilomita 200. Akifika pale Bukoba akapewa rufaa kwenda Mwanza, ni kilomita 400, niambie, huyu mgonjwa atafika Mwanza au ataishia njiani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wazo alilolileta la kujenga Hospitali ya Mkoa ya Rufaa katika Mkoa wa Kagera ni jambo ambalo halipaswi kusubiri. Hospitali ya rufaa ya mkoa iliyopo sasa ilijengwa mwaka 1923, tunakuwa tunafanya marekebisho kwenye

ujenzi kihandisi. *Rehabilitation* ni gharama kubwa kuliko kujenga jengo jipya kwa sababu, Waziri atabomoa ukuta anahisi ni mbovu, atabomoa mwingine ataingia gharama kubwa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri hili jambo lisisubiri mwaka unaokuja, atafute hata pesa ya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo katika Mkoa wetu wa Kagera yapo. Tusaidie tupate hospitali bora ya mkoa ya rufaa, ambayo itakuwa inakidhi matakwa yote na iko *full equipped*. Mgonjwa akiumwa asipate rufaa kwenda kwingine kwa sababu, umbali ni mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukafanya utalii wa afya. Sisi tunapakana na Masaka, kutoka Masaka kwenda Kampala ni kilomita 200, lakini kutoka Masaka kuja Bukoba ni kama kilomita 180. Tunapakana na Rwanda, tunapakana na Burundi, zile wilaya za karibu na lile eneo wanaweza kuja kutibiwa katika hospitali yetu ya Mkoa wa Kagera na sisi tukaingiza pesa. Kwa hiyo, pale kuna fursa ya pesa. Mheshimiwa Waziri katika Hospitali yetu ya Rufaa kwa sasa, ya Bukoba Mjini, ninamwomba sana, tuna upungufu kidogo pale, pamoja na shughuli zote alizozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tuna upungufu wa wataalamu bingwa ambao ni wa muhimu na labda ndiyo inasababisha watu kupata rufaa kwenda mbali. Tuna wataalam bingwa wa radiolojia, wataalam wa jua, tusaidie tupate wataalam wa radiolojia, lakini tuna ukosefu wa wataalam bingwa wa afya ya kinywa na meno, ganzi na usingizi, lakini pia, tuna shida kubwa sana ya wataalam wa TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba wakati Waziri anamalizia hotuba yake, ajaribu kutuambia, kama mifumo haifanyi kazi mgonjwa atibiwe, halafu baadaye aingizwe kwenye mfumo kwa sababu, kwenye Hospitali yetu ya Rufaa, pale Bukoba Mjini, mifumo imekuwa changamoto, mtandao umekuwa changamoto kubwa sana. Kama kuna kifaa kinahitajika pale ajaribu kutusaidia, tuone tunaweza tukakipata vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata kifaa kimoja pale katika hospitali yetu, ambacho

ni mashine ya kutengeneza mazao yanayotokana na damu. Tusaidie tuweze kuipata katika hospitali yetu ya rufaa ya mkoa iweze kuwaokoa hao wananchi ambao wako pale. Mheshimiwa Waziri siku moja nimetembelea ile Hospitali yetu ya Rufaa ya Bukoba Mjini, nilisomewa risala, nilichokikuta pale na mimi kimenikuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa mfanyakazi wa muda kwa muda wa miaka 18, *contract terms*, ninajua machungu yake. Katika hospitali yetu na hospitali nyingine unaweza ukakuta tuna wafanyakazi wa *contract basis,* katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera wapo 52 na hospitali nyingine na nyingine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri, Afisa Utumishi wa Wizara ana mamlaka na uwezo wa kuomba kibali kwa Katibu Mkuu Kiongozi, hawa watu wapate ajira za kudumu kwa sababu, kazi wanayoifanya ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye ameajiriwa kwa mkataba wa miaka mitatu, leo ukienda kumpa *interview* na mwanafunzi aliyetoka shule, huyu wa miaka mitatu hawezi kutoboa hata siku moja, hawezi kushinda kwa sababu, huyu amekaa kwenye *experience wise* na huyu huku anaenda kufanya *theory*, atashindwa. Hili suala Waziri ajaribu kulichakata aone linaweza kufanyaje kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyosema ataleta tabasamu kwa watu, hiyo ni njia mojawapo ya kuwapa tabasamu watu kwa sababu, hawa watu wa mkataba wa muda kwanza hawana bima ya afya na pili, mafao yao yanakuwa ni madogo. Nimekuta pale hospitalini kwetu kuna madeni kidogo ya watumishi, ninaomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuyaangalia; kuna malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi pale, wanasema ni tangu mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Mheshimiwa Waziri hashindwi na jambo lolote. Yeye ni jembe na akiamua unaweza na Naibu Waziri wake, hebu ajaribu kuangalia, wanadai kama

shilingi bilioni 120 ambazo wakienda wakachakata na wakaona, inaweza ikasaidia katika kukidhi mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja na ninawaomba Wabunge tuipitishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamuita Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii Wizara ya Afya. Ninaona mambo mengi yamezungumzwa, lakini kuna vitu vya msingi sana tunavisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinasema mifumo isomane; ninafikiri, kama wanavyoratibu mfumo kusomana kwenye hospitali za Serikali, mfumo huo uende na kwenye *pharmacy* za watu binafsi au *pharmacy* za kampuni. Kwa nini ninasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anatibiwa kwenye hospitali kwa kutumia bima, daktari anamwandikia dawa, zile dawa hazipo pale! Akitoka nje na kabima kake anatakiwa aweke mfukoni, ampigie simu binamu yake amtumie hela aende kwenye *pharmacy* kununua dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni mifumo isomane hata kwenye kampuni mbili au tatu za dawa nchini, ili nikiandikiwa dawa nitumie ile risiti ya daktari ya kuniandikia dawa. Niende kwa kutumia ile risiti kwenye ile *pharmacy* niweze kupata dawa ninywe na kesho niendelee na maisha mengine. Siyo unatoka hospitali kwenda kutafuta dawa, inatakiwa umtafute binamu akutumie hela ndio ukanunue tena dawa. Hiyo siyo mifumo kusomana, hapo mifumo haisomani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili. Mimi nimesoma Sheria ya Kodi ya mwaka jana. Kodi imepunguzwa sana kwenye pombe ambazo hazina madhara kwenye mwili, lakini wameenda

kuongeza kodi kwenye pombe zenye madhara mwilini. Mimi katika akili yangu ambacho nilitarajia…

MHE. ASHA J. FERUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nilitarajia…

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Asha Feruzi.

TAARIFA

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumkumbusha mchangiaji anayechangia kwa sasa kwamba, sasa tunajadili Bajeti ya Wizara ya Afya na siyo habari ya vileo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya pili. Napenda kumkumbusha Mheshimiwa mchangiaji aliyepita kuwa, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha mifumo kusomana katika *Government Sector* na *Private Sector*. Ninaomba akarudie hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupokea kwa sababu, amedakia harakaharaka. Asubiri kwanza ajifunze. Asikilize maana yangu, hoja yangu inawalenga Wizara ya Afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada…

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inasema hivi, nisiki…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kwa mujibu wa Kanuni tunapaswa kuchangia Kibunge na unapopewa Taarifa, Kanuni

inakutaka ama ukubali au upokee na humu ndani ya Bunge tunaitana kwa majina kwa kuanza na *title* ya mtu, kwa maana ya Mheshimiwa, ndiyo unafuata jina lake.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa. Nimetumia sekunde 45, muda wangu ulindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili. Nimesoma Sheria ya Kodi ya mwaka jana, wameongeza kodi kwenye pombe ambazo hazina madhara, wamepunguza kodi kwenye pombe zenye madhara. Mfano *master*, konyagi na vilevi vingine. Katika tafsiri yangu maana yake ni nini?

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Getere. *(Makofi)*

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anachangia kwa jinsi anavyoona yeye, lakini kwa taratibu zetu za Kibunge, hatakiwi kusoma, natakiwa kuchangia kwa kuangalia pointi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ninaipokea kwa sababu, kuongea bila kusoma ndiyo nina *PhD* kwenye hilo eneo. Twende kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kwamba, aliyesema haviendani na Wizara ya Afya ni kwamba, magonjwa ya ini, figo, sukari na magonjwa mengine makubwa yanazidi kupamba moto kwa sababu, vijana wetu wengi wananunua hizi pombe za bei ndogo wanakunywa, hawali kwa sababu ya *stress* ya maisha. *Nilitarajia Serikali yenye akili ingeweka kodi kubwa kwenye pombe zenye madhara na siyo kuweka kodi ndogo kwenye pombe zenye madhara, inayompa access mtu wa*

kawaida kuchukua shilingi 500 kununua konyagi kwa sababu, V Master ni shilingi 500. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Profesa John Kabudi.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, URATIBU, NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina Kanuni, lina lugha na heshima yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni Serikali inayoheshimiwa. Namwomba mchangiaji afute maneno aliyoyasema ya Serikali yenye akili, kwa maana ya kwamba, Serikali hii haina akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshauri aweke *microphone* yake mbali kwa sababu, hata ikizimika bado anaweza kuongea. Kubwa afute *statement*, afute tamko lake la kuonesha kwamba, hii Serikali haina akili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, kwanza ninaomba uondoe haya maneno ambayo yameelekezwa hapa na *Chief Whip*, halafu uipokee Taarifa na uendelee kuchangia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu ya tatu ni, haya nikae mbali! Haya nakaa mbali sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja… *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, kwa mujibu wa kanuni unapaswa kufuata Maelekezo ya Kiti. *(Makofi)*

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* nyingine. Jambo…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada Mligo, nimekuelekeza ufute yale maneno uliyotamka, halafu upokee Taarifa iliyotolewa na *Chief Whip,* ndipo uendelee kuchangia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay,* nilikuwa sijakuelewa bosi wangu. Maneno niliyoongea na ninayokumbuka waliyosema nifute ni kwamba, *Serikali yenye akili na Serikali ambayo haina akili. Ninachokumbuka sijataja ni Serikali ipi kwa hiyo, wameniwahi tu sijataja, huenda ni ya Marekani au Kenya. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, tafadhali futa.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta kauli. Ninaendelea na hoja yangu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wamesema wanahitaji huduma bora kwa Watanzania. Wakati huohuo...

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sigrada, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Fadhili Liwaka.

TAARIFA

MHE. FADHILI A. LIWAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na nia yake njema, Mheshimiwa Sigrada na kuwa na moto wa kujenga hoja, Bunge hili na nchi hii inaendeshwa kwa Sera za Kidiplomasia. Hata kufananisha Nchi ya Marekani au Kenya kwa maneno aliyoambiwa afute na *Chief Whip*, bado ni

kulichonganisha Taifa letu na Mataifa mengine kwa hiyo, ninaomba Kiti chako, afute au aache kuchangia, kama itafaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fadhili Liwaka tumesikia maelezo yake na Mheshimiwa Sigrada kwa hayo yaliyoelezwa si vyema kutaja au kutoa mifano ya Serikali za nchi nyingine. Kwa hiyo, ninaomba pia, ufute haya maneno na uendelee kuchangia.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niendelee kuchangia, nimefuta. Nimefuta, nimefuta na nime...

MWENYEKITI: Mheshimiwa ninaomba ukae chini.

Waheshimiwa tunaendelea. Nilimtaja Mheshimiwa Eric Shigongo. *(Makofi)*

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mungu kwa kunipa nafasi na bahati ya kuwa ndani ya jengo hili ili niweze kutoa mchango katika ujenzi wa Taifa langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa yale mema ambayo yamefanyika katika Jimbo la Buchosa, tumejenga vituo vingi vya afya, zahanati za kutosha na vilevile tunaendelea kujenga mpaka hivi sasa. Tumepatiwa *ambulance* za kutosha ingawa bado ninaomba tupatiwe *ambulance* kwa ajili ya majini kuhudumia visiwa vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo bajeti ya afya, nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mchengerwa, Naibu Waziri, lakini Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu yangu Dkt. Seif Shekalaghe kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme ukweli na wala tusipindishe maneno, tumepiga hatua kubwa sana kama Taifa kwenye Sekta ya Afya na maneno haya yanayo ushahidi wa kutosha kabisa, huwa SIYOngei maneno bila ushahidi, ninataka niwape *data*

kuonesha ya kwamba Taifa letu limepiga hatua kubwa sana katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 tulipata uhuru wa Nchi yetu, Tanzania kwa mujibu wa ripoti niliyoisoma ya utafiti iliyofanywa na mtaalam wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inasema, mwaka 1961 tulikuwa na vituo vya afya 22, nchi nzima. Mwaka 1961 tulikuwa na *dispensary* 700, mwaka 1961 tulikuwa na Madaktari wa Kitanzania 13. Leo ninavyoongea miaka 65 baadaye, Tanzania tunazo *dispensary* 8,714, ninavyoongea tuna vituo vya afya kutoka 22 mpaka 1,361, ninavyoongea sasa kuna Madaktari 12,000 kutoka Madaktari 13 mpaka, kazi kubwa sana imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matokeo hayo ya kazi kubwa iliyofanyika umri wa kuishi wa Mtanzania umeongezeka. Mwaka 1961 Mtanzania aliishi kwa miaka 37 *life expectancy,* lakini *life expectancy* leo ni miaka 67. Jirani zetu wana miaka 66, jirani mwingine ambaye mimi siwezi kumtaja jina ana miaka 65. Umri wa kuishi umeongezeka, siyo ajali ni kutokana na huduma za afya kuwa bora. Ninaipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kazi nzuri iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1961 baada ya kupata uhuru Rais wetu wa kwanza, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alitangaza maadui watatu, adui wa kwanza ujinga, maradhi na umaskini, akamteua Waziri wa Afya wa kwanza, Waziri wa Afya wa kwanza Derek Bryceson ambaye kwa mara ya kwanza aliamua kufanya utafiti akimtumia mtafiti, *source of scientist* kutoka Uingereza aliyekuwa akiitwa *Richard Titmuss*, alifanya utafiti ule akaja na mambo matatu ambayo lazima niyaongelee. Kwamba ili Tanzania iwe Taifa lenye afya kwa wakati ule ilikuwa ni lazima tufanye mambo matatu:-

(a) Tuwekeze kwenye kinga *(preventive medicine)* lazima kuwekeza kwenye kinga;

(b) Kufundisha wataalam wa afya kwa sababu hatukuwa nao; na

(c) Kupanua miundombinu ya afya. Hayo yamefanyika, kwa miaka 65 nimekutajia tumepiga hatua kubwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarejea kwenye hoja yangu ya kinga. Sina matatizo na *cure*, sina matatizo na tiba, tiba ni sawa, lakini ninatamani tuwekeze zaidi kwenye kinga kuliko kuwekeza fedha nyingi kwenye *cure*. Ninaomba nirudie tena, ninaomba Taifa langu liwekeze sana kwenye kinga kuliko kuwekeza sana kwenye *curative medicine*. Huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga hata Waswahili wana msemo wao wanasema kinga ni bora kuliko tiba. Ninamwomba sana Waziri turudi nyuma, kilichofanyika mwaka 1961 kifanyike leo, tuweke fedha nyingi zaidi kwenye kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma bajeti yetu, nimeisoma bajeti vizuri sana, sijaona fedha za kutosha zimewekwa kwenye kinga, ndiyo maana ninamkumbusha Mheshimiwa Waziri na ninakuomba sana atakapokuja hapa atueleze kwamba amerekebisha kiasi gani ili aweke fedha ya kutosha kwenye kinga. Bila kinga Taifa hili haliwezi kuwa Taifa bora, tunahitaji kuwa na Taifa bora la watu waSIYOuguwa kila siku na hilo litawezekana kama tutaweka fedha nyingi kwenye kinga na pia kuongeza bajeti yetu ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Abuja lilisema bajeti ya afya ya nchi ya Afrika lazima iwe 15% ya bajeti yote ya nchi nzima. Sisi hatujafika 15%, ninaipongeza Serikali yangu angalau imefika asilimia saba. Ninaiomba Serikali iongeze bajeti ya afya ili kusudi tuweze kuhudumia watu wetu vizuri tusiweze kuwa na Taifa ambalo watu wake wanaumwa, Taifa gonjwa huwa na uchumi gonjwa. Ili nchi yetu iweze kwenda mbele kwa kasi, ni lazima tuwahudumie watu wetu waweze kuwa na afya iliyobora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee jambo langu la miaka yote, ninataka nizungumzie juu ya suala zima la homa ya ini. Tangu 2014 nipo kwenye mapambano dhidi ya homa ya ini, mnanijua kila nikisimama hapa ninaongelea habari ya homa ya

ini. Ninayo njia ya kuhakikisha ugonjwa huu unakuwa *eliminated* kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii niliyonayo hapa niwapongeze sana vijana wangu wa *THA* ambao tunapambana nao kwenye vita hii, wapo hapa ndani, tunapambana vita hii tangu 2014, lengo letu ugonjwa huu uondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe hesabu ndogo tu ili nchi yetu iweze kuwa na kinga ya jumla *herd immunity* tuchanje 90% ya watu wetu. Tunao watu 65,000,000, hivyo 90% yake ni 58,000,000. Mwaka 2002 mzee wetu Mkapa, Mungu amrehemu, aliamua kuwachanja watoto wetu kwenye nchi hii wanapofikisha wiki sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kwamba watoto wenye miaka 25 kurudi chini wote katika nchi hii wamechanjwa. Tafsiri yake ni nini? Watoto wenye umri wa miaka 25 kurudi chini katika nchi yetu ni 70%, ambapo 70% ya 58,000,000 ni 40,000,000. ukiiondoa 40,000,000 kwenye 58,000,000 unabakiza 18,000,000. Ina maana mzigo tulionao wa kuchanja katika nchi yetu ili uondoe ugonjwa huu ni 18,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisaidie, tumeshindwa kuchanja watu 18,000,000. Kama tumepata shilingi 200,000,000,000 za kutoa mikopo kwa vijana wetu tumeshindwa kuchanja watu 18,000,000 ili ugonjwa huu uishe? Inawezekana, jambo hili linawezekana kabisa kwa sababu kuwachanja watu 18,000,000 ni shilingi 72,000,000,000, kama hatuna hiyo pesa kuna taasisi inaitwa *GAVI* (*Global Alliance for Vaccination Initiatives)* ambao wanatoa fedha kwa nchi maskini kununua chanjo. Viongozi wangu huku wote wanaifahamu taasisi hiyo, kama *GAVI* hawana pesa ipo taasisi nyingine inaitwa *CDAF (Centre for Disease Analysis Foundation)* ambao wananunua chanjo kwa jumla kwa nchi maskini na kufanya chanjo iwe nusu bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanjo ukinunua moja kwa moja India bila kutumia madalali utaifikisha Tanzania kwa 1,350. Chanjo tatu ili chanjo ikamilike ni 4,030, hatuwezi kukosa 4,030 kuwachanja watu wetu. Kwa uchungu kabisa ninasema watu

wanakufa, ugonjwa unaenea, maambukizi yanaongezeka na tunaweza kuwachanja watu wetu wasiendelee kufa uwezo huo tunao. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ninamwamini kwenye Wizara zote alizopita amefanya kazi nzuri sana, zuia watu wetu kufa kwa homa ya ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho na la muhimu sana *Pentavalent* hiyo chanjo ya watoto inatolewa kwenye umri wa wiki sita. Mama ambaye ameambukizwa akizaa kutoka siku ya kwanza, mtoto anakuwa hana kinga mwilini mpaka wiki sita. Huu muda wa hizi wiki sita mtoto anaambukizwa, kwa mwaka mmoja tunatengeneza watoto wagonjwa 10,000. Hatuwezi kuendelea namna hiyo, Mheshimiwa Waziri, anisaidie, atakapokuja hapa ninaomba majibu ametenga kiasi gani kwa ajili ya *birth dose*. Ile chanjo anayopewa mtoto wakati wa kuzaliwa maana hatuchanji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine zote zinachanja, Ethiopia wameshamaliza ugonjwa huu, Egypt wamemaliza ugonjwa huu, sisi hatuchanji kwa nini? Hatuna fedha ya kutoa *birth dose*! Siamini, Waziri asipokuwa na majibu, Mheshimiwa Mchengerwa ni rafiki yangu sana, tunaelewana sana, shilingi moja itabaki hapa mpaka nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ninaunga mkono hoja, Mheshimiwa Mchengerwa chapa kazi, tupo pamoja, ninamwamini, hajawahi kuniangusha. Mungu ibariki Tanzania, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas; wajiandae Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera na Mheshimiwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya. Ninaomba kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya hasa katika kuboresha afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Afya tumesikia uwekezaji mkubwa ambao umefanywa katika Wizara yetu ya Afya hasa katika hospitali yetu ya Taifa, hospitali zetu za kanda, lakini vile vile *specialized hospitals*, hospitali za mikoa, wilaya lakini pia na katika vituo vya afya na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa udhati kabisa pamoja na timu yake kwa jinsi ambavyo wanafanya uongozi mzuri sana na wa kipekee kuleta maono makubwa ya kimkakati na ya mageuzi katika Wizara yetu ya Afya kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kupongeza watumishi wote wa sekta ya afya ambao wapo chini ya Wizara ya Afya, lakini pia TAMISEMI ambao wanatoa huduma nzuri sana katika hospitali zetu, katika zahanati zetu, katika hospitali zetu za Halmashauri, lakini pia na hospitali za Taifa na Kanda. Kazi wanayoifanya ni kubwa sana na ni nzuri na hasa tunasema ni kazi ya kujitolea lakini ina *risk* nyingi sana, kwa kweli wanafanya kujitolea pakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nipende kuchangia mambo machache, nitachangia katika eneo la hospitali ya Muhimbili, bima ya afya, lakini vile vile nitazungumzia viwanda ambavyo Mheshimiwa Waziri ameleta hoja hiyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hospitali yetu ya Taifa kwa kweli tunaomba tuendelee kuungana na Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia kwamba ni mradi wa muhimu sana na ni mradi wa pekee sana, ambao nchi yetu inauhitaji hasa katika kipindi hiki na hasa tukiwa tunaelekea katika uwekezaji au katika kuitekeleza Dira ya Maendeleo ya 2050, afya ni kitu cha msingi sana, hasa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Taifa ndiyo ambayo itakuwa inapokea wagonjwa ambao wameshindikana kutoka hospitali za Kanda na zile *specialized hospitals*. Tumeona

uwekezaji mkubwa ambao umefanyika, hasa huduma za kibingwa, bingwa bobezi, lakini vilevile na uwekezaji katika miundombinu na hata upande wa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Taifa imeanza tangu mwaka 1905 na imekuwa mpaka leo, lakini bado uwekezaji na maboresho ya miundombinu yaliyofanyika hayajawa makubwa kiasi cha kutosheleza mahitaji tuliyonayo sasa. Kwa hiyo ni wakati sahihi sasa kwa nchi yetu kuwekeza hospitali hii, kuijenga upya ili iweze kukidhi mahitaji ya watu milioni 65 tulionao leo na ambao wataongezeka baada ya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hospitali yetu inao uwezo wa kuhudumia Watanzania ambapo ina vitanda 1,500, lakini tunapoelekea tunataka tujenge hospitali ya vitanda 2,801. Kwa kanda yetu ya Afrika Mashariki, hospitali ambayo ni kubwa kwa sasa ni hospitali ya Kenyata ambayo ina vitanda 2,400, lakini ukienda hapo chini Hospitali ya Mulago ina vitanda 1,600. Kwa hiyo, tutakuwa tumezidiwa na Misri ambayo ina vitanda 3,200 na South Africa pekee. Kwa hiyo, sisi kwa ukanda huu tutakuwa tunaongeza, kwa hiyo ni mradi wa pekee na wa muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huu ni mradi muhimu sana na tuunge mkono kama Wabunge, uwekezaji huu ufanyike katika miaka mitano na tuweze kuona *icon* hii ya kuboresha huduma za afya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuone upandikizaji wa viungo ukiwa unafanyika katika majengo mazuri yenye vifaa na yenye wataalam na hapa ni hospitali ya Taifa. Tunataka tuone pia huduma bobezi kwa upande wa akina mama, huduma bobezi kwa upande wa watoto, huduma bobezi kwa upande wa magonjwa ya ndani, kwa ajili ya magonjwa ya upasuaji yaweze kuwa na miundombinu stahiki vilevile iwe na vifaa stahiki na hii tutakwenda kuipata katika Hospitali ya Muhimbili mpya ambayo inapendekezwa na Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Wizara kuiunga mkono ili pia pamoja na utoaji wa huduma hiyo, tuweze kupata

ithibati ya kutambulika kikanda, tutambulike kimataifa ili huduma yetu ile ya tiba utalii kwa maana *(medical tourism)* iweze kukua na tuweze kupata fedha za kigeni kupitia huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunatoa huduma, *medical tourism*, tunaamini kwamba tunakwenda kuokoa fedha za kigeni ambazo zilikuwa zinatumika kupeleka wagonjwa nje, zile fedha zitabaki ndani kufanya kazi nyingine. Kwa hiyo, tuendelee kuunga mkono mradi huu na tuwekeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pamoja na miundombinu mizuri ambayo tunaiwekeza hapa bila watumishi ambao wamefunzwa na ambao ni wabobezi hatuwezi kufikia lengo ambalo limelengwa la huduma bora za afya. Tunatoa huduma bobezi katika hospitali ya Taifa, hospitali za Kanda lakini tuna madaktari wetu bobezi, tuna wauguzi wetu bobezi wengi ambao bado muundo wa utumishi wa umma hauwatambui, wanalipwa kama mabingwa na wengine kama ni wauguzi wanalipwa kama wauguzi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wale mabingwa wetu watambuliwe kwenye muundo wa utumishi wa umma ili watiwe moyo lakini pia wapate stahiki zao kwa huduma nzuri za ubingwa wanazotoa kwa wagonjwa wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapowaacha kwa muda mrefu haki zao zinapotea, lakini pia wanavunjika moyo. Kwa hiyo tunaomba hili litazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pamoja na hiyo tuboreshe hospitali zetu za Kanda, tuboreshe pia hospitali zetu za mikoa, kwa maana ya kuhakikisha kwamba huduma za kibingwa katika hospitali za mikoa zipatikane kama zilivyotajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Hata kama kwa sasa hatujafikia tuendelee kuongeza wigo kwa kuwapeleka wataalam wengi kwenye mafunzo ili tuwe na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa hoja ya Bima ya Afya: hakika hii ni hoja muhimu sana, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuleta kama sehemu ya Ilani na tunaipongeza Wizara kwa kuanza utekelezaji, lakini mambo machache ambayo ningependa kuangaliza. Mheshimiwa Waziri, tunaomba tuangalie suala la *financing* ya Bima ya Afya kwa wote; shilingi 150,000, ni hatua ya kuanzia lakini bado Watanzania walio wengi si rahisi sana kupata shilingi 150,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Wizara na mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Afya tuna haja ya kuendelea kuangalia kwa undani namna ya kusaidia ugharamiaji wa Bima ya Afya kwa wote ili Watanzania walio wengi waweze kupata huduma hizi za bure kutokana na bima ya afya iliyo nzuri na ambayo ina *financing mechanism* iliyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba tunahitaji kupeleka Bima ya Afya, hii italeta kwenda kubadilisha *health-seeking behaviour* ya wananchi walio wengi kwa sababu kila mtu anaona yupo *insured*, wengi watakwenda kwenye vituo vya afya. Tumeona takwimu bado zahanati hazitoshelezi tunahitaji kujenga, lakini vilevile bado vituo vya afya ni vichache tunahitaji kuweka nguvu. Kwa hiyo, tunapokwenda ku-*promote* Bima ya Afya kwa wote lazima uwekezaji katika miundombinu uende sambamba ili kuhakiki kwamba tunaweza kupokea mzigo mkubwa ambao unakwenda kuletwa na Bima ya Afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa upande wa *MSD*. Mheshimiwa Waziri anajua *MSD* inafanya kazi nzuri sana, lakini bado mifumo ya *MSD* na vituo vya afya havisomani. Tunahitaji kuona *MSD* inapopeleka dawa katika vituo iwe ni zahanati, iwe ni hospitali ya Wilaya, iwe ni kwenye kituo cha afya, iwe ni hospitali ya mkoa, iwe inaona jinsi ambavyo dawa zinatembea na zinavyotoka ili kuhakikisha kwamba *stock* zetu zinakuwepo kwa wakati, lakini pia kuhakikisha msawazo wa madawa ili kuepusha *expire date* za madawa na kuondoa uharibifu wa madawa haya. Kwa hiyo ninaamini kwamba mifumo ikisomana itaweza kusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto moja katika vituo vyetu. Tuna ule mfumo wa kuwa na maduka ya dawa katika hospitali, nimwombe Mheshimiwa Waziri, hili jambo liwe *reviewed*, hatuwezi kuwa-*convince* wananchi wetu kwa kuwaambia hatuna dawa leo kwenye *pharmacy* ya hospitali, lakini pale mbele ya hospitali kwenye duka la hospitali kuna dawa. Kwa nini, mwananchi asiamini kwamba hizi dawa zimetolewa hapa zikawekwa kwenye *pharmacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mfumo uwe *reviewed* ili tuhakikishe kwamba tunapata mfumo mzuri ambao utahakikisha wananchi wanapata dawa wakati wote ndani ya *pharmacy* zile za hospitali na siyo kuwa na maduka mengine ndani ya hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa viwanda, tunajua mahitaji yetu zaidi ya 85% ya madawa, lakini vilevile na vifaa tunaagiza kutoka nje ya nchi. Hakika ni wakati sahihi wa kuwekeza viwanda vya utengenezaji wa madawa pamoja na vifaatiba hapa nchini. Niombe sana Mheshimiwa Waziri tuone namna ambavyo tunaweza tukasaidia pia uwekezaji katika uzalishaji wa malighafi za uzalishaji wa madawa, hiyo nayo iende sambamba ili tusiwe tunaagiza malighafi nyingi kutoka nje na bado tukawa tunapoteza fedha za kigeni nje. Tuanze kuwekeza uzalishaji wa malighafi, uende sambamba na mkakati wa utengenezaji wa viwanda hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tumealika wawekezaji kutoka nje, lakini niombe wawekezaji wa ndani pia wapewe fursa na wawekewe mazingira mazuri ya kuwavutia ili wawekeze katika eneo hili la utengenezaji wa madawa. Hili ni zuri kwetu kiuchumi, lakini pia kutengeneza ajira kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo ninaomba sana zipo sheria za kikodi, zipo sheria za uagizaji wa bidhaa mbalimbali ambazo zinahitaji kufanyiwa mapitio ili kuhakikisha kwamba tunapoanza uwekezaji huu wa viwanda, basi mazingira yawe rafiki kwa watu wanaokuja kuwekeza kuhakikisha kwamba wanafanya uzalishaji kwa gharama nafuu ili tupate dawa zilizo bora, lakini za bei nafuu na ambazo zinakidhi mahitaji yetu. Kwa

hiyo, ninaomba sana hilo la kuhakikisha kwamba mazingira ya kisheria na kikanuni nayo yamefanyiwa mapitio ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa sehemu ya mwisho. Tunajua ugonjwa wa homa ya ini ni ugonjwa ambao kwa kweli unaathiri Watanzania walio wengi, tuna asilimia kubwa sana. Ninaomba sana kama ambavyo Wabunge wameshauri, nimalizie kwa kuomba chanjo ya homa ya ini, bado ipo kidogo sana kwa watenda kazi wa sekta ya afya. Kwa hiyo, ninaomba uhamasishaji ufanyike, vilevile chanjo hii kwa watoto iweze kuzingatiwa na kupewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuwatambue wageni waliopo Bungeni jioni ya leo. Wapo wageni wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Waziri wa Afya, ambao ni wawekezaji kutoka China.

Wapo pia wadau wa sekta ya afya; yupo ndugu Cedou Mandingo, Babu wa Kitaa ambaye ni balozi wa saratani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ambaye ni Mheshimiwa Maarifa Mwasitete, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Mkoani Songwe. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Eric Shigongo kutoka kampuni ya *Tanzania Health Alliance* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ambao ni Taasisi ya Wanamaombi wanaoliombea Taifa kutoka mikoa mbalimbali Nchini Tanzania. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na uchangiaji; sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie. Kwanza kabisa kabla sijasahau na kwa sababu ya hotuba ya Waziri wa Afya ilikuwa ni nzuri zaidi, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, niseme; mfumo wa utoaji wa huduma za afya nchini kama tunavyojua kwa mujibu wa Sera ya mwaka 2007 ni *pyramid in nature*. Maana yake ni kwamba, huku chini kabisa tuna zahanati, vituo vya afya na hospitali zile za halmashauri, ambayo hiyo inasimamiwa utekelezaji wake na TAMISEMI. Halafu tuna hospitali za rufaa za mkoa, za kanda na zile za kitaifa ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Afya. Wizara ya Afya kwa pamoja na mambo mengine ndiyo inayoandaa sera na mwongozo, pia inasimamia hiyo asilimia kama ishirini katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimesema hivyo, uangalie jinsi ya utekelezaji wa hiyo *pyramid*, ndipo unakuja kuona kwamba tumekuwa tunasuasua huko nyuma; ukiangalia tangu Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani mwaka 2021, kuna uwekezaji mkubwa sana umefanyika kwa kila *level*. Ukiangalia kwenye afya ngazi ya msingi kuna zahanati nyingi zimejengwa, vituo vya afya vingi vimejengwa na hospitali za wilaya zimejengwa kama 77.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa ujumla ni hicho kipindi vituo vya kutoa huduma za afya kama 3,330 vimejengwa. Vifaa na vifaa tiba kwa ngazi zote kuanzia *digital X-rays, ultrasound* na *CT scan* hadi ngazi ya juu vyote tumeona kutoka kwenye hotuba ya Waziri na wote tunajua mpaka huko nyumbani mwa shahidi tumekuwa *equipped*. Maana yake ni kwamba sasa Watanzania wanapata huduma ambazo ni nzuri, zaidi na hii tunagawanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye ngazi ya juu kabisa ya kitaifa tunaona kwamba tumekuwa na Hospitali ya Muhimbili na

taasisi zake; taasisi zake nazo kuna uwekezaji mkubwa umefanyika, kama vile Mloganzila na kadhalika. Sasa, ili kutekeleza hiyo piramidi yote, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wizara ya Afya unaona wameamua sasa kwamba; tumewekeza sana huko chini, sasa twende kwenye utalii tiba; tuwekeze kwenye Hospitali ya Muhimbili Mpya ambayo itakuwa na vitanda vingi; itapunguza muda wa wagonjwa ambao wanapelekwa pale ku-*save life* kupata huduma kwa haraka zaidi na pia ninasikia itakuwa pia na mafunzo kwa wataalam namna ya kutumia vifaa vya kisasa ambavyo vitakuwa vimenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaunga mkono hiyo Hospitali ya Muhimbili Mpya ifanyike ili angalau kwa Nchi za Afrika Mashariki na Nchi za Kusini mwa Afrika tuwe nchi ya kwanza ambapo watu wanatoka huko baada ya kwenda India waje wakatibiwe hapa; kwa hiyo tunaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaunga mkono pia kwa sababu tumejenga vituo vya kutoa huduma ya afya vingi; na ili Watanzania wapate huduma vizuri, tunaunga mkono pia hoja ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema, ya kujenga viwanda vya dawa, vitendanishi pamoja na viwanda vya kutengeneza vifaa na vifaa tiba. Ninadhani nalo hilo ninaliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi tena, kwa sababu nilisema ni *pyramid;* ukiangalia pia vipaumbele vya Wizara ya Afya wamesema wanataka kuwekeza zaidi katika kinga ya kuzuia magonjwa ya kuambukiza, milipuko na magonjwa yasiyo ya kuambukiza; pia wamesema kuwa wanataka kupambana kuhamasisha uchangiaji wa utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye kinga; kama alivyosema Mheshimiwa Shigongo, lakini pia na sisi tunaangalia kwamba, hata *prevention is better than cure*. Tiba ni muhimu, hata Mheshimiwa Rais alipokuja hapa Bungeni; ukiangalia kwenye hotuba yake alisema; tunataka kuwekeza zaidi katika kinga ili kusudi kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na ustawi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kinga ukiangalia, njia ambayo ni nzuri kabisa ya kutumia kinga ni utoaji wa huduma ya afya ngazi ya msingi. Ambapo hapo; pamoja na kwamba tumejenga zahanati nyingi, tunatakiwa tuwekeze zaidi katika zahanati, vituo vya afya ambapo pale ndipo wanapotibiwa watu walio wengi. Kwa nini tunataka tufanye hivi; kwa sababu itakapofika mwaka 2030 tutapimwa ni kwa kiasi gani yale malengo endelevu tumeyafikia na *indicator* mojawapo ni kuangalia vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia baada ya kuwa amewekeza uwekezaji mkubwa sana kwenye sekta hii ya afya; mwaka 2015 vifo vya mama na mtoto vilikuwa ni 556 kwa vizazi hai 100,000; mwaka 2022 vikashuka kwa kasi kikubwa vikawa 104. Kwa hiyo tunastahili kuwapongeza. Mwaka 2030 tunataka kwenda chini ya vifo sabini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii sekta huku kwenye vifo inaonekana tuko vizuri; lakini tunapokuja kwenye vifo vya vichanga, siku sifuri hadi 28 hatujafanya vizuri sana. Mwaka 2015 tulikuwa na vifo 25 kwa vizazi hai 1,000; mwaka 2022 ilikuwa ni 24 kwa vizazi hai 1,000; tumepunguza kwa digiti moja. Ukiangalia tunatakiwa 2030 iwe 12 kwa 1,000. Ukija kwa upande wa vifo vya watoto chini ya miaka mitano mwaka 2015 ilikuwa 67 kwa 1,000, baadaye tukaja 43 kwa 1,000, tunatakiwa twende 25 kwa 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo *indicator* zote mbili, Watanzania walio wengi wanatibiwa kwenye afya ngazi ya msingi. Kwa hiyo, hapo inabidi pia tufanye kazi ya ziada kuhakikisha kwamba tunaboresha hii sekta kwa mwaka kesho na miaka mingine inayokuja kabla ya kufika 2030 ili kusudi Watanzania walio wengi waweze kutibiwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu anataka ile *universal coverage access,* afya kwa wote; baada ya kuruhusu hii Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Ili tuweze kufikia hiyo kwa sababu wanaotibiwa wengi ni maskini na tumetenga fedha nimeambiwa kwa zaidi ya shilingi 48,000,000,000 tayari Watanzania kutoka kwenye kaya maskini wananufaika na hii. Kwa hiyo tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ya Bima ya Afya inabidi iangaliwe kidogo, kwa sababu inaonekana inawabana inataka wawe ndugu tu wa damu. Hata hivyo kuna makundi mengine kama yale ya bodaboda, mama lishe; kama ikiwezekana basi nao waweze kupata fursa ya kuweza kunufaika na hii bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi inavyotumika pia, *NHIF* wanapokwenda kule kubainisha zile kaya; tusitumie sana tu *data* ya *TASAF*, tujaribu kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa karibu sana ili tuweze kuwabainisha watu ambao wanastahili kupata hii huduma. Kwa hiyo ningependa nichangie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeongeza vifaa vingi vya kisasa, *ultrasound, digital X-rays* na kadhalika imesababisha kuwa na upungufu wa watumishi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba watumishi waendelee kuajiriwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali hii; kwenye hotuba ya Waziri pia imesemwa kuwa wamejenga hospitali za rufaa za kanda, zile 10. Mkoa wa Mara tunayo hospitali yetu, ile ya kwangu, ambayo ni ya muda mrefu; tulikuwa tunaomba nayo kasi iongezeke ya kukamilisha majengo ambayo yanatakiwa yajengwe pale. Kwa mfano jengo la dharura *(EMD)* pale halipo tunaomba waongeze kasi ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nimesema kwamba ili tuweze kufanikiwa kufikia *indicator* hizo za *SDG 2030* pia tunatakiwa tuwe na *zero malaria*. Magonjwa kama haya *malaria*, magonjwa ya *diarrhoea*, haya yanatibika sana kwenye afya ngazi ya msingi ili tupunguze kasi ya kwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hapa Tanzania sekta ya afya hii inahudumiwa na Wizara mbili; ninadhani Mheshimiwa Waziri Mchengerwa anajua, wakati tulipokwenda TAMISEMI tulianza kufanya kazi naye na sasa amekwenda Wizara ya Afya; ili tuweze kufikia haya malengo vizuri, Watanzania walio wengi wanatibiwa kwenye afya ngazi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana hilo Mheshimiwa Mchengerwa aweke rekodi yake pia, hasa kwenye bajeti ya mwakani; kwa sababu kwenye bajeti hii tunaona kwamba imewekeza kidogo; na hata TAMISEMI walivyoleta huku ilikuwa ime-*focus* kwenye maboma. Ninadhani, ili tuweze kufikia malengo ya 2030 mwakani inabidi tuwekeze sana kwenye kukamilisha vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini ninasema hivyo; akina mama zaidi ya 80% wamejifungulia kwenye vituo vya afya; Tanzania walio wengi wanatibiwa ugonjwa nje ya *OPD* wanatibiwa kwenye *primary health care*. Kwa hiyo kuwekeza juu ni vizuri; lakini wao kama sekta ambayo inatoa mwelekeo tunashauri kwamba watusaidie zaidi mwakani na kuendelea ili sekta ya afya huku chini watu waweze kupata huduma. Hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninadhani nikija kwa upande wa Butiama; kwa mfano, nina kata 19, kata tisa bado hazina vituo vya afya. Tunaona, tukiongeza vituo vya afya kama ulivyosikia kwa Waheshimiwa Wabunge wengine itasaidia. Akina mama wengi wakijifungulia huku na wakifanya *scissor* kwenye vituo vya afya itapunguza itabaki kule hospitali za rufaa zitakuwa zina-*deal* na mambo ambayo ni *serious* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninadhani nirudie tu kusema kwamba uwekezaji uliofanyika na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye sekta ya afya ni wa mfano na anastahili kupongezwa. Tunaomba awekeze sasa kwenye hiyo Hospitali Mpya ya Muhimbili, vifaa tiba, wataalam, zaidi watumishi wengi waajiriwe kwenye ngazi ya msingi na wale *Community Health Care* waongezeke zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya; wajiandae Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila.

MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetukutanisha sote mahali hapa siku ya leo tukiwa na afya njema. Pia ninaomba niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa ndani ya sekta ya afya na kupelekea kuongeza bajeti ya sekta ya afya. Hii inaonesha jinsi gani Rais wetu anakwenda kutuongezea mchango na Serikali itaweza kuwa mchango chanya katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nitoe pongezi kwa Waziri wa Afya, kaka yangu Dkt. Mchengerwa. Pia ninaomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Florence Samizi na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya katika sekta ya afya. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa programu aliyoianzisha, ya 'Ongea na Waziri' ambapo unawafikia moja kwa moja wananchi na kutatua changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niendelee kwa kumshukuru. Nikiwa mwakilishi wa wanawake ninaomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake kubwa za kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga na kusababisha vifo hivyo kupungua kutoka vifo 556 katika vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 104 katika vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya watoto wachanga pia vimepungua kutoka vifo 24 katika vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo 19.5 katika vizazi hai 1,000. Kutokana na haya mapinduzi makubwa tunaona Mheshimiwa Rais pia amepewa tuzo ya The *Gate Foundation* ya Kimataifa; pia tumeona kupitia mkutano uliofanyika wa Wakuu wa Nchi wa Afrika, Addis Ababa Ethiopia mwezi Februari, Rais pia ametunukiwa kuwa kinara wa kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee tumeona sasa Mheshimiwa Rais amekuwa ni Rais wa kwanza duniani na Afrika nzima kwa

kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga. Kwa kusema hayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuheshimisha sana sisi wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijikite katika mchango wangu. Kwanza kabisa ninaomba nitambue, katika siku mia za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan baada ya kuingia madarakani kupitia sekta ya afya tumeweza kuona ajira 5,000 zilizotangazwa na watumishi wa afya wamekwenda kufika katika maeneo mbalimbali ya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza pia kuona mchakato wa bima ya afya kwa wote umeanza na kutoa shilingi 48,000,000,000, ambapo kwa nchi nzima tutakwenda kuwa na wanachama 1,400,000. Kipekee ninatoa shukrani kwa niaba ya Mkoa wa Rukwa, ambapo tumepata kunufaika 48,000, na mpaka sasa wamesajiliwa watu kwa 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niongeze kwa kusema tunatambua mchango huu mkubwa wa Serikali katika sekta ya afya. Hata hivyo nina ushauri wa kutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii tumeona; ushauri wangu mkubwa kwao Wizara ya Afya; tunaomba mchakato huu wa awamu ya kwanza uishe haraka, ambao ni kwa makundi yenye uhitaji. Vilevile baada ya kumaliza mchakato huo wa makundi ya kwanza tunaomba pia huduma ambazo zitakwenda kutolewa ziweze kuwa huduma bora kwa kuzingatia dawa kuwepo muda wote, kuzingatia wahudumu wa afya wawe na lugha ambazo ni rafiki na lugha nzuri kwa wananchi ili wakapate kuona faida ya kujiunga na bima hiyo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niendelee kutoa ushauri kwa Serikali kupitia mchakato wa bima ya afya. Zoezi la bima ya afya la makundi mengine nalo tunaomba liende kwa haraka. Makundi mengine yakiwemo wajasiriamali, wakulima, boda boda, mama lishe, wachimbaji na kadhalika. Kwa kuwa hadi sasa ni asilimia nane tu ya wananchi ndiyo wamejisajili katika Mfuko wa Bima ya Afya *(National Health Insurance Fund)*; hivyo tuna *gap* kubwa sana. Tunaomba Wizara sasa wafanye

kuhamasisha pia ili makundi mengine nayo yakajisajili katika utaratibu wa bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninaomba sasa nijikite katika ombi langu. Ombi langu kubwa; nimetumwa na Wanarukwa na nimetumwa na wanawake wa Mkoa wa Rukwa. Tuna changamoto kubwa ya hospitali ya rufaa. Hali inasababisha adha kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa kusafiri kwenda mikoa ya jirani kufuata huduma za kibingwa; na vilevile kuna changamoto zingine, tumepoteza na ndugu zetu kwa vifo kupitia kutokuwa na huduma hiyo ya madaktari bingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba zoezi hili lifanyike kwa haraka na kabla ya kufunga bajeti hii. Mheshimiwa Waziri atapohitimisha tunaomba; ili nikawape majibu Wanarukwa walionituma; kwamba atatupatia kiasi gani katika kuelekeza kwenye ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba vilevile tujue, ni lini fedha hizo zitaletwa Mkoa wa Rukwa ili kuanza mchakato huo. Kwa kuwa tunakumbuka mwaka jana bajeti ilipitishwa, lakini fedha hazikufika, shilingi bilioni 2.1. Ni imani yetu kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi na akiahidi anatimiza, chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaamini sasa fedha tutazipokea na Wanarukwa tutatembea kifua mbele na kujinyanyua katika ustawi wa afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kipekee ninaomba nihitimishe kwa kumwomba pia Mheshimiwa Waziri, kupitia huduma ya *dialysis*; kwa kuwa tunaona ugonjwa wa figo umekuwa ni ugonjwa ambao sasa hivi ni hatarishi sana kwa Watanzania pia na kwa Wanarukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba, jambo hili ni kama *emergency*; tunaomba aangalie katika bajeti hiyo ya trilioni 1.8 namna gani atatusaidia ili wana Rukwa sasa wakapate huduma ya *dialysis* ya kusafisha figo na kuepusha vifo visivyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia miamoja, nikitambua kwamba utu wa Mtanzania pia unajengwa kwa ustawi wa afya iliyo bora. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mungu, mwingi wa upendo kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kujadili Hotuba ya Wizara ya Afya. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, bingwa mama mpenda maisha ya Watanzania aliyeboresha maisha ya Watanzania kuanzia ngazi ya msingi hadi ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri wa Afya, Naibu Waziri, timu yote ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na kwa hotuba njema kabisa ambayo sasa inagusa maisha ya Watanzania hasa upande wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite kwenye mchango wangu. Kimsingi iko hoja muhimu sana ambayo imeletwa hapa na Wizara. Hoja msingi ni ujenzi wa Muhimbili mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Taifa letu tumepiga hatua kubwa sana kwenye upande wa afya na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa *champion* kwa kupunguza kifo cha mama na mtoto. Hii inaonesha dhahiri kabisa kwamba, yapo mataifa yatahitaji kuja kujifunza kwetu. Tunapozungumza Tanzania, Wabunge wote tukubaliane kwamba, pamoja na miji mingine kukua, lakini Jiji la Dar es Salaam ndiyo jicho la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na hali hiyo kwa huduma za kiafya, Muhimbili ndipo eneo pekee ambapo mataifa yote yanatupima kwa maana ya kuboresha huduma za afya. Niungane kabisa na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kwamba, tunayo sababu kubwa ya kuijenga Muhimbili mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa vizuri, gharama ya ujenzi na kwa namna ambavyo Muhimbili inavyohudumia wagonjwa, lakini bado tunao wataalam wetu wengi pale, tumeoneshwa zaidi ya watumishi 4,000 lakini ukiitafuta Muhimbili ukiwa Dar es Salaam unapata shida. Leo tunakwenda kujenga Muhimbili ambayo ndiyo itakuwa jicho katika nchi yetu na mataifa mengine ambapo tutapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wabunge wenzangu kwamba jambo hili tulipitishe kwa moyo mmoja na kwa msingi ule ule kwamba sisi tunapimwa na mataifa mengine, tumefanikiwaje kuonesha kwamba Watanzania tunawahudumia kwa kuboresha afya zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na michango hiyo ambayo imeainishwa hapa na namna ambavyo Watanzania tulikuwa tunapoteza fedha, zaidi shilingi bilioni 96.8 tulikuwa tunazipoteza kwa maana ya wagonjwa wetu kwenda nje, lakini tukijenga Muhimbili mpya tumeelezwa tutaziokoa hizo fedha shilingi bilioni 96.8. Hali kadhalika kwa msingi huo kwamba Muhimbili mpya itakapojengwa itatusaidia kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu sasa wanaendelea kupata huduma katika maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu ninataka kuyaleta hapa. Pamoja na kazi nzuri zilizofanywa za kibingwa na za ubingwa bobezi, tunayo changamoto kubwa kwenye *issue* ya *dialysis* (watu wanaohudumiwa kwenye damu upande wa figo). Gharama bado ni kubwa, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba tupime kwanza wagonjwa wanaougua pengine wanafanyiwa kusafishwa damu zaidi ya mara tatu kwa wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa hawa wanakuwa hawana uwezo wa kuzalisha, kwa hiyo wanabaki na wanaowahudumia wategemezi. Kwa hiyo, tuone namna gani Wizara inaweza ikaangalia namna ya kuweza kupunguza gharama hizi na pengine Serikali kuchukua sehemu ili kupunguza mzigo ambao ni mkubwa, wananchi hawawezi kuukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambazo zinaendelea na ambazo tumekubaliana, ninataka nizungumzie pia kwenye *level* ya hospitali zetu za kanda na za mikoa. Kimsingi ninatoka Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora ni miongoni mwa mikoa mikubwa hapa nchini, lakini ni miongoni mwa mikoa mikubwa yenye historia katika nchi hii. Mkoa wa Tabora wameeleza wenzangu, tunayo hospitali ya mkoa, lakini zipo baadhi ya huduma za kibingwa hazipatikani Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi nimwombe Waziri na watendaji wa Wizara, Mkoa wa Tabora kulingana na historia yake tuwaombe sana, wafikirie na sisi Mkoa wa Tabora kuwa na hospitali ya kanda ambayo tunaamini tutawasaidia wenzetu wengine wa kutoka Shinyanga, kutoka Mpanda na wengine wa kutoka Mbeya. Kwa hiyo, eneo la Mkoa wa Tabora ni muhimu sana kulifikiria kupata hiyo hospitali ya kanda ili itengeneze heshima ya Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ambayo nimeleta ombi, naomba pia nijikite kwenye *issue* ya bima ya afya. Niwaombe ndugu zangu Wabunge pamoja na Watanzania wote. Lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha sasa kila mwananchi anaweza kupata huduma bila kupata vikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya kwa Wote itatusaidia kila mwananchi kuhakikisha kwamba anapata huduma mahali ambapo anahitaji. Wapo wananchi wetu wengi kulingana na uchumi wao ulivyo mgumu inafika mahali wanashindwa kuendelea na huduma za matibabu kwa maana ya ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba sana ndugu zangu wataalam, kwanza kama tulivyoelezwa na Waziri kwamba mifumo yote isomane kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya pamoja na sekta binafsi, ili tutakapoanza kutekeleza jambo hili tusije tukawa na vikwazo, wananchi wakafika mahali wakaanza kulalamika, niwaombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania wote na wananchi wa Ulyankulu tum-*support* Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye suala la bima ya afya ambayo ukiiangalia ina gharama ndogo. Shilingi 150,000 kwa kaya watu sita ni sawa na shilingi 25,000 kwa mwaka ambayo ni fedha ndogo sana. Hayo ndiyo yalikuwa maoni. *Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yalikuwa maoni. Nisikose kuwasemea wananchi walionileta hapa. Jimbo la Ulyankulu ni miongoni pia mwa majimbo ambayo bado yana jiografia ngumu; jiografia ngumu ya barabara, lakini jiografia ngumu kwa maana ya huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ulyankulu ili upate hospitali ya wilaya kwa pande zote mbili, upande mwingine ukitaka kwenda Kahama ni zaidi ya kilometa 130, kwenda Makao Makuu ya Wilaya ni zaidi ya kilometa 170 na kwenda mkoani ni zaidi ya kilometa 140. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuiomba Wizara na kaka yangu Profesa Shemdoe yupo hapa; tuangalie kituo kimoja cha afya, tukiboreshe kiwe na hadhi ya kuweza kutoa huduma kwa *level* ya Hospitali ya Wilaya katika Jimbo la Ulyankulu, ili kuondoa umbali wa kusafirisha hawa akina mama na hasa wajawazito ili kuweza kuokoa maisha yao. Ninamwomba sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niendelee kuiomba Serikali na Wizara kwamba kwenye maeneo haya tumejenga vituo vyetu vya afya. Niwaombe sana tuangalie yale majengo muhimu. Kwa mfano, majengo ya mionzi ni heri yakapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba majengo haya yanaimarishwa kwa maana ya kupata huduma bora kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la akina mama. Mchangiaji mmoja nimshukuru alieleza kwamba, akina mama ni kiwanda ambacho kinatutengeneza sisi wote tuliopo hapa. Ni vizuri majengo ya kujifungulia yawekwe kwenye hadhi ya heshima, ili wale akina mama wanavyokwenda kujifungua, wajifungulie maeneo yenye heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi nimalizie kwa kusisitiza suala la msindikizaji wa mjamzito. Hili jambo niombe Wizara ilipe kipaumbele na ilipe kipaumbele kuonesha kwamba akina mama wajawazito wanavyokwenda kujifungua waweze kupata mtu wa kusindikiza, ili kum-*handle* kuhakikisha kwamba hili zoezi analifanya kwa wema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu akubariki sana na ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba yupo safarini kwa shughuli za kikazi, hivyo katika kipindi ambacho hatakuwepo Bungeni, amemteua Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kukaimu shughuli za Serikali hapa Bungeni hadi atakaporejea. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, nilimtaja Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, ajiandae Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii nzuri, niweze kuchangia katika Wizara yetu hii, Wizara ya Afya ambayo ina mambo mengi mazuri ya kuweza kujivunia kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya ziara kwenye taasisi mbalimbali za Serikali yetu ya Tanzania. Tumeenda kwenye hospitali mbalimbali na kiukweli mimi ni mmoja wa mashuhuda wa mambo mazuri ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia na timu yake ya Wizara ya Afya chini ya Mheshimiwa Mchengerwa kwa mambo mazuri waliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ile tumeona vifaa vya kisasa, tumeona majengo mapya mazuri mengi yanaendelea kujengwa, lakini pia tumejionea mipango mizuri ya taasisi zetu katika namna ya kuendelea kujiboresha na kuwa imara sana. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuendelea kumpongeza kaka Mchengerwa, Mheshimiwa Waziri wetu; Naibu Waziri na Katibu

Mkuu wetu Dkt. Shekalaghe na timu yake nzima kwamba kazi wanayoifanya. Sisi kama Wajumbe wa Kamati tunaifurahia na kwa kweli tumeendelea kupata imani kubwa sana juu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usipoumwa huwezi kujua ni nini kinatendeka katika hospitali zetu. Usipopata fursa ya kwenda kufanya ziara kama sisi Wabunge tulivyokwenda, huwezi kujua kuona Serikali inafanya vitu gani vikubwa. Binafsi nilibaki kustaajabu, ila nikafurahi moyoni mwangu kwamba Serikali yangu inafanya vizuri katika suala la afya. Kwa hiyo, hili nimeona leo kwa ujasiri kabisa niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, nimpongeze Waziri na timu yake nzima, kwamba kwa kweli ziara ile tuliifurahia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni hii ya leo nitapenda kuchangia kwenye baadhi ya mambo, kwa maana ya kuboresha katika utendaji wa Wizara yangu. Pia, kuna maombi maalum kwa Mheshimiwa Mchengerwa kwa kuangalia Wizara inafanya kitu gani, kuweza kuboresha baadhi ya maeneo. Moja, nitaanza na *TFNC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TFNC* tunakumbuka ni moja kati ya taasisi ambazo zilikuwa zimeorodheshwa kufutwa, lakini ukweli ni kwamba *TFNC* ipo inafanya kazi zake na kiukweli ipo katika *stress* tu ya kwamba ni kama imefutwa lakini kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongelea *TFNC* ni (Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania). Ndiyo taasisi pekee ambayo inafuatilia masuala yote ya hali ya lishe katika nchi yetu. Sasa nilikuwa nawaza tu, wanaona shida gani Serikali yetu kuirejeshea hadhi yake *TFNC*, ili ipate morali nzuri ya kuendelea kupambana na hali ya lishe ya Watanzania? Kwa hiyo, hili tumwombe Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wetu mpendwa, kaka yetu, aende akaangalie namna ya kurudisha hadhi ya *TFNC* ili iwe na amani katika utekelezaji wake wa kazi za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ninatamani niendelee kuomba pia, unajua kufanya makosa kupo kwenye maisha hatukatai. Kama lilifanyika kosa la kuondoa *TFDA* na

kuweka *TMDA* na kupeleka kipengele cha chakula *TBS* siyo dhambi kurudisha. Unajua kuna tofauti kubwa kati ya kudhibiti na kuthibitisha. Sasa *TBS* tunajua ni watu wa kuthibitisha, halafu *TFDA* ilikuwa ni udhibiti. Sasa ilikuwaje mpaka udhibiti wa chakula ukapelekwa *TBS*? Sielewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku tunavyoendelea kufanya kazi na Wizara yetu na namna tunavyoona mambo yanakwenda, tumeona ipo haja ya kurudisha *TFDA* na kuondoa *TMDA*. Kile kipengele cha chakula ni muhimu nacho pia kikawa na udhibiti. Tumeona hali ya lishe ya Watanzania jinsi ambavyo imekuwa ikiendelea kuchezewa na wadau mbalimbali ambao hawalitakii Taifa letu nia njema katika afya zetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula ndicho kitu ambacho kama kitapewa kipaumbele, tutapunguza matumizi ya dawa kwa asilimia kubwa, kwa sababu chakula ndicho kitakachotupa kinga, lakini kitatusaidia pia hata hali zetu za lishe kuwa vizuri. Mtu vitambi vitapungua na nini, lakini *under* udhibiti. Siyo kwamba vitu vinaingia tu bila ya kuwa *controlled*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa atusaidie wanapokuwa na *cabinet* yao huko waweze kushauri *TMDA* iongezewe kipengele cha *food* ili iwe *TFDA* kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine na ninashukuru Wizara ya Afya ndiyo waliokuwa wamenipa ahadi ya kwamba ndani ya miezi sita katika bajeti ya mwaka juzi kwamba, sera ya chakula itakuwa *updated* yaani itaboreshwa au itatengenezwa kwa uzuri kwa upya. Niwaombe Mheshimiwa Waziri wangu Mchengerwa, sera ya chakula ni muhimu kwa Taifa letu kwa sababu sasa hivi mambo mengi yanakwenda katika sera ambazo zinakubalika kimataifa. Sasa kama sera tuliyonayo ya chakula ni ya mwaka 1992, leo ni lini? Kwa hiyo, hili ninaomba walichukue kwa uzito wakalifanyie kazi. Sisi wataalam wa lishe tunaona ni jambo la msingi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nitataka nikiongelee, ninataka niende *direct* kwenye Hospitali ya

Kibong'oto. Hospitali ya Kibong'oto inafanya kazi kubwa kwenye matibabu ya *TB*. Mheshimiwa Waziri asione tabu kuiongezea hadhi na kuifanya iwe taasisi. Ikiwa taasisi itakuwa na vigezo vizuri zaidi vya kuweza kuwahudumia Watanzania vizuri zaidi katika kipengele cha *TB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia takwimu ambazo ziko hapa, bado *TB* nalo ni tatizo. Kwa hiyo, watusaidie waipe hadhi ile Hospitali ya Kibong'oto, waipe hadhi ya taasisi ili iweze kutoka ilipo kwenda hatua kubwa zaidi. Tulitembelea majengo yalikuwa ni mabaya, hayana mvuto, lakini ninaamini itakapokuwa taasisi na wenyewe jicho lao litakuwa karibu pale ili kuweza kuiboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nitataka kuongelea ni suala la *MOI*. Tulifanya ziara *MOI*, tukaenda Jakaya, tukaenda na Muhimbili. Kuna vifaa tiba vingine ambavyo *MOI* wanashindwa kupata vifaa tiba vingine kutoka *MSD*. Sasa hapa nimwombe Waziri, *MOI, MSD* na zile Taasisi kama ya Moyo, waangalie ni vifaa gani maalum ambavyo vinawapa changamoto ya uagizaji *MSD*, ili watengeneze utaratibu ulio mzuri zaidi wa kuweza kupata hivyo vifaa. Kama *MSD* hawawezi kununua basi wawape nafasi hawa wawe na utaratibu wao mzuri wa kuweza kuvinunua vifaa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kupongeza suala la bima ya afya. Lengo la bima ya afya ni kila Mtanzania atumie bima ya afya, lakini madirisha yetu ya kupokea *cash* bado yapo wazi. Tunaonaje kwamba mgonjwa akija awe *registered* kwa ajili ya bima ya afya, ili tuweze kufikia malengo kama Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo mgonjwa anakuja anahudumiwa kwa shilingi 50,000 halafu akija tena ahudumiwe kwa shilingi 50,000? Kwa nini wasimrekodi waangalie namna ya kumshawishi aweze kulipa hiyo shilingi 150,000 ili waweze kufikia malengo, kuliko wachukue shilingi 50,000, halafu mmwambie tena akatafute shilingi 150,000 tena arudi kujisajili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani waangalie namna nzuri ya kukaa na wagonjwa wanavyokuja hospitalini na

kuangalia namna ya kuwasajili kwenye bima ya afya kuanzia hospitalini. Hii itatusaidia kama Watanzania kuondoa hiyo *double standards,* wengine wanakuja na *cash*, wengine wanakuja na hiyo bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kumalizia niwaombe Wakurugenzi wote, *incharge* wote ambao wanashindwa kufikia makusanyo ya malengo, waunde timu maalum ya kwenda kujua nini kinawakwamisha wasiweze kufikia malengo ya ukusanyaji wa fedha. Haiwezekani malengo wanajipangia wao, wao wao wanashindwa kufikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anashindwa kufikisha hata 50% au 60%, huyo mtu anakuwa kweli ana uwezo mzuri wa kusimamia hiyo taasisi? Wasiwaonee aibu, kama mtu hafanyi vizuri, wamwondoe.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele, wajiandae Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko na Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka.

MHE. DICKSON N. LUTEVELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya. Kwanza kabisa ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana sana Mheshimiwa Rais wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na *Comrade* Mchengerwa, Waziri wa Wizara hii ya Afya kwa kazi nzuri na njema sana ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona jitihada ambazo zimewekwa katika kuhakikisha kwamba, miundombinu ya afya lakini afya za Watanzania zinaendelea kulindwa kwa kuhakikisha kuwa tunakuwa na dawa, tunakuwa na miundombinu rafiki kwenye hospitali zetu pamoja na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi nzuri, tumeona pia ongezeko la vituo vya huduma za afya, lakini pia tumeona ajira zikitolewa kwa watumishi wa kada ya afya. Pia, tumeona namna ambavyo maeneo mbalimbali huduma na vifaa tiba vikipelekwa kwa wingi sana. Katika hili tunaipongeza Serikali, lakini pia tunaipongeza Wizara chini ya *Field Marshal Comrade* Mchengerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo ambazo nimezitoa naomba pia nitoe mawazo yangu machache kwenye eneo hili. Tumekuwa na mafanikio makubwa, lakini yapo maeneo ambayo bado yanahitaji maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Mafinga ni halmashauri inayokuwa kwa kasi, ni eneo ambalo liko barabarani, eneo ambalo unapokwenda Zambia na unapokwenda Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini magari yote yanayotoka Dar es Salaam yanapita kwenye eneo hilo. Hivyo basi katika eneo hilo kunatokea ajali nyingi sana, pia kwa sababu kuna shughuli nyingi sana za uchumi ikiwemo shughuli za uvunaji wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga yenyewe kwenye bajeti, inapewa bajeti ya hospitali ya halmashauri ya mji, lakini kimsingi hospitali hii inahudumia zaidi ya mikoa miwili, yaani wapo wagonjwa wanaotoka Mkoa wa Morogoro, wapo wagonjwa wanaotoka Mkoa wa Mbeya, lakini pia wako wagonjwa wanaotoka mikoa mingine wakiwa wanapita. Sasa basi ukiacha hao tu wanaopita njia hospitali hii pia inahudumia wilaya nzima na hii inatokana na namna ambavyo huduma zinavyotolewa kwenye hospitali ya wilaya ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri wangu kwamba huduma ziboreshwe kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ikiwemo watumishi na kuboresha miundombinu. Hospitali ile ipate usajili kwenye mtandao ili ipunguze mzigo kwa hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga, kwa sababu sasa hivi unakuta hospitali inaelemewa kwa sababu bajeti yake ni ndogo, mzigo unaobeba ni mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo eneo lingine ambalo pia ninaomba nitoe ushauri ni pamoja na upatikanaji wa dawa. Bado wananchi wengi wanakumbana na tatizo la upatikanaji wa dawa hasa kwenye maeneo ya hospitali, zahanati pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri Wizara pamoja na kazi nzuri inayofanyika tuangalie namna ya kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana kwenye zahanati pamoja na vituo vya afya kwenye maeneo yetu ili kupunguza msongamano kwenye hospitali hizi zilizoko katika ngazi ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara iongeze bajeti ya *MSD* kwa ajili ya upatikanaji wa dawa mijini na vijijini. Wizara pia, ihakikishe mfumo wa kidijiti, watu wanaelimishwa sana kuhusu mfumo wa kidijiti ili kuepusha upotevu wa dawa. Kwa sababu katika maeneo mengi, ukisoma kwenye *data* inaonekana upatikanaji wa dawa ni 90% *and above*. Ukienda kwenye uhalisia unakuta dawa zile hazipo. Kwa hiyo, ninashauri Serikali kupitia Wizara hii ya Afya mfumo wa kidijiti uimarishwe mpaka kwenye ngazi zile za chini ili kuhakiki na ku-*manage* upatikanaji wa dawa kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishauri Wizara kuhakikisha kuwa kila kituo cha afya kinapata vifaa tiba vya kutosha. Tumejenga vituo vya afya vingi na vinafanya vizuri na watu wameamini, lakini tatizo kubwa ni vifaa tiba. Maeneo mengi vifaa tiba SIYO vya kutosha. Kwa hiyo, ninaomba niishauri Wizara ihakikishe inaboresha, inaongeza upatikanaji wa vifaa tiba hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Bima ya Afya kwa Watu Wote. Ninaomba niipongeze Serikali, ninaipongeza Serikali kwa sababu imeonesha dhamira njema ya kuhakikisha kuwa wananchi wote wanahudumiwa kutoka kwenye bima hii ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iongeze kampeni ya elimu ya bima ya afya kwa wote hasa kwenye maeneo ya vijijini. Wananchi wengi

hawana elimu ya kutosha kuhusu bima ya afya kwa wote. Tunaipongeza Wizara katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri wamesoma taarifa na *data* za namna ambavyo watu wamefikiwa. Ukiangalia idadi ya Watanzania na namna ambavyo watu wamefikiwa unaona kabisa kwamba mpango huu bado unahitaji jitihada za kutosha kuwapa wananchi elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichangie kuhusu punguzo la gharama za bima hii ya afya. Ninaomba sana niishauri Wizara, pamoja na nia njema ya Serikali, shilingi 150,000 bado ni hela nyingi sana kwa Watanzania wetu hasa walioko vijijini, kwa hiyo, ninaomba Wizara iangalie jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Wizara ihakikishe kuwa vituo vya afya vitakavyotumia hizi kadi za bima basi vinakuwa na dawa za kutosha pamoja na wataalam wa kutosha watoa huduma. Kwa sababu imeonekana katika maeneo mengi watu walioitikia kwenye huduma hii ya afya wanapokwenda kule wanakuta watumishi ni wachache. Kwa hiyo, ninaishauri Wizara kama ikiwezekana waombe kibali cha kuongeza watumishi wengine kwa sababu baada ya huduma hii ya bima ya afya kwa wote watu wataitikia sana kwenda kupata matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo ninaomba niseme kwamba Serikali pia iongeze kwenye maeneo mengi. Kwa mfano, kwenye hospitali yetu sisi ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga hivi ninavyoongea hatuna *ambulance* hasa kwenye hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, unakuta *ambulance* tunayotumia ni *ambulance* zinazotoka kwenye vituo vya afya, lakini pale hospitali ya wilaya hamna. Kwa hiyo, unaona ni mfano ambao pamoja na mpango mzuri lazima tuhakikishe vifaa hivi vinapatikana bila mkwamo kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine ninaomba niipongeze sana Serikali kwa kutoa vibali vya ajira kwa wataalam wa afya 5000. Jambo hili ni jambo zuri sana limefanyika hivi karibuni, tunampongeza Mheshimiwa Rais. Pamoja na hayo katika halmashauri yetu bado tuna upungufu wa madaktari, tuna upungufu wa wauguzi lakini pia tuna upungufu wa wataalam wa afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Adonis Alfred, ajiandae Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka.

MHE. ADONIS A. BITEGEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kukushukuru kwa kuupa nafasi kwenda kuchangia siku ya leo. Pia nianze kwa kupongeza jitihadi za Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kusema ukweli amefanya kazi kubwa sana kwa kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Afya. Kwanza kuwekeza zaidi kuona kwamba tunapata huduma bora za afya, lakini pia kuona kwamba huduma hizi bora zinafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia uongozi wa Wizara ya Afya chini ya Mheshimiwa Mchengerwa na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na timu yake nzima. Hakika tumeona na dhamira ya dhati kuleta mageuzi katika Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mazuri mengi yamefanyika, lakini kutokana na muda nitasema machache na hasa kwa kuzungumzia Wilaya yetu ya Muleba ambayo mimi ni mwakilishi wao kupitia Jimbo la Muleba Kaskazini. Katika Jimbo la Muleba Kaskazini tumeona kwamba tangu ameingia Uongozi wa Awamu ya Sita, kuna ongezeko kubwa la vituo vya kutolea huduma za afya sasa hivi vimefikia 45 kutoka vituo 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kuona kwamba chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeweza kupata hospitali ya wilaya kwa mara ya kwanza na ujenzi huo unaelekea kukamilika, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumetiwa imani pamoja na kauli ya karibuni ya Waziri wa Afya kwamba Hospitali ya Mkoa

wa Kagera itafanyiwa ukarabati mkubwa. Itajengwa pia hospitali ya magonjwa ya mlipuko katika Mkoa wa Kagera. Tunashukuru sana kwa Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kusema ukweli wananchi wa Mkoa wa Kagera tunashukuru sana na tuna matarajio makubwa sana kwa Serikali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na Huduma za UKIMWI, kwa hiyo nitazungumza machache sana sitapenda kurudia waliyosema wenzangu. Nianze kwanza kukugusia kwamba umuhimu wa kuwa na kupitia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ili kuona kwamba inaendana na mabadiliko ya kiuchumi, ya kijamii na teknolojia hasa kwenye sayansi ya matibabu ya magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba ile Sera ya mwaka 2007 licha kuwa ni nzuri, lakini pia inahitaji kufanyia maboresho zaidi ili kuendana na Dira ya Mwaka 2050. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba Sera hii ikafanyiwa mapitio, lakini pia pamoja na kuwa na sheria ya afya ni muhimu sana kwamba hii tukawa na Sera pamoja na Sheria ya Afya ili kuendana mabadiliko ya kiteknolojia katika tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba sasa hivi tuna huduma mbalimbali za kibobezi kama za upandikizaji wa viungo. Ninaamini kabisa tukiwa na sera na sheria ambazo zinaendana na mahitaji ya dira mpya ya maendeleo, lakini pia pamoja na maendeleo katika tiba itasaidia sana katika kutoa uongozi mzuri wa mwelekeo wa matibabu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuchangia na kuipongeza Serikali ni suala la uwekezaji ambao Serikali inaufanya katika kujenga mazingira bora ya ujenzi wa viwanda vya dawa. Ninaipongeza za Serikali tangu ameingia Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, nimeona jitihada kubwa sana ambazo zinafanyika kuona kwamba zinavutia uwekezaji katika sekta ya uzalishaji wa dawa. Kuundwa kwa ile *task force* ni jitihada kubwa sana, ninaipongeza sasa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kabisa kwamba tuendelee kujipanga zaidi kuona kwamba tunakuja na *package*

nzuri au vivutio vizuri zaidi ambavyo ni shindani kuweza kuvutia zaidi wawekezaji hapa nchini. Hili ni suala la msingi sana kwamba tunapojipanga zaidi tuone kwamba tunaweka mazingira bora zaidi na ya kishindani ili wawekezaji kutoka nje wakija Tanzania, wapende kuwekeza Tanzania zaidi ya nchi nyingine pengine za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda sana kulisisitiza hapa ni kwamba, wakati tunapigania na kuweka mazingira mazuri na kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda lakini tupambane kuona kwamba tunajenga uwezo wa *local content*. Yaani wale wawekezaji wadogo tuwawezeshe kuona kwamba wanafikia pia vigezo vya kuweza kujenga viwanda katika maeneo ambayo yametengwa ili nao pengine hapo baadaye waweze kukua na kuwa wazalishaji wakubwa wa dawa na vifaa tiba. Nami ninaamini kabisa nchi kama Misri, Bangladesh, India zilifanikiwa kwa kuweka mikakati madhubuti. Tunaweza pia tukajifunza kwao kujua nini walifanya wakafikia hatua kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulichangia limesemwa hapa ni suala la umuhimu wa kujenga mfumo wa kiuongozi wa Idara za *Pharmacy*. Sote tunajua kwamba kwenye Sekta ya Afya mchango mkubwa sana ambao ukifanyika na hasa hata kwenye bajeti ni wa ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna haja pia ya kuona kwamba kwenye ngazi za kimaamuzi, ngazi za Wizara tunakuwa na idara au kurugenzi kamili ambayo itaweza kuwajibika katika kusimamia masuala ya ugavi pamoja na usalama wa dawa na vifaa tiba. Ninajua suala hili limekuwa likizungumzwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri tena Serikali iliangalie na kuona namna gani inaweza ikatoa kipaumbele kwenye ngazi ya Wizara, lakini pamoja na kwenye ngazi za hospitali ngazi ya za kanda, hospitali maalum na za rufaa kuona kwamba kwenye *management* za hizo hospitali, basi Wafamasia wanapewa nafasi za kiuongozi ili kuweza kujumuika katika kuboresha huduma za afya pamoja na ugavi wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la, limesemwa hapa suala la miundo ya kiutumishi ninaamini hili suala ni suala mtambuka. Kwenye upande wa udaktari ninajua hapa kwamba, mfumo wa kiutumishi umetambua uwepo wa madaktari bingwa. Pia kuna haja kuangalia kuona kwamba wale madaktari ambao wanaenda kubobea, madaktari bobezi, basi muundo utambue na kutoa motisha husika kwenye ngazi ya mishahara na motisha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wafamasia, ukiangalia muundo wa Wafamasia na hata Wauguzi umeangalia sana katika uzoefu wa Mfamasia muda aliofanya kazi Serikalini katika kupanda vyeo. Kwa hiyo, ni muda muafaka sasa hivi, wale Wafamasia ambao wanaenda kubobea katika maeneo bingwa zaidi, basi wakapewa nafasi zaidi ya kutambulika katika miundo ya kiutumishi. Vilevile, kwenye upande wa Wauguzi basi miundo itambue uwepo wa ubobezi katika maeneo mbalimbali kama ya matibabu ya kansa, *ICU* na kadhalika ili waweze nao pia kutambulika na katika miundo ya kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wenzangu kuunga mkono ujenzi wa Muhimbili mpya. Hili ni suala la msingi sana kwamba tunahitaji kuwa na hospitali kubwa na yenye kukidhi vigezo vya kimataifa ambayo itasaidia sana katika kutoa wa huduma bora zaidi. Ninaamini kwamba uwepo wa huduma za kibobezi, za kibingwa pamoja na vifaa bora zaidi, pamoja na teknolojia mpya za matibabu zitafaa zaidi kuwepo katika maeneo ambayo yana miundominu ambayo itaweza kutosheleza uwepo wa hizo huduma. Kwa hiyo, ninaunga mkono kabisa kuwepo kwa mimi ujenzi wa Muhimbili mpya ili kuweza kubadilisha huduma zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la kuzungumzia ni suala la bima ya afya kwa wote. Ninaunga mkono jitihada za Serikali ambazo zinafanyika mpaka sasa hivi, tunaenda vizuri zaidi. Hata hivyo, ushauri wangu ni kwamba, tunapokwenda mbele zaidi tujaribu kuangalia zaidi. Ninajua kwenye usajili tunatumia kanzidata ya *TASAF* pamoja na utaratibu wa *NHIF*, tuangalie kuona kwamba kuna kaya nyingine maskini pengine haziko katika

makundi haya pengine ya *TASAF* au *NHIF* tuone namna gani tutazijumuisha katika bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la msingi ni kwamba ukiangalia machapisho mbalimbali kuhusiana na bima ya afya kwa wote katika nchi za Afrika. Mojawapo ya changamoto kubwa sana imekuwa ni kwamba ni rasilimali fedha. Kwa hiyo, tunapokwenda mbele zaidi katika awamu ya pili, basi tujipange zaidi kuona kwamba tunaongeza pengine ukusanyaji wa kodi zaidi tuweze kumudu kwenda kukizi gharama za za bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi ni kwamba, tuangalie namna gani tunaweza tukakusanya kodi zaidi katika maeneo mengine kama ya vileo ili kuboresha zaidi makusanyo na kuweza kuchangia katika bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani niyaseme hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka na Mheshimiwa Asha Salum Motto, ajiandae.

MHE. ASHA R. BARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa ninampongeza Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake kubwa sana kuhakikisha kwamba Wizara hii ya Afya inakuwa bora na inakuwa na vitu vya kisasa, vifaa vya kisasa na kadhalika. Nikisema vifaa vya kisasa, ninasema vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara hii chini ya Waziri Mheshimiwa Mchengerwa, pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Florence kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii kuhakikisha wanapata hospitali za kisasa na majengo yanakuwa ya kisasa, ambayo yameboreshwa na wamepata vifaa tiba kwa ajili ya Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanzia kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Dar es Salaam, Jimbo la kaka yangu wa Mheshimiwa Abbas Tarimba. Pale zamani kulikuwa na kiwanja kimoja ambacho ni karibuni na viwanja vya *leaders* ambacho *Shishi Food* alikuwa ameweka pale jengo lake la mgahawa, lakini siku aliyovunjiwa alilia sana kwa uchungu kwa nini amevunjiwa ile sehemu. Sasa hivi huyo *Shishi Food* akienda kuangalia lile eneo alilovunjiwa, maana yake siku hiyo alisema nimevunjiwa eneo hili na lile eneo lilikuwa *open space* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pamejengwa kituo cha afya. Kituo cha afya kikubwa sana, ambacho kina sehemu ya kujifungulia akina mama, imeboreshwa na vifaa vya kisasa na nikisema vifaa vya kisasa, vifaa tiba vyote viko pale. Ni hospitali moja kubwa sana, utafikiri ni hospitali ya mkoa kumbe kile ni kituo cha afya tu. Kwa hiyo kwa hilo niipongeze Wizara kwa kazi moja kubwa sana ambayo wameifanya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachia hapohapo kuna hospitali nyingine, watu wengine hawawezi wakafahamu iko Magomeni Makuti. Kuna kituo cha afya nacho kimejengwa kikubwa sana cha kisasa, kwa hiyo, ninaipongeza Wizara hiyo. Hapo hapo ninaipongeza Wizara ya Afya kwa kuboresha hospitali hizi kubwa za Mkoa wa Dar es Salaam; Mwananyamala, Magomeni, Temeke, pamoja na Ilala Amana, zimekuwa ni hospitali kubwa, huduma zote za kijamii zinapatikana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea hospitali ambayo ipo Mloganzila. Hospitali ya Mloganzila ni hospitali ya rufaa kama ilivyokuwa Muhimbili, lakini ina vifaa vya kisasa utafikiri uko India *Apollo Hospital* pale. Ni hospitali kubwa na ni safi na inatoa huduma zote pale hiyo Mloganzila. Kwa hiyo, ninaipongeza sana wizara na ninampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia, kwa kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma za afya na bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kupongeza na hii ninaweza kusema ni bima ya jamii kwa watu wote. Bima kwa watu wote tunaita kama *slogan,* bima kwa Watanzania wote bima ya afya. Huu mpango ukikamilika kwa Watanzania wote

tutakuwa tumepunguziwa makali na afya zetu zitaendelea kuwa bora, tutaendelea kuijenga Tanzania tukiwa na afya zetu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kujengwa Muhimbili ya kisasa. Ninataka kuongelea pia upanuzi au ninaunga mkono hoja kujengwa Muhimbili ya kisasa. Nitaizungumzia Hospitali ya *MOI* na kwa nini ninakubali kwamba ijengwe Muhimbili mpya, Muhimbili ya kisasa na kwa nini ninaunga hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya *MOI* ni hospitali ambayo inapokea wagonjwa wengi sana. Wagonjwa wanaopata ajali: kuna ajali za bodaboda, kuna ajali za bajaji, kuna ajali za mabasi pale na wagonjwa wengine ambao wanaumia au wanapata *injuries* za miguu, mikono na kadhalika. Ningeomba hata kama Mkurugenzi wa *MOI* ananisikia hapa, ajaribu kuomba pale *MOI* chini kuanzia *reception,* au vyumba vya madaktari vingeboreshwa jamani, vyumba vya madaktari wa *MOI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa unapoingia kwa Madaktari Bingwa, ambao wanaunganisha miguu yetu, mimi ni mwathirika pia wa miguu. Ukiangalia pale watu wanapelekwa na *wheelchair,* unakuta *wheelchair* nyingine siyo rafiki, unakuta wamejazana pale kwenye korido, njia ya kupita hakuna. Yaani mpaka umwambie mtu mwenye *wheelchair* sogeza hapa na mimi nipite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi binafsi nimeona niunge hoja, Muhimbili ipanuliwe, iwe kubwa. Hasa ukiangalia Hospitali ya *MOI* kule nyuma, unaweza kuona na ni Kinondoni, kuna jangwa pale. Tunasema linaenda lile jangwa mpaka Kinondoni Mkwajuni, kuna nafasi kubwa sana pale. Kwa hiyo, Hospitali ya *MOI* ipanuliwe iwe kubwa, tuwekewe vifaa rafiki, wananchi pale watibiwe kwa raha bila msongamano na afya zetu zirudi kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaokwenda na *antenna*, wakati mwingine utakuta unapishana na vitanda vya watu wana majeraha makubwa makubwa. Kwa hiyo, tukipata korido

ambazo ni kubwa za kuweka vitanda, huku ukingoja kwenda kumwona Daktari Bingwa, inakuwa inatupa unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mimi kwa leo niishie hapo, niombe tu muda wangu naona umekwisha. Nilikuwa nina mengi ya kuongea, lakini niunge mkono hoja ya Hospitali ya Muhimbili ijengwe mpya ambayo itaweza kuleta hata wagonjwa kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Salum Motto, ajiandae Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Ninaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua sekta ya afya kuwa ni sehemu muhimu sana, katika maendeleo ya kiuchumi pamoja na ya kijamii. Tumeona Serikali hii imeendelea kuwekeza kwa kiwango kikubwa sana katika miundombinu, katika rasilimali watu, katika vifaa tiba, lakini katika kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu, kuna ujenzi unaotaka kuanzishwa sasa hivi, ujenzi wa Muhimbili. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara, tunaunga mkono kwa juhudi hizi za ujenzi huu wa Muhimbili. Maana kwanza utaleta wageni wengi Tanzania, lakini Tanzania pia tunaenda kuongeza ajira kwa vijana, lakini hata kiwango cha uchumi kitapanda pia, kupitia hiyo hospitali itakayoenda kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Sita ni awamu ya matumaini na matokeo yanayoonekana. Manufaa yanayotokana na uwekezaji unaofanywa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi Mkoa wa Mtwara pia ni wanufaika namba moja.

Mpaka sasa tuna jumla ya zahanati 283, tuna vituo vya afya 49, tuna hospitali 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mkoa wa Mtwara tuna kata 191, ukiangalia zahanati ziko 283, ni dhahiri kwamba karibu kila kata tuna *almost* zahanati mbili na kuna kata nyingine zina *almost* kama zahanati tatu. Kwa hiyo, ametuinua wanawake wa Mkoa wa Mtwara hata wananchi wote kwa ujumla, hatupati shida tena ya kuhangaika kutumia sana miti shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi hospitali 12, tumebahatika pia kuwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Ligula, lakini pia tumebahatika kuwa na hospitali ya kanda ya rufaa, ya Kanda ya Kusini Mtwara. Kwetu sisi Mtwara ni faraja kubwa sana na tunajivunia kuwa na hospitali hii ya kanda, kwa sababu ingeweza kuwekwa kwenye mkoa mwingine, lakini imekuja kuwekwa Mkoa wetu wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tunamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutuvisha nguo kwa ujenzi huu wa wa kutupatia rufaa ya Kanda ya Kusini katika Mkoa wetu wa Mtwara. Mtanzania wa Mtwara sasa hivi, ana thamani sawa na Mtanzania wa Dar es Salaam. Hospitali za kanda ni usawa wa kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika uwekezaji huo, ninaomba nitoe changamoto tulizonazo Mkoa wa Mtwara. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Ligula ina upungufu wa watumishi (Madaktari Bingwa), kwa sasa hospitali hii ina madaktari watano tu na kwa mujibu wa ikama, hospitali ya wilaya au mkoa inapaswa kuwa na madaktari 30. Kwa hiyo, ukiangalia hapa tuna 17% ya uwepo wa madaktari, 83% ni kwamba tuna ukosefu wa madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hili lipo ndani ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri na ninatanguliza shukurani zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara. Ninajua baada ya kumaliza zoezi hili Mheshimiwa Waziri, nina imani atatupelekea madaktari katika Hospitali ya Ligula. Ahsante kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ligula pia tuna mradi wa jengo la *OPD,* lenye ramani ya ghorofa. Mradi huu ulianza tangu 2022, lakini haujakamilika mpaka sasa. Ninaomba ambapo kwa kuanzia ni kwa gharama za shilingi bilioni tatu na zilishatoka kwa ujenzi wa awali. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, aseme neno moja tu wananchi wa Mkoa wa Mtwara na wao wapate tabasamu, ni lini mradi huu utaenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ligula pia tuna mradi wa jengo la matibabu kwa watoto wachanga *(NICU),* ofisi za wafanyakazi, vyumba vya wafanyakazi, pamoja na sehemu za kubadilishia nguo watumishi mle ndani. Jengo hili lina thamani ya shilingi 538,000,000, ambapo ujenzi wake ulianza toka 2024. Ujenzi ulitarajiwa kumalizika 2025 mwezi Agosti, lakini mpaka sasa ujenzi huu bado haujamalizika. Mheshimiwa Waziri, ninajua liko ndani ya uwezo wake, ninaomba atoe neno ili wananchi wa Mkoa wa Mtwara na wao waweze kuona faraja yao, juu ya ujenzi huu wa jengo la watoto *NICU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hospitali pia ya rufaa ya kanda, kwa maana ya Kanda ya Kusini. Hospitali hii pia, ina ukosefu wa Madaktari Bingwa na Bingwa Bobezi katika vitengo vifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kitengo cha meno, hatuna Daktari Bingwa kwa ajili ya meno. Pia, tuna Kitengo cha hematolojia, Kitengo hiki ni kwa ajili ya magonjwa ya damu, hatujapata pia daktari bingwa. Pia kuna kitengo cha ekolojia, ambapo kuna wataalam wa kansa. Kansa ni changamoto kubwa, Mkoa wa Mtwara na sisi tayari maabara ipo, lakini hakuna wataalam, kwa hiyo daktari wanahitajika wa kufanya hiyo *urology* pamoja na patholojia. Patholojia ni wataalam wa kupima *tissue* zinazotokana na kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia wataalam ambao wameenda masomoni, wana changamoto ya kupata ile *Samia scholarship*. Mheshimiwa Waziri hili nalo pia liko kwenye mikono yako, nina imani utaenda kutusaidia, wataalam hawa na wao waweze kupata udhamini wa *Samia Scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kwa masikitiko, changamoto pia tunayo katika hii hospitali ya rufaa, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025, Bajeti ya Wizara ya Afya ilikuwa shilingi 1,700,000,000,000. Katika bajeti ile kulikuwa na bajeti kama ya shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufaa, kwa maana jengo la mama, *laundry* pamoja na nyumba za watumishi. Mpaka sasa ninapoongea hatujapata hata shilingi 100 kwenye mradi huu. Mheshimiwa Waziri, baba yangu msikivu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. ASHA S. MOTTO: …ninaomba Waziri atoe neno kuhusiana na kiasi hiki cha pesa. Ni lini Serikali itapeleka hizi hela, na ukizingatia muda uliobaki ni mchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, nitachangia kwa maandishi, kwa sababu nilikuwa na *agenda* nyingine ya tiba asili. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano; wajiandae Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa fursa hii ya muda huu, lakini kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amejalia uwepo wetu hapa tukijadiliana Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo zito jambo ya la afya ya mwanadamu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Afya, kumpongeza Waziri wa Afya na Naibu wake, lakini na wale watendaji wa afya Tanzania nzima ambao ndiyo wanahakikisha afya ya Mtanzania inadumu siku zote. Alipata kusema msemaji mmoja, anasema: "*Discipline is choosing between what you want now and what you want most.*" Nidhamu nzuri ni kuchagua kile unachopenda sasa, lakini kile unachopenda zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema mwingine: "*Future belongs to those who believe in the beauty of their dreams.*" Ubaadaye mzuri uko kwa wale wanaoamini ubora wa zile ndoto zao. Kwa sababu ya weledi mzuri wa watendaji wazuri, lakini wanaomsaidia Waziri wa Afya na Naibu wake, yaliyoongelewa kwenye hotuba yanatupa matumaini makubwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Wizara ya Afya kwa mabadiliko makubwa ya sekta ya afya kule Bumbuli. Tuna vijiji 83, lakini tunazo zahanati 34, hali ya hapo nyuma ilikuwa ya ajabu kidogo, lakini pia tuna vituo vinne vya afya. Sasa katika ombi langu, kabla sijachangia maeneo machache, vituo hivi vinne kulingana na jiografia, vinahitaji kuboreshwa kwa sababu, vingine vingi bado huduma haijakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matarajio makubwa kwa malengo tuliyoyapata katika wasilisho la leo, basi ninaamini tunaenda kupata matarajio makubwa. Kuna Kituo cha Afya cha Mgwashi, Kituo cha Afya cha Tamota, Soni na Milingano, lakini cha Milingano bado ujenzi haujakamilika. Sasa kwa kuwa sekta hizi mbili zinashirikiana na TAMISEMI, ninadhani zitafanya maboresho makubwa ili kuongeza tabasamu kwa wananchi walioko kule Bumbuli pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jambo moja katika sekta hii. Tuanzishe ile *National Digital Health Records*, jambo hili limekuwa likisumbua sana, kwa sababu vituo vya afya kule pembeni ni vichache na jiografia haijakaa vizuri. Kungekuwa kuna muunganiko mzuri wa mfumo wa Kitaifa kuanzia zahanati, kituo cha afya, wilayani, zile za rufaa za mkoa mpaka Taifa. Ili mtu anapotoka Dodoma, kama *CT scan* amefanyiwa Dodoma, basi akifanyiwa rufaa kwenda Muhimbili, Daktari wa Muhimbili azipate hizi kwenye mfumo mmoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasisitiza haya? Hii itapunguza gharama kwa Mtanzania wa kawaida. Pia, itapunguza msongamano katika maabara zetu, lakini pia itapunguza muda wa mgonjwa na kuongeza usahihi wa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimejitahidi nchi nyingine jirani zetu kufanya mifumo hii. Ingawa nyingine ni ndogo sana, kama Rwanda huwezi kuilinganisha sana, kulingana na upana wa Tanzania. Ziko zingine, Kenya imejitahidi kidogo, lakini haya yaliyoelezwa kwa Tanzania yanaonesha yataleta maboresho makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine pia ambacho ningeshauri, angalau kuwe kuna *feedback,* mfumo wa tathmini wa huduma kwa wananchi, kwa wale ambao wanatibiwa. Angalau ukifika pale hata simu tu ziwe zinatosha kuweka miadi na daktari, hata simu ya kawaida. Kuna wakati watu tunawahi Muhimbili pale kuanzia saa moja unatumia masaa sita, lakini kwa sababu leo tunaenda katika Tanzania ya mapinduzi ya kidijitali, hili linawezekana likaboreshwa vizuri na likaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tena kwa yale tuliyoyasikia mazuri ya kubadilisha, ya kupanua Hospitali yetu ya Rufaa ya Kitaifa ya Muhimbili. Tunajua ipo Mloganzila, lakini ipo Muhimbili. Sasa tungetarajia, kuwe kuna *specialized towers* kwa pale Muhimbili, kuwe na *tower* ya saratani, kuwe na *tower* ya moyo, kuwe kuna *tower* ya mambo mengine. Huduma nyingine zisogezwe kule Mloganzila, ili kuondoa msongamano na kurahisisha huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziwepo pia hospitali za kikanda: Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kati. Kuna wakati unafikiria mtu aliyepo kule Mtwara, kwa mtani wangu Mheshimiwa Dkt. Nawanda, aanze kuja mpaka Muhimbili, kwa kweli inakuwa haijakaa vizuri, lakini kwa kutumia mifumo ya kidijitali, *telemedicine* bado kuna mambo makubwa yanaweza yakafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwa ulimwengu huu wa kidijitali, zikiunganishwa zahanati, zikiunganishwa na vituo vya afya na hospitali za rufaa, kuna tiba kubwa sana, kuna tija kubwa sana inaweza ikapatikana. Nikimwangalia ndugu yangu Mchengerwa na timu yake, wana nia nzuri ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanaenda kufurahia huduma ya afya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. RAMADHANI H. SINGANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilimtaja Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa na mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara ya Afya. Nianze na Hospitali ya Wilaya ya Gairo. Mheshimiwa Waziri, hii hospitali ya Wilaya ya Gairo, wakati Mheshimiwa Rais alipokuja kuifungua hospitali ya Wilaya ya Gairo, alipata zile changamoto pale kwamba, ile hospitali inatumika eneo kubwa kwa watu wa Kongwa, watu wa Kilindi na watu wa Kiteto - Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa maagizo ziongezwe idadi ya dawa zitakazokwenda kwenye ile hospitali ya wilaya, kwa sababu wanachoangalia wanaangalia idadi ya watu waliopo Wilaya ya Gairo, lakini hawawaangalii wale ambao wako nje ya Wilaya ya Gairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, alisema kwamba pale paletwe *ambulance,* kwa sababu ile *ambulance* inayotumika hospitali ya wilaya, inatumika sana kwa ajili ya watu wa barabarani, kwa sababu pale Gairo ni katikati ya Morogoro na Dodoma. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri ashughulikie pale. Ile hospitali wakati Mheshimiwa Waziri, akiwa TAMISEMI alituletea *DMO,* lazima niseme kwamba, ametuletea *DMO* mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, imekuwa ni mshindi wa kwanza katika kutoa huduma Tanzania nzima, katika hospitali za halmashauri. Gairo ndiyo ya kwanza, kwa hiyo, lazima nimsifu

DMO pamoja na watumishi wote wa Hospitali ya Wilaya ya Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni Hospitali yetu ya Mkoa wa Morogoro, ambayo sasa tunaita Hospitali ya Rufaa. Kwa kweli, hawatutendei haki Wizara ya Afya. Kulikuwa na ile *CSR* ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, tuliambiwa tutafute eneo tutajengewa hospitali ya rufaa, tukaenda tukapata eneo zaidi ya eka 100. Sasa hivi hakuna chochote, hatujui kinachoendelea kitu gani kuhusu Hospitali ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ikumbuke hospitali ya Mkoa wa Morogoro, mkoa ule ni mkubwa katika Tanzania nzima. Hata idadi ya watu na wilaya zake ziko mbali, kwa mfano kama Mlimba, mtu atoke Mlimba kwa ndugu yangu hapa Rwakatare, mpaka afike pale ni kilometa zaidi ya 300. Mtu afike Malinyi kwa dada Mecktridis pale, zaidi ya kilometa 200 na kitu. Atoke kwa Zuberi huko, atoke Gairo, atoke Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kile kihospitali cha mkoa, vijengo vya zamani, hata wagonjwa wengine wakiingia pale kwa mashaka tu, mara ukuta unataka kubomoka. Muda mwingine wanakufa kwa mashaka, siyo tena kwa ajili ya ugonjwa. Tulikuwa tunaomba sana, ndugu yangu Mheshimiwa Mchengerwa atusaidie sana. Hospitali ya Mkoa wa Morogoro tupate hospitali ya rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshika leo shilingi ya Waziri, lakini kwa sababu yeye ni mgeni acha niache, lakini tunaomba sana Hospitali ya Mkoa wa Morogoro tupate hospitali ya rufaa. Kiwanja tunacho, kila kitu kipo, siyo pale, eneo lile liko katikati ya mji, ukienda pale mpaka aibu, watu wanalala mpaka barabara ile ya kwenda Morogoro hoteli, watu wanalala pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine, kuna hospitali moja ya kwa ndugu yangu hapa, huyu wa Ifakara, Mheshimiwa Asenga. Pamoja na kuwa ile ni Hospitali ya Kanisa *St. Francis*, lakini inasaidia sana yale maeneo ya Mahenge, hata huku Gairo, Malinyi, Mlimba, isaidiwe na Serikali. Wale sasa hivi hawana uwezo, hata juzi tumeenda na Asenga pale tumechangachanga,

tumetoa vitu, vifaa kwenye ile hospitali, inachukua lile eneo ni kama mkoa nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ile Hospitali ya *St. Francis* waiangalie kwa jicho la huruma. Kikubwa zaidi, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, yuko kwenye wakati mgumu kwenye hii Wizara, kwa hiyo, kama asipokuwa ngangari, kwa kweli anaweza akachomoka, kwa sababu hii sehemu ya dawa, ni sehemu kuliko dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatumia dola bilioni moja kwa mwaka, ni sawasawa na karibu shilingi trilioni 2.7 za Kitanzania, kwa ajili ya kuagiza dawa. Hii inaonekana watu waliohodhi ni yale mapapa makubwa makubwa, kwa ajili ya kuleta dawa. Katika hizo dawa mimi sitaki kupepesa macho, nyingi ni feki na zina *milligram* chache. Unaweza kuandikiwa dawa *milligram* 500, ndani kuna *milligram* 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti wa hali ya juu sana, mpaka mimi nilichukua vidawa dawa fulani nikavipeleka nchi fulani. Kama vile vidawa vya gesi vinaitwa *Magnesium*, sijui vinaitwa nini vile. Ninakwenda kule, yule jamaa nimeenda dukani nikamwambia, ninataka kama hii, akanitajia bei inafanana na Tanzania. Nikamwambia mbona Tanzania hizi bei rahisi, akanitolea boksi, akasema sisi haturuhusiwi kuuza, hizi chukua bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye mpango wa kujenga viwanda, pale walipoweka eka 400, kwenye ile hospitali Mloganzila. Ninaomba viwanda vya Watanzania, kama ni watu wa nje waje wajenge Tanzania, kama kila kitu kije kijengwa Tanzania. Hii habari ya kutegemea watu wa nje kuagiza dawa huko, hiyo habari tuachane na hiyo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango ni mzuri na huu mpango lazima utekelezwe. Tunajua kuna vita kubwa sana na ninawashukuru Wabunge, hawa walioingia Bunge jipya hili. Hawa wengi humu, siyo wale watu wa kubabaishwa na shilingi shilingi. Piga makofi kwa Wabunge wapya wote wa humu ndani na wa zamani waliorudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii nikija kuona mpango huu kuna mtu anaukwamisha, nitatafuta majina na nitakuja nayo hapa. Nitayataja, bora niitwe Kamati ya Maadili, lakini nitayataja majina ya watu wanaokwamisha mambo ya viwanda vya nchi hii. Hata vyombo vya ulinzi na usalama, lazima wao waunge mkono hili suala, kwa sababu hili suala Waheshimiwa Wabunge hawalielewi. Hili ni kuliko dawa ya kulevya na watu wamejipanga wanapinga viwanda vya dawa visiwepo Tanzania, lazima niwaambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko bega kwa bega na Mheshimiwa Waziri, tunamuunga mkono na tunaomba ahakikishe kwamba, viwanda vinapatikana. Kwa sababu, leo wafikirie palikuwa na ile shida ya *COVID*, dawa zinatoka nje, mara tunatishwa zingine zinapunguza nguvu za kiume. Wanaume wengi hawajachoma zile, mara wengine sijui wanawake wanaambiwa hawazai, mara sijui nini, lakini ya kweli, ukipiga sindano nyingine kwanza mpaka uumwe, unaamka siku ya pili. Tungekuwa na viwanda vyetu hapa, tungekuwa hatuna mashaka. Watanzania wana imani sana na vitu vyao, kwa hiyo wangechoma zile sindano, tungekuwa hatuna shida. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Iran na Marekani wamefunga ule mlango wa bahari pale kwao. Je, pakitokea shida ya dawa, tutakosa hata *Panadol* za kula hapa Tanzania, maana yake hatuna viwanda. Kwa hiyo, yeyote atakayekuwa anapinga huu mpango wa nchi hii kuwa na viwanda, huyu ni mchawi wa nchi na haitakii mema hii nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, tutakuwa tunaweza kuangalia hii dawa kweli imetengenezwa ina *milligram* 600 ina *milligram* 500. Tunahakiki wenyewe, tunajua ni kweli, kama kiwanda hakitengenezi tutakifungia, watu watakuwa waoga watatengeneza viwango vya uhakika vya dawa. Leo hii, watu wanasikia tu India, sijui wapi Kenya, kuna madaktari wazuri lakini Tanzania kuna madaktari bora sana na ni wazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ndugu yangu mmoja nilimpeleka India, nikaenda kushangaa dawa alizopewa na daktari wa Tanzania ndiyo alizopewa India. Zaidi ya hizo

alizopewa hapa hakupona, alizopewa kule kapona, lakini dawa ni ile ile. Hata ukienda, ukiangalia maboksi yanayotumika India ya dawa, kama ni *Panadol*, kama sijui ya *Amoxiclav*, kama ni nini, ukiangalia ni tofauti. Sasa kwa nini, wasitupe kama inayotumika kwao. Kwa hiyo kuna shida sana kwenye dawa hizi za binadamu. Tunao madaktari wazuri sana, lakini dawa zinatuangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme, hata hizi dawa wanaandika tu, dawa *Made in* sijui Italy, *Made in* sijui wapi, yote ni uongo. Yanatengenezwa huko huko, yanaandikwa tu *Made in* fulani, unapigwa hela pale, unaacha kununua dawa 5,000, unaenda kununua dawa 25,000, kumbe ni ile ile tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba umakini na kwa sasa wakati bado tunaendelea kuwa na viwanda. Kuomba umakini wa namna ya dawa zinavyoingia na kuhakiki hizi dawa, ni kweli yanatoka nchi fulani. Hata pamoja na kuwa shida sana, kama hamna viwanda kupima *milligram*, lakini kidogo inaweza ikatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo, katika Kikao chetu cha Ishirini na Sita, Mkutano wa Tatu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kukumbusha, kwa mujibu wa Kanuni ya 74(1), imeeleza mambo yasiyoruhusiwa Bungeni wakati wa mijadala. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusome na tuzingatie, lakini tunakumbusha pia Mbunge anapopewa maelekezo na Kiti hapaswi kukaidi, bali anapaswa kufuata maelekezo ambayo Kiti kinamwelekeza.

Kiti pia kinawajibika kulinda utaratibu bora wa majadiliano ndani ya Bunge na ikibidi pale ambapo panatokea mchangiaji anataka kuhatarisha utaratibu bora wa majadiliano, Kiti kinaweza kumkatisha mzungumzaji asiendelee kuongea.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusisitiza tuendelee kuzisoma Kanuni zetu na tujifunze kwa kuwa huo ndiyo mwongozo wa majadiliano yetu ya Shughuli za Bunge hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 12 Mei, 2026, saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 1.49 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 12 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)